

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 30 Aprili, 2019

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Tukae. Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAJI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MWENYEKITI: Ahsante, Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Maswali, tunaanza Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

Na. 146

Ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda

MHE. ANNA R. LUPEMBE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakarabati Shule ya Sekondari ya *Mpanda Girls?*

MWEYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanya ukarabati wa Shule za Sekondari Kongwe nchini kwa awamu kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha. Katika Awamu ya kwanza, Serikali imekarabati shule za sekondari 53 kwa gharama ya shilingi bilioni 53.6 ikijumuisha ujenzi wa Shule za Sekondari za Nyakato na Ihungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu ya pili Serikali imepanga kukarabati shule 17 kongwe za Sekondari nchini ikiwemo Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda. Jumla ya shilingi bilioni 16 zimetengwa kukarabati shule hizo. Mionganoni mwa fedha hizo shilingi milioni 986 zimetengwa kwa ajili ya Shule ya Wasichana ya Mpanda. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lupembe.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Shule hii ni kongwe halafu iko kwenye eneo ambalo ni hararishi, kuna bwawa ambalo lina wanyama wakali ambao wanaingia katika eneo la shule kwa sababu

shule hii haina uzio kabisa; na shule hii ina upungufu mkubwa sana wa madarasa na vilevile ina upungufu wa mabweni; na kwa kuwa Serikali imepanga fedha na imesema hapa kuwa *imeji-commit* na pesa tayari zipo; sasa naomba *commitment*, ni lini Serikali itakarabati shule hii kwa sababu wanafunzi wa shule hii wanapata taabu sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, shule hii ina wasichana takribani watoto 888, ni watoto wa kike ambao wanapata shida sana; usiku wakiugua hakuna gari katika shule hii: kwa kuwa hii shule ni kongwe, ni lini Serikali itatuletea gari katika shule hii ya Sekondari ya *Mpanda Girls*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu. Jiandae Mheshimiwa Kapufi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba zimetengwa fedha shilingi bilioni 16 kwa ajili ya kukarabati shule nyingine mwaka huu wa fedha na *commitment* ya Serikali ni kwamba ukarabati huu unaanza mara tu tutakapoanza kutekeleza bajeti ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal la pili, ametoa hoja ya gari na ni kweli kwamba kwa shule hizi kongwe na kutokana na mazingira ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge, naomba tupokee ombi hili tutalifanyia kazi kwa kadri uwezo wa Serikali utapopatikana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kapufi, Mheshimiwa Mwanne, Mheshimiwa Mwakasaka na Mheshimiwa Nape.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nikirejea hapo katika Shule ya Wasichana ya Mpanda kimechimbwa kisima kirefu, tatizo lilitobaki ni ufungaji wa *pump* na ukizingatia ni shule ambayo ina watoto wa kike peke yake.

Ni lini Serikali itakamilisha suala la ufungaji wa *pump* kwenye shule hii? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tunapokarabati hizi shule kwanza tunaangalia mfumo wa majengo, mabweni, bwalo, madarsa, Ofisi, majengo ya utawala, mfumo pia wa maji na mfumo wa umeme. Kwa hiyo, kama alivyozungumza kwamba kuna kisima ambacho kimechimbwa katika eneo hilo, wakati wa ukarabati litaangaliwa. Tutatenga fedha kwa ajili ya kupata maji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuwa na wanafunzi wengi katika shule hii kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba ni zaidi ya wanafunzi 800, watoto wa kike, halafu kusiwe na huduma ya maji. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanne.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya ukarabati katika shule za sekondari yanafanana na shule za msingi, Mkoa wa Tabora katika Manispaa ya Tabora, Shule ya Kanyene iliezuliwa karibuni madarasa manne tangu mwaka 2018 Machi, mpaka leo haijafanyiwa ukarabati, wanafunzi wanapata taabu. Nini kauli ya Serikali kwa leo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nipokee maombi na maelekezo ya Mheshimiwa Mbunge tutayafanyia kazi. Mpaka Bunge lijalo tutakuwa tumepata majibu ya tatizo hili katika eneo la Tabora. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakasaka.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Shule ya wasichana ya Tabora (*Tabora Girls*) ni shule kongwe sana hapa nchini ambayo pia ina vipaji maalumu. Shule hii kwa muda mrefu imetelekezwa kuhusu uzio. Ile shule haina uzio kabisa kwa miaka mingi na tayari juhudzi za viongozi mbalimbali nikiwemo mimi mwenyewe tumeshaanza mkakati wa kujenga uzio huo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutusaidia katika kukamilisha uzio huo wa Shule ya Wasichana Tabora?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Nape.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namwomba Mheshimiwa Mbunge tuonane tuone. Kama wananchi wameanza kujitolea na wadau mbalimbali akiwepo Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya wananchi wake anaowawakilisha hapa Bungeni, basi tuonane tuone ni changamoto gani zilizopo na sehemu gani ya kuweza kusaidia kumalizia uzio huo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami naulize swali dogo la nyongeza. Katika jitihada za kuboresha miundombinu ya elimu Mkoani Lindi, kwa misimu miwili, mitatu iliypita tulikubaliana kukata fedha kutoptana na malipo ya korosho ya shilingi 30/= kwa kila kilo ili kukarabati miundombinu na kujenga miundombinu mipya. Sasa iko miundombinu ambayo ilianza kujengwa kwa sababu ya hali ambayo sote tunajua, miundombinu hiyo sasa imesimama kwa sababu hiyo fedha haikupatikana.

Je, Serikali iko tayari kusaidia kumalizia miundombinu hii katika Mkoa wa Lindi hasa upande wa elimu? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia ya Serikali kuendelea kukamilisha miundombinu ya elimu na hasa ile ambayo imeanzishwa na wananchi na ndio maana tumepeleka fedha za kiutawala mwezi Januari, tumepeleka fedha za maboma karibu shilingi bilioni 29.9. Kwenye bajeti hii ambayo imepitishwa, zaidi ya shilingi bilioni 90 inaenda kusimamia miundombinu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipokee maombi ya Mheshimiwa Mbunge, tutazingatia maoni yake. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu mazuri, tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Rashid Akbar.

Na.147

Matumizi ya Gesi Inayotoka Mtwara na Songosongo

MHE. AJALI R. AKBAR aliuliza:-

Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa gesi kutoka Mtwara na Songosongo inatumika kwa asilimia sita tu:-

(a) Je, kwa nini Kiwanda cha Saruji cha Dangote na Mtwara *Cement* Mkoani Mtwara havijapatiwa umeme wa gesi asilia hadi leo?

(b) Je, kwa nini Wananchi wa Mtwara wasiunganishiwe gesi asilia kwenye nyumba zao?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Rashid Ajali

Akbar, Mbunge wa Newala Vijiji, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kiwanda cha Saruji cha Dangote kimeunganishwa na miundombinu ya gesi asilia ambapo awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa kuwezesha matumizi ya gesi asilia kuzalisha umeme kwa ajili ya kiwanda cha Dongote ilikamilika na kuanza kufanya kazi mwezi Agosti, 2018.

Aidha, hadi kufikia Mwezi Aprili, 2019 kiwanda cha Dangote kimeanza kutumia wastani wa futi za ujazo milioni tano kwa siku kwa kuzalisha umeme. Awamu ya pili ya mradi ilikamilika mwezi, Desemba, 2018 na sasa kiwanda cha Dangote kinatumia gesi ya wastani wa futi za ujazo milioni 15 hadi milioni 20 kwa siku kwa ajili ya uzalishaji wa Saruji. Jumla ya gharama za mradi ni shillingi billioni 8,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa *TPDC* inaendelea na utekelezaji wa mradi kwa kuagiza na kujenga miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia majumbani, viwandani na katika Taasisi mbalimbali kwa Mikoa ya Mtwara, Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza gesi asilia Mkoani Mtwara imeshaanza ambapo kwa sasa kazi ya ununuzi wa vifaa, mabomba, mita za kupimia gesi pamoja na vifaa vya kupunguza mgandamizo wa gesi inaendelea. Inategemewa zaidi ya Kaya 120 za awali zitaunganishwa mabomba ya gesi Mkoani Mtwara kwa matumizi ya nyumbani ifikapo Mwezi Juni, 2019. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Akbar.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kuna taarifa ambazo ni rasmi, kwamba pamoja na kwamba Dangote amepatiwa gesi hii na baadhi ya viwanda vilivypo Mkuranga, sasa vile viwanda

vimeshindwa kutumia ile gesi katika kiwango ambacho ni tarajiwa. Ina maana wanatumia gesi pungufu na vingine vimetoa *notice* ya kufungwa.

Je, ni lini sasa Serikali itapunguza bei ya gesi hii ili viwanda hivi visifungwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, (b) nina taarifa rasmi vilevile kwamba kuna wawekezaji ambao walikuwa wametoka mashariki ya mbali; China na Uturuki, wapatao wanne ambao waliokuwa wamekusudia kuja kuwekeza hapa nchini. Ikumbukwe kwamba faida ya gesi siyo kwamba ni kwa kuuza tu, lakini vile viwanda vingeweza kulipa kodi, kutoa ajira na faida nyingine ambazo Taifa lingeweza kupata tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kwamba bei ya gesi yetu ni Dola 5.5 *per metric tones* wakati katika Soko la Dunia ni Dola 3.7 *per metric tones*. Sasa je, Serikali ina mkakati gani na kwa nini sasa isifanye *sub...*

MWENYEKITI: Swali, swali swali!

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, swalni kwamba, naomba kwamba Serikali ipunguze bei ili wawekezaji hawa wasikimbie ili tupate faida nyingine zitokanazo na viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu maswali mwili ya nyongeza ya Mheshimiwa Akbar, Mjumbe wa Kamati yetu ya Nishati na Madini. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya katika ushiriki wake kwa Kamati yetu inayosimamia Sekta yetu ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali mawili aliyojelekeza; la kwanza Mheshimiwa Mbunge ameeleza

namna ambavyo viwanda vilivyounganishiwa gesi ikiwemo Dangote na viwanda nya Mkuranga kwa mfano Goodwill, kwamba vinaona bei ya gesi ni kubwa; nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo suala limewasilishwa Wizarani; na kwa kuwa wapangaji wa gesi hii ni wa bei ya gesi asilia (*EWURA*) pamoja na Taasisi ya *PURA* ambayo ina-regulate Sekta ya Nishati upande wa gesi kuhusu masuala ya *upstream*, ni kwamba ndani ya Serikali jambo hili limepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia *EWURA* kwa kuwa ni kazi yao kupanga hizi bei za gesi itafanya kazi kuangalia mchakato mzima. Pia ni lazima nikiri kwamba gharama ya uzalishaji wa gesi hapa nchini hii gesi ambayo inatumika ni zaidi ya shilingi *USD5.36*. Kwa hiyo, utaona, lakini nia ya Serikali ni kuwezesha viwanda kutumia gesi na kuzalisha malighafi. Kwa hiyo, hili jambo limepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili Mheshimiwa Mbunge ameulizia kwamba kuna wawekezaji kutoka nchi mbalimbali ambao wameonesha nia ya kuwekeza, sisi kama Serikali ya Awamu ya Tano kwa kweli imeandaa mazingira ya kukaribisha uwekezaji katika maeneo mbalimbali hasa viwanda nya mbolea katika Mkoa wa Mtwara na eneo la Kilwa. Hata sasa iliundwa Kamati ya Wataalam kufanya mapitio ya gesi hasa katika suala zima la kuwezesha viwanda hivi na wawekezaji katika kuwekeza kwenye suala la mbolea. Kwa hiyo, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge suala hili limefanyika, sasa hivi kinachofuata ni kikao baina ya wawekezaji na tangu mwezi wa Nne pia kilifanyika kwa ajili ya kupanga bei na kukubaliana. Hata wale wawekezaji kwa mfano Kampuni ya *Helm* na *AGya WDya Egypt* walishapewa mwelekeo na namna ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimthibitishie tu kwamba Serikali ipo tayari kuwakaribisha wawekezaji na waje tu na mazungumzo yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mama Salma.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Lindi na Mtwara ni Mikoa jirani sana. Katika majibu yake ya Msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema gesi ya Mtwara itasambazwa majumbani katika Mkoa wa Mtwara, Pwani, pamoja na Dar es Salam, Lindi wameiruka. Sasa je, ni lini Lindi watasambaza gesi hii majumbani? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi, anataka kujuua Lindi lini? Mheshimiwa Waziri mhusika.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kwamba ni kweli mpango wa kwanza unaanza na Mikoa mitatu ya Dar es Salaam pamoja na Mtwara na Lindi. Kwa sasa tumeanza kusambaza Dar es Salaam na tarehe 40 mwezi huu wataanza kujenga mabomba Mtwara na tarehe 30 mwezi Mei wataanza utaratibu wa kujenga mradi wa kusambaza gesi majumbani Lindi.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa muda. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvumi, Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara.

Na. 148

Kuanzisha Skimu ya Ufugaji na Kilimo cha Kisasa

MHE. ALEX R. GASHAZA aliuliza:-

Zamani kulikuwa na maeneo yaliyokuwa yametengwa kwa ajili ya Mifugo na Kilimo katika kutekeleza Sera ya Matumizi Bora ya Ardhi, lakini idadi ya watu inavyoongezeka, maeneo hayo yanavamiwa na kusababisha migogoro:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya kuanzisha Skimu ya Ufugaji bora na kilimo cha kisasa ili kuepukana na migogoro ya wakulima na wafugaji?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hapo awali yalikuwepo maeneo mengi yaliyokuwa yametengwa kwa ajili ya wafugaji nchini ambayo kwa sasa yamebungua kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la shughuli za kijamii kama vile kilimo, makazi na shughuli nyingine za kiuchumi. Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini imetenga maeneo ya malisho kuyagawa kwenye vitalu na kuyatoa kwa wafugaji kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jukumu la kuanzisha "Scheme" za ufugaji wa kisasa unaozingatia kanuni za ufugaji wa kisasa, Serikali kupitia Wakala wa Mafunzo ya Mifugo Nchini (*LITA*) imeandaa mpango kabambe wa kuanzisha "*Incubation Youth Center*" ambapo vijana waliohitimu Vyuo vya katika ngazi ya Cheti na Diploma watapata fursa ya kuanzisha miradi ya ufugaji kwa vitendo kwa muda maalum chini ya wakala na watakahitimu watakuwa na fursa nzuri ya kujiajiri kupitia ufugaji. Pia, watakuwa na fursa ya kuanzisha mashamba ya mfano katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imezindua rasmi mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani na Wafugaji kuhusu ufugaji bora nchini nchi nzima. Mafunzo hayo yanakusudiwa kutolewa kwenye Halmashauri zote nchini na yameanza kutolewa katika Wilaya ya Simanjiro, Mkoani Manyara ambapo wafugaji 750, Maafisa Ugani 32 walipata mafunzo rejea na katika Wilaya ya Kaliua, Mkoa Tabora mafunzo rejea yalitolewa kwa wafugaji 438 na Maafisa Ugani 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo hayo yamejikita katika uboreshaji wa Kosaafu za mifugo, udhibiti wa magonjwa, matumizi sahihi ya madawa na viuatilifu, uboreshaji wa viuatifu, uelewa wa Sheria, Kanuni na Miongozo

ya Sekta ya Mifugo ili kuepukana na migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Aidha, mafunzo yanalenga kuwaongezea wafugaji maarifa kwa kuwapatia teknolojia mpya ili kuhamasisha Ufugaji wa Kisasa na Wakibashara nchini. Mpango huu unalenga kuongeza uzalishaji wa malighafi zitokanazo na mifugo yenye viwango bora ili kukidhi mahitaji ya viwanda vyta nyama maziwa na ngozi vinavyoendelea kujengwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na juhudhi hizo, Wizara imeendelea kuhamasisha wafugaji kuanzisha maeneo ya kuzalisha malisho bora ili kuongeza uzalishaji. Pia Wizara imeanzisha mashamba darasa ya mfano 365 katika maeneo mbalimbali nchini ili kuchochea wafugaji kujifunza na kuzalisha mbegu na malisho.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gashaza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa katika Jimbo la Ngara hakuna maeneo yalijotengwa kwa maana hakuna *blocks* kwa ajili ya malisho ya mifugo, sasa Serikali kupitia Wakala wake wa Mafunzo ya Mifugo Nchini *LITA*, wako tayari kuanzisha kituo hiki cha *Incubation Youth Center* katika Wilaya ya Ngara ambako kuna mifugo mingi zaidi ya Ng'ombe 75,000 ili kuweza sasa kuwawezesha vijana kuanzisha mashamba darasa ili waweze kujikumu kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa upo mnada ambaa Serikali iliweka fedha nyingi, mradi wa Mursagamba uliojengwa zaidi ya miaka 20 iliyopita, natambua kwamba Serikali imepeleka fedha sasa kwa ajili ya kukarabati ili uweze kuanza kutoa huduma, ni lini sasa mnada huu utafunguliwa ili uanzesha kutoa huduma?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Alex Gashaza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba Chuo chetu cha *LITA* kilichopo pale Mkoani Kagera, katika Wilaya ya Karagwe katika *ranch* yetu kubwa ya Kikurura *complex* tutakitumia kwenda kufanya mafunzo ya hii *program* maalum ya *Incubation Youth Center* kwa ajili ya kuwanufaisha watu wa Wilaya ya Ngara, vijana mahususi kwa ajili ya kuweza kutumia fursa ya mifugo iliyokuwa mingi kuzalisha na kupata ajira na kuinua kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni juu ya mnada wa Mursagamba; ni kweli katika bajeti ya mwaka 2018/2019, Serikali na Wizara yetu ya Mifugo tulitenga pesa kwa ajili ya kuweza kuufanya marekebisho mnada wa Mursagamba na hivi ninavyozungumza, utaratibu wa kuweza kukamilisha hatua hiyo unaendelea na mara tu baada ya kukamilishwa kwa hatua hiyo tutakwenda kuufungua na tutamkaribisha Mheshimiwa Mbunge Gashaza ambae ailipigia debe sana kuhakikisha mnada huu unafunguliwa ili na yeze aweze kushiriki kikamilifu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu na Wilaya ya Ngara kwa ujumla wake.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shangazi, wajiandae Mheshimiwa Yussuf na Mheshimiwa Julius.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Kijiji cha Mkundi ya Mtae, Tarafa ya Umba ambayo kimsingi Tarafa hii karibu eneo kubwa ni wafugaji, pana migogoro ya ardhi ambayo ni baina ya wakulima na wafugaji na mara kadhaa nimejaribu kuwasiliana na Wizara kuona namna bora ya kutatua mgogoro katika eneo hili ambalo kimsingi eneo hili lilikuwa ni eneo la wafugaji. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuboresha maeneo haya hasa katika sekta nzima ya ufugaji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejipanga vyema katika kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji na tumeunda Kamati ambayo inatembea nchi nzima katika kuhakikisha kwamba migogoro ya wakulima na wafugaji inapatiwa suluhi na kwisha kabisa. Kijiji alichokitaja cha Mkundi Mtae ambapo kipo katika Tarafa nzima ya Umba ambayo sisi kama Wizara ya Mifugo tumekitambua kijiji hiki na maeneo mazima ya Tarafa ya Umba kuwa ni maeneo yanayoshughulika zaidi na shughuli za ufugaji. Nataka nimhakikishie Wizara yetu inayo mipango mizuri ya kuhakikisha kwamba fursa na uwekezaji katika mifugo inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye Mwenyewe Mheshimiwa Mbunge Rashid Shangazi ameleta maombi ya kuboresha majosho yaliyoko katika eneo hili. Naomba nimhakikishie kuwa, majosho yale yamechukuliwa na Wizara yetu na yapo katika mpango wa kuhakikisha yanarekebishwa na yatakapokuwa tayari yamerekebishwa sisi katika Wizara tutakuwa pamoja na yeye kwenda nae pale kwenda kuyazindua kwa ajili ya kuboresha sekta yetu ya mifugo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf, ajiandae Mheshimiwa Kalanga.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimrejeshe Mheshimiwa Naibu Waziri katika swali la msingi la kanuni za ufugaji bora na kilimo cha kisasa. Sasa ni wapi Mheshimiwa Waziri anaweza akatuambia kwamba ni *sampling area* ambapo Serikali inafanya ufugaji bora na kilimo cha kisasa ambacho kitaondoa hiyo migogoro baina ya wafugaji na wakulima, *sampling area* katika nchi ni wapi ili wengine wakajifunze?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Mheshimiwa Waziri unajibu vizuri sana, lakini jibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwanza kwa pongezi zako hizi za kunielekeza kuwa najibu vizuri sana isipokuwa nijibu kwa kifupi na nitafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Yussuf kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wapi katika nchi? Nataka nimhakikishie tunayo maeneo mengi sana katika nchi ambayo yana wafugaji wanaofuga kisasa katika mikoa mbalimbali. Kwa kuwa amenitaka nijibu kwa mfano sehemu moja tu ambayo Mtanzania au Watanzania wanafanya; ukienda katika Mkao wa Morogoro utakutana pale na Mfugaji wa kisasa anaitwa Profesa Shemu mwenye ng'ombe zaidi ya 700, ng'ombe wa kisasa wanaozalisha maziwa, huyu ni mmoja wa mfano. Ukienda Wilayani Chato kwa Mheshimiwa...

MWENYEKITI: Inatosha, ahsante. Mheshimiwa Julius.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Moja ya tatizo kubwa linalowakabili wafugaji wa nchi hii hata wakianzisha ufugaji wa kisasa ni upatikanaji wa mbegu bora, lakini mpaka sasa ukifuatulia katika maeneo ambayo kuna *artificial insemination* ng'ombe waliopo no *Borana* pamoja na *ZEBU* wale wa Mpwapwa. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inaingiza mbegu bora nchini kwa ajili ya kusaidia wafugaji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mfugaji, Mbunge wa Monduli, Mheshimiwa Julius Kalanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango kabambe mzuri sana wa kuhakikisha tunaboresha mbali kwa

maana ya kwa safu zetu mifugo katika nchi kwa kusimamia mikakati mikubwa mitatu:-

(i) Wa kwanza ni ule wa *artificial insemination* ambao umeenea nchi nzima katika vituo yetu.

(ii) Wa pili ni ule wa kutumia njia ya asili kwa kutumia madume bora ambayo yanapatikana pia katika mashamba yetu. Ukienda katika shamba kama vile la Mabuki-Mwanza, Sao Hill - Iringa na kwingleko tunao *Bulls* wa kutosha ambao wanawenza kwenda kuboresha mifugo hiyo.

(iii) Ya tatu tunao mpango tunaita "*multiple ovulation*" ambapo mpango huu unakwenda kukamilika mwaka huu kuititia shamba letu la Mpwapwa ambao huu utakwenda kumaliza kesi hi ya kupatikana kwa mifugo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kalanga na...

MWENYEKITI: Ahsante, utamjibu *canteen. (Kicheko)*

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo.

Na. 149

Changamoto za Zao la Tumbaku

MHE. RICHARD P. MBOGO aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali italeta mbegu bora ya tumbaku kama inayolimwa katika nchi nyingine Kusini mwa Jangwa la Sahara?

(b) "*Produce cess*" ilishushwa kutoka asilimia tano mpaka asilimia tatu ili mkulima afaidike kwenye bei ya kuza lakini hakuna utekelezaji kwa Makampuni ya Kununua Tumbaku na kwenye Halmashauri mapato yameshuka. Je,

Serikali inaweza kupitia upya Sheria hiyo na kurudisha kama awali?

(c) Je, ni lini Serikali itakaribisha Kampuni nyingine za kununua Tumbaku ili kuongeza ushindani na kuondoa hofu kwa wakulima?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, uhitaji wa aina ya tumbaku hutofautiana kati ya mteja na mteja. Tumbaku inayozalishwa nchini kwa sasa inatokana na mbegu zinazopendwa na wanunuzi waliopo. Wizara imepokea maombi kutoka Nchi ya China ya kuuziwa aina ya tumbaku inayotokana na mbegu zinazolimwa katika Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Utaratibu wa kupate mbegu za tumbaku aina za PVH 2254 na KRK 26 kutoka Malawi na aina ya MHW 86 kutoka Zambia umeanza ili mbegu hizo ziweze kuzalisha tumbaku inayokidhi soko la China kuanzia msimu wa 2020/2021.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ilipunguza ushuru wa mazao ya biashara katika mwaka wa fedha 2017/2018, kutoka asilimia tano hadi asilimia tatu ili kuongeza kipato cha wakulima. Utekelezaji wa Sheria hiyo umefanyika kwa mwaka mmoja tu wa fedha wa 2018/2019, hivyo Serikali itafanya tathmini ya utekelezaji wa sheria hiyo na kama itabainika utekelezaji wake katika tasnia ya tumbaku hauna tija kwenye mapato ya Halmashauri na kipato cha mkulima, Serikali haitasita kuchukua hatua na kupitia upya sheria hiyo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza ukiritimba wa Kampuni zinazonunua Tumbaku nchini, Serikali inaendelea

kuweka mazingira wezeshi ili kuzivutia kampuni nyingine zaidi na kuleta ushindani. Kufuatia jitihada hizo, Serikali imefanikiwa kupata kampuni zingine za kununua tumbaku ikiwemo Kampuni ya *British-American Tobacco (BAT)* ambayo imeonesha nia ya kununua tumbaku yetu moja kwa moja kutoa kwa wakulima. Taratibu za kufanikisha mpango huo zinafanyika ili Kampuni hiyo iweze kununua tumbaku ya wakulima kwa msimu wa Mwaka 2019/2020. Aidha, katika hatua nyingine, Serikali inakamilisha taratibu za kulipata soko la China kwa kutumia mbegu za tumbaku zinazozalishwa katika nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali juu ya majibu ya tumbaku, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, katika jibu la (b) kuhusiana na tozo (*Produce cess*) kwa kweli Serikali ilipunguza kutoka asilimia tatu mpaka tano. Ukiangalia *discount* hii ilikuwa ni karibuni asilimia 40 na mkulima hajafaidika. Kuhusiana na tathmini, binafsi kwenye halmashauri zetu tumekwishafanya tathmini mapato yameshuka. Sasa Je, Serikali iko tayari katika mabadiliko ya sheria yanayoletwa sasa hivi Mwezi Juni kwenye *Finance Bill* kurudisha hii *produce cess* kuwa asilimia tano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili dogo; Kampuni ya *Premium* ambayo inanunua tumbaku nchini ikiwemo Katavi, Chunya pamoja na Ruvuma mpaka sasa hajjalipa tozo za halmashauri pamoja na kwenye vyama vya msingi kwa sababu kwamba wana madai yao Serikalini ya marejesho ya kodi la ongezeko la thamani (*VAT refund*) na tangu mwaka jana tunafuatilia na mpaka sasa Serikali hajjalipa hii kampuni na wanadai takribani bilioni 12. Sasa Je, Serikali haioni kwamba kutolipwa kwa wakati fedha hizi inachelewesha utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi katika halmashauri zetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi kwa maswali yote mawili.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbogo kwa namna anavyofuatilia zao la tumbaku kwa manufaa ya wakulima wa tumbaku nchini.

Swali la kwanza la Mheshimiwa Mbogo anauliza kama tuko tayari kurudisha *produce cess* kutoka asilimia tatu kurudi kwenye asilimia tano. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, Mheshimiwa Mbogo ana hoja nzuri lakini kama nilivyojibu ni mapema kwa sababu tuko *kwenye fiscal year* ya kwanza katika utekelezaji wa hii sheria na Serikali tumesema hatutasita baada ya kufanya tathmini na kuona kuna haja ya kurudisha hiyo *produce cess*. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira angalau twende kwenye *fiscal year* kama mbili, tatu halafu baada ya hapo tutafanya tathmini na kuona namna ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la Mheshimiwa Mbogo, anasema kutolipwa kwa *VAT refunds* kwa muda kunaathiri malipo kwenda kwenye halmashauri na vyama vya ushirika. Kwa vile suala hili linahusu *VAT claims* basi nimwahidi Mheshimiwa Mbogo tutakaa na wenzetu Wizara ya Fedha na kuangalia namna ya *ku-expedites* ili Kamouni hii iweze kulipa madeni ya halmashauri na *AMCOS*.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Flatei wajjandae Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Ryoba na Mheshimiwa Kafumu.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Zao hili la tumbaku ina changamoto zinazofanana na zao la vitunguu swaumu. Je, mna mpango gani sasa wa kusaidia zao la vitunguu swaumu kama zao la biashara kama ilivyo tumbaku?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana, muda wetu umekwenda.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbogo Flatei kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitunguu swaumu pia ni zao muhimu ambalo linaweza kuwapatia wakulima wetu kipato na liko kwenye fungu la *spices*, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Flatei kwa sababu Serikali tuna mkakati wa pamoja wa kuhakikisha tunasaidia wakulima kupata masoko ya *spices*, basi na suala la vitunguu swaumu tutaliweka katika hilo fungu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ndassa, jiandae Mheshimiwa Ryoba, jiandae Mheshimiwa Kafumu na Mheshimiwa Sophia.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tulipitisha azimio humu Bungeni kwamba msimu wa pamba unatakiwa uanze tarehe Mosi Mwezi Mei kila mwaka. Hivi sasa kuna Walangazi tayari wameshaanza kuitapita na kununua Pamba kwa shilingi mia tano, mia sita, mia saba. Je, ni nini tamko la Serikali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, bei ya pamba.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali la Mheshimiwa Ndassa (*Senator*) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mheshimiwa *Senator* ni taarifa muhimu sana kwa Wizara ya Kilimo kwa sababu tarehe 29 Aprili, tulifanya Mkutano wa 15 wa wadau wa pamba na baada ya hapo jana tulikuwa tuna kikao cha kuitapia mwongozo wa msimu wa ununzi wa pamba na leo hii tunapitia masuala ya bei elekezi ili kuanza msimu tarehe Mosi Mei, 2019 na taratibu hizi zote ziko kisheria, kwa hiyo yoyote yule ambaye ananunua pamba kabla ya uzinduzi wa

msimu wa pamba ambao uko kisheria ni ukiukwaji wa sharia. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Ndassa baada ya hapa nitawasiliana na Wakuu wa Mikoa na kuhakikisha Serikali tunajipanga kuhakikisha mkulima hanyonyi...

MWENYEKITI: Ahsante, ameshakuelewa

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): ...kwa sababu shilingi mia sita au mia saba ni hela ndogo sana kwa mkulima.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ryoba, wajiandae Mheshimiwa Kafumu na Mheshimiwa Sophia.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kampuni ya *Alliance One* iliyokuwa inanunua tumbaku Serengeti illondoka wakati ambapo wakulima wako kwenye *peak* ya kilimo cha tumbaku. Baada ya kuondoka wakulima wakashindwa wapi wauzie tumbaku yao. Kwa kuwa Serikali ina jitihada ya kuwatafutia wananchi wa Serengeti kampuni nydingine ya kununua tumbaku, kwa nini wakulima wanaolima sasa hivi tumbaku wasiruhusiwe kuuza kokote watakako tumbaku yao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ryoba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Ryoba pamoja na wakulima wa pamba, Serikali inayo mikakati mizuri ya kuhakikisha tunawasaidia katika kupata masoko ya uhakika na nitumie nafasi hiui kumpongeza Balozi wetu Mheshimiwa Mbelwa Kairuki, Balozi wa China tunawasiliana nae na kuna ujumbe unaondoka mwezi huu mwishoni kwenda China kwa ajili ya kutafuta masoko ya tumbaku. Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Ryoba awe na subira, karibuni tutaweza kuwapa uhakika wakulima hawa wa pamba katika Jimbo lake.

MWENYEKITI: Ahsante. Dkt.Kafumu ajiandae Sophia.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Moja ya tatizo kubwa la wakulima wa pamba ni bei ndogo kwa sababu inasimamiwa na soko la dunia. Mwaka 2015/2016 na hata 2017, Serikali iliahidi kuanzisha Mfuko wa Kurekebisaha Bei ya Pamba. Nataka kuiuliza Serikali inasema nini juu ya ahadi hiyo ili wakulima wa pamba sehemu zinazolimwa pamba waweze kupata bei nzuri wakati wote?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, umeshalijibu hili lakini jibu tena.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kafumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge angependa kujua mkakati wa Serikali wa kuhakikisha tunasaidia kuinua bei ya pamba nchini. Kama mnavyojua suala la uinuaji wa bei ya pamba unatokana na *factor* mbalimbali ikiwemo *factor* ya tija na chini ya *SDP II*, Serikali tuna mpango mzuri wa kuhakikisha tunawasaidia wakulima wa pamba na mazao mengine nchini kuongeza tija sambamba na ku-*plan* mapema masuala ya masoko kwa wakulima wetu.

Kwa hiyo, kwa *combination* ya *factor* hizo mbili, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kafumu kwamba tutaweza kuleta uchochezi wa kuinua bei ya pamba pamoja na mazao mengine nchini. Ni muombe baada ya hapa tukae tuangalie hata hili suala la Mfuko wa kuinua zao hili inaweza ikawa ni sehemu ya mikakati ya Serikali kuinua zao hili.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa zao la tumbaku na pamba, ni lini Serikali itaongeza bei kwenye zao la chai katika Wilaya ya Rungwe na cocoa katika Wilaya ya Kyela? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, lini mnaongeza bei?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bei linakuwa *determined* na soko lakini moja ya mkakati wa Serikali kwenye zao la chai ni kuanzisha mnada hapa hapa nchini badala ya kutegemea mnada wa Mombasa. Kuhusu cocoa tunaendelea kuwasiliana na wanunuzi wa cocoa duniani ili kuona kama wanaweza wakanunua cocoa ya Tanzania. Kwa hiyo, mikakati ya Serikali ni mizuri kwa upande wa chai na cocoa na mkakati wa kuwa na mnada wa hapa hapa nchini utasaidia kuwapatia wakulima wa chai bei nzuri. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na swali la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene.

Na.150

Mashine ya Kujengea Iliyonunuliwa kutoka Marekani

MHE. JANET Z. MBENE aliuliza:-

Serikali ilinunua mashine ya kujengea kutoka Marekani kwa fedha nyangi sana kwa lengo la kuitumia kujenga nyumba nyangi za watumishi, ofisi na taasisi na kadhalika kwa haraka zaidi, mashine hiyo kwa muundo wake ina uwezo wa kujenga nyumba kwa bei nafuu zaidi na hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa nyumba za walimu, madarasa, maabara, mabweni, nyumba za wauguzi, madaktari na vituo vya afya:-

(a) Je, ni nyumba ngapi na kwa gharama gani zilizojengwa na Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa kwa kutumia mashine hiyo na kama zimejengwa kwa ujenzi wa kawaida zingetumia kiasi gani?

(b) Je, ni kwa nini mashine hiyo haitumiki kujenga nyumba zinazohitajika wakati kuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za Serikali?

(c) Je, Serikali iko tayari kufanya tathimini na kutuletea Bungeni mpango mzima wa kuanza kutumia mashine hiyo kujenga nyumba zinazohitajika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba nne zilijengwa wakati wa mafunzo kwa gharama ya shilingi 1,325,000,000 na majengo matano yalijengwa baada ya mafunzo kwa gharama ya shilingi 9,216,653,699.50. Gharama za majengo yote jumla yake ilikuwa ni shilingi 10,541,653,699.50. Majengo haya ni pamoja na ukumbi (*multipurpose hall*) na nyumba za kuishi katika Kambi ya Twalipo Dar es Salaam; Banda la Jeshi la Wananchi wa Tanzania la Maonesho Sabasaba; na Ofisi ya muda ya Kitengo cha Uwekezaji T/C. Nyingine ni Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Kihangaiko; Kiteule cha Kijeshi Tarime; Karakana ya Wakala wa Vipimo na Mizani Misugusugu Kibaha; ghala la kuhifadhiya nafaka la SUMA JKT kule Chita; na kumbi za burudani za SUMA JKT Mwenge Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo haya kama yangejengwa kwa ujenzi wa kawaida gharama zingefikia

shilingi 11,981,649,808.70. Mbali na teknolojia hii kuwa ya nafuu katika ghamara za ujenzi uliofikia asilimia 15%, unafuu mkubwa upo katika ujenzi unaokadirwa kuwa na asilimia 70%.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango kikubwa mashine hizi hazitumiki ipasavyo kutokana na ukosefu wa fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa *substructure* yaani ujenzi toka chini hadi usawa wa msingi. Malighafi inayotumka ni *steel coil* ambayo kwa matumizi ya Kijeshi kama fedha za maendeleo zingepatikana ingeweza kukidhi mahitaji.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, mitambo ya *UBM* (*Ultimate Building Machine*) ilinunuliwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za ujenzi ndani za Wizara. Hata hivyo, Wizara ya Ujenzi na Jeshi la Kujenga Taifa liko tayari kushirikiana pamoja na taasisi nyingine za Serikali katika ujenzi wa majengo hayo. Aidha, Wizara iko tayari kuandaa mpango kabambe kwa kutumia teknolojia hiyo ili kuwezesha ujenzi wa majengo mbalimbali ya Serikali. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbene.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Serikali kwa majibu mazuri na yenye kutoa matumaini lakini pamoja na hayo nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ni dhahiri kuwa mashine hii ingetumika vizuri ingesaidia sana kuondoa upungufu mkubwa sana wa majengo mbalimbali yanayohitajika katika kila sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuwa Serikali imekubali kuwa sasa iko tayari kushirikiana na Wizara nyingine kuhakikisha kuwa mashine hii inatumika vizuri zaidi. Je, ni lini sasa huo mkakati utafanywa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa upungufu wote wa nyumba za watumishi, madarasa, zahanati unafanyiwa kazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kiasi kikubwa teknolojia hii ni mpya na haijulikani vizuri, wako tayari kuitangaza ili hata *private sector* waitumie?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janet Mbene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipokee shukurani alizozitoa kwa kazi ambayo inafanyika kwa kuona kwamba kuna umuhimu wa kutumia mashine hizo. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi y kwamba upungufu unaokuwepo pale ni fedha za maendeleo, kama zingepatikana kazi hii ingeweza kuendelea vyema na nyumba nyingi zingejengwa kwa kutumia mfumo huo lakini kwa sababu pesa ni kidogo unakuta haiendi sambamba na mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kwamba Serikali iko tayari kwa maana ya Wizara kushirikiana na Wizara zingine kuweza kufanya kazi hiyo. Kama Wizara zingine zitakuwa zipo tayari pengine kugharamia *material* yale ambayo yana bei kubwa basi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iko tayari kushiriki katika ujenzi kwa sababu ndio wenye teknolojia hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Bagwanji Maganlal Meisuria kwa niaba yake Mheshimiwa Machano.

Na.151

Vurugu Wakati wa Uchaguzi – Zanzibar

MHE. MACHANO OTHMAN SAID (K.n.y MHE. BAGWANJI MAGANLAL MEISURIA) aliuliza:-

Mara nyingi wakati wa chaguzi mbalimbali Zanzibar kunatokea hali ya fujo na ukosefu wa amani na kusababisha wananchi kukosa amani na wakati mwagine kutoshiriki katika chaguzi husika:-

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Zanzibar juu ya suala hilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Maganlal Meisuria, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa nyakati za uchaguzi hukumbwa na vitendo vya uvunjifu wa amani hususani wakati wa kampeni na wakati wa kupiga kura. Hata hivyo, Serikali kuitia Jeshi la Polisi huchukua hatua mbalimbali kudhibiti vitendo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwafahamisha wananchi kuwa ni jukumu la Serikali kuhakikisha amani na utulivu vinatamalaki nchini wakati wote bila kujali nyakati au majira mbalimbali katika mwaka. Jeshi la Polisi linaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa Askari ya ukakamavu, upelelezi na kuongeza vitendea kazi ili kuwajengea uwezo na weledi wa kuzuia na kukabiliana na vitendo vya uvunjifu wa amani vinavyojitokeza hususani wakati wa uchaguzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machano.

MHE. MACHANO OTHMAN SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa matatizo makubwa ya Askari Polisi wakati wa uchaguzi ni uchache wao, je, Wizara iko tayari kushirikiana na vikosi vya SMZ kuongeza idadi ya Askari wakati wa uchaguzi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa imedhihirika kwamba kufanya uchaguzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ule wa Zanzibar kwa siku moja unaleta matatizo zaidi. Je, Serikali iko tayari kutenganisha chaguzi hizi na kufanywa siku mbili tofauti? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Maswali mafupi majibu nayo yawe mafupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Machano Othman Said, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anauliza kama tuko tayari na ndivyo ambavyo inatokea kwamba vyombo hivi vinafanya kazi kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la mabadiliko ya uchaguzi, nadhani hili suala linazungumzika na ni hoja ya msingi. Kwa hiyo, tunaichukua tuone kipi kinaweza kufanyika kwa kutilia maanani maoni yake.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Saada na Mheshimiwa Ally Saleh (Alberto).

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri ameelezea jinsi gani vikosi vyetu vitashiriki katika kuhakikisha kwamba amani inakuwepo wakati wa uchaguzi. Changamoto inayoonekana ni kwamba kunakuwa na uchache wa muda wa kutoa elimu ya uchaguzi (*voters education*). Je, ni kwa kiasi gani wamejitayarisha kushirikiana na Tume ya Uchaguzi kuona kwamba hiyo *voters education* inatolewa kipindi kirefu zaidi kabla ya uchaguzi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la nyongeza ya Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge Welezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba wakati wowote tutakuwa tayari kushirikiana na Tume za Uchaguzi pale ambapo watapanga ratiba zao vizuri. Naamini kabisa Tume hizi zimekuwa zikijifunza kulingana na changamoto zilizopita. Kwa hiyo, kama kulikuwa na mapungufu ya muda watarekebisha utaratibu huo na sisi tutakuwa tayari kushirikiana nao pale ambapo watapanga ratiba hizo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ally Saleh (Alberto)

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na hoja ya Mheshimiwa Bagwanji kwamba wakati wa uchaguzi kunakuwa na fujo nydingi Zanzibar. Ni kweli vilevile kwamba wakati huo kunakuwa kama uwanja wa vita Zanzibar; vifaru, magari ya deraya na vitendo vya kiharamia vingi vinafanywa na vikosi vya SMZ. Je, ni lini Serikali ya Muungano itaacha kutaka *interest* za matokeo ya Zanzibar kwa kuingilia kwa njia mbalimbali na badala yake waaachie mfumo wa demokrasia ufanye kazi na mshindi apewe ushindi wake? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la nyongeza ya Mheshimiwa Ally Saleh, Mbunge Malindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si sahihi kwamba Serikali imekuwa ikiingilia chaguzi. Hata hivyo, kuhusiana na hoja yake ya ulinzi kuimarika nyakati za uchaguzi Zanzibar hii inatokana na vitendo vya kiharamia ambavyo vimekuwa vikifanywa mara nyingi na hasa na vyama na upinzani.

Tumeshuhudia katika uchaguzi mbalimbali hususani Chama Kikuu cha Upinzani Zanzibar wamekuwa wanaongoza katika ukiukwaji wa taratibu za sheria za uchaguzi. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa uthibitisho nikiwa nasimamia Jeshi la Polisi, nakijua nachokizungumza kwamba nathibisha kwamba Chama Kikuu cha Upinzani Zanzibar kimekuwa kikikiuka taratibu za uchaguzi na kufanya vitendo ambavyo ni kinyume na sheria. Kwa hiyo, Jeshi la Polisi ama vyombo vyaya dola vitakuwa imara zaidi kudhibiti uvunjifu wa sheria ambaa unafanywa na vyama hivyo katika chaguzi mbalimbali.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcemba.

Na. 152

Zoo iliyopo Tabora Manispaa

MHE. MWANNE I. MCHEMBA aliuliza:-

Tabora Manispaa kuna Zoo ya Wanyamapori ambayo ilijengwa muda mrefu na mpaka sasa wanyama wanapungua na kuifanya kukosa maana:-

Je, Serikali iko tayari kupeleka wanyama hao katika zoo hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bustani ya wanyamapori ya Tabora ina ukubwa wa ekari 35.67 ambapo ekari 28.15 ni eneo la wanyamapori na ekari 7.52 ni eneo la makazi. Bustani hii ilianzishwa na Idara ya Wanyamapori mwaka 1967 ikiwa na aina mbalimbali za wanyamapori wakiwemo chui, simba, duma, fisi, pundamilia nyumbu, swala na ngiri. Kwa sasa, bustani hiyo ina jumla ya wanyamapori 256 wa aina tofauti 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1972 bustani hii ilikabidhiwa kwa Mkoa wa Tabora ili kusimamia kwa ukaribu. Mwaka 2001, Ofisi ya Mkoa wa Tabora ilikabidhi shughuli za usimamizi wa bustani hii kwa Manispaa ya Tabora. Manispaa ya Tabora iliisimamia hadi mwaka 2012 ilipoirejesha kwa Idara ya Wanyamapori kutokana na kuongezeka kwa ghamama za uendeshaji. Katika Idara ya Wanyamapori, bustani hii iliisimamiwa na Mfuko wa Wanyamaporি Tanzania (*Tanzania Wildlife Protection Fund*). Mwaka 2018 bustani hii ilihamishiwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamaporи-TAWA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza tija katika bustani ya wanyamaporи, TAWA inaandaa mkakati wa kusimamia bustani ya wanyamaporи zilizopo chini yake ikiwemo hii ya Tabora. Mkataba katika TAWA na mtaalam mwelekezi wa kuandaa mkakati huo umeshasainiwa ambapo mtaalamu huyo ataanza kazi hivi karibuni. Mkakati utakapokamiliika utaainisha aina na idadi ya wanyama watakaowekwa katika bustani, aina ya huduma zitakazotolewa kwa wageni na kiwango cha tozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mcchemba.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambayo yanaridhisha na yanakidhi swalı langu, naomba niulize maswali mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı la kwanza, kwa kuwa mpaka sasa Bodi ya TAWA hajakabidhiwa rasmi uendeshaji wa shughuli hiyo ili waweze kutekeleza mipango waliyotarajia.

Ni lini sasa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itawakabidhi TAWA ili waweze kufanya kazi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari tuongozane siku ya Jumamosi akaone hali halisi ambayo naizungumzia? Ahsante? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, la msingi muongozane mengine mtasema huko huko. (*Kicheko*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwanne Mcemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumpongeza kwa sababu amekuwa akifuatilia kwa karibu sana kuimarishwa kwa bustani hii kama chanzo cha mapato cha Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la kwanza, naomba kumhakikisha kwamba taratibu za kukabidhiwa kwa TAWA zimekamilika na ndiyo maana mshauri mwelekezi amepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda Tabora kwenda kuangalia bustani hiyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Boni.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpaka wa hifadhi wa Guruneti na Mto Rubana katika Vijiji vya Hunyali, Mariwanda, Kihumbu, Sarakwa na Mgeta lakini limekuwa tatizo la *buffer zone* inayotoka kwenye mto kuelekea vijijini na kuzuia watu kwenda kunywesha ng'ombe na malisho kwenye maeneo haya. Mheshimiwa Waziri alishatoa maelekezo ya mdomo

lakini ni lini Serikali itapeleka sasa vigezo vy a kisheria vy a kuondoa eneo hilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, siyo zoo tena, kaja na mengine huyu. Jiandae Mheshimiwa Bobali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kwamba kutokana na matatizo ya mwingiliano wa shughuli za kibinadamu na wananchi na hifadhi pamekuwepo na migogoro mingi ambayo sasa hivi kama ambavyo nimekuwa nikijibu maswali yangu mengi Serikali inayafanya kazi. Nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala lake tumekwishalizungumza, tunasubiri maelekezo ya Kamati ambayo iliundwa na Mheshimiwa Rais itakapotoa maelekezo tutatengeneza *buffer zone* ambayo itaruhusu wafugaji kwenda kwenye mto kunywesha mifugo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri anajua kwamba kijiji cha Ruhoma, Jimbo la Mchinga kimevamiwa na tembo na wanakula mashamba ya wakulima. Nataka kujua hawa watu mnafanyaje kuwa-*compensate* gharama zile za mashamba yao kuliwa na tembo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri kwamba, tatizo la wanyama kuvamia mashamba na makazi ya watu limeongezeka. Limeongezeka baada ya usimamizi wa maeneo haya yenye wanyamapori pia, kuimarika na watu waliokuwa wanafanya mauwaji ya wanyama kwenye hifadhi zetu kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limesababisha pia, uharibifu mkubwa wa mazao kwenye maeneo mbalimbali. Lakini utaratibu upo kwamba, pale ambapo wanyama hawa wanapovamia eneo na kuharibu mashamba ya wananchi utaratibu umewekwa kwamba, afisa wetu wa wanyamaporii apewe taarifa. Tunamuelekeza anakwenda pale anafanya tathmini na tathmnini ile inapofika katika Wizara yetu tunaelekeza kulipa mara moja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Tendega.

Na. 153

Wakinamama Wanaojifungua Watoto Njiti Nchini

MHE. GRACE V. TENDEGA aliuliza:-

Tanzania ni mionganini mwa nchi ambazo watoto wengi njiti huzaliwa na akinamama wanaojifungua watoto hao njiti wengi wao ni waajiriwa ambao hupata changamoto ya likizo ya uzazi inayotosha kwa malezi ya awali ya watoto hao njiti:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha akinamama hao wanaongezewa likizo ya uzazi?

(b) Akinamama hao wanapojifungua pia, hupata changamoto ya vifaa kama vile vifaa vya kukamulia maziwa, dawa na gharama za matibabu; Je, Serikali imejipangaje kuwasaidia gharama za vifaa hivyo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kutokomeza suala la akinamama kuzaa watoto njiti?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kazi ya Mwaka 2004, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2015 inaelekeza kuwa mama aliyejifungua mtoto mmoja apewe likizo ya malipo ya siku 84 na siku 100 kwa mama aliyejifungua watoo pacha, sheria hiyo pia imeweka wazi kuwa mama anayenyonyesha anatakiwa kupewa saa mbili kwa siku, ili apate muda wa kunyonyesha. Serikali haina muda wa kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa sasa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza sera ya Afya ya Mwaka 2007 ya Kutoa Huduma Bila Maipo kwa Makundi Maalum wakiwepo akinama wajawazito na mwongozo wa uchangiaji unaeleza wazi kuwa, kundi hili halipaswi kugharamia huduma za afya pale wanapohitaji. Hivyo, basi, Wizara inafanya juhudhi kubwa katika kuboresha huduma kwa akinamama wajawazito, hususan, wanapojojfungua kwa kutumia njia mbalimbali. Kwa sasa Wizara inatekeleza Mpango wa Pili wa kuboresha afya ya uzazi na mtoto, yaani *One Plan II* ya mwaka 2016 mpaka 2020 ambapo imeweka vipaumbele mahususi vya kuboresha afya ya watoto wachanga ikiwemo watoto njiti nchini. Kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara imetenga fedha bilioni 22.5 kwa ajili ya huduma ya mama wajawazito na katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 inatarajia kuomba idhini ya Bunge kutumia fedha kiasi cha bilioni 29.5 kwa ajili ya kundi hili na hivyo hakuna akinamama wanaojifungua wanaoripotiwa kukosa huduma za dawa na vifaa tiba kabla na baada ya kujifungua katika vituo vya Serikali.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kujikita katoka afua mbalimbali kwa lengo la kudhibiti visababishi vya kuzaliwa watoto njiti, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha akinamama wajawazito wanaanza kliniki mapema mara tu wanapohizi kuwa na ujauzito, kuhudhuria kliniki ipasavyo, ili kuchunguza na kutibiwa magonjwa

mbalimbali, ikiwa yatabainika kwa kuzingatia vilevile ushauri wa lishe n.k. Afua nyiningine zinazolenga kuokoa maisha ya watoto wachanga kama vile uanzishwaji wa vyumba maalum vyta matunzo na matibabu ya watoto wachanga, kwa maana ya *neonatal care units*, sambamba na upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, kwa ajili ya watoto wachanga ikiwemo watoto njiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tendega.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ninapozungumza watoto njiti nina maana wanazaliwa kabla ya miezi tisa haijatimia:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; dawa ya kusaldla mtoto ili aheme vizuri inayoitwa *surfactant* inauzwa shilingi laki sita kwa dozi moja na inategemea hali ya mtoto ambayo amezaliwanayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama una mtoto mmoja shilingi laki sita, kama umejifungua watoto wawili ni shilingi 1,200,000/=. Na watoto walio wengi wanatoka katika familia zenyet hali duni na kipato cha hali ya chini, kama wanashindwa tu kwenda nao kliniki itakuwa na hii shilingi laki sita. Je, sasa Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba, dawa hizi zinatolewa bure, ili kunusuru maisha ya watoto hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba, likizo ni siku 84 kwa mtoto mmoja na siku 100 kwa watoto mapacha, lakini hawa ni watoto njiti. Kama amejifungua kabla ya miezi tisa tusema miezi saba ina maana kuna miezi miwili ambayo iko kabla ya miezi ile tisa. Sasa je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba, wazazi wote wawili, baba na mama, wanapata likizo yenye malipo kwa miezi hiyo iliyopo kabla ili waweze kutunza hawa watoto njiti? Asante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Grace tendega kwa swali lake zuri. Na nianze kwa kutoa tafsiri ya mtoto njiti, watoto njiti wako katika makundi mawili; kuna wale ambao wamezaliwa kabla ya wiki 37 na kuna wale ambao wanazaliwa na uzito mdogo kuliko ule ambao tunatarajia, kwa maana ya kilo 2.5 kwa hiyo, wote hawa tunawaweka katika *group* hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, watoto ambao wanazaliwa njiti mara nyingi wanazaliwa na changamoto mbalimbali, hususan wale ambao wamezaliwa kabla ya umri wa wiki 37. Na moja ya changamoto ambayo wanayo ni matatizo ya kupumua, mapafu yanakuwa hayajakomaa na wanahitaji dawa ambayo ni *surfactant* kukomaza yale mapafu. Na nikiri kweli, gharama za *surfactant* ni kubwa na sisi kama Seriakali tumeliona hilo, tunajaribu kuliangalia utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba, tunatoa afua kwa akinamama ambao wamezaa watoto njiti. Hatutaweza kuitoa bure, lakini tutaweka utaratibu ambao unaweza ukapunguza gharama katika utaratibu ambao tunao sasa hivi wa kuagiza dawa moja kwa moja kutoka viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili linahusiana na kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa wazazi ambao wana watoto njiti:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, watoto njiti wanazaliwa wakiwa na changamoto nyingi pamoja na matatizo ya kupumua, wengine wanazaliwa na viungo bado havijakomaa, ikiwa ni pamoja na ubongo na wengine wanaweza wakapata matatizo mengine endapo hawatapata matunzo ya karibu. Lakini jiwhakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, sasa hivi kwa mujibu wa teknolojia watoto ambao wanazaliwa hata akiwa na wiki 22 kwa maana ya miezi mitano, wana uwezo mzuri sana wa kuweza kukua na kuishi vizuri. Na mtoto ambaye ameweza kuzaliwa na...

MWENYEKITI: Muda, muda.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalotaka kulisema kwa kifupi tu kwamba, Serikali inaweza ikaliangalia suala hili kwa maana ya kuwa, pale kama mtoto ana matatizo mzazi anaweza akawa anapewa ruhusa kwa mujibu wa kanuni na taratibu ambazo tunazo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khadija, Mheshimiwa Mboni na Mheshimiwa Senator Lubeleje.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa, *rate* ya mama wanaojifungua watoto njiti imekuwa ikiongezeka nchini. Serikali ina mipango gani ya ziada kuweza kuwasaidia wamama wajawazito kuepukana na tatizo hilo, lakini pia ni sababu gani zinazowasababisha wamama wajawazito kujifungua watoto njiti? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Jamani, huyu ni Daktari, sasa ataanza kutoa elimu hapa na muda wetu mnauona.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa sisi kama Serikali tunasisitiza sana, mama anapopata ujauzito kuhakikisha kwamba, anaenda kliniki na sisi katika kliniki tunaweza tukabaini visababishi ambavyo vinaweza vikasababisha mama kuzaa mtoto njiti na kuweza kuvitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kifupi tu visababishi ni vingi, moja ni uzito wa mama mwenywewe; ikiwa mama ana uzito mdogo au uzito mkubwa inaweza ikasababisha kuzaa mtoto njiti, maambukizi ambayo mama anaweza akayapata, matumizi ya vileo, *stress* ambazo anaweza akawanazo mama wakati wa ujauzito ni sehemu ya visababishi ambavyo vinaweza vikasabaisha mtoto kuzaliwa njiti.

MWENYEKITI: Asante. Mheshimiwa Mboni, jiandae Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kutokana na changamoto ya kuzaliwa kwa watoto njiti kuwa ni changamoto kubwa sana, hususan, katika maeneo ya vijijini. Na kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amezungumza kwa kutueleza baadhi ya sababu ambazo zinasababisha *miscarriage* au kuzaliwa kwa mtoto njiti ni dhahiri kwamba, zipo ambazo zinazuilika na ziko ambazo hazizuiliki.

MWENYEKITI: Swali, swali.

MHE. MBONI M. MHITA: Je, Serikali ina mpango gani madhubuti, hususan, maeneo ya vijijini, ili kuweza kutoa elimu ambayo itaweza kuwasaidia akinamama kuweza kuepuka kupata kuzaa watoto ambao ni njiti? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, elimu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, visababishi vingi na viashiria vya ujauzito ambavyo vinaweza vikaleta shida, mara nyingi tunavibaini pale akinamama wanapokwenda kliniki. Na ndio maana sisi kama Serikali, tunahimiza sana akinamama kwenda kliniki angalau mara nne katika kipindi chao cha ujauzito. Lakini vilevile unapokwenda kliniki wanaweza wakawapa elimu kuhusiana na visababishi mbalimbali ambavyo nimevitaja, ili waweze kuviepuka na kuweza kuzaa watoto ambao wamefika wiki 37.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Mwalongo, halafu Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, lengo la kujenga vituo vya afya na zahanati ni kupunguza vifo vya akinamama wajawazito pamoja na watoto, lakini kwa kuwa, tatizo la

upungufu wa madaktari ni kubwa sana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unasemaje kuhusu hilo, kuongeza madaktari katika vituo vya afya na hospitali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kwamba, tuna changamoto ya rasilimali watu, lakini Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba, tunakabiliana na changamoto hii. Na katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19 Serikali ililajiri watumishi wa afya takribani 11000 na tunaendelea sasa hivi mkakati tuliokuwanao ni kuziba mapengo ya hawa ambao wamestaafu, waliofariki na katika kipindi cha mpito. Lakini Serikali inaendelea kuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba, katika vibali vya ajira mpya na watumishi wa afya wanakuwemo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwalongo, jinandae Mheshimiwa Lyimo, jiandae Mheshimiwa Hawa.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Njombe, Kibena, ina kituo cha watoto njiti, lakini kituo kile kina mazingira duni sana na kinahudumia mkoa mzima. Na sasa hali ya hewa inakwenda kuwa ya baridi sana kuanzia mwezi wa tano. Je, Serikali iko tayari kutusaidia Wananchi wa Njombe kupata huduma haraka iwezekanavyo katika kituo cha watoto njiti cha Kibena Hospitali? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali na kupitia hospitali zetu za rufaa za mikoa kwa sasa, moja ya msisitizo mkubwa ambao tumeuweka ni pamoja na

kuboresha huduma za watoto wachanga, ikiwa ni pamoja na njiti. Sijajua, hususan, jambo gani ambalo analiongelea pale, lakini katika Mkoa huu wa Njombe sasa hivi tuko katika hatua za mwisho kujenga hospitali ya rufaa ya mkoa na lengo letu ni kwamba, baada ya hapo ile Hospitali ya Kibena tuirudishe katika ngazi ya halmashauri. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mikakati yetu ambayo tunayo kama Wizara ni kuhakikisha kwamba, huduma za watoto wachanga, ikiwa ni pamoja na njiti katika Mkoa wa Njombe itapewa kipaumbele.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hapa Tanzania takriban watoto 213000 njiti huzaliwa kila mwaka na kati ya hao zaidi ya 9000 huwa wanafariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa natambua kwamba, tarehe 17 Novemba, kila mwaka ni siku ya watoto njiti duniani. Nilitaka Waziri atuambie kwa hapa Tanzania wanaadhimishaje siku hiyo kwa sababu, nadhani hata Wabunge hatuna taarifa; mnaadhimishaje siku hiyo kuhakikisha kwamba, tatizo hili sasa linapungua na wananchi wanalelewa vizuri? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge Viti Maalum, kwa ufuatilaji mkubwa na kuwa mdau wa masuala haya. Niseme tu kwamba, siku hii ya tarehe 17 Novemba, ni fursa kwetu kama Wizara kutoa elimu kwa jamii kwa njia mbalimbali kuhakikisha kwamba, na mara nyengi tunakuwa na kauli mbiu mbalimbali kuhusiana na kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na suala hili, visababishi vyake ni nini, huduma zake ni zippi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi kama Serikali sasa hivi tunahimiza sana hili suala la *Kangaroo Motherhood*.

Kinamama kuwalea watoto wao njiti kwa kupitia kupeana joto la mwili kwa mwili, ili kuhakikisha kwamba, wale watoto ambao mara nyingi wanakuwa na matatizo ya mapafu na kutunza joto basi waweze kupata joto pasipokutumia *incubators*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa, Mheshimiwa Sokombi, Mheshimiwa Jaku.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali nyongeza...

MWENYEKITI: Kwa kifupi.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Kitete ina wodi ambayo inalea watoto njiti, lakini wodi hiyo ni finyu na vifaa viliivyoopo ni duni. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha wodi ile na vifaa kuongeza, ili kuweza kuendana na kasi iliyopo pale?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya awali moja ya mkakati ambao tunao Serikali baada ya kukabidhiwa hospitali za rufaa za mikoa tumejielekeza katika maeneo makubwa matano:

(i) Kuhakikisha tunaboresha huduma za dharura;

(ii) Huduma za upasauji; na

(iii) Masuala ya *theatre*, vilevile tunataka tuboreshe huduma za mama na mtoto ikiwa ni pamoja na huduma za *ICU* pamoja na *ICS* za watoto.

Kwa hiyo, tumeshafanya tathmini za kina hospitali zote, ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Kitete na tumeshaweka Mpango Kazi wa kuboresha huduma hiyo katika Hospitali ya Kitete.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sokombi; *Chief Whip* wape watu wako, Mheshimiwa Sokombi.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa majibu ya Waziri anasema kuna mkakati wa kuanzisha vyumba maalum vya matunzo ya watoto na matibabu, yaani *neonatal care units* kwa maana hiyo, hivi vyumba havipo. Anawaambiaje Watanzania kwa muda huu atawasaidia vipi akinamama wanaopata matatizo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri; hamasisheni akinamama waende kliniki mapema.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kwamba, huduma za *neonatal care* hazitolewi. Ni baadhi kwamba, kuna baadhi ya hospitali zina vyumba maalum vya *neonatal care units* na baadhi ya hospitali hazina, watoto wanawekwa katika wodi moja. Kwa hiyo, katika mkakati ambao tunao sasa hivi ni kuhakikisha kwamba, kila hospitali ya rufaa ya mkoa inakuwa na chumba mahususi kwa ajili ya kutoa huduma kwa watoto wachanga, lakini si kwamba, huduma hizi hazitolewi kwa sasa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jaku.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu swalii hili karibu kwa ufahasa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri alikiri kuwa dawa hizi ni ghali na zina ghamra kubwa na Serikali isiogope ghamra kwa wananchi wake, wananchi ndio Serikali na Serikali ndio Wananchi na Mheshimiwa Lyimo alizungumza karibu watoto 9000 wanakufa kwa mwaka. Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itajaribu kuiga lini *formularkwa* Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya utawala wa Dkt. Ali Mohamed Shein, kutoa dawa zote Unguja na Pemba bure? Na Serikali ya Jamhuri ya Muungano imeiga mambo mengi kutoka Zanzibar, dawa...

MWENYEKITI: Swali moja, swali moja tu Mheshimiwa Jaku.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Je, ni lini Serikali ya Jamhuri ya Muungano itafuata nyayo za Mheshimiwa Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kutoa dawa bure kutoa dawa bure kwa wananchi na sio kwa mdomo, dawa zipo Uguja na Pemba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi. Na Mheshimiwa Waziri hongera sana umejibu *professionally* kabisa. (*Makof!*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kwamba, Serikali itatoa dawa bure kwa Watanzania wote milioni 55 haitawezekana. Kwa hiyo, sasa hivi sisi kama Serikali kuleta nafuu kwa wananchi kuweza kumudu gharama za matibabu tunajielekeza katika mpango wa bima ya afya kwa wananchi wote, ili wananchi waweze kupata matibabu kwa gharama nafuu.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa muda wetu umekwisha; wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo Jukwaa la Spika; wageni sita wa Mheshimiwa Spika, kutoka Benki ya *NMB Dodoma* wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Albert Jonkergouw, karibu Dodoma. Ndugu Juma Kimori Mkoo wa Kitengo cha Ukaruzi wa Ndani, karibu. Ndugu Filbert Mponzi, Mkoo wa Biashara na Serikali na Wateja wakubwa. (*Makof!*)

Ndugu Nsolo Mlozi - Meneja wa Kanda ya Kati, Ndugu Vicky Bishubo - Mkoo wa Idara na Serikali na Ndugu Grace Matemu - Meneja wa Tawi, Bunge. (*Makof!*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 50... (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Asimame tena.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, mikopo haitoki sasa hivi.
(*Kicheko*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 50 wa Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo (*SUA*) wakiongozwa na Rais na wanachuo, Ndugu Siwale Alphonce. Karibuni. (*Makofi*)

Wageni 37 wa Mheshimiwa Angelina Mabula, Naibu Waziri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi, ambaao ni Wabunge Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Spika wa Bunge hilo Ndugu Alphonce Msami. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mariam Mzuzuri, ambaao ni viongozi waandamizi wa *African Relections Foundation* Ndugu Maryvonne Pool, Ndugu Mercy Sila na Ndugu Paul Siniga.

Wageni wanane wa Mheshimiwa Ali Salim Khamis ambaao ni familia ya rafiki zake kutoka Zanzibar na Dodoma wakiongozwa na Ndugu Ahmed Khalifan. (*Makofi*)

Wageni 38 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambaao ni Kwaya ya Kanisa la Makenodia wakiongozwa na Mchungaji Vincent Malenda. (*Makofi*)

Wageni 54 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaao ni Wanamaoni wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Emmanuel Shemdoe. (*Makofi*)

Wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ambaao ni wanachuo wa *UDOM* wanatoka Masasi wakiongozwa na Ndugu Simon Kaajile. Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Hassan Masala ambaye ni mpigakura wake kutoka Nachingwea, Mkoani Lindi Ndugu Mohamed Chiwaso. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Sonia Magogo, ambao ni jamaa zake kutoka Mkoani Dar es Salaam wakiongozwa na mjomba wake Ndugu Jackson Kamugisha. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Zacharia Isaay ambaye ni ndugu yake kutoka Karatu, Mkoani Arusha, Ndugu Kasmiri Thimote. (*Makofii*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Hawa Chakoma, ambao ni viongozi wa Chama na Serikali kutoka Kata ya Mangindu Mkoani Pwani, wakiongozwa na Diwani Kata ya Mangindu Mheshimiwa Issa Mkali. (*Makofii*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni jamaa zake kutoka Mbulu, Ndugu Paschal James na Ndugu Serafina James. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Yosepher Komba ambaye ni mwanachama wa CHADEMA kutoka Nkuhungu Mkoani Dodoma, Ndugu Dina Kizigha. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Ally Ungando ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimboni kwake Kibiti, Ndugu Anwar Ahmed. (*Makofii*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Msigwa

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7). Kwa mujibu wa Katiba yetu, nchi yetu ni *republic* na sio *monarchy* na tuna mihimili mitatu; *Executive, Judiciary* na *Parliament*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Bunge letu limekuwa na viongozi yaani Mheshimiwa Spika na Naibu

Spika. Kwa hivi karibuni Naibu Spika kama sehemu ya uongozi wa mhimili wa Bunge amekuwa akiambatana na *Executive* muda wote katika ziara za *Executive*, jambo analolifanya ni sawa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia angekuwa anakuja anakaa hapa *gallery* anaangalia shughuli za Bunge zinavyoendelea, anaacha shughuli za *Executive* au sawa na Makamu wa Rais angekuwa anaenda kwenye Kamati za Bunge kuangalia shughuli za *Executive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachopenda kujua, naomba mwongozo wako kwa sababu tuna mihimili mitatu na inajitegemea, inafanya kazi na hili Bunge mara nyingi tumekuwa tukiambiwa huko nje ni dhaifu, ni kwa nini Naibu Spika ambaye aliapa Kinondoni... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: ...muda mwingi anazunguka kwenye ziara za *Executive* akiacha shughuli za Bunge? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa kwanza hili jambo halijatokea leo mapema Bungeni. Pili, Naibu Spika ni mteule wa Rais. Nakujibu nikuelimishe tu, sina sababu ya kukujibu. Taarifa zake za kuwepo au kutokuwepo Bungeni anayezijua ni Spika ambaye ndio mhimili wa Bunge. Sio wewe wala sio mimi. Kwa vile ni mteule wa Rais, muda wowote anaweza kuwa *summoned* na mamlaka ya juu kwenda kufanya kazi kwa aliyemteua. (*Makofii*)

Vilevile, sisemi wewe, wala usini-quote kama nakwambia wewe. Kuna maradhi yanaitwa *posttraumatic stress disorder*, sisemi wewe unayo. (*Makofii/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo hapa ...

MWENYEKITI: Katibu.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: *CUF* mwongozo.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:
HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka
wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Elimu, Sayansi na
Teknolojia**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. Jiandae Dkt. Tiiseleka.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja liliyopo mezani kwetu hapo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka 15, nchi yetu imekuwa katika harakati kubwa ya kupanua upatikanaji wa elimu na juhudini kubwa zimefanywa ili elimu imfikie kila mtoto wa Tanzania. Napenda sana niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi na hasa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufulsi kwa kazi kubwa wanayofanya hasa kwa kukubali baada ya kupanua elimu hii, kuitoa bure. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Waziri wa Elimu aliwasilisha bajeti ya Wizara ya Elimu na kwa muda tulipo sasa katika kupanua elimu, bajeti ile imetitendea haki Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa hiyo, napenda sana niipongeze Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara kwa kazi nzuri ambayo inaonekana kufanywa. Kwa upande wetu kwa wakati huu kazi kubwa ni kuboresha elimu, kuishauri Serikali pale ambapo inaweza kufanya vizuri zaidi katika kutekeleza suala hili la kuboresha elimu hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kuboresha elimu, jambo la kwanza lazima uwe na walimu. Niendelee kusema kwamba tunaendelea kuiomba Serikali ihakikishe kwamba

inapeleka walimu wengi wa kutosha hasa katika shule za msingi. Wiki iliyopita, sisi katika Wilaya ya Mwanga tumepewa walimu wachache; tuliomba walimu 386, tumepewa walimu 30 hivi na tunategemea kupewa wengine mwezi wa Sita. Kwa hiyo, mwezi wa Sita utakapofika tungependa tuone *significant* kabisa walimu wa kutosha kabisa ili waweze kufundisha watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuhusiana na bajeti hii kwamba ili elimu ya Tanzania iboreke, ni muhimu Serikali ichukue hatua ya kuboresha Idara ya Ukaguzi. Wafanyakazi wa Idara ya Ukaguzi wengi wanaomba kuondoka kwa sababu mishahara, madaraja na marupurupu yao na nafasi ya kazi wanayokuwa nayo siyo nzuri kama wale ambao wanaofanya kwenye kufundisha na kusimamia elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo la kwanza ambalo napenda kupendeleza, Wizara iangalie Idara ya Ukaguzi wa Shule na imlinganishe Mkaguzi Mkuu wa Shule na Kamishna wa Elimu. Kule kwenye mikoa, Mkaguzi Mkuu wa Kanda awe sawa sawa na wale Manaibu *RAS* wa kule kwenye mikoa na wale wafanyakazi ambao wanafanya kwenye Idara hii waweze kupewa vyeo sawa sawa na Maofisa wa Elimu wanaoshiriki katika kuendesha elimu katika Wilaya zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ni muhimu sana idara hii ipatiwe vifaa; magari na vifaa vyta ukaguzi ili kuhakikisha kwamba wanaweza kuwafikia walimu na kwamba ripoti ya ukaguzi wa shule na ukaguzi wa kila mwalimu katika kufundisha unaongezea katika sifa za mwalimu kupandishwa madaraja na kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunapotaka kuboresha elimu ni muhimu sana tulenge tunafanya nini? Katika miaka ya kwanza miwili ya shulenii, ni vizuri sana tuache kuwafundisha kila kitu watoto wa Darasa la Kwanza na la Pili. Tulenge kuwafundisha vitu vitatu peke yake kwa miaka ile ya kwanza mitatu ya shule; Darasa la Awali, Darasa la

Kwanza na Darasa la Pili tuwafundishe zile K tatu; Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na namna ya kutumia namba katika maisha. Tuache kuwafundisha masomo yote, tuwafundishe hivyo vitu vitatu tu ili wakitoka hapo wamevishika na wanaweza kujifunza mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi hii ya elimu ya msingi na hata sekondari, ni muhimu sana tuboreshe hii mitaala na tutunge sasa vitabu ambavyo vina tija, vinaweza kuwafundisha watoto wetu wakajifunza, wakaelewa kinachofundishwa. Tusiongee juu ya joto la mwili wakati tunaongea juu ya homa, tuongee juu ya Malaria; tutibu Malaria tusitibu joto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, ni muhimu sana tutunge vitabu vizuri na katika kila somo kuwe na wataalam wallobobeza katika somo hilo ambaao wanatoka kwenye taasisi za nchini humu, taasisi za Serikali kama Vyuo Vikuu, taasisi zisizo za Serikali, Vyuo vya Ualimu na hata Shule zetu za Sekondari na Msingi. Tutoe wataalam wa masomo hayo ambaao wataandaa mitaala, vitabu vya kutumia na wale ambaao watafanya *review*, wataviangalia kama vinafikia *standard* inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika ngazi hiyo ni kwamba katika sekondari, shule zetu nydingi hazina maabara. Tumeacha kazi ya kutengeneza na kujenga maabara, tumewaachia wanavijiji. Wanavijiji hawajui sayansi na hawana uwezo wa kujenga maabara, lakini tumewaachia. Hii ni kwa sababu katika hatua ya upanuzi tulifika mahali hela zimetuishia, lakini kwa sasa hatuna sababu yoyote ya kuwaachia wanavijiji watujengee maabara ya sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapendekeza kabisa Wizara ya Elimu itenye fedha kwa makusudi kabisa, ijenge na kumalizia maabara zote ambazo zipo huko kwenye Shule zetu za Kata. Hili litatusaidia, tukisema tunataka kuongeza wanasyansi, tuanze kuwafundisha wanasyansi. Hivi sasa haiwezekani. Tunavyo vifaa vya maabara lakini

vimewekwa stoo na vikiwa stoo haviwezi kufundisha watoto. Kwa hiyo, ninashauri sana tujenge maabara na tufanye hili jambo liwe la makusudi kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, niliwahi kupendekeza hapa kwamba ni muhimu sana tuwapatie watoto wote mikopo ya kusomea katika Vyuo Vikuu. Katika hotuba ambayo imesomwa jana tumeletewa na Waziri, juhudhi kubwa sana imefanywa kutafuta fedha kwa ajili ya mikopo lakini mimi nadhani hakuna sababu yoyote...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Profesa. Mheshimiwa Dkt. Tisekwa halafu jiandae Mheshimiwa Mama Salma.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Niungane na Wabunge wote ambao wamewapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Naibu Katibu na Watendaji wote pamoja na Wakuu wote wa Taasisi wa Wizara hii kwa kweli kwa kazi nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu na usikivu wako. Kwa jinsi ninavyokufahamu, kwa kweli ukisikiliza hii taarifa imesheheni na umetumia ile *smart approach* kwamba unasema nitafanya nini kwa muda gani, kwa hiyo, ni rahisi hata kuwa *measurable* tutaweza kukuuliza mbona ulisema hiki kuliko zile tulizozoea kwamba tukipata fedha, tukifanya hivi ndipo tutafanya; lakini umeonyesha. Kwa mfano, kuanzia *page 134 – 213* imesheheni mambo gani yatafanyika. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mwakilishi wa Vyuo Vikuu nimekaa na Uongozi wa Serikali ya Wanafunzi pamoja na Viongozi wa *Academic Staff* takribani vyuo 10 hivi, wamenituma kwamba upeleke salamu kwa Mheshimiwa Rais wetu kwamba wana imani na Mheshimiwa Rais wetu pamoja na wasaidizi wake wote akiwemo Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu jinsi wanavyotekeleza mipango ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanasema wanapongeza sana, lakini vijana wa Vyuo Vikuu wanashukuru sana kwamba mikopo sasa hivi inapatikana kwa wakati pamoja na kwamba kuna changamoto za hapa na pale, lakini wana-*support* sana zoezi lile la vyeti feki. Wakifkiria jinsi wanavyo-*toil* halafu mwingine anapata cheti feki anapata kazi. Kwa hiyo, wanapongeza sana Mheshimiwa Rais kwa zoezi hili pamoja na elimu bure. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda nizungumze mambo machache kuhusu changamoto za wanafunzi. Zipo changamoto nyingi lakini kuna mambo ya msingi ambayo mwanafunzi akiyapata, akili yake itatulia na atasoma vizuri. Kuna suala la Bima ya Afya, mikopo na hosteli; na mambo mengine nitakuletea kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bima ya Afya bado ni tatizo. Wanafunzi wanaingia mwaka wa kwanza kwa mfano, toka wanavyoingia mwezi wa Kumi unakuta mwanafunzi hapati kabisa Bima ya Afya, sasa tatizo ni nini? Nakumbuka nilizungumza hili tatizo wakati nikiwa kwenye Kamati ya Huduma, bado tatizo linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ashughulikie kwa sababu vijana hawa wanahitaji kupata afya ili waweze kusoma. Pia wakati mwingine mwanafunzi anapata Bima ya Afya mwezi wa Tano, mwezi wa Saba ina-*expire*, wanaomba *expiring date* iendane na ile *date of issue*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo; mikopo inakwenda vizuri lakini bado kuna changamoto. Wamepongeza sana ule mtindo wa *fingerprints*, wanapenda utumike huo, lakini kuna wakati vijana wanasaini mkopo wanasema fedha zimekuja, lakini wanaweza wakaka zaidi ya hata ya mwezi fedha hizi hazijaja, kwa hiyo kuna shida. Hata hivyo, wameipongeza sana Bodi ya Mikopo Taifa kwa jinsi wanavyoshirikiana na wanafunzi hawa, tatizo bado liko kwenye kanda. Kwa hiyo kwenye kanda muweze kuelekeza nguvu waweze kuwasaidia hawa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *hostels* ni muhimu sana kwa vijana wetu. Wapo wanafunzi wanabakwa usiku, mfano hapa *Muslim University*, Mipango, wasichana wawili wamebakwa wakati wanatoka shule wanakwenda majumbani kwao, kwa hiyo *hostels* fedha zilizotolewa tunaomba zitolewe zote ili ziweze zikajenge kule Mzumbe, *SUA*, Dar es Salaam kama tunavyoona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa na maadili; wakati wa *orientation* nimwombe Mheshimiwa Waziri ajitahidi kwamba *orientation* vijana hawa wapewe namna ya maadili. Kwa mfano suala la rushwa ya ngono, suala hili mara nyingi wanaelekezwa Walimu wa kieme tu, lakini kwa jinsi nilivyokaa na wanafunzi na walimu hii ina-*apply* kotekote, wapo wanafunzi wa kike amba wanawa-seduce Walimu wa kieme na meseji nimeziona. Kwa hiyo tunaomba rushwa ya ngono, hasa kwa Wahadhiri vijana ndio wanatuhumiwa zaidi, lakini hawa *Seniors Professors* wako vizuri, vijana wanawapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *fieldwork*; kwa mfano upande wa *mining*, *petroleum* na gesi ni shida, vijana wanapelekwa kwenye vikampuni vidogovidogo. Sasa kama tunataka tutumie wataalam wazawa, inabidi yale makampuni makubwa yasaidie kuwapokea hawa vijana wetu kwenye suala la *field* kwa sababu *field* nayo ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitisha humu ndani asilimia 15 kwa ajili ya kulipa mkopo. Kwa kweli asilimia 15 hii bado ni kubwa, kama inawezekana waweze ku-review, kwa sababu huyu kijana anapoanza kazi, kwanza tayari anatoka kwenye familia ya kipato cha chini, halafu bado unambebesha tena asilimia kumi ya penati akichelewa kulipa; bado alipe asilimia 15, anatakiwa alipe asilimia 30 ya *tax*, sijui mambo ya bima na kadhalika, *please*, tunaomba waangalie, asilimia 15 ni kubwa sana. Mbona mikopo ya vijana kule halmashauri tumeondoa riba; kwa nini tusiondoe na huku kwa vijana wetu ili tuweze kuwasaidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wahadhiri, vyuo vikuu tunategemea sana Wahadhiri wetu wafanye kazi vizuri, lakini kuna hii, Mheshimiwa Waziri anajua, yeye ni profesa ametoka kule, suala la *harmonized scheme*. Kule mwanzoni watu walijirriwa wakiwa na *GPA* ya 3.5, wengine 3.8, baada ya *harmonized scheme* wanatakiwa wote kuwa na 3.8, sasa hii inaleta changamoto kwa ambao walijirriwa kwenye 3.5, ni vizuri wakaanza pale walipoanza hii sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna suala la stahiki za Walimu kama walivyoongea Wabunge wengine. Walimu wanadai *arrears zao*, wanadai *responsibility allowances, housing allowances, for so many years*; wanashubiri nini jamani? Hawa nao ni binadamu wana majukumu yao, lakini wasije wakashawishika sasa wakaanza *underground* migomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nikiangalia kwenye bajeti yetu hii *universities* maana yake kuwe na *research and development*; fedha hazipo. Serikali wanatoa kiasi kidogo, sasa hili Taifa tutaendeleaje? Kwa mfano, sasa hivi kuna uhaba wa ajira, Walimu ni wachache, hawaaajiri lakini bado *researches* zenye hata *promotion* haziji. Unajua hadhi ya chuo kikuu lazima watu wapande wafikie ngazi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi kuna hili suala la Walimu ambao ni *Senior Professors* kustaafu

kwenye *age* ya 65. Sasa wale wengine sasa hivi mnasema Maprofesa waliostaafu wasipewe hata mikataba labda kama chuo kiwagharamie. Vyuo hawana fedha za kutosha, lakini tukumbuke kwamba hawa Maprofesa ambao tunawaacha, nafikiri ni kwa Tanzania tu, wangefikiria, kama suala ni *gratuity* wangefanya kama India, India profesa anastaafu kwenye *age* ya 65 lakini wanalipwa mishahara *gratuity* haipo. Kwa nini wasikae chini waongee? Kwa sababu vyuo vyetu vitakosa *credibility*, hili wanalionia, tutakwenda kwenye bomu kama la sekondari; shule za Serikali hazi-*perform*, *private* zina-*perform*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali imetumia fedha nydingi kumuandaa Profesa, unajua kumwandaa profesa sio kazi ngumu, wanawaacha watachukuliwa huko na *private sector*, hata nchi za nje, baadaye tutakosa sifa tutaanza kuagiza ma-TX. Sasa kumlipa TX cha bure ni gharama, TX umsomeshee mtoto, umlipe kwa dola na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *please*, nimwombe Mheshimiwa Waziri hebu wakae walifikirie...

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Mama Salma Kikwete.

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Jiandae Mheshimiwa Kishimba.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla ya kuanza, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa hiki kibali cha kuweza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia na kutoa ushauri kwenye Wizara hii muhimu sana ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ndiyo mhimili wa Taifa letu

kwani elimu ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu la Tanzania. Sio Tanzania tu bali nchi yoyote duniani bila elimu hakuna kitu chochote ambacho kinaweza kikafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nitoe pongeze sana kwa Mheshimiwa Profesa Ndalichako kwa kazi nzuri, pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na viongozi wote katika Wizara hiyo kwa kazi kubwa na nzuri ambazo wanazifanya katika kusukuma gurudumu hili la elimu katika Nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya ya kuendeleza elimu na hasa ile elimu bure. Elimu bure kwa kweli tumeweza kuona matokeo yake na matokeo yake ni pamoja na kuongezeka wanafunzi wengi sana kwenye shule zetu za msingi, hii ni kwa sababu ya elimu bure ambayo inatolewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kila mwezi zaidi ya bilioni 23 na ushehe zinatolewa kwa ajili ya kuboresha hii elimu. Mheshimiwa Rais tunampongeza sana kwa kusimamia llani ya Chama chetu, Chama cha Mapinduzi, chama tawala kwa kazi kubwa anayoifanya. Endelea kufanya hivi Mheshimiwa Rais, sisi tuko nyuma yako kukuunga mkono kwa Tanzania inayowezekana, kwa Tanzania mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipotoa taarifa yako tumeona kuna dira, kuna dhima na kuna majukumu. Dira ya Wizara ni kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa pamoja na stadi, lakini sambamba na hilo kuna dhima; kuinua ubora wa elimu pamoja na mafunzo. Sambamba na hilo kuna majukumu; majukumu yapo jukumu la kwanza mpaka jukumu la 13, lakini la kwanza ni kutunga na kutekeleza sera, utafiti na huduma za maktaba na mambo mengine mbalimbali. Kwa kweli dira, dhima na majukumu

ya Wizara yanaendana hasa na uboreshaji wa elimu hii tunayoitaka na tunayoitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na kuwa na dira, dhima na majukumu, nataka niende kwenye eneo la Walimu wa Sayansi. Kupanga ni kuchagua, tunataka tuboreshe elimu, hatuwezi kuboresha elimu kama hatutakuwa na Walimu wa kutosha hasa Walimu wa Sayansi. Nini tunachotakiwa tufanye kwenye eneo hili; kila kitu ni maandalizi, tuliandaa llani ya Chama chetu cha Mapinduzi tukasema kwamba ifikapo mwaka 2015/2020 tunataka tununue ndege; tumenunua, tunataka tujenge reli ya kisasa; tumejenga, tunataka tuwe na vitu ambavyo vitaonekana kwa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini nimesema haya; kwenye hili maana yangu ni kwamba watoto wanaanza kwenye ngazi ya awali, shule za msingi, sekondari hatimaye wanakwenda kwenye elimu ya juu; naomba tuwaandae watoto hawa tangushule za msingi, tuwaangalie kwamba watoto hawa wanataka wawe akina nani. Hili jukumu ni letu sisi kama wazazi, vilevile ni jukumu la Walimu. Walimu tuna uwezo wa kuwajua watoto hawa wanawenza kuwa ama wanasayansi au wanabiashara na fani nyingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusipolianza hili mapema ni vigumu, hata tukianza kwenye *level* ya vyuo kama huku hatujawaandaa watoto hawa kuwa wanasayansi hatutaweza kupata Walimu waliokuwa bora wakawenza kuleta mabadiliko kwenye eneo la sayansi. Kwa hiyo, hili naomba lazima tuzingatie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapochagua wanafunzi tuweke malengo, malengo yetu ni nini; kuwapata Walimu wa sayansi. Basi tusichague tu ilimradi huyu anaweza kuwa Mwalimu, tuangalie sifa, tujipange, kama tunataka kuboresha tuangalie wa *Division I*, wa *Division II* basi hawa waende kwenye eneo la ualimu, sio wale ambao kwa kweli maksi zao haziridhishi ndiyo tunawachagua kwenda kufanya kazi ya

ualimu, hili halitakuwa na tija kwetu. Ni lazima tuwekeze kwenye hili, sisi kama Serikali tuna uwezo wa kusema hili tunataka hili hatulitaki, sisi ndio wenyewe maamuzi, tukiwashawishi watoto hawa wanaweza kufuata kile ambacho tunakitaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyoanda Mainjinia, tunavyoanda Madaktari, hali kadhalika tuwaandae watoto hawa kwenda kwenye fani hiyo ya ualimu. Kwa kufanya hivyo tutapata Walimu wa Sayansi mahirisana na hapo ndipo tutakapoweza kutafsiri dira, dhima na majukumu ya Wizara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka twende kwenye shule za ufundi; shule hizi ni muhimu sana kwa ustawi wa Taifa letu hasa ukizingatia kwamba tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda na tunaelekea kwenye uchumi wa kati ifikapo 2020. Hili ni muhimu kwa sababu kubwa moja; lazima tuwapate hapa mafundi wa katikati, wale mafundi mchundo, ili tuweze kuendana na hali ya sasa tuliyokuwa nayo. Kwa sababu shule zilikuwepo; kulikuwa na Tanga, Ifunda, *Mtwara Technical*, Dar es Salaam na zote zilikuwa zinafanya hizi kazi. Kitu kikubwa tu sasa hivi ni kufanya hayo maboresho na kurejesha hilo ili tuwe na mafundi hao wa katikati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka nizungumzie Bodi ya Mikopo; tunaishukuru Serikali kwa kuwashughulikia watoto yatima na wanaotoka katika mazingira magumu, watoto hawa wameweza kupata...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mama Salma kwa mchango mzuri.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, mengine nitayaandika. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jumanne Kishimba, ajiandae Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niungane na Wabunge wenzangu walioshangia kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Suala hili la elimu naona kama ni suala kubwa kuliko hata suala la Katiba. Ukiangalia juzi *TRA* walitangaza nafasi 70 za kazi, waliojitokeza ni wanafunzi 40,000. Suala hili ni suala ambalo Wizara ya Elimu ilitakiwa isikitike na iogope sana na vyuo vikuu vilitakiwa visikitike na vishangae sana. Wewe una watu 40,000 wakapata kazi watu 50, hawa wengine wanakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu yetu hii tulirithi kutoka kwa wakoloni, kwa Waingereza haina pingamizi, wakimaliza watu laki tisa wakastaafu, Uingereza kwa mfano, watakaomaliza shule au *university* watakuwa milioni moja. Kwa hiyo laki tisa watapata kazi, hawa laki moja Serikali inaweza kuwatunza na kuwahifadhi. Lakini kwetu sisi wanaomaliza shule wanaweza kuwa milioni moja wanaopata kazi ni 50,000 kwa hiyo tukiendelea na utaratibu huu nadhani tunatengeneza bomu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili naona kila mtu anaogopa kupasema lakini ukweli ni vizuri tukubaliane na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao wao ndio watunga sera za elimu, tukubali iundwe Kamati au Tume ambayo itachunguza suala zima la elimu kwa Tanzania. Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, amejaribu kuliongea hili suala mara mbili, mara tatu, lakini naona kama watu hawalichukulii kwa uzito. Watu 40,000 ukachukua 50,000 kama wangkuwa Uwanja wa Taifa wakasema hawatoki mule uwanjani utakuwa na kazi ngumu sana ya kuwatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri watunga sera watutengenezee Sera mpya ya Elimu ambayo itawafundisha watoto wetu kutoka shulenii, darasa la kwanza wafundishwe shughuli zao za nyumbani; iwe biashara, kilimo, ufugaji na asilimia 50 ya maksi wapate kutoka huku, asilimia 50 wapate za darasani. Itatusaidia wakati mtu anakuja kumaliza sekondari au *university* hata unapomwambia aende

akajitegemee kweli anayo sababu ya msingi na anafahamu atajitegemea nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kumwambia mtu aende akajitegemee, wewe umechukua pesa zake milioni 10 za *universitykampa unayosema* wewe ni *degree*, lakini kiukweli umempa karatasi. Umempa karatasi kwa sababu ni sawasawa na mtu amecheza *DEC*; hii *degree* hakuna mahali inapotambuliwa kokote, hata kama unaumwa huwezi kuiweka dhamana *pharmacy*, huwezi kuiweka dhamana benki. Sasa inawezekana kweli; mimi nimesomesha mtoto wangu, nimeuza mifugo yangu nimelipa milioni 10, wewe umenipa *degree* halafu wewe unaniacha mimi nikazunguke mtaani na ile *degree* na sidhani ukifika kwenye mji ulioathirika kama huo mimi mwenyewe ni muathirika wa *degree*, ninao watoto sita wana *degree*, kwa kweli inahuzunisha sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa bora watunga sera tukubaliane kwamba vyuo vikuu kabla havijatangaza nafasi za shule vikatafute ajira pia na vyenyewe, vieleze mishahara kwamba tumepata *NBC* shilingi laki nane mshahara, tumepata *NSSF* laki tano, sasa tunaanza kusajili lete milioni tano nitakupa *degree* kazi hii hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, linaweza kuwa suala la kuchekesha, lakini hali ni mbaya sana kule mtaani; watu wanazo *degree* kila kona. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini muda wa kusoma vilevile watunga sera wauangalie upya. Ni kweli nani alifanya *research* kwamba ubongo wa binadamu unahitaji kila mwaka darasa moja, kama yupo atuambie. Wakati huu nafasi za ajira hakuna, unachukuliwa mtoto wako miaka 17 unarudishiwa ana miaka 25, unaambiya katafuteni kazi ya kujitegemea, mnajitegemeaje? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watakubali watunga sera mwaka mmoja watu wasome madarasa matatu au manne ili watu wamalize shule mapema itatusaidia sana ili

mtu akimaliza shule arudi huku tuje tuendelee na maisha kijana akiwa bado mdogo. Leo wanakaa naye muda wote wanakuja kukurudishia wewe miaka 25, huwezi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye familia zilizoathirika kwenye suala hili la elimu ukasema elimu ni ufunguo wa maisha, watakwambia hapana, elimu ya leo ya Tanzania ni kifungo cha maisha. Maana yake ni gereza ngumu sana; umefungwa wewe, amefungwa mtoto, amefungwa mama na pesa zimekwendwa na umezeeka, wote mna vyeti viko ukutani na majoho ya siku ya *graduation*, cha kufanya hakuna, mnatazamana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia ya kubeza elimu lakini wakati huu uliopo ni lazima tufanye mabadiliko makubwa sana vinginevyo tunaziona nchi nyingi sana duniani sasa hivi zina matatizo makubwa kama haya. *South Africa* wanalo tatizo kwa sababu wote wamefuata elimu hii hii tu ya Mwingereza ambayo ni sukuma *document* basi, hakuna kitu kingine. Mwisho wa yote leo tuna shida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana sana, kwa kuwa suala hili linaonekana limemtesa kila mtu, Mheshimiwa Waziri akubali kuunda Tume kama Mheshimiwa Rais Mstaafu Benjamin Mkapa alivyosema ili ijaribu kuchukuwa maoni kuhusu suala hili. Tume hiyo ijumuushe na wananchi wa kawaida siyo lazima wawe wasomi tu wawepo na watu wengine maana sasa hivi waathirika ni wengi sana sana, kiasi ambacho hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda kijijini kwenye majimbo ukiwaliza wananchi ni mtoto yupi mwenye faida hapa kijijini. Kama siyo uongo wanakwambia mtoto ambaye hajasoma ndiye mwenye faida kijijini. Anafuata wa darasa la saba, wa *form four* halafu wa *degree*. Wanasema wenye *degree* wanasema ni kama viazi viliviyoshindwa kuiva. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema hivyo kwa sababu hawezu kulima au kufanya kazi yoyote, anasubiri ajira

na ajira hakuna. Kama zimetangazwa nafasi 50,000 walioomba ni 40,000 na hawa ndio wana *email* na *internet*, je, ambao hawana *email* na walioghairi ni wangapi. Je, watu hawa wa po wapi sasa hivi na wanafanya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu alifikirie sana suala hili. Najua watu wengi wanaogopa kulipasua. Nasikia Mheshimiwa Waziri anasema aboreshe elimu lakini unaboresha elimu ipi kama watu hawajapata kazi uliyozalisha? Bidhaa inaboreshwpa pale ambapo bidhaa uliyopeleka sokoni wateja wamesema tunataka bidhaa aina fulani, ukisema unataka kuboresha elimu unaboresha ipi kama watu walio bora... (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mapunda, Mheshimiwa Dkt. Sware na Mheshimiwa Zainab Bakar wajiandae, ninyi wawili ni dakika tano tano.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye Wizara hii. Wamekuwa wasikivu sana na tunaona kazi zinafanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachina wana msemo usemao, ‘ukitaka mafanikio ndani ya mwaka mmoja panda mahindi, ukitaka mafanikio baada ya miaka kumi mpaka ishirini panda miti, ukitaka mafanikio yatakayodumu kizazi na kizazi basi wekeza kwenye elimu’. Serikali ya Awamu ya Tano

imejitahidi sana kutengeneza miundombinu ya elimu kwa kuhakikisha kila mtu mwenye uwezo wa kwenda darasa la kwanza anakwenda na afike mpaka *form four* na kujitahidi kuweka maboma, madarasa na madawati ili wanafunzi waende shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miundombinu mizuri inayoendelea kuwekwa na Serikali tuna changamoto kubwa moja ambayo kama nchi lazima tuwe na tafakari. Changamoto ni ubora wa elimu ambayo tunaitoa nchini. Ukiangalia kwa umakini matatizo yote ambayo yapo kwenye sekta ya elimu yameshindwa kujibu swali tunatoa elimu kwa ajili ya nini? Baada ya kutoa elimu matokeo ya ile elimu nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwetu sisi mafanikio ya elimu tunayahesabu kwa viwango vya madarasa yaani tullkuwa na wanafunzi 2,000 wenyewe uwezo wa kwenda darasa la kwanza wote wakaenda darasa la kwanza, wote wakamaliza darasa la saba, wote wakaenda *form four*, wote wakaenda chuo kikuu ndiyo kipimo chetu cha elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa upande mmoja tunatatua tatizo moja tu *we call it delaying techniques* kumpa mtu matumaini kwamba kuna *promise land* inaweza ikaja huku mbele, kuna maana na asali iko huko mbele lakini *in reality* hicho kitu hakipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu wa elimu ulipaswa umuandae mwanafunzi katika *level* atakayoishia yoyote ile imwezeshe kuishi. Kama nguvu zake ni kuishia darasa saba akimaliza darasa la saba awe na uwezo wa kuishi. Kama ana nguvu za kufika *form four*, hawezikwenda *form five* na *form six*, elimu aliyoipata imsaidie akifikia pale aweze kuishi hali kadhalika mpaka *university*. That's why today unakuwa na *engineer* ambaye hawezihata kutengeneza barabara na unakuwa na daktari ambaye badala ya kupasua mguu anapasua kichwa. Hii ni tafsiri kwamba elimu yetu hajamtengeneza vizuri wanasema umepata elimu lakini haujaelimika, tunatengeneza watu wenyewe elimu lakini hawajaelimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri kuna mambo mawili lazima uyaangalie ndiyo yatakayotusaidia. Jambo la kwanza ni Sera yetu ya Elimu. Sera yetu ya Elimu ya mwaka 2014 ina changamoto mpaka leo haitekelezeki kwa sababu yawezekana stadi haijafanyika vizuri au tu kuna mtu anaamua ku-*roll a ball*, sisi kwenye mpira tunasema unaamua tu kukokota mpira uwende basi ukifika golini likiwa goli sawa mipira ukipaishwa sawa, tuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine mnaitengeneza wenyewe kwa nyaraka na miongozo mnayoitoa. Kwa mfano, Waraka Na.5 wa mwaka 2011 unasema mwanafunzi katika mwaka atahudhuria vipindi siku 194 lakini kama kutakuwa na mtoro hatafukuzwa shule mpaka asihudhurie siku 90 mfululizo, unatengeneza nini hapa? Huu Waraka unatengeneza mazingira ya mwanafunzi kuwa mtoro kwa sababu hatahudhuria darasani siku 30 atakuja siku mbili, hatahudhuria tena 30 atakuja siku tatu ili tu zile siku 90 mfululizo ambazo kwa mujibu wa Waraka mlioutoa ndiyo unazipa mamlaka shule na vyombo vyake kumfukuza huyu shule matokeo yake tunatengeneza wazembe ndani ya shule. Niiombe sana Wizara iangalie Waraka Na.5 wa mwaka 2011 ambao unasema mwanafunzi atafukuzwa shule tu endapo hatahudhuria vipindi mfululizo kwa siku 90, hii si sawa iangaliwe tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine, kipimo chetu cha ufaulu ili mtu atoke kidato cha pili kwenda kidato cha tatu anapaswa kuwa na D mbili au awe na A moja au na B moja au C moja. Taafsiri ya D mbili ya *form two* ni zero au 'F' ya *form four*. Maana yake *from day one* unaianaa zero na kuipalilia iende. Kwa nini mtu huyu kiwango chake cha kuvuka darasa kiwe D mbili ambacho tunajua ni kiwango cha chini kabisa cha kufaulu, tatarajie mbele aje afanye mambo mazuri, kitu hicho hakizekani na tukienda hivi tutatengeneza kizazi cha zero cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunaongelea sayansi na teknolojia (ICT). Mpaka leo ni ya ajabu nchi yetu

haina *combination* ya kidato cha nne yenye somo la *ICT*. University tuna *computer science*, kidato cha tano na sita hakuna *ICT*. Niombe Wizara, najua mmeshafanya kazi, mko katika hatua za mbali kwenye hili hakikisheni *ICT* iwe po kati ya *combination* za *form five* na *form six*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuna jambo ambalo sielewi Serikali mnalichukulaje kati ya uhusiano wa Serikali kwenye upande wa elimu na *private sector*. Kwa sasa inavyoonekana uhusiano wa Serikali na *private sector* kwenye elimu siyo kama hawa *equal partners* wanaotoa huduma katika jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia historia *private sector* imetusaidia sana kutoa elimu sehemu Serikali haikuweza kutoa kwa miaka mingi. Nitoe tu mfano, kwa Mkoa wa Lindi, Mtwara na Ruvuma mpaka mwaka 1997 kulikuwa hakuna hata *high school* moja, waliokuwa wanataka kusoma *high school* za Serikali ilikuwa lazima watoke nje ya mikoa hii niliyoitaja na ikitokea hakuna nafasi basi waende wakasome *private* kidato cha tano na sita kipindi kile zilikuwa shule tatu tu Mbeya ama akasome Irambo, Sangu na Meta, hawa watu wamesaidia sana *ku-cover gap* ambayo Serikali haikuweza kufanya katika kipindi kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unakuta kama kuna aina ya upendeleo kwenye kutoa adhabu kati ya shule za Serikali na shule za *private* endapo zitakuwa zimekosea. Mwaka jana kulikuwa na uvujaji wa mitihani wote tulizisikia shule za Serikali kule Chemba mlisikia na shule nyingine, zile shule za *private* zote zimefungiwa, zile shule za Serikali hazijafungiwa.

Mheshimiwa Mwyekiti, sasa watu wanaauliza, hivi kumbe ukiiba mtihani kwenye shule za Serikali adhabu yake ni ndogo tu mwalimu anaondoka, ukiiba mtihani kwenye shule ya *private* unafungiwa, matokeo yake *private* wataendelea kuwa makini (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako mzuri.
(Makofii)

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Sware dakika tano na Mheshimiwa Zainab Bakar dakika tano.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi ili name niweze kutoa mawazo yangu katika Wizara hii iliyo mbele yetu. Ni dhahiri kwamba uchumi wa nchi, maendeleo ya jamii na ya mtu mmoja mmoja kwa kiwango kikubwa hutegemea masuala ya elimu kwa upana wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hizi dakika chache nitagusia Sera yetu ya Elimu kwa ujumla na hali ya elimu katika vyuvo vyetu vya elimu ya juu pamoja na dhana nzima ya sayansi na teknolojia. Sera yetu jinsi ambavyo tunazidi kuirekebisha nafikiri illikuwa inakidhi wakati nchi yetu illikuwa inasimamia sera ya ujamaa na kujitegemea lakini kwa nyakati hizi sasa za soko huru na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, Tanzania Sera yetu ya Elimu na mitaala ya elimu yetu inawafanya vijana tunaowazalisha wanakuwa siyo *competitive* kwenye soko ndani ya nchi, *East Africa Community* na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa nini Sera yetu hii inatuweka katika dhama za zamani na siyo za kisasa. Mfano mdogo tu kwenye mitaala, mitaala yetu tunayoitunga ni mepesi na rahisi kufuatilia lakini *realistically* haituvushi pale tunapotaka kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano tu mzuri tuna somo la *Development Arts and Sports* kwa wanafunzi wa *grade one*. Hili ni somo la vitendo lakini unawafundisha watoto ukuti ukuti, *jumping rope theoretical* na unawapa mtihani tunataka kukidhi nini wakati hili ni somo la mchezo. Kwa hiyo, tuangalie tunataka ku-*achieve* nini kuanzia elimu ya msingi, sekondari mpaka vyuvo au *technical school*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la muda wa kuanza shule na usafiri kwa wanafunzi vijiji na mijini. Kwenye

bajeti ya mwaka 2017/2018 nilitoa *proposal* hebu tuangalie kwa upya muda watoto wanaotakiwa waanze shule hususani wa shule za msingi. Unapoanza safari yako yoyote saa kumi na moja au saa kumi na mbili alfajiri unakutana na wanafunzi vitoto vya miaka sita, saba wamelala saa ngapi, wanaamka saa ngapi, *efficient* inatoka wapi? Unaawaambia saa kumi na mbili na nusu wafike shule, saa moja masomo yanaanza na kadhalika, wanafunzi wa vijjini wanatembea kwa umbali mrefu saa ambazo si sawa na wanafunzi wa mijini usafiri nao ni wa shida na wanapata shida, kwa hiyo, *by the time* mtoto anafika shulenii amechoka *mentally* na *physically* hawezikupokea kile anachofundishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo kwa walimu wanaowafundisha hawa wanafunzi wanakuwa kwenye level za *stress*. Ndiyo maana unakuta adhabu zinazotolewa zinaweza zikawa za kupitiliza kwa sababu kwanza mwalimu huyu hana mshahara unaomkidhi, ana malimbikizo ya mishahara na marupurupu mbalimbali kitu ambacho hakimpi *motivation* vya kufundisha *plus* anavyoenda shule tayari ana *stress*. Kwa hiyo, *level* ya elimu haiwezi kupanda au kuwa *improved* kwa mazingira tunayoishi sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti suala lingine kwenye sera ambalo nataka liangaliwe ni mitihani ya kuhitimui *especially* ya darasa la saba. Wanafunzi hawa hatuwatendei haki kwa sababu ni siku moja ya kukutathimini wewe uende kutoka *level* moja kwenda nyngine. Nafikiri tuangalie jinsi ya kuwafanyia tathmini wanapotoka daraja moja kwenda lingine, wale ambao labda unasema hawakufaulu kwa sababu pia kuna malalamiko mengi ya kuvuja kwa mitihani na usahihishaji mbovu, kwa hiyo, unampa *one time chance* ambayo siyo *fair*. Basi yule ambaye hajafaulu apewe nafasi ya ku-reseat au *assessment* nyngine zitafutwe au hawa wanafunzi ambao kwa asilimia kubwa vijana, zaidi ya vijana milioni tano au sita tunawaacha hawaendi sekondari kwa sababu hakufauli hii elimu ya msingi tuwape *alternativelabda* za kwenda shule za *vocational training* au ku-reseat ile mitihani ya *primary* kama wana nia ya kwenda sekondari waweze kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala linguine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja tu.

MWENYEKITI: Haya, chukua dakika moja.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine adhabu kali zifuatiliwe upya kwa sababu zinaenda kinyume na haki binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nigusie suala la elimu ya juu na sayansi na teknolojia. Kama Wizara inavyosomeka ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia lakini hii sanyansi na teknolojia haiwi *reflected* hata kwenye bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) ilitengewa shilingi bilioni moja ikasomeka sifuri hawakupata chochote safari hii, nasoma hapa kwenye randama wametengewa shilingi bilioni 3.5 tena kwa fedha za nje...

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Zainab Bakar dakika tano.

MHE. ZAINAB M. BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunitunuku zawadi ya kusimama hapa. Pili, naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaelezea suala la bajeti kushuka. Bajeti ya Wizara ya Elimu imeshuka sana wakati tunaiangalia Wizara hii kama ni Wizara mama na dira

ya Wizara zote. Nasema hivyo kwa sababu Wizara hii ndiyo inayozalisha madaktari, mameje, wahandisi na viongozi leo tunaipunguzia bajeti. Mwaka jana tulitenga 1.4 mara hii tumeshuka mpaka 1.3. Hivi kweli tupo tayari kuisaidia Wizara hii ambayo ndiyo kioo cha nchi hii ama tunaibeza tu? Kwa sababu mfumo wowote mzuri ndiyo utatufanya tupate matokeo mazuri na wanafunzi na viongozi bora lakini tukiendelea hivi tutaendelea kuwatumbua viongozi kutokana na kwamba hatujaweka ufanisi mzuri katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna vitendea kazi kutokana bajeti yetu tumeiweka katika upungufu huu. Tutaendelea kukosa madawati, maabara na vyumba vyakusomea wanafunzi kutokana na kushuka kwa bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu ndiyo tegemeo la nchi hii lakini leo tunawazalilisha au wako chini kabisa. Tunashindwa kuwaongezea mishahara ambayo itawakidhi kwa mahitaji yao ya kila siku. Mwalimu huyo huyo asomeshe mtoto wake na anahitaji pesa za matumizi mengine mwisho wa siku anakuwa na msongo wa mawazo na ndiyo maana anafanya mambo mengine ambayo hayaeleweki. Kwa hivyo, tunakuomba Mheshimiwa Prof. Ndalichako uwaangalie kwa jicho la huruma walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na suala la uhamisho. Uhamisho wa ualimu imekuwa ni kilio. Tunawatenga walimu na wenza wao kwa kipindi cha muda mrefu, waonane likizo hadi likizo, hiyo siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu yupo Kigoma mwenza wake anafanya kazi Dar es Salam, hatuoni kwamba tunawazalilisha na kwamba Serikali au Wizara hii inavuruga ndoa za walimu wetu? Kwa nini tusiwape uhamisho wakawa karibu na wenza wao? Hivi ni Serikali ya Mapinduzi ndiyo mkakati wake kuona ndoa za watu zinavurugika? Nataka unipe majibu kuhusu uhamisho wa walimu ambao wenza wao wako mbali kama watapewa uhamisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuja kwenye suala la kubadilishwa kubadilishwa kwa mitaala hili limekuwa ni suala la kawaida na kwamba hakufanywi tafiti za kina na wala walimu hawashirikishwi katika masuala haya ya kubadilisha mitaala, jambo ambalo linapelekea wanafunzi wetu kufeli sana. Kwa mfano mzuri nikija kule kwetu Zanzibar sidhani kama walimu wa Zanzibar wana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ngombale, jiandae Mheshimiwa Chuachua.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na niweze kusema. Nianze na suala zima la Bodi ya Mikopo ya wanafunzi, kuna tatizo ambalo linatakiwa lifanyiwe kazi. Tunawakopesha wanafunzi kwa riba kubwa hali ya kwamba wanasomea elimu ambayo hawana uhakika wa kuja kupata ajira na kwa sababu hiyo, itawachukua miaka baada ya kuwa wamehitimu kuja kupata ajira, matokeo yake watakapokuwa wameanza kupata ajira ile riba inakuwa imeongezeka mara dufu kwa hiyo, wanaanza kazi hali ya kwamba wanamzigo mkubwa wa riba ya Bodi ya Mikopo.. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama Bodi ya Mikopo inakusidia, inakusudio la kufanya biashara kusudio la Bodi ya Mikopo siyo kufanya biashara, ni kutoa huduma. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri tutoe mikopo lakini tupunguze riba, riba ni kubwa sana kubwa mno na kwa sasa mnakata asilimia 15 ya mshahara kwa hiyo mtumishi anaanza kazi lakini kiasi kikubwa cha pesa tayari kinakwenda kwa Bodi ya Mikopo. Kwa hiyo, naomba hili lifanyiwe kazi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jingine nizungumzie suala zima la wastaaifu na stahiki zao. Tunawapandisha watumishi madaraja kwa maandishi tu na siyo vitendo, tunapandisha madaraja hakuna mabadiliko ya mishahara matokeo yake wanapokwenda kwenye kustaifu mafao yao

yanakuwa kiduchu. Ni miaka mingi sasa zoezi la upandishaji wa madaraja limekuwa lakubabaisha babaisha watumishi hawa wanaenda kustaafu kwa mafao kidogo kwa sababu wanapandishwa madaraja lakini bila utekelezaji na matokeo ya mafao yao yanakuwa madogo. Kwa hiyo, niombe Wizara ijitahidi kwamba watumishi na hasa wale wanaokaribia kustaafu wapandishwe madaraja ili basi mafao yao yaweze kuwa angalau manono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ni suala la elimu bure, hii elimu bure Serikali ijpambanue na iwe wazi elimu bure iwe ni kwa suala zima la ada tu, Serikali iwe wazi iwe wazi kwa wadau wa elimu kuchangia elimu na hasa wazazi tamko la elimu bure limeenda kuharibu uelewa na kiasi kwamba wazazi sasa na hasa wa vijiji huko wanaona kuchangia elimu siyo sawa sawa kwa sababu Sera ya Serikali ni elimu bure. Serikali sasa iwe wazi, iwe wazi kwamba suala la kuchangia elimu ni lazima isipokuwa Serikali yenyewe ubure huu unaozungumzia upo kwenye suala zima la ada tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine nizungumzie suala la elimu ya watu wazima, hasa suala zima la kisomo cha watu wazima. Wakati wa enzi za Baba wa Taifa suala hili liliisitizwa sana na Tanzania ikawa ni nchi inayopigwa mfano kwa kuwa imepiga hatua kwenye kuhakikisha kwamba watu wazima wanapata elimu hasa zile *skills* tatu za kuandika, kuhesabu na kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili jukumu liliipewa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima sasa hivi hii Taasisi inaonekana hili jukumu lake la msingi kana kwamba wameliacha na wamejikita zaidi kwenye hizi elimu rasmi. Katika maeneo yetu bado kuna watu wengi ambaao hawajui kusoma hawajui kuhesabu, hawajui kuandika. Na ukisoma kwenye ukurasa ule wa 38 wa Hotuba yako, unasema ndiyo kwanza mmeandaa mkakati wa kuona namna gani mnajikita katika hili eneo. Nasema mmechelewa mfanye haraka bado tuna watu wengi ambaao wanahilo tatizo, huo mkakati wenu uwe

wa haraka ili basi kuweza kunusuru watu wengi ambao wanamatatizo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo ningependa niliseme ni suala zima la elimu jumuifu *inclusive education*. Ukurasa wa 17 umeeleza kwamba Serikali ina mpango mkakati wa kuanzia mwaka 2018/2021 wa kuhakikisha ina mkakati wa hii *inclusive education* yaani elimu jumuishi lakini mpaka sasa hivi mko katika hatua ya uchapishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hili suala kama limechelewa sana na tunaposema *inclusive education* ni nini. Huu ni mpango ambao wanafunzi wa aina yote wale walio na ulemavu na wasio na ulemavu watafundishwa katika darasa moja. Kimsingi suala hili kama litafuatiliwa na kutekeleza litawasaidia sana na litawasaidia sana walemvu kwa sababu kwa kufanya hivyo walemvu wanaweza waka-coop na kujifunza kutoka kwa wenzao ambao wasio walemvu. Lakini kwa kufanya hivyo na wale ambao wasio na ulemavu watakuwa familia na wale wenye ulemavu. Huu ni mpango mzuri sana lakini mpaka sasa inaonekana limezungumziwa kwa miaka mingi lakini utekelezaji wake unachelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe na niishauri Wizara suala hili ni zuri na lifanyike kwa haraka lakini liendane sambamba pamoja na kutoa mafunzo kwa wale walimu ambao hawa-*skills* za kuwafundisha walemvu. Liendane sambamba na kutoa motisha kwa walimu ambao wataenda kuwafundisha watoto walemvu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini liendane sambamba na kuwa na idadi kubwa ya walimu katika darasa hilo, kwa sababu katika darasa ambalo linawatoto walemvu na wasiowalemvu, kuwa na mwalimu mmoja ni mtihani lazima kuwepo na mwalimu ambaye hana hiyo *skills* za kuwafundisha watoto walemvu na yule ambaye ni mwalimu wa elimu maalum. Suala hilo naomba Serikali ilifanye kwa haraka kwasababu kundi hili la watu wenye ulemavu linaendelea kutengwa na kunakuwa na *tendency* ya kuwa

na *over protection* lakini kunakuwa na *tendencyya isolation* kwa hiyo tukiwachanganya hawa itawasaidia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala zima la maslahi ya walimu. Walimu hawa wamekuwa wakifanya kazi kubwa kwa ari lakini bado Serikali haijaona namna gari inaweza kuwamotisha. Niombe Serikali itakapokuja basi itoe matumaini kwa walimu kwa kuongeza mishahara yao lakini itoe motisha kwa walimu kwa kuongeza madaraja yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la *teaching allowance*, *teaching allowance* Mheshimiwa Ndalichako wewe ni mwalimu kazi ya ualimu ni kazi nzito, walimu tulivushe hili kundi basi lazima tuone uwezekano wa kuwapa *teaching allowance* kitu hiki kitawasaidia sana na kilifanyika wakati wa mzee Mwinyi *teaching allowance* inawezekana katika kipindi hiki cha Mheshimiwa Dkt. Magufuli, na hilo mtaliweza kama mnaweza kufanya mambo makubwa makubwa na mazito mazito, fanyeni hili kwa walimu basi, fanyeni tuwarushie hiyo *teaching allowance*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la Sera ya Elimu. Wakati wa Baba wa Taifa, Sera yetu ya elimu ilikuwa *education for self-reliance* elimu inayotolewa basi imuandae mwanafunzi aweze kujitegemea lakini sasa sera yetu na muundo wetu wa elimu ni kama haueleweki, tunatoa elimu tuna watu wanahitimu lakini hawana uwezo wa kujitegemea sasa hivi tumekuwa na *fashion* ya kuwa na vyuo vingi vinavyotoa *degree* lakin baada ya kuwa tumekamilisha wanafunzi hawa wamepata *degree* hawawezi kujitegemea. Kwa hiyo, lazima tuje na mitaala ambayo itamuandaa mwanafunzi ili aweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Chuachua jiandae Mheshimiwa Muhamama, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Kamala.

MHE. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha kwamba Serikali anayoiongoza inatimiza na kutekeleza ahadi ambazo imeziweka kwa wananchi hususan kwenye sekta ya elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri, kumpongeza Naibu Waziri, pamoja na Makatibu wake, Manaibu Katibu Mkuu lakini kwa namna ya kipekee nimpongeze sana Dkt Pilap ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara hii. Kwa jumla watu hawa wanafanyakazi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Elimu kwenye upande wa kuimarisha miundombinu ya shule zetu naitambua, lakini natambua pia kazi hiyo wanashirikiana vizuri na TAMISEMI. Sikupata fursa kuchangia wakati wa TAMISEMI lakini lazima niseme hapa kwamba halmashauri ya mji wa Masasi ambayo ndio Jimbo langu, limepata fedha zaidi ya shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na shule za sekondari. Tunawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika fedha hizo tumepata pia bahati ya kupata fedha za kujenga shule mpya, shule ya msingi, shule ya kisasa kabisa yenye thamani ya zaidi ya milioni mia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara tena kwa kazi kubwa ya kuimarisha vyuo vyetu vya maendeleo kwa kweli vyuo vya maendeleo ya wananchi vilikuwa vimeachwa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo yoyote kiasi kwamba hata wale waliokuwa wanakwenda kusoma pale kwa kweli walikuwa hawapo katika wakati mzuri. Lakini

niseme tu kwamba vyuo hivi ni vyuo vya wananchi masikini wananchi wa kawaida kabisa ambao kimsingi wanavitegemea sana katika kujenga stadi zinazoweza kuwafanya waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Masasi, katika awamu ya pili kimetengewa fedha zaidi ya shilingi milioni mia tano katika kuimarisha miundombinu yake. Niipongeze sana Wizara kwa uamuzi huu wa kukiboresha chuo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niwaombe sasa Serikali waone namna wanavyokwenda kwenye *stage* nyingine ya kuimarisha sasa ujifunzaji wa vijana wetu katika vyuo hivi. Kuna tatizo kubwa sana la walimu katika vyuo hivi, lakini pia kuna tatizo kubwa sana la vifaa vya ufundi katika kujifunza vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo cha Wananchi Masasi, kinahitaji walimu 24 lakini kina walimu sita tu kina upungufu wa walimu 18. Nilikitembelea Chuo hiki nikakisaidie kompyuta chache lakini hazitoshi hawana vifaa vya kufundishia, hawana vifaa vya kufundishia aina mbalimbali za ufundi hata baadhi ya vifaa vinakuja vinakuwa ni mali tu ya waalimu na wanafunzi kwa kweli hawapati muda wa kushirikishwa kikamilifu katika kujifunza. Wizara ione namna ambavyo inaboresha vyuo hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo wazo tunavyo vyuo vya watu wenye ulemavu, watu wenye ulemavu watu wasioona tunavyo vyuo. Nchi hii ina sita sita tu vyuo hivi viko chini ya Wizara yenye dhamana inayoshughulikia walemvu. Lakini ninaushauri kwamba ni vema sasa Serikali ione kwasababu Wizara hii ndiyo yenye Sera ya Elimu na ndiyo yenye *methodology*, nashauri vyuo vyote vile sita ambavyo tunavyo ambavyo kwa kweli viro katika hali mbaya sana vichukuliwe na Wizara ya Elimu ili viweze kupata huduma inayostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vyuo hivi sita vilivyopo katika nchi hii chuo kimoja kipo katika Jimbo langu la Masasi, kinaitwa Chuo cha Wasioona cha Mwengemtapika, Chuo hiki sasa kimebaki majengo tu hali ni mbaya sana, naomba Waziri Serikali ione namna ambavyo Wizara ya Elimu inaweza kupewa dhamana ya kuviendesha na vyuo hivi navyo ili viweze kutoa mafunzo yanayostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kama alivyosema Mbunge aliyetangulia ni muhimu sasa hata katika vyuo hivi kufanya elimu jumuishi tufanye *inclusive education* tuungane wale wasioona na watu wenye maumbile mengine ya kawaida ili waweze kufanya kazi zao kwa vizuri zaidi, tuisiwaterenge na huko ndiko dunia inakoelekea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la elimu ya ufundi, Mheshimiwa Mbunge aliyeppita amezungumza kwamba mionganoni mwa mambo ambayo yanatusumbua sana ni kutoona kwamba kila *level* ya *education* lazima iwe *level of exit*. Lazima iwe *level* ambayo inaweza kumfanya ajitegemee, hili ni jambo la msingi sana kuliko mambo mengine yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ina mambo mengi, lakini mionganoni mwa mambo hayo ni kuwajenga vijana wetu kifikra na kuwajenga vijana wetu kiustadi ili waweze kujitegemea. Katika shule za msingi katika miaka ya 70 mpaka miaka ya 80 karibu na 90, ukisoma malengo ya shule ya kuhitimu shule ya msingi, ilikuwa ni kumuwezesha mtoto anayehitimu shule ya msingi na kushindwa kuendelea mbele aweze kufanya kazi za kujitegemea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la msingi sana kipindi kile tulikuwa tuna shule ambazo ni shule za msingi lakini ni shule za msingi zenye fani za ufundi, tulikuwa tuna shule za msingi zenye fani za kilimo. Ni lini tumefanya utafiti tukaona ni dhambi kuendelea na shule za msingi zenye mashamba? Ni lini tumefanya utafiti tukaona ni dhambi kuendelea na shule za msingi zenye karakana ya ufundi wa kawaida kama ufundi seremala, ili baadhi ya watoto watakaotoka pale

ambao wameshindwa kuendelea au hata kama waliweza kuendelea wanaendelea katika elimu ya sekondari huku wana *skills* wana-study zinazoweza kuwafanya waweze kujitegemea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ione namna ambavyo itarudisha elimu ya ufundi na kuimarisha vyuo vya ualimu ambayo vilikuwa ni vyuo vya ufundi kutoka katika elimu ya msingi mpaka katika elimu ya Chuo Kikuu. Wabunge wengine wamezungumza inawezaje unamfundisha mtu *Bachelor degree ya Education* ukitegemea aende kufundisha baadaye unataka ajitegemee wakati hakuna msingi wowote huku chini uliojengwa wa kumfanya aweze kujitegemea hapo baadaye ni muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya shule za *private* zipewe mwongozo wa kuwa shule za *private* za msingi ambazo zinatoa elimu ya ufundi, na elimu ya kilimo, lakini baadhi ya shule zetu za zamani ambazo zilikuwa zinatoa mafunzo ya ufundi ziendelee kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nieleze suala la elimu nje ya mfumo rasmi, tangu 2016 katika hotuba zote nilizochangia kwenye Wizara ya Elimu nimezungumza kuhusu *non formal education*, nashukuru leo Mheshimiwa Ngombale naye amezungumza. Nimekuwa nikisema kwamba Wizara ya Elimu siyo Wizara ya wale waliopo madarasani ni wizara ya watanzania wote. Wapo watanzania wengi sana ambao wanauhitaji wa elimu lakini hawajajengewa fursa za makusudi za kuipata elimu hiyo, wapo watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alitoa tamko la kwamba watoto ambao wanapata ujauzito hawataendelea kusoma katika mfumo rasmi, tamko lile lilikuwa linamaana sana lakini halikuwa linamaanisha kwamba watoto hawa hawawezi tena kupata fursa ya elimu. Fursa zipo lakini wizara ina mikakati gani kusaidia watu hawa? Wizara ina mikakati gani kuwasaidia watoto hawa wanaopata ujauzito nje ya mfumo rasmi waweze kusoma? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunafahamu kwamba tunawasajili watoto wa miaka sita, miaka saba kwenda shule za msingi tunajua watoto wangapi wa miaka minane na miaka tisa wapo huko mitaani na hawapati fursa ya kwenda katika mfumo rasmi wa elimu? Tunajua kwamba kiwango cha watu wasiojua kusoma na kuandika kinaongezeka kila siku? Serikali inakuja na mkakati gani? Tukipata majibu ya Waziri anayoweza kutuambia kuna *program* ya MEMKWA na nilikuwa ni mwezeshaji huko wakati wangu, tunaweza tukaambiwa kuna mukeji ...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante mengine andika mchango wako mzuri, Mheshimiwa Dkt. Kamala, jiandae Mhagama, jiandae Mheshimiwa Tauhida.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ninayo mambo machache ambayo ningependa kuchangia naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ningependa kulichangia, sote tunafahamu kwamba hivi sasa tunajenga Tanzania ya viwanda lakini ili tuweze kujenga Tanzania ya viwanda kada muhimu sana inayoweza kutusaidia kujenga Tanzania ya viwanda ni vyuo vya ufundi (*Technical Colleges*) hivi sasa tunazo *Technical Colleges* nadhani tatu, tuna Arusha *Technical College*, tuna kule Mbeya halifu tuna Dar Technical.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashauri Mheshimiwa Waziri, aje na mpango wa makusudi na wa dharura ili tuanzishe vyuo vyote kama hivyo kwa ajili ya Kanda ya Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi rafiki yangu hapa nyuma anasema Kanda ya Kati nilikuwa sijalipanga, naomba niongeze pia na Kanda ya Kati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Waziri tukifanya hivyo tutaweza kujenga Tanzania ya viwanda kwa spidi kubwa zaidi. Uwezekano wa kufanya hivyo upo, na uwezekano wa kupata fedha za kutekeleza jambo hilo upo na Waheshimiwa Wabunge tupo hapo tutakushauri zaidi hizo fedha utazipata namna gani. Jambo muhimu ni kuja na mpango na huo mpango upate baraka za Bunge zima na tutafanya hivyo, tutaweza kujenga Tanzania ya viwanda kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimeangalia bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kitu kimoja kilichokuja kwenye kichwa changu ni kwamba shule hizi za msingi na shule za sekondari ni shule ambazo zipo lakini hazina mwenyewe. Kwa sababu unakuta Wizara ya Elimu ndiyo inapanga sera na viwango na kila kitu, lakini inapokuja kwenye kugawa walimu, ukimwambia Mheshimiwa Waziri hapa, shule yangu fulani haina walimu, atakwambia hilo jambo linashughulikiwa na Wizara nyingine. Ukimwambia kuna tatizo la madarasa sehemu fulani, ataniambia jambo hilo linashughulikiwa na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nami naona hizi shule za msingi na sekondari zipo lakini hazina mwenyewe; na mwenyewe ni Wizara ya Elimu. Kwa hiyo, nashauri kwamba wakati umefika Serikali ifikirie kurejesha utaratibu wa zamani, mambo ya elimu yote yasimamiwe na Wizara ya Elimu ili ziwe na mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kuna shule moja inaitwa Shule ya Msingi Kajunguti, iko kilomita 10 kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Misenye. Shule hii ina walimu wawili tu, walimu wote wawili hawakai pale. Hii shule haina mwenyewe, maana wakati fulani ilitolewa na KKKT, lakini ukiwaliza KKKT shule hii mlitoaje? Mlitoa nyaraka zinazosema mmeitoa? Wanasema hawakutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni shule ambayo haina mwenyewe. Sasa nikagundua kwamba siyo hiyo tu, ni shule zote za Tanzania zipo, lakini hazina mwenyewe na mwenyewe ni wewe, ndiyo maana nashauri leo hii utaratibu

wa zamani urejeshwe ili kuweza kuweka sawa utaratibu wa elimu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo nimekuwa nikisikia muda mrefu kwamba Waheshimiwa hawa walimu wanaofundisha kwenye shule za msingi, siku moja nilikuta Afisa Elimu mmoja wa Wilaya, aliita Walimu wa Shule za Msingi ofisini kwake, akawa anawakemea, anawatukana kama watoto wadogo. Nikaangalia nikasema aah, huyu Afisa Elimu, hawa walimu nao si wamesoma kama yeye! Unakuta kwamba akishakuwa Afisa Elimu anaona walimu kama watoto wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nilipojaribu kufuatilia zaidi nikakuta na lenyewe halina mwenyewe, kwa sababu mwisho wa siku kumbe wanaosimamia maadili ni watu wengine. Sasa hizi ni vurugu. Ndijo maana nasema turejeshe ule utaratibu wa zamani na walimu tuwanyime kila kitu ambacho hatuwezi kuwapa, lakini tuwape heshima wanayostahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine niliseme, tuna uhaba wa walimu tunakubali, lakini uhaba huo wa walimu sawa, lakini wale wachache waliopo tuwagawe sawa. Haina sababu unasema kuna uhaba wa walimu lakini unakuta shule nyingi zina walimu 20, shule nyingie 10, shule nyingine ina wawili, shule nyingine ina mmoja tu, hii sio sawa sawa. Hao wachache waliopo tuwagawe sawa. Sasa hilo nitaliletea hoja maalum kuonyesha ni jinsi gani wale wachache waliopo tuwagawe sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mwisho ningependa kuisitiza, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyofanya kule Jimboni kwangu kwa kukarabati Chuo cha Maendeleo ya Wananchi. Natambua mwanzoni fedha hazikutumika vizuri, baadaye alikuwa mkali akaelekeza kwa karibu, akafuatilia, sasa naona kazi imefanyika vizuri. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunisaidia na chuo hicho sasa kimekarabatiwa vizuri na mambo yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nirudie kusisitiza, turejee kwenye utaratibu wetu wa zamani wa kusimamia elimu. Tukiendelea kama tunavyoendelea sasa, hizi shule zote, sekondari na kila kitu zitakuwepo lakini zitakuwa hazina mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri, utakuta sehemu kubwa amejikita zaidi kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo vikubwa vikubwa lakini kitu ambacho ni cha msingi kabisa walimu, wanafunzi unatakiwa uwaandae tokea kule chini waliko. Sasa Mheshimiwa Waziri anasubiri waje mpaka huku juu, anawapokea kwenye vyuo vikuu na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna haja ya kulitafakari hili jambo na kuja na mpango mbadala wa kurejea kwenye utaratibu wetu wa zamani. Bila kufanya hivyo, tutaendelea kuwa tunafikiri tunaendelea mbele lakini kumbe tuko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Mhagama halafu Mheshimiwa Tauhida na Mheshimiwa Mbatia wajiandae.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kuwashuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Madaba kwa kuitikia wito wa Mheshimiwa Rais wa Hapa Kazi Tu kwa vitendo. Wameshiriki kikamilifu katika ujenzi wa miundombinu ya elimu yakiwemo madarasa, mabweni na mabwalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee niwapongeze wananchi wa vijiji vya Wino, Lilondo na Maweso ambao katika umoja wao wamechangia zaidi shilingi milioni 104 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba makazi yao yanapata

maji lakini shule zote za sekondari na za msingi wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti niwapongeze wazazi wa shule zote za msingi za Madaba. Kwa namna ya pekee, wazazi wa Shule ya Msingi Njegea, Igawisenga, Turiani, Kifaguro, Mahahanje, Likalangilo na shule nyingine ambazo katika umoja wao katika kila mwaka wanachangishana zaidi ya shillingi milioni 10 kwa ajili ya kupata walimu wa ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali na kwa namna ya pekee Wizara hii ya Elimu na TAMISEMI ambao wameunga mkono jitihada za wananchi wa Madaba kwa kuhakikisha kwamba ile miundombinu ambayo wazazi wameendela kuijenga, Serikali inalkamisha. Tumepata fedha nyingi kwa ajili kukamilisha, lakini kutokana wingi wa mahitaji yetu, bado hizo fedha hizo hazitoshii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sikupata nafasi kuchangia kwenye Wizara ya TAMISEMI, nitumie nafasi hii hii pia kuiomba Wizara ya TAMISEMI watuongee bajeti na kuhakikisha kwamba madarasa, mabweni na mabwalo ya shule zetu za msingi na sekondari yanakamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya hizo shukrani kwa wananchi wa Madaba na kwa Wizara, nitumie nafasi hii kutoa wito kwa Wanamadaba kuhakikisha kwamba tunaendelea kuunganisha nguvu zetu kwa pamoja kwa sababu tuna jukumu la pamoja kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata elimu bora na wanapata katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoe ushauri kwa Serikali. Tunayo changamoto kubwa sana ya walimu katika shule zetu. Hili siyo kwa Shule za Madaba pekee, ni shule za sekondari karibu taifa zima. Tatizo hili la walimu pengine tunaweza tukalichukua kama dogo, lakini madhara yake yanaonekana dhahiri katika maeneo tunayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna vijana waliohitimu kidato cha nne katika shule zetu mbalimbali. Kijana huyu tangu anaanza *Form One* mpaka anamaliza kidato cha nne, kwa sababu ya kukosa Walimu darasani, wametumia madarasa yetu kama vijiwe vyta kujadili masuala ya siasa na kujadili Serikali katika mambo wasiyotaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa wanapotoka mashulenii wanahamishia mijadala kwenye vijiwe na kwenye mitaa yetu. Kwa kadri tunavyoendelea, Taifa hili sasa linalekeea kupata wanung'unikaji na siyo watenda kazi katika Taifa hili. Jambo hili leo tunaweza kulichukulia mzaha mzaha, lakini kwa kadri siku zinavyokwenda, tunazalisha vijana wa kijiweni ambaa hawana ajenda nyingine zaidi ya kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imeelezwa kuhusu sera yetu ya elimu. Nimeona Wizara imeweka mkakati wa *ku-review* hii sera sayansi, teknologia na ubunifu. Hili lisichukue muda. Mwaka 2018 tumeona huo mchakato ukiangalia kwenye hii taarifa ya Wizara ambayo ni nzuri sana, lakini unaona katika ukurasa wa tisa wanassema Wizara imeanda Rasimu ya Mapitio ya Sera ya Sayansi Teknologia na Ubunifu. Mwaka umeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa bajeti Wizara inaendelea na mchakato na inasema itakamilisha Mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknologia ya Mwaka 1996 ili kuwa na Sera ya Sayansi Teknologia na Ubunifu inayoendana na mahitaji ya sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa miaka miwili inakatika; hili haliakisi kabisa kasi ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Naiomba Wizara Watanzania wanatambua umuhimu na wanaona jithada zinazofanyika na hawana tatizo, lakini tuongeze *speed* ya kufanya kazi. Tufanye *review* ya hii sera kwa wakati ili Watanzania waliopo mashulenii, waliopo kwenye vyuo vyetu za ufundi waweze kunufaika na hii sera. Tutaisubiri hadi lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini sera hii inayoenda kufanyiwa *reviewitizingatia* ukweli kwamba kila Halmashauri ya Wilaya tunahitaji kuwa na Vyuo vya Ufundu na siyo kimoja. Kwa sababu watoto wanaohitim ukidato cha nne ni wengi, wanaopata fursa ya kujiendeleza sekondari kwa maana ya kidato cha tano na cha sita na wanaokwenda Vyuo Vikuu ni wachache. Hawa wanaobaki tunawaachia ujuzi gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hatutaki *ku-capture*? Kwa nini hatuataki ku-*tap* hii rasilimali muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu? Namna nzuri ya kutumia hii rasilimali watu ambayo ina ari ya kazi ni kuiongezea ujuzi kuititia vyuo vyetu vya elimu. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri tuwajengee uwezo vijana wetu wawe na uwezo wa kiufundi na kiujasiliamali ili tuondoe tabia yao ya kulalamika, tuwajenge uwezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, walimu wetu katika maeneo mbalimbali wana hali ngumu sana. Wengi hawajapandishwa madaraja kwa muda mrefu. Kwa hili sisi Wabunge tumetekeleza wajibu wetu wa kuja mpaka kwenye Wizara zinazohusika kuyaeleza, lakini hayafanyiwi kazi. Wengine madaraja yamekwama kwa miaka minne, mitano; wengine posho zao za miaka mingi tunakwenda kujenga Taifa la walimu wanaolalamika ambao watawaza wanafunzi na vijana wanaolalamika na mwisho tutapata Taifa la walalamikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tauhida halafu Mheshimiwa Mbatia.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa

wanazozifanya. Tunawapongeza, jitihada zinaonekana wanafanya kazi vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na kikosi chake chote anachofanya kazi tunawapongeza; na kama Watanzania hatuna la kuwaambia zaidi ya kuwaambia waendelee kufanya kazi. Sisi tunasimama, ni wajibu wetu kuangalia maeneo gani tunaweza kuboresha ili tujenge Tanzania kwa nia moja na kwa nia ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametumia muda wake vizuri na muda mwingu kuboresha elimu ya juu na ameitendea haki. Michango ya Waheshimiwa Wabunge itaendelea kuboresha katika malengo yake na misimamo yake ya kutaka Tanzania iwe na elimu bora na yenye malengo na yenye ufanisi. Ndiyo maana halisi ya michango inayotoka ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri achukue fursa kwa muda uliobaki. Tukiwa kama Wabunge wenzake tuungane kwa pamoja tuboreshe elimu ya msingi. Muda uliokuwepo kwa sasa, autumie kuboresha elimu ya msingi. Ametumia muda ipasavyo kuboresha elimu ya juu, sasa tunataka kuboresha elimu ya msingi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa wakati huu, kati ya vitu ambayo vinapaswa kuboreshwa katika elimu ya msingi ni pamoja na kupeleka walimu wa kutosha ndani ya shule. Katika elimu ya msingi tunahitaji walimu wa kutosha. Mheshimiwa Waziri aweke mikakati, ashirikiane na Mawaziri wenzake kuona wanashusha walimu ili wave kuwapatia elimu ya msingi ya kutosha wanafunzi wa shule za msingi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri kwa masikitiko kabisa, nilikuta shule moja, nakumbuka Liwale; nimebahatika kutembea Liwale kijiji kwa kijiji, nilikuta shule ina Mwalimu Mkuu na Mwalimu mmoja, lakini kuna watoto

vijana wa *form four* na *form six*, wakaamua kujitolea kuwasomesha wanafunzi wa *kijiji* kwao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna watu wanaamua kujitolea ndani ya *vijiji* vyao, maeneo wanayotoka, kufanya kazi kwa uzalendo, kwa nini tusiwape kipaumbele na fursa ya ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi *kijana* anakaa Kigoma unamshawishi kukumwondoa Kigoma kumpeleka Liwale, mazingira anayokumbana nayo huwa magumu. Ndiyo maana kelele kubwa za Wabunge kutokuwepo walimu wa shule kusomesha, hususan kwenye elimu ya msingi. Walimu wanakimbia kwa sababu ya mazingira wanayokumbana nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimchukua anayetoka *kijiji* kile kile, hata suala la *kukaa* na makaazi kwake inakuwa rahisi. Kama hakukumbana na familia yake akaishi, basi atakuwa ana mategemeo ya pale anapoishi. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwenye suala la walimu aweke mkakati na mkakati wake kwa uwe kipindi hiki cha Bunge tulichokuwanacho, mwaka mmoja na nusu ili tuweze kumalizia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa ikiwa ni mara ya pili niklongelea suala la Wizara ya Elimu. Kati ya kero kubwa ambayo naona inaitendea dhambi nafsi yangu, kuwepo shule na *bar* ikawepo karibu. Nimeshaizungumza Bungeni, kwangu kimekuwa kilio kikubwa. Haiwezekani tuwe na shule na Bar iko pemberni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kama Watanzania tunategemea nini? Shule na Bar ipo pemberni; tuna mikakati gani kwa wanafunzi wetu? Tena unakuta ni shule za watoto wa *primary*, tunategemea nini Mheshimiwa Waziri? Hili niliilomba niliwahi kulizunguza. Hili halihitaji bajeti. Linahitaji tamko. Lazima tujue. Haiwezekani ijengewe na *Bar* hapo hapo. Tunawafundisha nini watoto wetu? Leo mtoto akitaka kununua soda, anakwenda *Bar*, akitaka maji anakwenda *Bar*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichonifanya nisimame kuongea, watoto wanafanya mitihani ya darasa la saba wote wanachungulia nje muziki unapigwa usiku. Hatuwatendei haki Watanzania. Ninalizungumza mara ya pili nikiwa Bungeni. Mheshimiwa Waziri toa tamko, wenye *Bar* waondoke kwenye shule, tunataka tuwatengeneze mikakati wananchi wa Tanzania na wananchi wa Tanzania. Anayejenga *Bar* kama mwenda wazimu tunamwambia aondoe *Barkatika* shule, hatutaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine niliokuwa nalo, natamani sana kuona tunaambukiza uzalendo wananchi wa Tanzania, tuanze kuwawekea uzalendo kwenye utoto wao. Yaani tukimplekea mtoto wa shule wa *primary* kumpeleea uzalendo tunatakuwa na nchi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalendo uanze kusomeshwa chini. Mtoto wa darasa la kwanza na la pili ukimwambia itifaki ya Tanzania hajui. Tumpe itifaki ya Tanzania kupita wimbo. Waliotunga nyimbo za nyingi za Tanzania na nyimbo nyingine wapo, kwa nini tuisiwatumie? Mtoto tangu yupo chini, mdogo, afundishwe uzalendo wa nchi yake. Haya tunayopiga kelele humu ndani yataondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yawe ni historia ya kuiwekeea mkakati, Kama somo la historia, basi liwekewe makakati wa kuanzia chini kuja juu, liwe na uzalendo ndani yake. Haya tunayopiga nayo kelele yote yataondoka. Hivi kama mtoto wa Kitanzania, tumemjengea msingi wa uzalendo wa historia yake ya Tanzania katika somo la historia ipasavyo, unavyodhani tutapata shida na ma-engeenerwa nchi hii? Unavyodhani, tutapata shida na Madaktari wa nchi hii? Wote watawajibika katika misingi ya uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalendo ni kila kitu. Kati ya mambo mengi tunayoyafanya, tunasahau kuwapa uzalendo. Tumwangalie Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, moja ya kitu kinachomsumbuu ni uzalendo, nafsi yake imejawa na uzalendo. Uzalendo ndiyo uliokufanya

kufanya mambo mazuri na yenyе tija. Tuambukize uzalendo kutoka chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutoe mifano ya dini zetu zote mbili ambazo ni kuu; dini ya Kikristo na Kiislamu, inampandikiza mtoto imani akiwa mdogo. Leo mtoto wa Kiislamu anapelekwa Chuoni toka mtoto. Dini ya Kikristo wana *Sunday School*, watoto wadogo wanafundishwa dini. Nini maana yake? Maana yake ni kuweka misingi ya dini akiwa mtoto. Tuweke misingi ya uzalendo kwa watoto wetu wakiwa wako chini. Hatuwezi kuweka uzalendo wakiwa juu, hawatakuwa wazalendo hata siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya, lakini pia aliangalie suala la riba ya mikopo kwa wanafunzi. Atumie mama fursa yake, natamani nimhamasishe kama mama, lakini kuna watu watanipa mwongozo. Kama mama atumie fursa yake, ahurumie Taifa hili, ashikane na Kiongozi wetu na Rais wetu tufanye kazi ambayo ye ye anataka tuifanye. Mambo madogo tu tukiyarekebisha elimu yetu itakaa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Mbatia, jiandae Mheshimiwa Bobali.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii ya Elimu. Sekta ya Elimu kwa sababu zilizo nje ya uwezo wetu, Kitifa inatakiwa kuwa na mifumo mitatu, yaani *formal, non-formal and informal education*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera zetu za elimu, zinadhishirisha hilo kwani watoto wetu huondolewa mikononi mwa wazazi yaani hasa mama zao na kupelekwa shulenii chini ya walezi wengine yaani walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu ndiyo walezi wa Taifa, hoja kwa kielelezo humu ndani Bungeni hata Serikalini zaidi ya theluthi moja ni Walimu, nitatoa mfano, Serikalini na humu Bungeni, Mwalimu John Joseph Pombe Magufuli, Mama Janet Magufuli, Mwalimu Jenista Mhagama, Mwalimu Kilagi, Mwalimu Kabudi, Mwalimu Mwakyembe, Mwalimu Joyce Ndalichako, Mwalimu Susan Lyimo, Mwalimu Salma Kikwete, Mwalimu Profesa Mbarawa, Mwalimu Philipo Mpango, Mwalimu Grace Tendega, Mwalimu Shamsi Vuai Nahodha. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Mwalimu Haonga.

MHE. JAMES F. MBATIA: Ndiyo na Mwalimu Haonga. Nikitaja kwa uchache, hapa ni Mwalimu, Mwalimu, Mwalimu. Nenda kwa Makatibu Wakuu, Katibu Mkuu Akwilapo Mwalimu, dada yangu Semakafu Mwalimu, wote ni Walimu, Walimu. Mama aliye na mtoto mchanga asipopata mahitaji msingi hawesi kumnyonyesha ipasavyo mwanaye, rai yangu, tumuenzi Baba wa Taifa hili, kwa kuwapatia Walimu wetu upendeleo wa makusudi katika mishahara yao na stahiki zao. Msemo wa hakuna mwingine kama mama, kwa heshima tuseme Tanzania hakuna mwingine kama Mwalimu, kwani sisi sote humu ndani ni zao la Walimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu, Mwalimu John Joseph Pombe Magufuli, rai yangu kwake, awe mstari wa mbele kesho Mei Mosi, awe wa kwanza kuongeza mishahara ya Walimu na stahili zao kwa upendeleo wa makusudi, kwa kuwa Walimu ndiyo sekta kuu ya uzalishaji katika Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulinde uhuru na heshima ya Taifa letu, yaani Tanzania kwa kuwapatia walezi wetu, Walimu mishahara na stahiki zao zenye kukuza na kuhifadhi utu wao ili waweze kuwa na furaha ya ndani, wawe na uwezo na utu na rai ya kufundisha. Tutoke kule kwenye asilimia 60 ya Walimu sasa hivi ambao hawataki kufundisha warudi kwenye ari yao, warudi kwenye taaluma yao waweze kufundisha na kulilea Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na hilo kwa sababu naiangalia elimu ya Tanzania kwa miaka 25 ijayo, miaka 30 ijayo. Ukioma hotuba ya Kambi ya Upinzani, nimeisoma yote kwa makini ifikapo mwaka 2036 tutakuwa na Watanzania zaidi ya milioni 90. Mwaka 2045 tutakuwa na Watanzania zaidi ya milioni 120, je *critical mass* ya Watanzania, *critical thinkers* ya Watanzania watakuwa kwenye hali gani kama hatuondoi itikadi zetu, hatuondoi tofauti zetu tukajikita kwenye kuiangalia Tanzania miaka 30, miaka 50 ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bora, sawa na shirikishi kwa wote, mfumo wetu rasmi wa elimu wa sasa, kwa mfano Sera ya Elimu ya mwaka 2014 elimu msingi, ukiangalia na mitaala yake. Mitaala ya darasa la saba tayari imeshafundishwa darasa la nne, la tano na la sita. Ukiangalia Sheria ya Elimu ya mwaka 1978, kwa nini hatukubali kuwa na mfumo ambao ni shirikishi, ni sawa, na ni elekezi kwa wote, badala ya kila Waziri anayekuja anakuja na mfumo wake na matamko yake ambayo tunaharibu elimu ya Taifa la Tanzania, lazima tuiangalie Tanzania kwa miaka zaidi ya 50 ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kwenda Finland, Finland, kwa nini hata mwaka jana, wameweza kuwa ni watu wa kwanza duniani kwa watu wao kuwa na raha? Waliandaa mifumo yao ya elimu yenye kujenga utu wa binadamu kwa zaidi miaka 40 iliyopita. Wakasema Taifa letu, tunataka liwe na uelewa wa namna gani, Taifa letu watu wake wajitambue namna gani, Taifa letu tushirikishane namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana hapa tunazungumzia *formal education*, lakini *non formal and informal education* tunaiweka kwenye hali ya namna gani. Uandaaji wa sera hizi, Daktari ndiyo ukienda hospitalini anakwambia wewe umeugua kitu gani na unatakiwa utibewe namna gani? Leo hii, ukija kwenye Sera zetu za Elimu mitaala yetu inatengenezwa na watu wengine, ambao sio wale walezi, Walimu ambao wangekuwa ni shirikishi wa kutosha kwa sababu wanajua athari za watoto. Ukija hata kwenye

lishe yetu, siku 1,000 za kwanza, yaani miaka miwili na miezi tisa, watoto wetu wanapokosa lishe ya kuweza kujenga vizuri uwezo wao, kwa mfano jana niliona mtu mmoja, mvua imenesha, lakini kwa sababu yeye ameshazoea kwamba lazima kila siku aamke na amwagilie bustani, mvua huku inanyesha na huku anamwagilia bustani. Unakutatayari ana udumavu wa akili kwa sababu alikuwa amezoea tu na unajua kwamba ni mtu mwenye akili nzuri tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *so we must think big, and think global* namna gani tunawaacha, tunawakuza watoto wetu, namna gani tunawapa Walimu wetu ambao ndiyo walezi wakuu wa Taifa letu, waweze kuliangalia Taifa, waweze kuwa na utulivu, waweze kulea watoto wetu. Kwa sababu kama mama wewe, unamtoa mtoto wako unamkabidhi Mwalimu, ni kwamba umemwamini zaidi huyu Mwalimu kuliko hata wewe mzazi, kuliko hata mfanyakazi wa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako alikuwa Taasisi ya Elimu, alikuwa Baraza la Mitahani, ametoka huko amepewa dhamana hiyo, anaacha *legacy* ya namna gani kwa Taifa la Tanzania kwamba umeanzisha mfumo huu, tunaiona Tanzania ya miaka 50, tunaiona Tanzania ya miaka 30 yenye uelewa wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Naibu Waziri, Mheshimiwa Ole chonde chonde, tuache tofauti zote, tuwe na utulivu wa ndani, tukubali bila shaka, ukitaka kuliangamiza Taifa lolote lile anza kuua mifumo yake ya elimu inayolinda utu wa binadamu. Sasa hapa kila siku tunapiga kelele, hili, limetokea hivi, hili limetokea, tunakuwa *negative, negative, let us think positive, think globally, think big and tui* Tanzania ya miaka 50 ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitabu, leo hii Taasisi ya Elimu, inachofanya na vitabu, kwa mfano tangu mwaka 2014 vitabu vyatara la sita, vitabu vyatara la saba, viko, havionekani, viko wapi? Tunasema vinaandalishi,

vinaandaliwa, niombe chonde chonde wawachukue akina Mzee Walter Bugoya, tuachane na tofauti zetu. Tuseme yaliyopita, yamepita sindwele tugange yajayo, wawachukue akina Mzee Mtire Elibariki, wanavyo vitabu vingi tu. Wazungumze nao, wawe na *partnership*, washirikiane nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule binafsi naupongeze Mkoa wa Kilimanjaro, ambao unaongoza na nimekuja kufanya utafiti kwa nini unaongoza?. Utaona shule nyingi ni za binafsi ndizo zinazoongoza, sasa Serikali badala ya kupambana na hizi shule binafsi ionekane ni washindani, wawe na ubia nao wawe ni washirika wenzao, hata kuwapatia ruzuku kwa sababu wanaelimisha Taifa kwa niaba ya Watanzania wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo niombe Walimu tulioko humu ndani, na asilimia 35 ya shule za Sekondari za Mkoa wa Kilimanjaro ni Shule binafsi na niwapongeze sana na Shule za Walimu wa Vunjo. Nikiangalia Ikama ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi tunazungumzia Walimu, Ikama ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, shule za Sekondari za Serikali zina upungufu wa Walimu 685. Shule za Msingi zina upungufu wa Walimu 376, sasa licha ya kazi kubwa wanayofanya Walimu hawa na wa Vunjo kule Halmashauri ya Moshi na sehemu nyingine Tanzania nzima, ni namna gani tunawapa uwezo, shule unakuta ina Walimu wawili au watatu, sio Wabunge tuje hapa tuongee basi tumeondoka. Wakati wa kuitisha bajeti, Wabunge tuoneshe nafasi yetu kwa mujibu wa Katiba tuiambie Serikali hapana, ukiwekeza kwenye akili ya mwanadamu ndiyo miundombinu mikubwa yenye rasilimali kuu, kuliko rasilimali nyingine yoyote ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuipe Wizara hii bajeti ya kutosha, tufikiri vizuri, tuisimamie Serikali, la sivyo, watoto wetu miaka 20 ijayo, miaka 30 ijayo watakuja kuona kizazi hiki ni kizazi cha ajabu kweli, kwa mfano Joseph Roman Selasini hapa, Mbunge wa Rombo, baba yake alikuwa ni Mwalimu na aliwanasihi vizuri familia yao na unaweza kuona wamefika wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baba yangu alikuwa Mwalimu na unaweza kuona nimekuwa ni zao la namna gani, sasa hebu jamani tuache tofauti zetu, tulikumbuke Taifa letu, tumuenzi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wote humu ndani tukisema Tanzania, tunasema hakuna mwingine kama Mwalimu, tukisema Tanzania tunarudia hakuna mwingine kama Mwalimu, tukisema Tanzania tunasema hakuna mwingine kama Mwalimu. Tukisema mlezi wa Taifa la Tanzania, tunasema ni Mwalimu, mlezi wa Taifa la Tanzania tunasema ni Mwalimu, mlezi wa Taifa la Tanzania, tunasema ni Mwalimu. Sekta inayozalisha kuliko zote ni Wizara ya Elimu, sekta inayozalisha kulko zote ni Wizara ya Elimu tuache tofauti nyininge zote tukubali sote kwa pamoja, Taifa hili ni letu sote tulinyonyeshe Taifa hili, tumnyonyeshe mama Tanzania kwa kuipa upendo Sekta ya Elimu, ili Sekta ya Elimu iweze kuwa na utulivu wa ndani, iweze kuwa na furaha, inyonyeshe watoto wa Tanzania ili Mwalimu wetu aweze kuwa nambari moja katika Taifa la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nina tangazo kidogo, Mheshimiwa Anna Lupembe Mwenyekiti wa Ibada *Chapel* ya Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo muhudhurie kwenye *Chapel* ya Bunge ya Msekwa, Jumanne tarehe 30 kwenye Ibada saa saba, Waheshimiwa Wote mnakaribishwa.

Mheshimiwa Bobali, halafu Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze na hoja ya matokeo ya kidato cha nne na darasa la saba na namna yanavyo-reflect uhalisia. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi, matokeo ya kidato cha nne, ya mwaka 2017 nitaitaja Mikoa nane ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga ilishika nafasi ya 24, Ruvuma ilishika nafasi ya 25, Mjini Magharibi nafasi ya 26, Lindi nafasi ya 27, Kusini Pemba nafasi ya 28, Kaskazini Pemba

nafasi ya 29, Kusini Unguja nafasi ya 30, Kaskazini Unguja nafasi ya 31. 2018 Tanga 24, Mtwara 25, Mjini Magharibi 26, Lindi 27, Kusini Pemba 28, Kaskazini Pemba 29, Kusini Unguja 30 na Kaskazini Unguja 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amejifunza nini kwenye matokeo haya? Mikoa ni ile ile na kwa bahati mbaya mikoa yenye iko kwenye Ukanda mmoja, Ukanda wa Pwani. Tunapozungumzia *inclusive education* lazima iambatane na *inclusive performance* ambayo itakuja kuleta *inclusive development*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ukanda mmoja, watu wanafanya vizuri ukanda mwingine watu hawafanyi vizuri, tunakwenda kutengeneza matabaka katika Taifa letu. Mheshimiwa Waziri wa Elimu lazima aipitie Sera ya Elimu, lazima matokeo haya yamfundishe jambo, kwa nini Lindi kila siku wanakuwa wa mwisho? Kwa nini Kusini Unguja kila siku wanakuwa wa mwisho? Kwa nini Tanga kila siku na mikoa yenye iko kwenye Ukanda wa Pwani? Mimi siamini kama watu wanaokaa Ukanda wa Pwani, hawana akili, siamini kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko vigezo vingi vya kupima kwamba uelewa wao ni mkubwa na *performance* zao katika maeneo mengine ni mzuri. Hawa watoto wa pwani sio kwamba hawapendi elimu, kuna watu wanakuja na majibu mepesi kabisa, watu wa pwani hawapendi elimu, hawapendi kusoma, sio kweli. Wanasona, ukiwapeleka madrasa mtoto amesoma juzuuth thelathini, amehifadhi, anaweza akasoma *Quran* vizuri, kwa nini ashindwe kusoma kitu alichofundishwa kwa Kiswahili? Yaani mtu anaweza kutafsiri Kiarabu alichofundishwa, lakini eti kujibu methali ya haba na haba, hujaza kibaba, anafeli? Kuna namna lazima tutafakari na tuijulize, tusiwe na majibu mepesi, jambo hili ni kubwa kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo llingine amezungumza Mheshimiwa Mbatia, inawezekana Kilimanjaro wanaonekana nafasi ya kwanza kwa sababu ya

idadi ya shule za *private*, nadhani kama Serikali inataka wajitathimini waone *performance* ya shule za Serikali, watoe matokeo ya shule za Serikali peke yake kwanza, halafu wawe na matokeo ya shule za *Private*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lindi mathalani, Lindi shule za *private* hazifiki hata sita, ina maana hii *competition* inayokwenda, inakwenda Canossa na shule zingine zinakwenda kupambanishwa na shule hizi za kayumba zilizopo Lindi. Hakuna shule za *private* Lindi, sidhani kama Kaskazini Pemba au Kusini Pemba kuna shule za *private*. Kwa hiyo mtai-/label hii mikoa kama ni mikoa ya mwisho kila siku, kumbe hawapambani shule za Serikali na shule za Serikali, wanapambana shule za Serikali na shule za *private*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hoja *very sensitive*, Mheshimiwa Waziri ajaribu kuiangalia, lazima tuwe na *inclusive education* ili tuweze kuja kuwa na *inclusive development*, vinginevyo tutatengeneza matabaka ambayo wakati mwingine yanaweza kuja kuleta matatizo, haiwezekani kila siku Mikoa ya Pemba ndiyo ya mwisho. Bahati mbaya sana, panapotokea matokea ya kuwa wa mwisho, wanaoathirika ni Maafisa Elimu wa Mikoa, utasikia kila siku, Afisa Elimu wa Mkoa Lindi kabadilishwa, Afisa Elimu wa Mkoa sijui Mtwara kabadilishwa, Afisa Elimu Mkoa wa Tanga anabadilishwa na sio kubadilishwa, wakati mwingine kwenye mikutano hii ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, na wakati mwingine wanadhalilishwa pia. Sasa inawezekana unamlamu huyu, kumbe ye ye shule zake ni sa Serikali tupu. Anapambanishwa na maeneo ambako kuna shule nyingi za *private*. Hili ni jambo, ni jambo ambalo linahitaji tafakuri ya kina, na lazima waliangalie kwa umakini mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni juu ya hadhi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere; hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitembelea katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, nami ni mhitimu wa kile chuo na Mheshimiwa Waziri niliona aliambatana naye na Mheshimiwa Waziri Mkuu akatoa maagizo kwamba kile chuo kipandishwe hadhi ya kuwa Chuo Kikuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki moja baadaye ndani ya Bunge hili hili, mimi nikauliza swalilile lile, likajibiwana Mheshimiwa Naibu Waziri, akasema kwa sasa Serikali haina mpango wa kikipandisha hadhi Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, *ni-contrary* na kile alichokieleza Mheshimiwa Waziri Mkuu pale chuoni siku ile walipokwenda, sasa wanafanyaje kazi Mawaziri? Huku Mheshimiwa Waziri Mkuu anaagiza, kuwe na Chuo Kikuu kipandishwe hadhi, huku majibu ya Serikali ndani ya Bunge kwamba kwa wakati huu hakuna, lakini Mheshimiwa Waziri, hoja yangu ni nini? Hoja yangu kwanza ni kuthamini mchango wa Muasisi wa Taifa hili juu ya Sekta ya Elimu, kwanza hiki Chuo ndiyo chuo cha kwanza kabisa cha wazalendo kujengwa na wazalendo katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wenzetu kwenye Mataifa ya wenzetu, Baba zao wa Mataifa yao, wale Waasisi wa Mataifa wote, wamepewa majina ya Vyuo Vikuu. Ukienda Kenya leo, unakuta Kenyatta *University*, ukienda *South Africa* kuna Nelson Mandela *University*, ukienda Ghana unakuta Kwame Nkrumah *University*, kwa nini Tanzania hakuna Mwalimu Nyerere *University*, kuna shida gani, kwani kuna ukakasi gani? Elimu inayotolewa ni ile ile, kuna ukakasi gani wa kikipandisha hadhi Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kuwa *University*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nimeona katika ukurasa wa 184 mwaka huu wanaenda kutoa na Shahada za Uzamili, sasa kama wamefikia mpaka hatua ya kutoa Shahada za Uzamili? Kwa nini wanapata ukakasi wa kikipandisha hadhi chuo hiki kuwa Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu nasema, juu ya shule ya Sekondari ya Mchinga na Mheshimiwa Maftaha alitoa ushahidi hapa, shule ina vigezo, ina madarasa mengi, ina Walimu wengi, Walimu karibu asilimia 95 ni *graduates*, kuna shida gani kuipandisha hadhi ya kuwa *high school*? Jimbo la Mchinga hakuna shule ya *high school* hata moja, shule zote za sekondari zinazalisha watu wanaokwenda *high school*

wanakwenda nje ya maeneo yale na wakati mwingine wengine wanaachwa wanakosa nafasi kwa sababu ya uhaba wa shule za *A-level*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliangalie sana, mwaka huu tumeanza mchakato wa kujenga mabweni na nina hakika mpaka mwakani tutamaliza, wananchi wamehamasika sana, hebu waiweke kwenye mpango shule hii kuifanya ni mionganii mwa shule za *high school* itatusaidia sana kuondoa gharama za vijana wanaokwenda maeneo ya mbali kwenda kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mnafiki kama sitasema kuhusu Walimu, mimi mwenyewe nimefundisha miaka mingi najua maisha ya Walimu bado yana changamoto, mishaharara wanayopata ni midogo, lakini pia suala la upandishaji wa daraja. Walimu wamekaa wanatega masikio kusikia kesho Mheshimiwa Rais atasema nini, lakini kama hakuna itaenda vilevile, itapita bila bila tu kama hakuna chochote, wana-*demoralize* watu na matokeo yake *performance* inakuwa ndogo kwa sababu Walimu wana matatizo mengi kabisa, wengi tulikuwa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo, jiandae Mheshimiwa Marwa Ryoba na Mheshimiwa Maria Kangoye.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Leo nitachangia kwa masikitiko makubwa sana hasa nikikumbuka kwamba mwaka jana wakati kama huu nilikuwa na Naibu wangu Mheshimiwa Mwalimu Bilago, lakini leo hatunaye, kwa hiyo napenda tu niseme kwamba nina masikitiko makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kunukuu Mwanasayansi maarufu wa Kijerumani Bwana Albert Eisten, ambaye alisema:

"Dunia itaharibiwa sio na watenda mabaya bali kwa ukimya wa watu wema wakati maovu yanatendeka." (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ina wasomi wengi kuliko Wizara zote Tanzania. Kwenye Kamati yetu ambayo mimi ni mjambe imejaa Maprofesa ambao ndiyo ambao wanakaa kimya wakati wanaona mfumo wetu wa elimu unaharibika. Vilevile Maprofesa hao wanaongozwa na Profesa Ndalichako ambaye naamini ni msomi mzuri lakini hatuoni mfumo wa elimu ukibadilika. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni kama kiwanda, hauwezi ukapeleka muwa kiwandani ukatoka muwa lazima utoke sukari. Leo hii wanafunzi wanaanza *nursery* mpaka anamaliza darasa la saba hajui kusoma wala kuandika, amepoteza miaka yote saba. Ndiyo sababu naunga mkono alichokisema mzee Kishimba pale kwamba sasa hivi elimu badala ya kuwa ufunguo wa maisha umekuwa kifungo cha maisha. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunapoongelea elimu lazima tuongelee ubora wa elimu. Leo ambapo Sera ya Elimu ya mwaka 1995 ambayo ndiyo inatuongoza inatoa mitaala na vitabu tumeipigia kelele kwamba imepitwa na wakati lakini imekuja Sera ya mwaka 2014 ambayo hata miaka minne (4) haijaisha tayari inaanza kufanyiwa maboresho. Waziri anatumbia kwamba inafanyiwa maboresho kwa sababu haikupita kwa wadau, haiingii kichwani kwa sababu gani haikupitishwa kwa wadau?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunatumia sheria ya mwaka 1978 ambayo ilitumika kwenye Sera ya mwaka 1995 na inaendelea kutumika kwenye Sera ya 2014. Mimi binafsi najua kwamba huwezi kuwa na sheria bila kuwa na sera na kwa maana hiyo sera inapotengenezwa ndiyo unakuja kutengeneza sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya mwaka 2014 imesema bayana kwamba watoto watasoma mpaka darasa

la sita halafu baada ya hapo wote wataenda sekondari, ndiyo tunaita elimu msingi lakini leo hawaitekelezi. Waziri ukimuuliza atakwambia kwa sababu sheria hajabadi *lilika then* tunauliza *which come first* sheria au *policy?* Kwa hiyo, wakubali kwamba walizembea na hayo mabilioni ya pesa yaliyotumika kutengeneza hiyo Sera ya 2014 watuambie kodi za wananchi kwa nini zinatumika bila wao kuwa na mkakati maalum wa kuhakikisha wanapotengeneza sera wanaenda kwanza kuijaribisha halafu baadaye ndiyo inakuwa sera kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia suala la ubora wa elimu, baada ya hiyo Sera sasa kuwa na matatizo, wamekuwa na miongozo na mambo mengi sana. Kwa mfano, ukisikiliza Waraka Na. 5 na wakati huo nadhani Kamishna wa Elimu alikuwa Profesa, nimesahau jina lake alikuwa Profesa Balalusesa. Unaposema mwanafunzi hawezi kufukuzwa shule mpaka amekuwa mtoro kwa siku 90 mfululizo siku za *week days*, hii ina maana miezi minne kamili kwa sababu kama ni mwezi mmoja una siku 22 za kwenda shule *times 4* yaani miezi minne huyu mtoto akienda kwa mfano siku ya 86 bado hafukuzwi. Halafu Waraka huu uwe *applicable* pia kwenye shule za *private*, haiwezekani. Hakuna mwalimu mwenye shule yake ya *private* atakayeruhusu upuuzi wa namna hii. Haya mambo ndiyo sababu tunasema Tanzania mimi huwa sielewi tunaelekea wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wanasema kwamba mwanafunzi hawezi kufukuzwa mwaka anaofanya mtihani wa kumaliza shule. Ina maana kama uko darasa la saba, *form four*, *form six* huwezi kufukuzwa. Sasa na hii imepelekea kuporomoka kwa maadili kwa sababu mwanafunzi wa *form four* au *form six* akijua anafanya mitihani anaweza hata akaamua kumpiga mwalimu kwa sababu anajua hatafukuzwa mpaka Mahakama ithibitishe, hiyo Mahakama inathibitisha saa ngapi. Kwa hiyo, kuna mambo ambayo tunadhani hayajakaa sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo nije sasa kwenye matatizo makubwa ya walimu. Hapa nina barua ya

mmoja wa walimu hajapandishwa daraja toka mwaka 2003 amekuja kupandishwa juzi yaani mwezi huu wa nne ndiyo amekuja kulipwa mshahara wa kwanza kwa kupandishwa cheo toka 2003 anapokea Sh.140,000 mpaka juzi amekuja kupokea shilingi milioni moja sijui na laki ngapi, barua ziko hapa na ameendika *several times*. Sasa wako walimu wa namna hii wangapi? Kwa hiyo, nitampa Waziri husika atuambie ni kwa sababu gani wanawadhalilisha walimu kiasi hiki. Walimu ndiyo kila kitu kwa hiyo niombe sana Serikali iache kuwadhalilisha walimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala zima la Bodi ya Mikopo ya Juu. Tumelizungumza jana kwenye hotuba na hata Kamati, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inapata fedha nyingi sana *which is very good* lakini fedha hizi takribani zaidi ya asilimia 52 kwa mwaka huu zinaenda kwenye Bodi ya Mikopo, ile miradi halisi ya maendeleo kuanzia shule za msingi mpaka elimu ya juu, ndiyo sababu unaona majengo mengi ya vyuo vya elimu ya juu pamoja na vyuo vya ualimu haitekelezwi kwa sababu fedha zinaenda kwenye Bodi ya Mikopo. Kwa hiyo, ni ombi langu kwamba *vote* ya Bodi ya Mikopo iwe peke yake ili irahishe kwanza ufuatiliaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala haiingii akilini kwa sababu gani Tume ya UNESCO ambayo iko chini ya Wizara hii ina *vote* yake na inapokea shilingi bilioni 2 tu lakini Bodi ya Mikopo inapokea takribani shilingi bilioni 500 kwa nini isiwe na *vote* yake. Kikubwa zaidi tunachozungumza hii Bodi ni lazima iwekewe *vote* yake peke yake ili irahishe ufuatiliaji wa fedha zinazorejeshwa na ambazo zinatoka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba kuna miradi ya maendeleo mingi sana yaani kwa hiyo shilingi bilioni 863, shilingi bilioni takribani 400 ndiyo zinabaki. Jambo la kusikitisha miradi muhimu kama ya vyoo na usafi fedha za nje tu ndiyo zinahudumia. Kwa hiyo, leo tunahitaji wahisani watuchimbie vyoo, haiwezekani. Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu sana lizingatiwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *TET*. Wengi wameongelea kuhusu vitabu, mtakuwa mnawafukuza tu Wakurugenzi lakini sawasawa, haiwezekani *TET* wawe ndiyo wachapishaji, *editors, evaluators* na wana *approve*, haiwezekani na haiko mahali popote. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba lazima kuwe na *independent organ* ambayo itakuwa inapitia vitabu hivyo. Pia *editor* atakayejulikana amehariri vibaya hyo ndiye achukuliwe hatua. Kwa mfano, haiwezekani *SUMATRA* yenewe iwe inamiliki mabasi, kwa hiyo na huku haiwezekani hao *TET* watunge vitabu, wasambaze na ndiyo sababu tunapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho naomba sana Wizara sasa hivi wanataka kupeleka vitabu mpaka China wakati humu ndani hamjapeleka vitabu kwenye shule za *private*, mnaendaje China?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, mengine utaandika. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Marwa Ryoba na Mheshimiwa Maria Kongoye na Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mfumo wa elimu Tanzania umezeeka, umechoka na umechakaa. Ukiangalia sheria iliyoanzisha sekta ya elimu ni sekta ambayo tunalingana umri. Mimi sasa hivi ni mzee. Mfumo wa elimu ambao hauwezi kujibu matatizo ya nchi, huo mfumo umezeeka, umechoka lazima uangaliwe kwa upya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kitabu cha Kamati, ukurasa wa 12, nitanukuu baadhi ya maneno wanasema: "Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya maoni yanaendelea kutekelezwa na baadhi bado hayajatekelezwa kabisa. Baadhi ya masuala ambayo Kamati inaona yana umuhimu lakini bado hayajatekelezwa ni pamoja na; mimi nachukua ile (c),

kuangalia upya mfumo wa elimu yetu nchini ni jambo ambalo Kamati inaona halijafanyiwa kazi kwa zaidi ya miaka mitatu sasa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Biblia sehemu fulani inasema watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa. Sehemu nyingine Biblia inasema mkamate sana elimu usimwache aende zake, mshike sana maana yeye ndiye uzima wako. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka tu twende vizuri kama Waheshimiwa Wabunge. Watoto wanaomaliza darasa la saba ni wangapi ambao hawaendelei na sekondari? Watoto wanaomaliza *form four* ambao hawaendelei na *form six* ni wangapi? Watoto wanaomaliza *form six* ambao hawaendi vyuo vikuu ni wangapi? Mfumo wetu wa elimu ni mfumo unaowaandaa watu kwenda kuajiriwa si mfumo unaowaandaa watu kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tuchukulie tu takwimu ya 2017/2018, waliofeli mwaka 2017 darasa la saba ni 247,915 sawa na asilimia 27. Mwaka 2018 waliofeli ni 210,215 sawa na asilimia 22. Hawa wanaenda wapi na wana ujuzi gani? Kwa hiyo, ni lazima mfumo wetu wa elimu tuupitie upya. Mataifa yote duniani ambayo tunasikia ni matajiri kama Marekani, China, Finland na Uingereza lakini utajiri walionao sio *raw materials* bali ni *brain* na *brain* inahitaji uwekezaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu moja kwenye Biblia inasema bora hekima basi jipatие hekima, naam, kwa mapato yako yote jipatие ufahamu. Narudia, kwa mapato yako yote jipatие ufahamu. Maana yake uwekezaji kwenye elimu ni gharama na halikwepeki. Ili nchi yetu iweze kubadilika lazima mfumo wetu wa elimu tuubadili. Hiyo hatuwezi kuikwepa ni lazima tubadili mfumo wetu wa elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunasema kwa mfano asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania ni wakulima, hivi tunawafahamu hao wakulima? Unadhani wakulima ni wale

wanao-graduate, ni wenyewe *PhD* au ni maprofesa? Wakulima ni hawa waliofeli darasa la saba na *form four*, tumewapa *skills* gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni shahidi wakati naanza darasa la kwanza nilijifunza kupalilia na kutengeneza bustani shule ya msingi. Leo shule zote za msingi watoto anamaliza la saba hajui kushika jembe, tunamwandalia mazingira gani? Leo tunataka tupate wafugaji bora, kule shule ya msingi tunajua wafugaji ni darasa la saba, uongo? Wanaofuga ni darasa la saba, wana *skills* za ufugaji na *agriculture*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri masomo ya kilimo yako wapi, tume-concentrate na masomo mengine masomo ya kilimo hakuna, masomo ya biashara hakuna, tumeondoa. Wakati umefika tuko kwenye karne ya viwanda lazima watoto wetu wapate masomo ya usindikaji, kilimo na ujasiriamali kuanzia shule za msingi *and so forth* kinyume na hapo haiwezekani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba sana unilindie muda wangu, samahani. La pili ni lugha ya kufundishia na hapa naomba ninukuu *abstract* kidogo kutoka kwenye *blog* moja ya *Science Direct* kuhusu lugha ya kufundishia. Wanasema: " *The importance of learning a foreign language in childhood. Among philosophers, empiricism and the psychologist, behaviourists believe that language is a social creature and like other social behaviours are acquired. Language learning is natural. Babies are born with ability to learn it and that learning begins at birth. Many experts believe that learning the language before the age of ten years allow children to speak correct and fluent as an indigenous person. Therefore, whatever the earlier children become familiar with the foreign language, he/she have better chance to speak proficiency. Research suggests that from birth through age ten is the best time to introduce new languages to a child.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya kujifunza shulenii lazima ianzie utotonii, lazima Tanzania tujue sisi siyo kisiwa. Hii

biashara ya Kiswahili kuanzia darasa la kwanza *then sekondari* imeshapitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wapo wanaosema twenda kwenye Kiswahili, mimi niwaambie kama tunachagua kwamba ni Kiswahili tujuulize maswali, *who are we trading with*, tunafanya biashara na akina nani? Kama unataka kufanya biashara na China, Marekani, Rwanda, lugha sahihi siyo Kiswahili bali ni Kiingereza.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Ahsante, mengine uandike.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja tu nimalizie.

MWENYEKITI: Haya malizia sekunde kumi.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nikiuliza hapa Wabunge, Mawaziri na watu wengine wenye pesa wangapi watoto wao wanasona shule za Kiswahili kama sio *English Medium*, kama siyo shule za *private*.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. MARWA R. CHACHA: Kwa hiyo, *English is the solution.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana muda wako umekwisha. Mheshimiwa baba Haonga kaa chini, tafadhalii. (*Makofii/Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Kangoye.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri pamoja na Naibu wake wakiwemo Katibu Mkuu na Naibu wake pamoja na timu yote ya wataalam wa Wizara hii. Kwa kweli hotuba ni nzuri kwani imesheheni mambo mazuri ambayo yanaeleweka na sisi kama Wabunge kazi yetu ni kushauri pale ambapo kuna mapungufu na ndivyo ambavyo nitafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, nitakuwa sijatenda haki kama sitongooseza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri anayofanya ya kusimamia Serikali. Kama tunavyoona leo hii wanafunzi wanasoma bure kutoka shule ya msingi mpaka sekondari. Vilevile tunaona kuna utaratibu mzuri wa kutoa mikopo hata kama mapungufu yapo bado tutaendelea kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanikiwa kwa wananchi ni kufanikiwa kwa taifa lakini kuwa na elimu pekee bila ujuzi bado siyo suluhisho la kufanikiwa kwa wasomi wa Kitanzania. Hivyo basi, nitumie fursa hii kuishauri Wizara kuhakikisha kwamba inaweka mikakati ya kupitia mitaala iliyopo ili kuweza kutoa fursa kwa wanafunzi amba wapo mashulen i kushiriki katika michezo lakini katika mafunzo ya kazi za mikono kama ushonaji, ufinyanzi pamoja na ujasiriamali. Kwa upande wa michezo nipongeze Wizara kwa kurudisha michezo ya UMISETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini nashauri hivi? Ni kwa sababu ni wakati wa nchi yetu kujitafakari na kuhakikisha kwamba tunaanza kutengeneza wasomi wasio na fikra ya kuajiriwa tu ila wasomi wenye fikra ya kujajiri na kuweza kutengeneza ajira kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu katika kipindi cha Ubunge wangu ndani ya miaka hii michache nimeweza kutembelea shule kadhaa kwa nia mbalimbali. Naipongeza Shule ya Sekondari ya Misungwi kwa sababu kwa kweli imekuwa ni ya mfano mzuri na ningetamani sana siku moja Mheshimiwa Waziri atakapokanyaga Mkoa wa Mwanza aweze kufika pale ili aone. Kwa kweli shule hii imekuwa ikitoa mwongozo mzuri kwa wanafunzi wake vilevile imekuwa ikiwaandaa kwa ajili ya maisha baada ya masomo chini ya Mwalimu Mkuu Mr. Mbando kwa kweli ni mbunifu na anahitaji pongezi na shule ile inahitaji motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ile ina *club* ya ujasiriamali, wanatengeneza sabuni za maji na mbolea za maji na wanafundisha wanafunzi ujenzi wa nyumba za machupa ya plastiki. Kama haitoshi wanawafundisha wanafunzi wao wa jinsia ya kike kuweza kutengeneza taulo za kike ili waweze kujisitiri katika siku zao. Vilevile kama haitoshi kupongeza kwa hayo imekuwa na *Fema Club* ambayo imeongoza nchini kwa miaka kadhaa. Kwa hiyo, tunahitaji walimu wabunifu kama hawa na ni mategememo yetu kwamba hata pale ambapo *promotion* zinatokea kutoka kwenye ualimu kwenda kwenye Uafisa Elimu, walimu kama hawa akina mwalimu Mbando ndiyo wanaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu kwa walemovu, kwa kweli bado haliridhishi, wanafunzi wenyе changamoto ya ulemavu ni wengi, shule hizi zimekuwa ni chache mno. Kwa mfano kwa Mkoo wa Mwanza zipo shule tatu tu ambayo ni Shule ya Mitindo iliyoko katika Wilaya ya Misungwi, kuna shule mbili za Wita na Itumbili katika Wilaya ya Magu. Kwa kweli shule hizi ni chache kulingana na mahitaji. Na uchache huo unalazimisha wanafunzi ambao wana changamoto ya ulemavu kwenda kwenye shule za kawaida ambazo hazina miundombinu inayowafaa, lakini vilevile hakuna wataalam wanaoweza kuwaelimisha vizuri kwa kiwango ambacho kinahitajika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile shule hizi pamoja na uchache wake bado kuna upungufu mkubwa wa *hostel*.

Nikitoa mfano wa shule ya Itumbili iliyoko Magu ina wanafunzi 105, lakini katika hao ni 48 tu ambao wanaweza kuwa *accommodated* katika mabweni. Kwa hiyo, tunaona umuhimu wa kuongeza *hostel* katika mashule haya, na ukiangalia wanafunzi wengi wanatoka umbali mrefu, wengine ni wa kubebwa, wanapelekwa shule kwa kubebwa, wengine wanatembea kwa shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi langu kwa Wizara hii kwamba iweze kuangalia changamoto hiyo. Kama Mbunge wa vijana kwa nafasi yangu nimeweza kuwafikia mpaka sasa wanafunzi 26 ambao nimeweza kuwagawia baiskeli za watu wenye ulemavu ili waweze kufika shulenii. Sasa najiuliza, kama Mbunge nimeweza kufika hao watu, kwa Serikali hii ambayo inatoa elimu bure ni kwanini isiweze kuwafikia wanafunzi hawa ili *at least* waweze kupata baiskeli za kuwafikisha shulenii. Mheshimiwa Prof. Ndalichako, ni imani yangu unapokuja kuhitimisha nitasikia neno kuhusu hilo, kama tunaweza kutoa elimu bure na kama tunaweza tukatoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, ni kwanini tusiweze kuwasaidi wanafunzi hawa ambao wanaenda hata kwenye shule za kawaida kwa mwendo mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia kuhusu mikopo nikakumbuka kwamba lipo suala la kipaumbele katika utoaji wa mikopo. Tumeona wanafunzi ambao wamefaulu kwenda vyuo vikuu ambao wanatoka kwenye mazingira magumu wakipata mikopo, wakipewa kipaumbele, lakini tumeona wanafunzi ambao wanasona masomo ya ualimu na masomo ya sayansi wakipewa kipaumbele. Ni kwanini wanafunzi hawa wenye ulemavu wasipewe kipaumbele katika utoaji wa mikopo pale ambapo wanafaulu kwenda shulenii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na upungufu wa *hostel*/kama ambavyo nimesema hapo awali, kwa wanafunzi wenye ulemavu bado kumekuwa na upungufu mwingi katika shule hizi. Kwa mfano mashine za kupima usiku, vitabu vya nukta nundu, karatasi za kuandika nukta nundu, vifaa...

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri, mengine utaandika. Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja na mengine nitawasilisha kwa maandishi. (*Makofii*)

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa nami kuchangia hii hoja iliyopo mbele yetu. Naomba nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Prof. Joyce Ndlichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2019/2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii pia kuungana mkono na Wabunge wote wa chama tawala na watanzania wote wenye mapenzi mema na nchi hii kwa kumpongeza Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutoa elimu bure ambayo pia ni lengo namba nne la maendeleo endelevu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilichangia bajeti ya elimu, naomba nichukue fursa hii kuishukuru sana Serikali yangu kwa kutekeleza baadhi ya maombi ambayo sisi kama Wabunge tulionomba Serikali hii iyafanye. Nikichukulia mfano katika Mkoa wa Dodoma, mazingira ya utendaji kazi katika udhibiti wa elimu kwamba Wizara imetoa kiasi cha milioni 152 kwa ajili ya Wilaya za Chemba, Bahi, Chamwino na Jiji kwa ajili ya kujenga Ofisi za Wadhibiti Ubora wa Elimu, pongezi sana kwa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, pia zimetolewa fedha kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi za Udhibiti Ubora wa Elimu katika Wilaya za Kongwa na Mpwapwa. Naomba niwatie shime, niwatie shime watendaji wa Wizara chini ya uongozi wa Waziri, pamoja na kelele zote ambazo mnaambiwa kwamba Serikali haijafanya kitu kwenye suala la elimu naomba mtembee kifua mbele watanzania tuko

pamoja na ninyi, mnafanya kazi nzuri sana pamoja na ufinyu wa bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ambayo nilikuwa naomba niishauri Wizara ijaribu kuona inaifanyia kazi, hasa kwa suala la watumishi wa walimu waliopo Wizara ya Elimu, wengi wamekuwa wakicheleweshewa kupandishiwa madaraja kwa muda mrefu. Nikichukulia kwa mfano, mwalimu aliyeanza kazi TAMISEMI mwaka mmoja pamoja na mwalimu aliyeanza kazi Wizara ya Elimu ngazi zao za mishahara zinatofautiana. Kwamba huyu wa TAMISEMI yuko *TGTS I*, wakati wa Wizara ya Elimu *TGTS G*, hii inapunguza sana ari ya utendaji wa kazi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri hili mlione ili kusudi sasa muweze kuwapandisha waalimu hawa madaraja kwa muda amba unaotakiwa. Kwa sababu imetokea pia kuna baadhi hata wakati wa kustaaifu wamekuwa wakitofautiana kupata yale mafao kwa hiyo hii inakuwa inawakatisha sana tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nilipenda kufahamu kwanini Wadhibiti Ubora wa Elimu hawapati posho ya madaraka? Kwa sababu wao ndiyo wanaokuwa wakiwakagua hawa waalimu katika shule lakini cha kushangaza ni Waalimu Wakuu, Waratibu Elimu Kata ndiyo wanaopata posho. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake, nilikuwa naomba ajaribu kunieleza, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba Wadhibiti Ubora katika ngazi ya wilaya na ngazi ya kanda nao wanaweza kupata fursa ya kuweza kupata posho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 129 hadi 130 ya hotuba hii amezungumzia kuhusiana na suala la elimu ya ufundu, kwamba Wizara ina mpango wa uendelezaji wa elimu ya fundi *study* kwa muda mrefu ambao watatoa washiriki 10000 lakini kwa muda mfupi watakuwepo washiriki 24000. Ushauri wangu kwa Wizara, kwa kuwa kuna baadhi ya shule za msingi zina vituo vya ufundu *study*, hebu Wizara ione kwamba vituo hivi vifufuliwe wapewe walimu wawepo, vifaa viwepo pamoja na bajeti iandaliwe ili kusudi vituo hivi

viweze kufanya kazi kwani vina msaada mkubwa sana katika maeneo ya vijiji. Kutokana na vituo hivi tunaweza tukapata mafundi mbalimbali kutoka hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 25 wa hotuba hii pia Waziri amezungumzia kuhusu suala la kuimarisha *study* za utoaji ushauri na unasihi kwamba kuna waalimu 300 watapewa mafunzo hayo. Nilikuwa naomba niishauri Serikali kwamba hawa walimu wawe wengi zaidi kwa sababu suala la ushauri na unasihi linahitajika sana kuanzia shule za msingi hadi shule za sekondari na hadi vyuo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iangalie kwa upya zaidi na kuongeza bajeti katika hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nilikuwa naomba nizungumzie kuhusu elimu maalum. Sisi katika Mkoa wa Dodoma tuna Shule ya Bulgiri, wasiliona. Nilikuwa niilombe Wizara waone sasa umuhimu wa kuweza kutupatia vitabu vyta kutosha hasa vile vyta nukta nundu kwa sababu bado kuna upungufu wa vitabu hivi ili watoto wetu waweze kupata elimu iliyo bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upungufu wa waalimu wengi wamelizungumzia, na mimi naomba nilizungumzie...

MWENYEKITI: Kengele ya pili tayari, malizia.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Hili ni tatizo la kitaifa, lakini pia upatikanaji wa fedha za kutosheleza. Baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kemi dakika tano, Mheshimiwa Masoud dakika tano.

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Wizara yetu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nianze kwa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa maamuzi

yake makubwa na ya msingi kabisa ya kuamua kutoa elimu bila malipo. Hili jambo limekuwa zuri na limeongeza sana wanafunzi kwanza kuanzia shule ya msingi na sekondari, lakini jambo hili limekuja na changamoto nyingi sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kwenye miundombinu ya elimu msingi, kwenye shule zetu za *primary* kuna upungufu wa madarasa kwa asilimia 85, kuna upungufu wa vyoo kwa asilimia 83, kuna upungufu wa walimu kwa asilimia 60. Sekondari vivyo hivyo, hii ni kutokana na ripoti ya CAG, madarasa kwenye sekondari ni asilimia 52, maabara asilimia 84, madawati asilimia 86.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwiano wa ongezeko la wanafunzi kuanza shule na uwiano wa miundombinu bado havilingani. Tumeongeza wanafunzi kwa asilimia 17 lakini mpaka hivi tunavyoongea ni asilimia moja tu ya madarasa ndiyo yameongezeka, inafika mahali darasa moja linakuwa na wanafunzi 100 – 150. Kiuhalisia hili suala linakuwa gumu na vilevile hatuwezi kupata elimu ambayo itakuwa bora kwa uwiano mwalimu mmoja na wanafunzi 150. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wenzangu wamezungumzia kuhusu upungufu wa walimu. Kuna upungufu mkubwa sana wa waalimu, hususan walimu wa sayansi. Nikitoa mfano Wilayani Mwanza kwenye Jimbo la Buchosa, kuna shule hakuna kabisa walimu wa sayansi na mwisho wa siku tunakuja tunategemea wanafunzi wa *form two* wafanye mitihani ya Taifa ya NECTA ambayo inahusisha na masomo ya sayansi. Hawa wanafunzi tunawadahili vipi kama hakuna mwalimu na mwisho wa siku tunataka wafanye mitihani na wafaulu mitihani yao. Hili suala linakuwa ni gumu kwa kweli na nadhani ifike wakati muafaka sasa tuangalie kwa jicho la kipekee suala la kuongeza walimu shulenii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia pia kuhusu suala la elimu kuwa chini ya TAMISEMI. Ni maoni yametolewa na Wabunge wengi na pia Kamati pia imezungumzia hili suala ifike mahali sasa, suala la elimu

lijitegemee kama elimu. Itakuwa rahisi *ku-monitor*na itakuwa rahisi vilevile kufuatilia, ufuatiliaji wake itakuwa tunajua ni nani yuko *accountable* na hili suala. Mwisho wa siku ndiyo tunaongea shule hazina walimu, ukienda kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu anakwambia siyo la kwangu liko TAMISEMI, lakini ingekuwa chini ya Wizara moja inakuwa rahisi na uwazi pia ungepatikana ukaonekana na kujua ni namna gani tunaangalia suala la elimu kwa ujumla wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeongelewa ni suala la adhabu ambayo imetolewa mwaka jana baada ya mitihani kuibiwa. Kilichofanyika kwenye shule za *private* ni kama uonevu. Shule za *private* baada ya mitihani kuibiwa, mitihani imerudiwa na shule za *private* zimefungiwa haziwezi kufanya mitihani kwenye shule zao. Wanafunzi inabidi watoke shule moja waende shule nyingine wakati wa kufanya mitihani, lakini kwenye Wilaya ya Chemba, Halmashauri ya Chemba ni shule pia zimefutiwa mitihani lakini kwa sababu ni shule za Serikali, bado wao wanafanya mitihani kwenye shule zao. Naomba Mheshimiwa Waziri akija kujibu atuambie hii adhabu imetokana na nini na kwa nini kunakuwa kuna *double standard*. Shule za Serikali zinapewa adhabu tofauti, shule za *private* zinapewa adhabu tofauti, Mheshimiwa naomba ukija ku-wind up utuambie ni nini kinapelekea suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hiki kitabu cha ripoti ya wizara, *page* namba 146 naomba nisome, kinaandika, kuandika muhtasari wa lugha ya Kichina kidato cha tano na cha sita ambayo inafundishwa katika shule za sekondari kumi na sita, zimetajwa shule hapo. Naomba ifike mahali tuwe na kipaumbele tujue tunataka nini. Kama mpaka leo...

MWENYEKITI: Malizia, malizia!

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia. Kama mpaka leo hatuna vitabu vyatagarasi la kwanza mpaka la tatu kwenye shule za *primary*, hatuna Mtaala ambao unatuelezea kwenye shule za msingi, sasa inakuwaje tunaanza kuanza kuandika Kichina na

tunatengeneza muhtasari wa South Sudan wakati hapa penyewe Tanzania ambapo darasa la kwanza mpaka la tatu hawana vitabu mpaka leo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri, Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ningependa kumuomba Mheshimiwa Waziri, matokeo ya mitihani ya kidato cha nne *form four na form six* kwa Visiwani hasa Unguja na Pemba kuendelea kila wakati kuwa siyo mazuri kulingana na takwimu ambazo zinatokea, hivi wewe halikukeri hili? Pia una mkakati gani hasa wa zaida kuona kwamba matokeo kutoka Visiwani, Unguja na Pemba kwenye mikoa yote sasa yanabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vyaa sayansi shule za sekondari (*O'level*) kuna upungufu mkubwa sasa wewe na mwenzako Wizara ya Elimu Zanzibar mna mkakati gani wa ziada? Leo yaani mitaala inabadilika inachukua muda mrefu kufika kule Zanzibar, sasa kuna tatizo gani la ziada ambalo linaonekana hili kuna upungufu kama huu na bado naona tu na matokeo ya Zanzibar kila siku yanaendelea kuwa mabaya hili jambo mkae mlione.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana, kuna kwenye NECTA Baraza la Mitihani wewe ndio ulikuwepo Mheshimiwa mwenyewe huko, lakini uwiano wetu washiriki walotoka Zanzibar ni wa aina gani kiasi ambacho kwamba Zanzibari kule wapo na washiriki wao na jinsi gani ya kushirikishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mlisema matokeo mabaya Kusini Pemba, Kaskazini Pemba, Kusini Unguja, Kaskazini Unguja, Mjini Magharibi, lakini wewe ulikuwepo jikoni. NECTA je, Zanzibar iko kiasi gani mtuambie na sisi tunapata uchungu kweli kuona Zanzibar bado hatupati

matokeo mazuri kumbe kuna mambo ambayo yanahitaji yatelekezwe. Ningombwa sana Mheshimiwa Waziri utupe mpango makakati baina yako na mdau mwenzako wa Zanzibar kuona kwamba matokeo hasa ya *form fourna form six* kwa upande wa Visiwani Unguja na Pemba yaani Zanzibar yanakuwa mazuri, hilo lilikuwa la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili suala la fedha za maendeleo kuhusu wahisani. Tumesema muda mrefu sana kwamba hatuwezi kupata maendeleo ya kweli kama tunategemea wahisani hawa wafadhili. Ukingalia katika maeneo mbalimbali kuna kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari 4590 *item* kwenye *Sub Vote 2001*, bilioni 30.8 zote za wahisani. Kwenye Idara ya Udhibiti bora vilevile, nako kuna bilioni 16 *Education Program for Result*, fedha za wahisani. Kwenye elimu, Idara ya Elimu ya ualimu nako vilevile, *Teachers Education Support Program billion 15.4*, zote ni wahisani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bajeti yote ya maendeleo imeenda kwenye wahisani, wahisani, wahisani hawa ambao hawaleti fedha, nawashangaa na ndiyo maana tukasema leo tutumie vitabu hivi na wale wenzangu waliosema kwamba hata kwenye fedha za maendeleo ambazo za mikopo zimeenda kule.

Kwa hiyo kuna *Volume II*, kuna *Volume IV*, kuna Randama hapa, juzi tulipokuwa tunatumia vitabu hapa wengine wanasema tutavua nguo, tutavua nguo, alisema Waziri mmoja hapa na kama leo angekuwepo Waziri Kangi leo ningemwambia vua nguo kwa sababu sisi tunatumia vitabu, vua kweupe mchana kweupe hapa. Haiwezekani tunataka maendeleo ya kweli ikawa tunatenga asilimia zaidi ya 60 kwa wahisani, haiwezekani hata kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *higher education*, elimu ya juu Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na uko makini kweli leo. Nenda kwenye 2228 nako ni vilevile, kuna *Support on Research and Development*. Tunakwenda kufanya utafiti kutuwezesha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha

Ardhi, MUHAS kufanya utafiti kwa maendeleo ya elimu. Bilioni 10.4 kitabu cha *Volume IV*, mmedharau Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mmedharau MUHAS, mmedharau Chuo Kikuu cha Ardhi mmedharau, fedha hizi za wahisani yaani kila kitu wahisani, wahisani, hawa tunawaita mabeberu nawashangaa kweli kweli. Hakuna kitu ambacho kinakera kwamba fedha ... (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, mengine utaandika.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Atakayevua nguo na avue! (*Kicheko/Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa nawashukuru kwa michango yenu, jioni tutaanza na Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Goodluck Mlinga dakika tano, Mheshimiwa Khadija Nassir dakika tano na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, tutatazama na utaratibu mwingine. Nasitishughuli za Bunge mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilitishwa mpaka Saa 11:00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)

MWENYEKITI: Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa kwanza jioni ni Mheshimiwa Taska Mbogo. Jiandae Goodluck Mlinga.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema na leo tuko hapa Bungeni tunachangia hoja za Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, napenda kutoa pongezi kwa wafuatao. Pongezi za kwanza napenda ziende kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudini zake za kuwatumikia Watanzania na kwa moyo wake thabiti amba o umeonesha kubadilisha maisha ya Watanzania na dunia imeona na imekubali kwamba sasa tunaye Rais ambaye atakwenda kubadilisha nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Prof. Ndalichako na Makamu wake Mheshimiwa Ole Nasha kwa kazi nzuri ya kubadilisha elimu yetu nchini kwa kufuatilia mambo mengi ambayo yalikuwa hayaendi vizuri katika Wizara ya Elimu. Nawapongeza sana na ninawaombea Mungu mwendelee kufanya kazi kwa ajili ya maslahi ya Watanzania wote. (*Makoffii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuchangia mawili, matatu kuhusu Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa, Wizara hii ya Elimu imekuwa ikijitahidi sana katika kuboresha elimu, lakini lipo tatizo kubwa ambalo limekuwa tunaenda nalo sasa kwa muda wa miaka mingi. Tatizo hilo ni tatizo la wanafunzi kumaliza darasa la saba bila kujua kusoma na kuandika. Wengine kwa sababu siku hizi ni *multiple choice*, wanafikia kwenda sekondari lakini hawajui kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili limekuwa ni sugu, linahitaji tulifanyie upembuzi na labda iundwe Tume ambayo itashughulikia tatizo hili. Kama mtakumbuka, hapo nyuma hata Mheshimiwa Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alisema iko haja ya kukaa mezani kuangalia matatizo ya elimu nchini Tanzania. Kwa maana hiyo, ni kwamba wale watoto ina maana wanakuwa wamemaliza miaka saba wakitembea pale shuleni lakini hawajui kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaweza tukaangalia jinsi ya kutatua hili tatizo. Kwanza, elimu ya watu wazima iboreshwe ili waweze kwenda kule wakajifunze kusoma na kuandika. Zaidi ya kuboresha, vijijini kwetu kuna wananchi

wengi sana Watanzania ambao hawajui kusoma na kuandika. Hata unapokwenda kwenye vijiji vya wafugaji, kule mkoani kwangu Katavi kuna wafugaji, kwa hiyo, wale wana tabia ya kuhamza hama na *majority* yao hawajui kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kile Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima ambacho najua kwamba kipo lakini kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 15 nimeona hakijaelezea sana. Naomba uangaliwe utaratibu wa kuboresha namna ya wananchi ambao hawajui kusoma na kuandika ili waweze kujunga na hii elimu kama ilivyokuwa miaka ya nyuma wakati tunakua, miaka ya 1970 mpaka 1980. Elimu hiyo ilikuwa na mkazo na watu wengi walijua kusoma na kuandika kupitia elimu hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la kuboresha maslahi ya walimu. Kwa mfano, kule mkoani kwangu Katavi, Jiografia ya Makao Makuu ya Wilaya ni mbali. Unakuta kuna kilometra kama 150 kutoka kwenye kijiji kwenda kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Mwalimu huyu anapanda basi au bajaji ama kitu chochote, anakuja Makao Makuu ya Wilaya ambayo yapo kilometra 150. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Elimu iangalie utaratibu ambao inaweza ikaboresha maslahi au ikawapa marupurupu walimu wanaofundisha vijijini ili wawe na *interest* ya kwenda kufundisha vijijini. Tukichukulia tu kwamba mwalimu anayefundisha mjini anapata maslahi sawa na mwalimu anayefundisha vijijini, kwa kweli naona kwamba hii ina-*demoralize* katika kufundisha. Nafikiri kwamba si vizuri, tujaribu kuangalia tunaongeza marupurupu gani kwa walimu wanaofundisha vijijini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika kuboresha elimu, maana nimesema kwamba wanafunzi wanamaliza darasa la saba hawajui kusoma na kuandika; hii ni kwa sababu wanajaa darasani. Darasa moja lina watoto 200. Naomba Wizara ya Elimu iangalie ni utaratibu gani

tutaufanya kuongeza ujenzi wa madarasa? Kwa sababu kipindi cha kufundisha darasani ni dakika 40. Mwalimu mmoja hawesi akafundisha watoto 200 kwa dakika 40. Ina maana wale ambao ni *cream* ndio watakaojua kusoma na kuandika, wale wenzangu mie watabaki nyuma, watakuwa wanasisidikiza darasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuboreshe pia kwa kuongeza maslahi ya walimu na kwa kujenga madarasa mengine mapya, lakini nguvu hii pia tuwashirikishe wazazi pamoja na TAMISEMI kwa pamoja tunaweza kujenga madarasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia leo ni maabara zilizojengwa. Wananchi walitumia nguvu yao kubwa, walichanga michango mingi, karibuni kila shule imejenga maabara, lakini hizo maabara hazina vifaa. Niiombe Wizara ya Elimu iangalie, hili tatizo italiondoaje? Shule nydingi zina maabara, hata kule Katavi kuna shule zina maabara lakini hazina vifaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa ambavyo tulikuwa tunavitungia sisi, unaenda kwenye chumba cha sayansi unakuta kuna *Bunsen burner*, na kadhalika. Hivyo vifaa ni vigumu kwa shule kuvinunua na kuviweka kwenye maabara. Naomba Serikali iangalie ni jinsi gani itasaidia. Majengo mengi sana yamejengwa kwenye shule, maabara zimejengwa lakini hazina vifaa. Naomba Wizara ya Elimu iingilie kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu shule za ufundi. Naomba ili kutatua suala la ajira nchini, tuongeze shule za ufundi. Pia, kuna zile shule ambazo zilikuwa ni shule za wazazi. Kwa sababu zile shule za wazazi ziko karibu kila mkoa, zingeweza kugeuzwa zikawa Shule za Ufundsi ili watoto wetu waweze kujifunza na waweze kutoka wakiwa wameelewa kitu chochote kama ni kujenga, kushona na kadhalika ili waweze kujiajiri kwa sababu Serikali kama ilivyo hatuwezi tukaajiri wanafunzi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo la ajira nchini. Tuangalie ni mbinu gani tutazitumia ili kutoa tatizo la ajira nchini kwa kuzitumia shule za wazazi ambazo nafikiri ziko katika kila Mkoaa. Labda Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho anaweza akaniambia ni shule ngapi za wazazi ambazo ziko. Ninaamini kwamba kila Mkoaa una shule za wazazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni watoto wa kike, ambapo kiutaratibu Wizara huwa inapeleka pesa kule za kujikimu watoto. Hizi pesa kwa sababu watoto wa kike wana matatizo yao ya maumbile ya kibaiolojia, naomba sana Mheshimiwa Waziri, lile fungu lisigawiwe sawa na mtoto wa kiume kwa sababu mtoto wa kike... (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mlinga dakika tano na Mheshimiwa Khadija Nassir, dakika tano. (*Makof*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa namna ya pekee, naomba nipongeze uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga ukiongozwa na DC mahiri, mchapakazi, Ngolo Malenya kwa utaratibu wake wa kuweka mikakati na kutekeleza kwa ajili ya kuinua elimu ya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kule vyombo vya habari hakuna Lakini vyombo vya habari vingekuwepo tungeenda sambamba na watu wengine, lakini mimi nitazifikisha habari za Ulanga katika Bunge hili ili mjifunze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Ulanga tumeweka *lunch program* kuanzia shule ya msingi mpaka sekondari. Wanafunzi

wanaenda wanakula chakula huko huko wanapata muda wa kutosha wa kujisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna kambi kwa ajili ya wanafunzi wale wanaojiandaa kufanya mtihani. Sasa hivi tuna kusanya vyakula kwa ajili ya kupeleka katika shule ambazo watafanya mtihani kidato cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumebuni miradi kwa ajili ya kuinua vipato vya walimu. Tumewapa mashamba, yaani mwalimu akienda kule inaitwa "gusa unite." Akikaa huko, hawezি kuondoka tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeunganisha wadau wa elimu, tumepata zaidi ya shilingi milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa. Tumebuni utaratibu wa kufanya mabonanza kwa ajili ya kuwapa motisha wale walimu ambao wanafundisha katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Ulanga kuna maeneo hayafikiki kwa baiskeli, hakuna mawasiliano wala umeme. Kwa hiyo, tumeweka motisha kwa ajili ya kuwasaidia walimu kama hao wapate moyo kwa ajili ya kufundisha. Ndiyo maana Mheshimiwa Waziri katika maombi yetu tumeomba tuwekewe *VETA* ili kuwaunga mkono Ulanga kwa jitihada zote za kuinua elimu hizi wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Profesa Ndalichako. Unajua Profesa Ndalichako yuko tofauti na Maprofesa wengine, Profesa wa CCM, Profesa ambaye yuko *updated* kama *iPhone*. Naomba nimpongeze yeye pamoja na Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu wake Akwilapa pamoja na AveMaria. Wamekuwa wasikivu, wamekuwa wakiweka mikakati mizuri na kuitekeleza kwa ajili ya kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukilalam ika mwanzo lakini amekuwa akitusikiliza na kuyafanyia kazi. Ila kuna kazi kidogo naomba akae vizuri na watu wa *private*

schools ili aweze kwenda sawa kwa sababu TAMISEMI wamekuwa kama kivuruge; wanataka kusimamia shule za *private* na hao hao wamekuwa wanamiliki shule za Serikali. Sasa huyu *referee* mchezaji amekuwa anaharibu mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko kodi nyingi sana na ziko ambazo zimetolewa lakini bado wanachokonoa *private* kwa chini kwa ajili ya kuwadai hizo kodi. Kwa mfano, kila mwanafunzi mmoja anatakiwa alipe *fire shilingi* 20,000/=. Huu ni wizi mkubwa ambao Serikali inafanya kwa shule za *private*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa elimu bure. Walioongea hapa wanasesma elimu bure imefanywa kwa mustakabali wa siasa. Ndiyo nakubali, si iko kwenye llani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Sasa nataka wakawaambie wallowaambia elimu bure imefanywa kwa ajili ya siasa. Ulanga kwa mwaka huu wa fedha ambao unaisha, tumepeata gari moja kwa ajili ya ukaguzi wa elimu. Ulanga tumepeata pikipiki 19, wale waratibu wa elimu zamani walikuwa wanatembea kwa mguu, sasa hivi kila mratibu wa elimu ana pikipiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepeata shilingi milioni 214 kwa ajili ya kumalizia maboma ambayo wananchi walanza kujenga. Tumepeata zaidi ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na madarasa katika shule mbalimbali. Naipongeza Serikali kwa kutoa ajira kwa walimu 4,000 Ulanga; na yenyewe tumepeata japokuwa kidogo. Naiomba Serikali iongeze jitihada ya kuajiri walimu kwa sababu mtaani wako wengi, kuna walimu zaidi ya 100,000. Kwa hiyo, Serikali iongeze ajira kwa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ulanga tunazalisha wanafunzi wa *form four* 1,000 - 1,200 kwa mwaka. Wanaokwenda kidato cha tano na cha sita hawazidi 200. Wanabaki 1,000; hao 1,000 tunawapeleka wapi? Ndiyo maana nimekuomba Mheshimiwa Waziri, tusogezee *VETA*, eneo tayari tunalo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kukarabati shule kongwe lakini kwangu mmeisahau shule moja inaitwa Kwiro. Kwiro ni shule ya zamani wamesoma vigogo wakubwa, nikiwemo mimi. Kwa hiyo, naomba muikarabati hiyo shule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuongeza fungu la Bodi ya Mikopo kufika shilingi bilioni 423, lakini changamoto imekuwa kubwa kwa sababu wanafunzi ni wengi. Serikali imeshindwa kuchanganua kupata wanafunzi masikini halisi na wanafunzi wenye kipato cha juu. Kwa hiyo, tatizo limekuwa kubwa. Pia makato ya Bodi...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khadija Nassir, dakika tano.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa, napenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri lakini pia napenda kuipongeza Serikali kwa ujenzi wa maktaba mpya na ya kisasa. Maktaba hiyo ndiyo kubwa kwa *East Africa* nzima. Maktaba hiyo inakwenda sasa kuwapata watafiti wetu nguvu na ufanisi wa kuweza kufanya tafiti zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maktaba hiyo pia inakwenda kuwaisaidia wanafunzi wa elimu ya juu nchi nzima kuweza kufikia yale mahitaji ambayo yalikuwa yanatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vie muda wangu mchache, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Suala la kwanza ambalo nitaliongelea ni Sera ya Elimu *versus* Sera ya Uchumi wa nchi. Nchi zote duniani, Sera ya Elimu ndiyo inatoa dira na mwelekeo wa Sera ya Uchumi wa nchi. Kama tunavyofahamu, Wizara ya Elimu ndiyo mdau na ndiyo yenye dhamana ya kuleta rasilimali watu ambao wataweza sasa kujenga uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda na uchumi huu kwa kiasi kikubwa sana unahitaji rasilimali watu, wenye elimu na ujuzi wa *level* ya kat, sio *level* ya juu. Kama tutakubaliana na hilo, niiombe sasa Serikali yangu, nafahamu inasikia na ina lengo la kui-*support* hii Sera ya uchumi, iende sasa ikaboreshe mitaala katika vyuo vyetu vya stadi za kazi, iende ikaboreshe mitaala na ufanisi katika vyuo vyetu vya VETA. Kwa sababu hizo ndiyo taasisi ambazo zitatuletea nguvukazi ya vijana na watu ambao wataendesha viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo, naomba sasa kidogo niende nikagusie masuala ya watu wenye mahitaji maalum hasa wale wenzetu ambao wana shida ya kusikia au kwa lugha rahisi, viziwi. Hawa watu wenye kundi maalum hili wanakutwa na changamoto kubwa. Changamoto kubwa ni kwa sababu hawana uwezo wa kufanya mawasiliano ya moja kwa moja na watu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii inasababisha hata ufanisi wao katika masuala ya elimu wakiwa shulenii unakuwa mgumu sana kiasi kwamba huwa wanakosa msaada kwa wenzao. Rai yangu kwenye hili, napenda kuishauri Serikali ione sasa umuhimu wa kuanzisha elimu ya lugha ya alama iwe kama somo katika shule zetu ili sasa hawa wenzetu waweze kufaidika na mfumo wa elimu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Menyekiti, katika kufanya hili, hatuendi tu kuwasaidia watu ambao hawana uwezo wa kusikia kwa vile soko la ajira kwa wakalimani sasa hivi ndani na nje ya nchi liko *very hot*. Tunakwenda ku-*create* ajira kwa vijana ambao sasa watakuwa wamepatiwa elimu ya lugha ya alama kwa maana ya kwamba tutapata wakalimani ambao watapata ajira ndani na nje ya nchi yetu. Kundi hili lina changamoto nydingi sana. Hiyo ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee ya pili. Kati ya vyuo ambavyo tunavyo nchini, ni vyuo vinne tu ndiyo

ambavyo mpaka sasa vina wakalimani, kiasi kwamba kuna wanafunzi ambao wanafanikiwa kufika mpaka ngazi ya shahada, wanafika vyuoni na huwa wanakosa misaada ya kuweza kuendelea au ku-cope kwa sababu hawana vyuo husika au hawana vyuo maalum kwamba hawa vyuo vyao specifically ni hivi. Huwa tunawachanganya pamoja na wanafunzi wengine na wakifika kule wanakosa wakalimani wa kuweza kuwasaidia kuweza ku-cope na masomo.

Mheshimiwa Waziri, naomba hili ulichukue. Tuna watu wenye ulemavu wa kusikia ambao ni *very genius*, wanahitaji msaada mdogo tu wa wakalimani ili na wao sasa waweze ku-cope vizuri na masomo wakiwa vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nytingine kwa hawa wenzetu ni suala zima la ajira. Kila anayesoma ndoto yake ni kuweza kutumia elimu yake kumfikisha au kuweza kutumia elimu yake kumkwamua kwenye masuala ya kiuchumi, lakini kwa bahati mbaya sana bado Serikali...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Eh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kapufi.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote nami nimshukuru Mheshimiwa Waziri na timu nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuchangia naomba nianze eneo la elimu maalum kwa maana ya ukurasa wa128, nashauri jambo moja kwa maana ya wananchi tuendelee kuhamasisha mbali na kuhamasisha kuhakikisha hatuwafichi

watu hawa wenye ulemavu, tunawaandikisha ili waweze kushiriki katika nafasi ya elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la upungufu wa elimu, eneo langu la Mkao wangu wa Katavi, hasa kwa maana ya masomo ya *physics* na *mathematics*. Tatizo la Walimu kama tulivyoongea maeneo mengine na bahati mbaya, kuna Walimu wanapangwa kuja katika maeneo yetu, lakini hawafiki. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba hilo nalo alibaini. Kuna Walimu ambao wamekuwa wakijitolea kwa muda mrefu, labda tufike mahali tuone, hawa ambao wamekuwa wakijitolea labda ajira ziende kwa watu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo, bahati nzuri, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, aliweza kufika Mkao wa Katavi, aliweza kutembelea Chuo cha VETA, aliweza kutembelea shule ya watoto wa kile pale Mpanda na kwa ujumla wake, nishukuru upande wa VETA, waliwezesha fedha kwa maana ya ukarabati, lakini kuna upungufu wa takribani milioni 100 kwa maana ya awamu ile ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya ukarabati. Naomba hili Mheshimiwa Waziri alitilie maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwa maana ya eneo lile la majengo, kwa maana ya shule za sekondari, Mheshimiwa Waziri, upande wa Mpanda, shule ya wasichana, ni kweli tumeongea hapo nyuma, naomba kwa maana kama maeneo mengine nayo ile ni shule kongwe, ameiona yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri, tuna tatizo la uzio na ukarabati wa shule kwa ujumla wake. Najua mazingira mazuri tunapojaribu kutafuta kujua mwanafunzi anasomaje, anawezaje ku-*concentrate* ni pamoja na mazingira mazuri, yana nafasi yake kubwa sana katika ufaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, nami katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi, naendelea kushukuru, wakati Serikali imejipanga, kwa mfano, kwa maana ya *Arusha Tech*, imejipanga kwa maana ya kununua vifaa vipyta. Hili naliomba sana, dunia inakwenda kwa kasi, teknolojia zinabadilika, kwa hiyo, Wizara kwa kuliona hilo, kwamba ni

vizuri basi, tukaja na vifaa vipya, hili jambo naliunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Wizara, kwa maana ya Mtaalam Elekezi, ule ukurasa wa 18, ambaye anakwenda kutengeneza *capacity building*, kwa maana ya *labour market* ya vitu vingine vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho mwaka jana, kati ya tarehe 19 na 20, niilishiriki katika mukutano mmoja mkubwa Astana, huko Kazakhstan, wenzetu, pamoja na kwamba ni nchi ambazo zimepiga hatua. Katika mukutano huo, ambao ulikuwa na kichwa cha habari *Investing in Youth Living no One Behind*. Watu hawa wamechambua mambo mengi, lakini katika hayo waliyochambua na hili nimeliona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri. Nimefarijika sana kwa hilo, kwamba wenzetu ambao tayari wamekwishaendelea, lakini wameona kwamba namna pekee ya kufanya, ni kufanya katika sura ifuatayo:-

Kwanza, ni kuamsha ufahamu kuhusu elimu, afya, ajira na masuala ya kijamii, lakini ufahamu huu, *especially* kwa those ambao ni *disadvantaged*. Tukitoka hapo, wameamua kwenda na jambo moja, uwezeshaji zaidi, elimu bora, kwa maana ya *vocational training*, inayokwenda na ushindani na mahitaji ya soko la ajira, uchumi wa dunia na maendeleo ya teknolojia. Haya yote ambayo wajumbe wamekuwa wakiongea, kama hatuendi kuangalia mahitaji ya soko, uchumi wa dunia, mabadiliko ya teknolojia, tutaendelea kupiga kelele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo kama halitoshi, kuna suala, wenzetu wamekuja na kitu wanasema, *review and adjust the education system and vocational training in line with economic, social and entrepreneur realities*. Kwa hiyo, haya yote nilikuwa nasema, wenzetu huko duniani wameendelea kuaona kwa sura hiyo. Kwa hiyo, niombe, katika mazingira haya, ambapo nilijaribu kusoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri, bahati nzuri, nilipokuwa nikitoka ukurasa mmoja nafikiria kwamba jambo hili linalogusa kuwawezesha

watu kwa sayansi na teknolojia sasa hivi linapatikana wapi, nalikuta ukurasa wa pili, nikitoka ukurasa wa pili nalikuta ukurasa wa tatu. Kwa hiyo, katika hilo niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa kuheshimu muda, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya Chuo cha Ufundı Stadi Mkoani Ukerewe, ongezeko kubwa la vijana wanaomaliza elimu ya msingi na sekondari usioendana na uwepo wa miundombinu wezeshi kwenye taasisi za elimu umeathiri sana ufaulu wa vijana wetu. Hivyo ukichangiwa na jiografia ya Visiwa vya Ukerewe vijana wengi wamekuwa wanaona kuwa uvuvi ndiyo suluhisho lao kimaisha, hali hii imepekelekea uharibifu wa mazingira na uvuvi usio endelevu kwa sababu tu ya kukosa njia mbadala ya kuwawezesha kukabiliana na changamoto za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii uwepo wa Chuo cha Ufundı Stadi (*VETA*) katika Visiwa vya Ukerewe kutasaidia kwanza kuandaa vijana wetu kuelekea kwenye nchi ya viwanda, kuwaandaa vijana kuwa na fikra za kujajiri kiufundi zaidi badala ya fikra za kuajiriwa hali ambayo imekuwa inapelekeea kutumia muda mwingi kutafuta kazi badala ya kujajiri na kupunguza uvuvi haramu unaotokana na wimbi kubwa la vijana kuamini katika uvuvi tu, kumbe kuititia ufundi wangeweza kufanya shughuli nyingine za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuruhusu vijana kurudia shule hasa elimu ya msingi. Maeneo ya vijijini ambapo kutokana na mazingira, vijana wengi wamekuwa wanamaliza elimu ya msingi katika umri mdogo lakini pia wakiwa na uwezo mdogo kitaaluma hali ambayo huwapa mazingira magumu sana wazazi au walezi wa watoto hawa. Hivyo, iwapo Wizara itaruhusu watoto hawa kurudia shule, itawasaidia kuimarika kitaaluma na kukomaa kiakili kabla ya kuingia katika hatua inayofuata ya elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa washauri kwa watoto pale wanapohitaji kuchagua masomo (mchepuo). Vijana wengi wamekuwa wanachagua masomo kwa mkumbo tu ama fasheni na baadaye hugundua kuwa hawakuwa wamefanya chagua sahihi. Hii ni kutokana na kukosa ushauri wakati wa uchaguzi wa masomo. Hivyo, ni muhimu Serikali kuitia Wizara kuhakikisha kunakuwa na Walimu washauri kwenye mashule yote ili kusaidia kuwashauri vijana pale ambapo wanahitaji kufanya uchaguzi wa masomo ya kitaaluma.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza viongozi wa Wizara hii ikiongozwa na Waziri Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Naibu Waziri Mheshimiwa Ole-Nasha na Katibu Mkuu Dkt. Akwilapo. Nawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya na mabadiliko chanya yanaonekana kwenye sekte hii ya elimu. Mchango wangu utajikita kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Udhibiti Ubora wa Elimu (Ukaguzi wa Shule), kitengo hiki kipewe rasilimali za kutosha ili kitekeleze majukumu yake, wapewe rasilimali fedha na watumishi. Kitengo hiki kibadilishwe muundo, badala ya kuwa na ofisi ya kanda sasa zifunguliwe kwenye mkoa. Ofisi za kanda ziliweza kudumu wakati idadi ya shule za sekondari ni chache, kwa sasa idadi imeongezeka na hawawezi kukagua shule zillizopo kwenye kanda husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya *TRC (Teachers Resource Centre)*, huko nyuma tulikuwa na program ya *DBSPE (District Based Support to Primary Education)* na kulikuwa na mtando wa *TRC* ambazo zilitumika kutoa mafunzo kazini kwa Walimu wetu. Naomba vituo hivi vitumike kama lengo lake lilivyokuwa hapo awali. Vitengewe fedha za kutosha ili viweze kuendesha semina za Walimu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu iachwe ifanye kazi zake za awali za kutunza mtaala, shughuli ya ufundi wa vitabu na uhakiki wa machapisho yatakayotumika

kwenye mfumo wa elimu ipewe chombo kingine na sekta binafsi iachiwe kwenye uchapishaji.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa kuwa Mtanzania, mwakilishi wa wanawake wa Kilimanjaro Bungeni. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote ya viongozi wa Idara, Vyuo na Shule zote Nchini kwa juhudzi za kutoa elimu bora. Nawapongeza wazazi wote wenye wanafunzi mashulenii na kwenye vyuo ndani na nje ya nchi, pia nawapongeza wanafunzi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwezesha elimu bila malipo na kuendelea kuteua maprofesa kwenye nafasi mbalimbali jambo hili limewafanya vijana wengi sasa waheshimu elimu na ufaulu mzuri, vilaza sasa wameshastuka kuisha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni ufunguo wa maisha, wananchi wakiwa na elimu nzuri, Tanzania ya viwanda itawezekana, maradhi ya kuambukiza yatakwisha, rushwa itapungua au kwisha kabisa, ujambazi utakwisha na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu, Serikali imejiandaa vipi kuwapatia mtaji vijana wanaofuzu vyuo ambao hawajapata ajira ili waanze shughuli za ujasiriamali? Serikali ina mpango gani wa kuwapatia ardhi au maeneo ili vijana kununua viwanja vilivyopimwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya watu wazima, naomba kuisikia Serikali ina mpango gani kuhusu kuendeleza elimu ya watu wazima, yakiwepo mafunzo ya *IT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. LOLESLIA J.M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kushukuru kwa kupata nafasi

ya kuchangia kwenye hotuba hii. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kazi nzuri. Nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeelezea kwa undani utekelezaji wa miradi mbalimbali kitaifa iliyofanyika katika mwaka wa fedha 2018/2019. Nimpongeze sana kwa utekelezaji mzuri uliofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Wizara ni juu ya uimarishaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Serikali ianzishe vyuo vya ufundi vyenye ubora ili watoto wakihitimu wawe na uwezo wa kujajiri moja kwa moja. Kwa kuwa Sera ya Taifa inazungumzia juu ya kuwa na Chuo cha VETA kila Wilaya, nashauri sana sera hii itekelezeke kwa vitendo nikimaanisha kila wilaya ipate Chuo cha VETA chenye ubora. Hii itasaidia sana wahitimu wa darasa la saba na wahitimu wa kidato cha nne wapate ujuzi ili hatimaye wajajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali irudishe mfumo wa zamani ambapo katika shule za msingi na shule za sekondari kulikuwa na elimu ya kujitegemea na shule ziliikuwa na michepuo mbalimbali mfano kulikuwa na shule za sekondari zenye michepuo wa biashara, zingine michepuo wa kilimo, elimu hii ilikuwa inawajengea uwezo mkubwa wanafunzi kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa Chuo cha VETA katika Mkoa wa Geita. Kwa kuwa uhitaji wa elimu ya ufundi ni mkubwa sana, Serikali ione umuhimu wa kukamilisha mapema iwezekanavyo kwani katika Mkoa wa Geita na Wilaya zake hatuna Chuo cha VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika mapema kwa VETA Mkoa itasaidia kupunguza changamoto katika mkoa wetu. Ujuzi wa ufundi stadi unahitajika sana katika kufikia azma ya Serikali ya Viwanda vilevile katika kuongeza kipato na kupunguza umaskini kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika suala la kubadilishwa kwa mitaala bila ya kufanya utafiti wa kina na wala kushirikishwa kwa Walimu ambao ni wadau wakubwa sana. Hili ni suala lililozoleka kwa kipindi sasa, pia mtaala umejikita kuwakaririsha wanafunzi. Kwa mfano kwa upande Zanzibar sidhani kama Walimu wanashirikishwa ipasavyo. Hata hivyo, mitaala ikibadilishwa haipatikani kwa muda muafaka, tukizingatia wanafunzi wa Zanzibar wanafanya mitihani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa *form four* na *form six*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri, Mheshimiwa Ndalichako atuambie hii ni Wizara ya Muungano ama vipi. Kama sio kuna makubaliano yoyote waliyofanya na Wizara ya Elimu ya Zanzibar ama Serikali, ni yapi? Mbona hatuoni ofisi za Wizara ya Elimu ya Muungano kama ilivyo kwa *TRA* na Wizara ya Mambo ya Ndani. Kama zipo, Unguja ipo wapi na Pemba wapi? Je, Waziri ameshawahi kutembelea mara ngapi? Kwa nini Walimu walipwe na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar badala ya kulipwa na Serikali ya Muungano na kuzingatia wanatumwa na Serikali ya Muungano na kwa utofauti mkubwa wa mshahara wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yote hayo si masuala ya Muungano kwa nini Zanzibar tusiachiwe kuwa na mitaala yetu na kutunga mitihani wenyewe? Naomba Mheshimiwa Waziri anijibu masuala haya ili kuondoa ukakasi uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu waongezwe mishahara na kupandishwa madaraja kwa wakati na kupewa stahiki zao kwa wakati. Hii itasaidia Walimu kufanya kazi kwa ufanisi, tukizingatia wanatuzalishia viongozi. Tusikubali wafanye kazi katika mazingira magumu na msongo wa mawazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa uhaba wa Walimu wa sayansi, hiki ni kilio cha nchi nzima, kwa mfano katika wilaya nzima utakuta Walimu wa sayansi wawili mpaka wanne, hii ni hatari kubwa. Waziri atuambie ana mkakati gani

madhubuti wa kupata Walimu wa sayansi. Pia ina mkakati gani wa kuongeza wanafunzi wa kike kwenye masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupatiwa majibu na naomba kuwasilisha.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya elimu haiendani na uhalisia wa elimu yetu ya Tanzania kwa ilivyo sasa. Kwa hiyo naishauri Serikali ilichukue umuhimu wa mabadiliko ya sera ya elimu tuliyonayo hivi sasa ili tuboreshe elimu yetu ya Tanzania kama ilivyokusudiwa mfano, mitaala yetu inaelekeza wanafunzi kukaririshwa na siyo kuelewa na baada ya kuhitimu anafikiria kuajiriwa na si kuendelea na masomo ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Walimu yaboreshwe; kama tunahitaji kuboresha elimu yetu ya Tanzania ni lazima maslahi ya Walimu yaboreshwe kwa kuwa ndio wadau wakuu na muhimu wa elimu kwani suala hili ni muhimu sana kwa kuwaleta morari Walimu wetu na pia Walimu hawa wataachana na mawazo ya *tuition* au kuuza karanga kwa ufupi kuwaza kufanya biashara ndogo ndogo ili kujiongezea kipato cha familia na kusabisha kutofundisha wanafunzi vizuri. Kwa hiyo, naishauri Serikali izingatie jambo hili la kuhusu maslahi ya Walimu kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ibadilishe utaratibu wa michepuko bila kuangalia aina za masomo aliyofaulu bali waangalie alama ambazo mtu (mwanafunzi) amefaulu bila kubagua aina za masomo, kwa mfano, kwa sasa kipaumbele cha Bodi ni kwa wale wanaosoma masomo ya sayansi, ndio wanapewa kipaumbele kulingalisha na wanafunzi wanaosoma michepao mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuboresha elimu ya Tanzania bila kuboresha kitengo hiki cha Ofisi ya Ukaguzi kikitengea fedha za kutosha kama vile usafiri ili waweze kuyafikia maeneo yote yanayotakiwa kukaguliwa kwa mujibu

wa sheria kwa haraka na hii itarafishisha kufikia maeneo yasiyoweza kufikiwa kwa urahisi wakipata usafiri wa uhakika.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Elimu kwa kazi kubwa wanayoifanya. Elimu; iko haja ya kuangalia au kupitia upya mitaala yetu na Sera ya Elimu ili kuwaandaa wanafunzi kwa /eve/mbalimbali kujajiri na sio tu kutegemea kuajiriwa, elimu ya stadi za maisha iwekewe mkazo zaidi. Katika maeneo mengi mwananchi wamejitalidi kujenga mabomba kwa ajili ya madarasa na maabara, Serikali iangalie namna ya kuwasaidia wananchi hawa kumalizia majengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa shule kongwe. Serikali imefanya ukarabati wa shule kongwe za sekondari, zipo shule za msingi kongwe na zenye hali mbaya zinahitaji ukarabati mfano kwenye Jimbo la Korogwe vijijiini ipo Shule ya Msingi ya Madela Ratuba, shule hii ilijengwa mwaka 1952 na haijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Niombee Wizara isaidie ukarabati wa shule hii pia ipo Shule ya Msingi Ng'anzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundu; naiomba Serikai imaarische elimu ya ufundu. Kwenye Jimbo la Korogwe Vijiini tuna Chuo cha Ufundu Mnyuzi, chuo hiki kikipanuliwa, kikapewa vitendea kazi na kuongeza aina ya *course* zinazotolewa kitasaidia sana wanafunzi wanaoshindwa kuendelea na masomo kwa mfumo wa elimu ya shule. Chuo hiki kinaweza kusaidia wanafunzi wengi sana wa Wilaya za Korogwe, Lushoto, Muheza na hata Handeni. Naomba sana Wizara itusaidie kuboresha, kupanua na kuimarishe chuo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo; bado kuna manung'uniko ya baadhi ya Watanzania maskini kukosa mikopo kwa ajili ya kugharamia elimu ya juu. Ni vyema Bodi ya Mikopo ikaangalia hili lakini pia tayari kufanya marekebisho hata katikati ya masomo.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri sana inayofanywa na Bodi ya Mikopo hasa ufuatiliaji wa madeni, lakini pia na huduma nzuri hasa

ofisi yenu ya Dodoma watumishi na meneja wao wanasiliza hongera sana. Hata hivyo, wapo walipaji ambao wameshamaliza mikopo ambayo walikatwa zaidi ya walichokuwa wanadaiwa ambapo sasa ile fedha kurejeshwa inasumbua sana. Nashauri sana inapotokea hivyo wahusika warejeshewe zaidi yao ili waendelee kuwa Mabalozi wema wa Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuna suala la majina kufanana pamoja na kuwa marejesho hufanywa kwa kutumia *check number*, zipo *cases* ambazo kutokana na majina kufanana kunatokea nyakati makato ya mtu A anakatwa mtu B na yale ya B anakatwa A *and vice versa*. Nashauri Bodi iliangalie hili ili kuondoa mtu kukatwa mara mbili na mwagine kutokatwa marejesho. Ahsante.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, usahili wa vyuo; Serikali tumeona imefungia baadhi ya vyuo visivyo na sifa hali iliyosababisha usumbufu kwa watoto, wazazi wamepoteza fedha na wanafunzi wamepoteza muda, pia Serikali imechukua hatua gani kulipa fidia kwa usumbufu huo kwa maana hiyo hadi chuo kianze kudahili wanafunzi kuna uzembe pia kwenye mamlaka zilizotoa kibali, je, hatua zippi zimechukuliwa kwa watendaji walioruhusu vyuo hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlundikano wa wahitimu mtaani ambao hawana ajira, je, Serikali haioni sasa kuna haja kuweka somo la kujitengemea katika vyuo vikuu ili kuwajengea wanafunzi wanaomaliza vyuo kujajiri wenyewe badala ya kusubiri ajira toka Serikalini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya Walimu kutopandishwa mishahara na kupanda madaraja bila kupewa haki za kuongeza mishahara yamekuwa ya muda mrefu. Mazingira magumu ya Walimu kuanzia shule za msingi vijijini yanakatisha tama; Serikali kwa nini isije na mpango wa kujenga nyumba za Walimu kama ilivyowahi kuja na mpango kujenga vyumba nya maabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *motivation* kwa Walimu wanaojitolea tumeona katika vyombo nya habari, shule za kata zimetoa watoto bora, pia shule za kata Walimu ni wachache wanaofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamisho wa Walimu pasipo kulipwa haki na stahili zao; Serikali iliangular hili, Rais amewahi waambia Walimu wasikubali kuhama kama TAMISEMI haina fedha ya uhamisho. Yapo malalamiko bado ya uhamisho wa Walimu *especially* Walimu wa sekondari waliopewa shule za msingi kufundisha, Serikalini iangalie upya malalamko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wengi wapo mijini zaidi kuliko vijijini Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na uwiano sawa wa Walimu; inashangaza unakuta shule za msingi vijijini walimu ni wachache, wanalazimika kufanya kazi ngumu kugawana masomo na wengine kulazimika kufundisha masomo wasio na uwezo nayo, hawajasomea mfano sayansi kwa walimu wa *Arts*. Masomo ya sayansi ndio wanapewa kipaumbele kulinganisha na wanafunzi wanaosoma michepua mingine.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za mifumo ya elimu ya Tanzania limekuwa tatizo sugu ambalo sasa ni bayana kwamba tunahitaji mbinu tofauti, nyenzo tofauti na mikakati tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali haijaamua kutafiti kwa kina kujua nini hasa hitaji la Watanzania kuhusu elimu itakayokidhi. Kipaumbele cha kibajeti kwenda Wizara ya Elimu na Taasisi ya Utafiti ya *COSTECH* kimekuwa dhaifu na kisichokidhi haja kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala yetu inabadilishwa kila siku/kila mara na hivyo kuondoa *consistency* ya mitaala kwa Walimu na wanafunzi. Hata hivyo, kutowashirikisha Walimu katika suala la uandaaji mitaala, inaondoa *ownership* na vionjo na mahitaji muhimu ya ufundishaji na kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016, Serikali ilifanya jitihada kubwa kuhakikisha shule zetu zote nchini zinapata madawati ya kutosha. Ni bahati mbaya sana kuwa kuna shule katika Jiji la Dar es Salaam, licha ya kuwa na msongamano wa wanafunzi madarasani, hazina kabisa madawati. Mfano halisi ni Shule ya Msingi Toangoma iliyoko Kigamboni ambayo ina watoto 540 ambao wanakaa chini. Hili ni jambo la aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya elimu vinavyotolewa katika hatua mbalimbali za ukuaji kielimu. Watoto wetu katika shule za msingi wanaosoma katika mazingira dhaifu sana ikiwemo ukosefu wa vitabu yya ziada na kiada, ukosefu wa huduma za maji, umeme na madarasa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wa hisabati na sayansi, bado ni changamoto. Idadi ya shule imeongezeka wakati hakuna maandalizi kidhi ya Walimu wa kutosha. Tunawaza kuwa Tanzania ya viwanda, lakini ikiwa hakuna Walimu wa kuandaa watoto wetu. Maslahi ya Walimu nayo bado ni kilio kikubwa kiasi kwamba Walimu waliopo kazini wamevunjika moyo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu kubwa, elimu yetu imekuwa ikitolewa kwa nadharia. Elimu muhimu ni elimu kwa vitendo. Tuboreshe maabara, vyuo vya ufundi viongezwe na mazoezi kwa vitendo yawe sehemu kubwa ya mtaala ili mambo yanayofundishwa yaweze kukaa na kudumu katika fikra za wanafunzi wetu kadri wanavyokua na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhamisha Walimu wa Sekondari kurudi kuwa Walimu wa shule za msingi, halikuwa jambo la busara na tumewapeleka kama watu waliodharauliwa na kushushwa thamani na hivyo kutokuwa na moyo wa kufundisha. Kwa hiyo tujue hatujatatua tatizo, tumeliongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kuchangia hotuba ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mwaka jana bajeti ya Wizara ilikua bilioni 1.408 mwaka huu imeshuka mpaka kufikia bilioni 1.357. Upungufu wa bilioni tano, ni kwa nini Serikali inapunguza bajeti ukiangalia maisha yanapanda, shule zinaongezeka na wanafunzi wanaongezeka na mahitaji yanaongezeka zaidi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ya Elimu ya Juu pamoja na bajeti kuongezeka kufikia bilioni 424 ambapo bajeti halisi bilioni 4.3 sawa na asilimia 18 ya bajeti ya maendeleo na mikopo ya wanafunzi asilimia 52 ya bajeti. kuna changamoto ya mikopo ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitambulisho vya Taifa; wanafunzi wanakosa mikopo; kwa hivyo Serikali ishirikiane na *NIDA* ili wanafunzi wanaostahiki wapate mikopo kwa haraka ili wapate kuendelea na masomo mapema. Vile viko vyuo baadhi vina madeni kwa hivyo wanafunzi wanachelewa kupata mikopo hiyo. Kwa hivyo nashauri bodi watumie wanafunzi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya *VETA*, Serikali imepanga fedha kidogo sana. Vyuo vya *VETA* vina mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya vijana wetu kwa sababu vijana wengi wanaomaliza kidato cha nne na wale waliofeli darasa la saba wanataka wajunge na vyuo hivyo ili kupata ujuzi wa ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Serikali ya uchumi wa viwanda leo tukiwa na vijana wengi waliopitia vyuo vya *VETA* watapata ajira. Vile vile tunaishauri Serikali ijenge vyuo vya *VETA* kila wilaya ili vijana wengi wapate kujunga na vyuo hivyo.

Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kwa kazi nzuri sana wanayofanya na timu yake. Kukarabati shule kongwe ni kazi nzuri sana, ajira kwa Walimu wapya, ujenzi wa mabweni kwa watoto wa kike na kutoa elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kuhusu adhabu ya watoto watoro zaidi ya siku 90 itolewe, pia kwa *candidate classes*. Hivyo ilivyo inaharibu jina la shule, nafasi ya shule, maana watoto kama hawa hujitokeza siku za mitihani tu. Kukariri darasa kungezingatiwa ili elimu iimarishwe na ukaguzi wa shule uwe wa mara kwa mara.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema. Namnukuu Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Hayati Nelson Mandela; *"Education is the most powerful weapon which we can use to change our World"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya yanaonesha jinsi gani elimu ilivyo na umuhimu katika maisha ya mwanadamu ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uhaba wa madarasa; kufuatia kuongezeka kwa wanafunzi wa shule za msingi kuanzia *STD I – STD VII*, ufaulu umeongezeka (2019 – 17% *primary schools*) wanafunzi wameongezeka lakini bajeti inayotengwa haiongezeki. Hali hii imepelekea wanafunzi wa Kidato cha I (*Form one*) kukosa madarasa ya kutosha na kupelekea wanafunzi wengine kucheleva kujunga na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kupeleka fedha za ujenzi wa madarasa, bado fedha zinahitajika, bajeti iongezwe na Serikali ihakikishe kila mwanafunzi aliyefaulu anaingia darasani, kwa kujenga madarasa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga ilibahatika wakati wa Ukoloni wa Ujerumanilijengwa Shule ya kwanza Afrika

Mashariki na Kati, shule iliyozalisha pia Walimu waliopolekwa katika nchi jirani, hali iliyopelekea Tanzania kuwa na historia iliyotukuka katika maendeleo ya elimu. Kwa sasa Halmashauri ya Jiji la Tanga inazo shule za Sekondari, *High Schools*, vyuo lakini hatuna Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru Wizara kutupatia Tsh. 1.8 bilioni kwa ukarabati wa *Tanga Technical School*, lakini Tanga hakuna Chuo Kikuu cha Serikali. Naomba Serikali yangu iwaeleze wananchi ni lini itajenga Chuo Kikuu Tanga? Kama itakuwa tatizo ni fedha, mwaka jana niliomba kuipandisha Daraja Galanos High School kwa kuwa inazo "facilities" zote na nyongeza kidogo kuwa Chuo Kikuu. Je, kutoka mwaka jana 2018 hadi leo, Wizara inasemaje kuhusu kuipandisha Galanos *High School*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo ambalo Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu (3) Benjamini Mkapa atakumbukwa ni uanzishaji wa *Capitation Grants*, wa Tsh 12,000 – 10000 kwa kila mwanafunzi kwa mwezi. Kwa sasa kila muda unavyokwenda *Capitation Grants* inapungua. Naiomba Serikali ilieleze Bunge tatizo ni nini?

Kwa masikitiko makubwa Tanzania imepata taswira mbaya katika medani za elimu katika Afrika na Duniani kwa ujumla kufuatia matukio yafuatayo:-

(a) Mwalimu Mkoani Kagera kumpiga hadi kumuua mwanafunzi wa darasa la tatu bila hatia;

(b) Mwanafunzi wa kidato cha kwanza wiki mbili baada ya mauaji ya mwanafunzi STD III alipigwa hadi kupoteza fahamu;

(c) Mwalimu Mkoani Mbeya amemfunga mwanafunzi miguu juu kichwa chini, amempiga hadi amemvunja mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa matokeo hayo hapo juu ni kielelezo kuwa tunao Walimu ambao hawana sifa ya ualimu bali walitakiwa wawe *Field Force Unit* (FFU). Naiomba

Serikali iliambie Bunge, ina mkakati gani wa kusafisha sekta ya ualimu kwa kuwaondoa Walimu makatili? Zamani wanafunzi wakati tukisoma tulipenda tutakapomaliza shule tutakuwa kama Walimu wetu waliokuwa wakitufundisha, lakini siku hizi imekuwa kinyume, wanafunzi hawapendi kuwa Walimu kwa sababu, Walimu siku hizi wamekuwa wajasiriamali, mwalimu anaenda kazini (shule) amebeba deli la *ice cream*, chupa ya ladu, kashata, chipsi za mihogo, ubuyu na binjra. Yote hiyo Mwalimu anataka kuongeza kipato kwa kuwa mishahara midogo, wanasomesha watoto, wanahitaji kodi ya nyumba, bili ya maji na umeme. Hivyo naitaka Serikali iongeze mishahara ya Walimu na itamke ni lini itaanza kuongeza mishahara na lini itamaliza kulipa madeni ya Walimu?

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya elimu kwa maandishi. Hospitali ya MUHAS Mloganzila ilianzishwa kwa madhumuni ya rufaa na pia, *teaching hospital* ilikuwa kujengwe *hostel* na nyumba za Madaktari na wataalam wengine, ili kuwezesha huduma kupatikana kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hii ya Mloganzila imeanza kutoa huduma, lakini Madaktari wanaotakiwa kutoa huduma wanasafiri kutoka makazi yao, wengine maeneo kama Mbagala kwa muda mrefu njiani mpaka Mloganzila. Watumishi hawa hawapewi msaada wowote kama petroli/nauli kuwawezesha wafike kwenye kituo cha kazi. Matokeo yake ni kuwepo kwa upungufu mkubwa wa Madaktari na wataalam wengine wa afya. Ni muda muafaka sasa changamoto hiyo ya makazi ikapatiwa ufumbuzi na kwa muda huu wapatiwe nauli/mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madaktari Bingwa waliofika miaka 65 wanapewa mikataba ya muda mfupi na wakati mwininge hata malipo yao yanasuasua na hawalipwi kwa wakati. Huu ni udhalilishaji wa wataalam wetu waliotumikia Taifa hili kwa muda mrefu. Wanafunzi wanaohitimu kwenye vyuo vikuu vyaa tiba, wengi wao hawana *interest* ya

kufundisha, wengi wanakwenda kwenye *public health* na wengine nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha Madaktari Bingwa waliofikisha umri wa miaka 65 Wizara imeshindwa kuwatumia vizuri. Kwa nchi za wenzetu hawa ndio hazina kubwa ya Wahadhiri, wanafundisha mpaka uzeeni kabisa. Kwa sasa Madaktari Bingwa hawa wamehamia vyuo vya tiba binafsi/kanisa kama Bugando na *KCMC*, wengine wanakwenda nje ya nchi Botswana, Namibia, *South Africa* na kadhalika. Hivyo, muda si mrefu *MUHAS* itakuwa *3rd class teaching institution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, Wabunge wengi waliweka ukomo wa wataalam bingwa kuwa miaka 65, naishauri Serikali, ili kutumia hazina hii ya wataalam wapewe angalau mikataba ya miaka miwili-miwili na kulipwa *gratuity* kila wanapomaliza miaka yao miwili. Utakubaliana nami kwamba, umri wa kuishi umeongezeka, hivyo mtaalam bingwa wa miaka 65 bado ana nguvu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia hoja hii naomba kutoa shukrani kwa matumaini yanayoanza kuonekana kwa kwanza, kukarabatiwa kwa *FDC* ya Tarime. Hiki chuo kinasaidia wanafunzi toka Tarime, Ranya na hatu baadhi ya kata za mpakani za Serengeti, hivyo ni bora kile chuo kingefanywa kuwa chuo cha *VETA*. Pia napenda kushauri baada ya ukarabati basi viweze kupatiwa vifaa vya kisasa vya kujifunzia, karakana ya kisasa na vifaa vingine. Hii itaongeza ufanisi kwenye utoaji wa mafunzo kwa wanafunzi wetu na wakufunzi kwa ujumla. Vyuo hivi vya Maendeleo ya Wananchi vikitoa mafunzo yenye tija vitasaidia sana kutoa vijana watakaosaidia katika soko la ajira na huduma kwa Taifa letu kwani wengi watajajiri na kuajiri Watanzania wengi. Ikumbukwe huchukuliwa vijana waliokaza udahili wa *form one* na wale ambao wanakosa udahili wa *form five*. Ikizingatiwa

changamoto za nafasi hizo sanjari na ufaulu wa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kujuu *statusya* ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Tarime ambayo ni ya kidato cha tano na cha sita tu na ina mikondo mingi sana. Kwa kweli, ni shule ya tangu mwaka 1970, hivyo inahitaji kukarabatiwa na kuwa na hadhi ya aina yake maana shule za hivi ni chache sana Tanzania na lazima tuweke mazingira mazuri kwa wanafunzi ya kujifunzia. Pia, shule hii haina gari la dharura, mfano, mtoto akiugua. Tulikuwa na gari aina ya *Land Cruiser*, lakini lilichukuliwa kwa mazingira ya kutatanisha na hadi leo halijarudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alitembelea jimboni kwangu na kuahidi kutupatia fedha kwa ajili ya kujenga shule ya bweni kwa watoto wa kike. Tayari tuna eneo kwenye kata mbili, ningependa kujuu kama mwaka huu wa fedha tumetengewa fedha za kuanza ujenzi na ni kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuna shule mbili za kata ambazo zipo tayari na miundombinu ya kuwa *high school* mchanganyiko. Tumeomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ambayo ni shule ya Mogabini na ile ya Nyandoto. Je, lini tutapata hizo fedha, tumeshuhudia Halmashauri nyingine zinapata na sisi Halmashauri ya Mji tunakosa, ilhali tuna mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kusimamia elimu ya msingi na sekondari lazima tuboreshe mazingira ya kujifunzia kama vile madawati, madarasa, vitabu, maabara, maktaba, motisha kwa Walimu wetu kama vile kuwapunguzia *workload* kwa kuajiri Walimu wa kutosha, ili waendane na uwiano pendekewa, wapewe malipo ya ziada. Unakuta Walimu watatu shule nzima mlundikano wa wanafunzi zaidi ya wanafunzi 200 au 150. Walimu wapandishwe mshahara, walipwe posho ya nyumba kama hawana nyumba katika maeneo ya shule, maana upungufu wa nyumba za Walimu

ni zaidi ya 80%, walipwe madeni yao ya likizo na wapandishwe madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni kuhusu mikopo ya elimu ya juu; wanafunzi wengi wanaachwa kwa kigezo cha kuwa, alisoma *private*, lakini pia kuna wengine wamesoma shule za kawaida, lakini wanakosa fursa ya kusoma, hii si sawa na inajenga matabaka kwenye jamii. Ikizingatiwa huu ni mkopo. Ni muda sasa Serikali itenye fedha za kutosha kuwapa mikopo Watanzania wote wenye sifa. Maana Rais wakati wa kampeni 2015 aliahidi akiwa Tabora kuwa, kila Mtanzania mwenye sifa ataenda chuoni.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote natoa pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Naibu Waziri Mheshimiwa William Ole Nasha, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kazi nzuri na kwa hotuba hii nzuri iliyosheheni miradi mingi iliyo tekelezwa mwaka huu 2018/2019. Baada ya pongezi hizi naomba sasa nichangie hoja kwa kutoa maoni na ushauri wangu kwa Serikali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miundombinu; ukarabati wa Taasisi za Elimu; naishauri Serikali isilishie kukarabati vyuo na shule kongwe tu bali itenye fedha za ukarabati wa shule zake zote kila mwaka wa fedha. Kwa suala la shule kongwe, Wilayani Longido sisi tuna shule kongwe za msingi zilizojengwa tangu enzi ya ukoloni. Kwa mfano tuna shule ya bweni ya msingi ya Longido ambayo ilijengwa mwaka 1947 na majengo yake yamekuwa chakavu, hivyo inastahili kukarabatiwa na Serikali. Hii ndiyo shule ya msingi aliyosoma hayati Edward Moringe Sokoine, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mitaala; Taasisi ya Elimu Tanzania; suala la Mitaala, Miongozo na Vitabu; Serikali ijumuushe shule za awali katika mipango yake ya kuandaa mitaala, miongozo na kuchapa vitabu vya kiada na rejea. Msingi wa elimu bora huanzia ngazi ya elimu ya awali na si darasa la kwanza na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundji Stadi (*VETA*); nashauri Serikali iongeze kasi ya kuanzisha *VETA* katika kila wilaya nchini. Kwa kuwa, Wilaya ya Longido hakuna chuo chochote cha Serikali na tuna ardhi ya kutosha na kwa sasa tuna maji safi na salama ya kutosha pamoja na umeme Makao Makuu ya Wilaya na vijiji jirani, naikaribisha Wizara watujengee *VETA* ya Taifa inayolenga fani zifuatazo: Mifugo (*livestock production & livestock products*), wanyamapori (*wildlife nature conservation & tourism*), madini (*small scale mining skills*), huduma za kitalii (*Hospitality & Hotel Management*), Uashi na useremala, TEHAMA na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na uanzishwaji *VETA* kila wilaya, nashauri Serikali ianzishe chuo mahsusini cha Walimu wa sayansi, ili kuziba pengo la uhaba mkubwa tulionao wa Walimu wa sayansi katika shule zetu za sekondari na vyuo. Kwa kuwa, sisi Longido tuna ardhi, maji na umeme naikaribisha Serikali ijenge chuo hicho Wilayani Longido na kiitwe *Tanzania Science Teachers' College*. Chuo hiki kitakuwa ndio kiwanda cha kuzalisha Walimu wa fani zote za sayansi kwa ajili ya mahitaji ya nchi yetu katika ngazi zote husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; naipongeza Serikali kwa ongezeko la wanafunzi wanaopewa mikopo ya elimu ya juu. Naomba kuishauri Serikali itoe elimu ya jinsi ya kuzaja fomu kwa usahihi katika kila shule yenye wanafunzi wanaostahili kupewa mikopo ili kuondoa tatizo lilitopo la baadhi ya wanafunzi wenyе sifa kukosa mikopo kwa sababu ya kutojua jinsi ya kujaza fomu za maombi kwenye mitandao kwa usahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba niangalize Serikali kuhusu suala la uwepo wa vijiji vichanga nchini ambavyo bado havina shule za msingi sambamba na huduma zingine muhimu za kijamii kama zahanati, barabara, mawasiliano ya simu, maji na umeme. Kwa mfano, katika Wilaya ya Longido yenye jumla ya vijiji 49, tuna vijiji kadhaa ambavyo havina shule na hivyo, kuna idadi kubwa ya watoto ambaao hawaendi shule. Baadhi ya Vijiiji hivyo katika Wilaya

ya Longido ni pamoja na Engusero (Kata ya Naondoto), Nadaare (Kata ya Iloirienito), Wosiwosi (Kata ya Gelei Lumbwa), Leremeta (Kata ya Sinya) na Loondolwo (Kata ya Meinigoi). Naiomba Serikali itenge fedha za kuwaunga mkono wananchi kwa kuwachochaea kuanzisha shule za awali na msingi katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi yetu inaingia kuwa Tanzania ya viwanda bado upande wa elimu bajeti inazidi kushuka, sijui Serikali inajipangaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie suala la Walimu, Walimu ni wachache sana hadi leo hili zipo shule zina Walimu wachache sana ukilinganisha na takwa la elimu. Walimu hao hao wachache hawana maandalizi mazuri ya kufundishia; miundombinu si rafiki, maeneo wanayoishi, madarasa yenyewe na hasa shule za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya Walimu wanayoidai Serikali, kupandishwa daraja, nauzi za likizo na marupurupu mengine kwa kazi ngumu kama ya Mwalimu kumfundisha mwanafunzi aelewé kile anachojuja yeye, halafu haki zake za msingi halipwi, atakuwa na moyo gani wa kufanya kazi hiyo. Naomba Waziri anapokuja kuhitimisha aniambie kwa mwaka wa bajeti 2019/2020 Wizara yake imejipangaje kumaliza madai ya Walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kwa kuwa, kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaomaliza darasa la saba imefikia milioni moja kwa mwaka, wanaochaguliwa kujungu na kidato cha kwanza ni laki tatu tu, laki saba wanabaki, umri wao ni mdogo ni miaka 12 – 14, hawawezi kufanya kazi ya uzalishaji. Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kundi kubwa hili haliishii mitaani, kunakuwa na vyuo vya VETA kila wilaya ili kupunguza ongezeko la wahalifu nchini.

MHE. ZAINABU M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako Mbunge, pia Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa pamoja na wasaidizi wake kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuyatekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, wanafunzi wanaoenda kusomea fani ya ualimu wawe na vigezo vinavyohitajika kitaaluma, kwa sababu baada ya mafunzo ya ualimu wataenda kutoa elimu kwa watoto na jamii. Hivyo isiwe mazoea kwa mwanafunzi aliyepeata *division III*/au *IV*ndio aende kusomea kozi ya ualimu. Hivyo nashauri Serikali izingatia hili wachukue wanafunzi waliofaulu kuanzia *division one* na *two*. Ili kuleta tija katika elimu.

Naishauri Serikali ili kuweka msingi mzuri katika elimu mitaalaa iwe na masomo ya ziada kama ilivyokuwa katika miaka ya 1980, mfano Morogoro sekondari mitaalaa yetu ilikuwa unasoma masomo ya ziada (*woodwork, cookery, needle work, metal work, fineart*) pamoja na masomo yote ya kawaida. Hivyo mwanafunzi ndani ya miaka minne anakuwa na msingi wa kupata mafunzo ya masomo ambayo baada ya hapo kama hakupata nafasi ya kuendelea na kidato cha V – VI, atakuwa na uwezo wa kujajiri kutokana na masomo ya ziada aliyosomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali irudishe mitaalaa ile katika shule zetu za sekondari kuanzia kidato cha I – IV. Naishauri Serikali fedha zifikishwe kwa wakati ili kuweza kutekeleza majukumu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uhaba wa zana za kufundishia *teaching aids*, katika shule zetu. Nashauri Serikali itenye fungu la kutosha ili shule zetu ziwe na zana za kufundishia ili mwanafunzi aweze kuwa na uelewa zaidi katika somo analofundishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uhaba wa nyumba za walimu hususani maeneo ya vijijini. Hivyo nashauri Serikali ijenge nyumba za walimu maana hutembea umbali mrefu

sana kutoka walikopanga nyumba zao hadi kufika katika shule afundishayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwa na wakaguzi mara kwa mara katika shule zetu, nashauri Serikali iwe na vitendea kazi vya kutosha mfano magari ili kuwawezesha wakaguzi kufika kwa urahisi katika maeneo husika ya shule na sio kutoa taarifa ambazo si za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa walimu hususani katika shule zilizopo vijijini. Naishauri Serikali iweke miundombinu mizuri na motisha nzuri kwa walimu wanaofundisha shule za vijijini ili kuweza kuwavutia walimu wengi kufundisha vijijini na sio kukimbilia mijini kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iweze kutoa semina mbalimbali kwa walimu ili kuweza kuwajengea uwezo katika sekta hii na kujua wajibu na majukumu yao ya kila siku. Pia waweze kuwalea wanafunzi kwa maadili mema ya kiutamaduni wa mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa vyumba vya madarasa, hii hupelekea mlundikano wa wanafunzi katika chumba kimoja cha darasa, na humuwia vigumu mwalimu kuwafikia kuwafundisha wanafunzi wengi kwa wakati mmoja. Nashauri Serikali ijenge vyumba vingi vya madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iongeze mishahara kwa walimu na wakufunzi ili waweze kutoa elimu kwa usahihi. Maana wengi wanakuwa na msongo wa mawazo na kushindwa kufundisha vizuri wanafunzi wetu na matokeo yake wanafunzi hufeli katika masomo yao. Wakiongezewa mishahara na posho mbalimbali watahamasika kufundisha kwa weledi mkubwa zaidi na kupelekea wanafuzni kufaulu na kuwa na Taifa lenye watu waliopata elimu bora.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, je ipi sera ya elimu yetu ya sasa na inalenga kuandaa wahitimu wenye weledi gani?

- (i) Ngazi ya elimu ya msingi?
- (ii) Ngazi ya kidato cha IV?
- (iii) Ngazi ya kidato cha VI?
- (iv) Ngazi ya chuo kikuu?

Sera ya nchi yetu inakidhi kweli mahitaji ya soko? Mbona kama kuna ombwe la maandalizi? Rejea idadi kubwa ya wahitimu wasio na ajira katika ngazi zote walizohitimu. Kwa nini tusibadilishe mtizamo wa elimu yetu? Nashauri kuitishwe mjadala wa kitaifa, tupate maoni mbalimbali juu ya mfumo wa elimu uliopo na kama kweli bado unakidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini tathmini ya Serikali na mfumo wake wa elimu ya 7.4.2? Ukillinanisha na Kenya ya 6.2? Serikali haioni umuhimu wa kupunguza muda mrefu wa vijana kukaa elimu ya msingi wakati haiwapi ujuzi *specific*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ione kuwa huu ni wakati muafaka wa kufufua elimu za kujitegemea shulenii kwa nguvu na kasi ile ile kuondoa changamoto ya kuzalisha watoto wasio ajirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu juu ya mfumo wa mitihani ya mwisho kama kipimo cha ufaulu/daraja la kuvuka hatua nyingine iangaliwe upya. Mfumo utengenezwe vizuri ili kuwe na mfumo wa kutathmini ufaulu kwa kuwa kipimo cha mitihani wa mwisho hakiakisi uelewa wa mtoto/mwanafunzi; hii ni kwa sababu siku za mitihani zinakuwa *fixed/tension* ya mitihani na mambo mengine yanaweza kupelekeea mtoto *ku-fail* wakati amekuwa akifanya vizuri katika kipindi cha kujifunza. Nashauri badala ya *final exams* tujikite kwenye *collective assessment and final exams* iwe sehemu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa masomo mengi kwa wanafunzi katika ngazi zote, kuanzia darasa la kwanza hadi la saba. Hii inaweza kuanza kama *proposal*/na

ingependeza ikapendeza kufanyika kwenye *block* yote ya EA.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia mambo machache kwenye hoja hii iliyopo mezani, mahususi nikirejea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza na hoja ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Bodi hii imeshindwa kutambua wakopaji wake na wako wapi kwa sababu bodi haina mfumo wa kuwatambua ili kupata marejesho yake. Thamani ya deni hilo ni shilingi triliioni 4.6, rejea ripoti ya *CAG* 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu imeshindwa ujenzi katika Chuo cha Ualimu cha Ndala licha ya bajeti ya shilingi bilioni 46 kutengwa na wizara. Niombe Serikali ikaekeleze ujenzi wa chuo hicho cha Ndala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuchangia kuhusu ukaguzi maalum wa Chama cha Walimu (*CWT*). *CAG* alifanya ukaguzi maalum *CWT*na kuanika ubadhilifu mkubwa katika Chama cha Walimu. *CWT*ilifanya matumizi ya shilingi bilioni 26.8 bila kuzingatia bajeti; pesa hizi zilichepushwa kutoka kwenye matumizi husika na kufanya matumizi mengine. Malipo ya shilingi bilioni 11.5 yalifanyika bila uambatanisho toshelezi. Matumizi hayo hayakuwa na vielelezo kuthibitisha matumizi hayo, hivyo mkaguzi alishindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Malipo ya shilingi bilioni 3.3 yalifanyika bila kuidhinishwa na Katibu Mkuu na mweka hazina wa Chama cha Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia suala la Tume ya Huduma za Walimu (Fungu 40). Tume hii ilifanya malipo yasiyo ya kawaida, shilingi milioni 721 kulipa posho, *overtime* na safari hewa.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo; ni jambo lenye tija kuunganisha taarifa za Bodi

ya Mikopo na *TASAF*, ili kuondoa utata au usumbufu kwa walengwa wakati wa uombaji wa mikopo hiyo. Kwa kuwa watu wanaohudumiwa na *TASAF* wanakuwa na namba, ni muhimu wapewe namba na barua ya kuwatambulisha wakati wa kuomba mikopo ili kuondoa utata huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kutoa ushauri huu ni kuwa kuna wengine hufiwa na wazazi wao na kisha hupata kibali cha kifo. Kwa hiyo basi, ni vyema kibali cha kifo kitambulike wakati taratibu nyingine za kufuatilia cheti zinafanyiwa kazi kwani elimu ni haki ya kila mtoto wa kitanzania.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba mkubwa wa miundombini katika shule za msingi na sekondari nchini, bado kuna changamoto katika Sekta ya Elimu hususani katika miundombini na hii inapelekea kushuka kwa ufaulu na kusababisha walimu kuishi katika mazingira magumu na huku ni jukumu la Serikali kuhakikisha inatatua kero zao, hakuna Elimu bila walimu hivyo Serikali hii itatue kero ya nyumba bora kwa walimu wa Shule ya Msingi na Sekondari mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabweni, Shule ya Sekondari Mpanda *Girls* mpaka sasa haina uzio na shule inayotegemewa na wananchi kwa ufaulu wake, shule hii iko nje ya mji kidogo na imezungukwa na shughuli za kiuchumi stendi ya malori na mabasi makubwa soko na kilimo je? Hii shule ni ya wasichana kuzungukwa na shughuli hizi na pia shule haina uzio hamuoni kuwa Serikali inahatarisha usalama wa watoto na mimba kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viboko, shule hii, imezungukwa na bwawa na mito wakati wa usiku viboko wamekua wakizunguka kwenye maeneo ya mabweni na kuleta hofu kwa wanafunzi. Naiomba Serikali ione namna ya kutatua jambo hili kabla halijaleta madhara.

MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu kwa maandishi

katika wizara hii. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri sana wanayoifanya na kuitendea haki wizara hii ambayo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Joyce Ndlichako anastahili pongezi kubwa kwani mwenye macho haambawi tazama na mwenye masikio haambawi sikia. Changamoto nyingi zilizokuwepo zimepungua kwa kiwango kikubwa lakini pia elimu imeboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri na kubwa ambazo zimekuwa zikifanyika bado kuna changamoto ambazo zinaweza kuboreshwa mfano kurudisha michezo, kilimo na mchakamchaka mashulenii haya huko miaka ya nyuma yalikuwepo na matokeo mazuri yallionekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara sasa iandae mfumo mzuri wa kuwaandaa wanafunzi kisaikolojia kwani wanafunzi wengi wanaomaliza akili yao ni kupata ajira ambazo kupatikana si rahisi sana kiasi kwamba akikaa miaka mingi nyumbani bila kupata ajira anakata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba katika mchango nitoe salamu kutoka kwa wananchi wa Kalenga walionituma nimfikishie salamu za kushukuru sana Waziri wa Elimu Mheshimiwa Profesa Joyce Ndlichako kwa kuikumbuka shule ya msingi Kongwe ya Kalenga kwa kuwajengea maboma mawili ya madarasa yenyeye madarasa manne na uazio wa kuizunguka shule na matundu 16 ya vyoo pamoja na kukarabati nyumba za walimu ambazo zilikuwa zimechakaa kabisa na kushindwa kukaliwa na walimu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu sikiu kuwapatia Wizara ya Elimu pesa yote iliyoombwa katika bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii sambamba na kumpongeza mtoa hoja kwa wasilisho zuri lenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Mafia kwa kushirikiana na Mbunge wao, Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau wamefanikiwa kujenga Chuo cha Ufundu (*VETA*) na ujenzi wa Chuo hicho umekamilika takribani miaka minne iliyopita. Chuo hiki hadi sasa hakijapata usajili kutoka mamlaka husika kwa zaidi ya miaka miwili na nusu sasa. Moja ya hoja iliyotolewa ilikuwa ni kukosekana kwa umeme katika Chuo hicho. Ninayo furaha kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa suala la umeme limeshatatulika baada ya wakala wa umeme vijiji kufikisha umeme katika chuo hicho na unawaka hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mafia ina shule sita za Kata. Kati ya shule hizo, zote zina tatizo la *hostel* za wanafunzi ukiondoa shule moja tu, shule ya sekondari ya Kitomondo. Tunatambua changamoto ya ufinyu wa bajeti. Tunaiomba Serikali itusaidie Mabweni ya wanafunzi kwa shule za Kirongwe, Baleni na Micheni. Shule hizi zina dahili wanafunzi kutoka maeneo ya mbali hususan maeneo ya pembezoni kwenye visiwa vidogo vidogo vya Juani, Chole na Jibondo. Inawawia tabu kupanda vyombo vya Mashua na Boti kwenda na kurudi majumbani ukizingatia nyakati za pepo kali za Kusini na Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Kwanza nakupongeza sana kwa hotuba nzuri yenye ufanuzi mzuri wa sekta mbalimbali za Wizara yako. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja, naombaa kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa walimu; Wilaya ya Mpwapwa ina upungufu mkubwa sana wa walimu hasa

shule za sekondari za kutwa na hii inachangia kiasi kikubwa elimu kushuka katika Wilaya yetu ya Mpwapwa. Naishauri Serikali kupeleka Walimu wa kutosha katika Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa shule ya sekondari ya Mpwapwa na Chuo cha Ualimu Mpwapwa; kwanzna naishakuru sana Serikali kwa ukarabati uliofanyika katika Taasisi hizo mbili (Mpwapwa *High school*/na Mpwapwa *TCC*). Pamoja na ukarabati huo, nyumba za walimu ziliachwa na zina hali mbaya sana na zingine hazijafanyiwa ukarabati muda mrefu mpaka zimeweka nyufa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati nyumba za walimu, Chuo cha Walimu Mpwapwa na Mpwapwa *High school* ambayo ni shule kongwe hapa nchini ilianza mwaka 1926.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri katika shule ya sekondari Mpwapwa na Chuo cha Ualimu Mpwapwa; kwa usafiri ni muhimu sana katika Taasisi, Mpwapwa *High school* yenye wanafunzi zaidi ya 600 hakuna Gari kwa ajili ya huduma kwa wanafunzi na walimu. Pia Chuo cha Walimu Mpwapwa chenye wanachuo zaidi ya 1000 hakina Gari kubwa kwa ajili ya huduma ya Wanachuo. Je, kuna mpango gani wa kupeleka Magari katika Taasisi hizo mbili, Mpwapwa *High school* na Mpwapwa *TTC*? Pia Serikali ina mpango gani wa kukibadilisha Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu cha Mpwapwa kuwa chuo cha ufundi (*VETA*) kwa Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa, hakuna Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukushukuru wewe na Mwenyezi Mungu, Mungu muweza wa yote kwa kuniwezesha kusimama na kutoa mchango wangu katika sekta hii muhimu ya elimu, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono kwa sababu Waziri Profesa, Mama Ndlichako, Naibu Waziri

Ole Nasha, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Ave Maria, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Wahadhiri, walimu na wafanyakazi mnaofanya kazi nzuri sana kwa bidii na maarifa, wavumilivu, waaminifu na kwa uadilifu mkubwa na pia taarifa imeandaliwa vizuri, ina *data* za kutosha zinatuonyesha wapi tulikotoka na wapi tulipo na wapi tunakwenda, ninawapongeza sana. Naomba tuendelee kuwatia moyo, niendelee kuwatia moyo, endeleeni kuchapakazi, tuna imani kubwa nanyi na Mungu atawabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara ya Elimu; Utekelezaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo ya Matumizi ya Kawaida; pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya kupeleka fedha za mishahara, matumizi mengineyo ya fedha na miradi ya maendeleo kwa kiwango cha asilimia 60 ya Fungu Namba 46, naungana na uchambuzi wa Kamati kuwa lipo tatizo la upelekaji wa Fedha za miradi ya maendeleo ya fedha za matumizi ya kwaida.

Mfano, asilimia 37 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara ya Fedha ambayo haikidhi kutekeleza kazi zilizopangwa na asilimia 62.8 haitoshi kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa na hivyo basi kusababisha kushindwa kulipa fedha za nyumba za Wahadhiri, kukamilisha miradi ya maendeleo kama ilivyokusudiwa. Mfano, Chuo Kikuu Kishiriki cha *DUCE* na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kama ambavyo taarifa ya Kamati imeeleza. Ushauri:-

(a) Upelekaji wa fedha; naomba niungane na maoni yaliyotolewa na Kamati kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya sekta hii zipelekwe zote kama zilivyopitishwa na Bunge kabla ya mwaka wa fedha haujamalizika.

(b) Kubuni vyanzo vya mapato; pia nichukue nafasi kushauri Taasisi za Wizara hizi kuendelea kubuni vyanzo vya ndani ili kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli za uendeshaji kama ilivyofanyika katika vyuo vya *DUCE* na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kama ambavyo Wajumbe wa Kamati tulijionea na leo taarifa imewasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Tekonolijia; ilani ya CCM, ukurasa wa Ibara ya 52, Kifungu cha (k)(2) imetamka bayana kuwa katika kipindi cha 2015-2020, Serikali ya CCM itakamilisha ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo, Sayansi Shirikishi cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (Butiama) lengo ikiwa ni kuenzi wazo la Baba wa Taifa ambaye ye ye siyo kutoa wazo ye ye na Ndugu zake, Watima walitoa eneo tena bure wakaanza kujenga miundombinu ya maji, Bwawa la Kialano n.k.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupongeza Serikali kwa kazi zinazoendelea kama ambavyo Waziri ameeleza kwenye ukurasa wa 85 wa hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyakiti, maswali - Hati ya Kiwanja; hati ya kiwanja inapatikana lini? Na kiasi cha fedha kilitengwa na ujenzi unaanza lini? Naomba Waziri utakapokuwa unajibu tusaidie kujua ili wananchi wa Wilaya ya Butiama (Mara) na Watanzania kwa ujumla wasikie kwa sababu lengo la CCM la kuanzisha Chuo hiki siyo tu ni kwa ajili ya kumuenzi Mwalimu pia ni kuongeza wataalam katika sekta ya Kilimo na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bila malipo; napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wanawake ninaowaalika kuleta shukurani nyingi kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha za zaidi ya kiasi cha milioni 23 kwa ajili ya kugharamia elimu na kuwezesha watoto wa familia za wanawake na watanzania wanyonge, watoto hao kupata fursa ya kusoma bila vikwazo. Pamoja na pongezi hizo, naomba kushauri yafuatayo:-

(a) Mpango endelevu wa elimu bila malipo - Serikali tubuni chanzo cha mapato cha uhakika cha kutekeleza mpango huu kama ilivyo kwenye umeme vijiji na kwenye barabara.

(b) Ujenzi wa miundombinu; Serikali ishirikiane na wananchi kujenga miundombinu kama vile madarasa,

mabweni, nyumba za walimu, vifaa vyta kufundishia na vyta kujifunzia, kuendelea kuongeza walimu hasa walimu wa masomo ya sayansi, upatikanaji wa madawati n.k kwa sababu kwa sasa kuna baadhi ya shule darasa moja na wanafunzi 60 mpaka 200.

(c) Vyuo vyta *VETA*; naipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga vyuo vyta *VETA* katika Mikoa na Wilaya mbalimbali hapa nchini. Nashauri tuendelee kuongeza miundombinu ya vyuo vyta *VETA* ili viwe na uwezo wa kuwapokea vijana wengi zaidi kuliko ilivyo sasa.

(d) Serikali iendelee kukamilisha ujenzi wa vyuo vyta *VETA* katika Wilaya zote hapa nchini na kuanzia tuanze na wilaya zenyetani miundombinu ya majengo, vilivyokuwa vyuo vyta wananchi kama vile Wilaya ya Bunda, Kisangwa, Chuo cha Wananchi-Bweri, Musoma Mjini n.k.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoro shulenii na mimba za utotoni; pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Bunge kutunga Sheria kali kwa wale wote watakaomzuia mtoto kusoma kwa namna yoyote, hili tatizo la utoro limeendelea kuwa kubwa sana pamoja na mimba za utotoni. Ili kupunguza utoro shulenii, suala la chakula kwa watoto liwekewe mpango maalum unaotekelzaka. Ushauri wangu kwa Serikali, naomba suala hili la utoro mashulenii Serikali na jamii tulivalie njuga kwa kutumia Sheria hiyo tukakomesha utoro na mimba shulenii kwa sababu upo ulegevu wa utekelezaji wa Sheria hiyo kwa kisingizo hakuna ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Bodi ya Mikopo; naomba kumshukuru Rais wetu kipenzi cha Watanzania kwa kutambua changamoto ya fedha za mikopo na kufanya sua la kutoa fedha za mikopo kuwa ni mambo ya vipaumbele katika mipango ya Serikali ya kugawa rasilimali ya Taifa. Jambo ambalo limewezesha sasa Bodi ya mikopo kutoa mikopo kwa vijana wetu 1,227,583 mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 424,758,636,617.00, kukusanya madeni ya shilingi 128,076,510,388.48 sawa na asilimia 81.2, kati ya fedha

1577 zilizokuwa zinadaiwa. Pongezi nyingi sana. Pamoja na pongezi naomba kushauri yafuatayo:-

(a) Naomba Serikali iwe na mipango mizuri hata ya kujidhamini katika Mabenki kuititia mtaji tulionao ambao Serikali imekwishautoa ili suala la mkopo liwe kwa vijana na watoto wetu wote wenye uhitaji.

(b) Utaratibu wa elimu za ujazaji fomu ya maombi ya mikopo itolewe kwa watoto wote waliopo kwenye shule za sekondari na elimu kuititia mitandao mbalimbali ili kutoa fursa kwa vijana na wazi kuwa na uelewa wa pamoja juu ya vigezo vyta kupata mikopo na utaratibu wa kujaza fomu na kuzifikisha katika Taasisi kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu katika vyuo vikuu; pamoja na kazi nzuri inayofanyika ya kujenga miundombinu katika vyuo vyetu hapa nchini. Ningependa kujua Je, Serikali imejipangaje kujenga Mabweni katika vyuo vya ufundi vya Vyuo Vikuu ili kuondokana na changamoto inayokabili vijana wetu hasa wasichana kushindwa kulipa kodi katika nyumba wanazopanga, kutembea umbali mrefu n.k. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga miundombinu, barabara na majengo yenyehadhi ya jina la Chuo – Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Wakuu pamoja na watumishi wote wa wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Wizara kwa maboresho ya utendaji wa kazi hususani katika maeneo yote yanayohusu elimu, hii ni pamoja na Taasisi zote za Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maneo muhimu yanayochangia ufaulu ni pamoja na kuwa na Maktaba za

kisasa zenye vitabu. Nalisema hili kwa kutolea mfano wa maktaba ya kisasa iliyojengwa kwa ufadhili wa nchi hisani ya China katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hakka naipongeza Nchi ya China na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyakiti, nashauri sana kuwa na maktaba kama ile katika vyuo vyote. Najua ni ghamara lakini katika elimu huwezi kuepuka suala la ghamara. Tuanze kidogo kidogo katika vyuo vyote hii itasaidia sana kuzalisha wataalam wazuri na kuimarisha elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuru Serikali kwa kutupatia Gari kwa ajili ya udhibiti wa elimu katika jimbo langu kwani Jimbo la Kilindi ni mionganoni mwa maeneo yenye changamoto sana kwa sababu ya ukubwa wake lakini miundombinu isiyoridhisha. Pamoja na kutupatia Gari tunayo changamoto kubwa nayo ni kukosa Dereva lakini hatuna kasma ya matengenezo ya Magari na mafuta pia kwa maana kifungu cha mafuta hakipo. Niishauri sana Serikali, ili tija ipatikane ya uwepo wa chombo hiki pamoja na stahiki za watumishi na eneo hili. Aidha, hatuna jengo kwa ajili ya watumishi, tunalo eneo naiomba sana Serikali itujengee Ofisi za Watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze juhudhi za Serikali katika kuhakikisha ujenzi wa vyuo vya VETA katika ngazi za Mikoa na pia katika ngazi za wilaya. Vituo hivi vitatoa tija kwa vijana wetu katika kutatua changamoto ya ajira kutoa ufundi mbalimbali lakini dhima ya viwanda vya kati haitofanyiwa bila kujenga VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 43 wa hotuba yako kipengele (vii) nimeona jitihada za Serikali za maandalizi ya michoro na zabuni kwa ajili ya ujenzi wa vyuo viwili vua ufundi stadi vya Wilaya ya Kilindi na Karagwe. Hili jambo kubwa sana Kilindi wanashubiri ujenzi wa VETA kwa hamu kubwa sana kwani ni mionganoni mwa maeneo ambayo yana vijana wengi ambaao hawabahatiki kuendelea na masomo lakini ni mionganoni mwa maeneo yenye fursa za madini, jamii ya wafugaji pia hivyo kupata chuo cha VETA

kitasaidia sana vijana wetu. Niiombe sana Serikali iongeze jitihada za ujenzi kama inavyoahidi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwanza naomba kukujulisha kuwa binafsi ni mhitimu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere zamani kivukoni. Mheshimiwa Waziri hebu tusaidie kutatua hoja hii, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea Chuo cha MNMA akiwa ameongozana na wewe Waziri na kukuagiza kuwa wizara ifanye mchakato wa kukipandisha hadhi chuo hiki na kuwa chuo kikuu. Je, mmefikia wapi hadi leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku mbili tu baada ya agizo lile la Waziri Mkuu, nikauliza swali la msingi hapa Bungeni kuhusu hoja hiyo hiyo ya kupandisha hadhi chuo hiki lakini majibu ya wizara yako yalionyesha kutokubaliana na hoja ya kukipandisha hadhi chuo hiki na kuwa chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nadhani ni muda muafaka sasa chuo hiki kipewe hadhi ya kuwa chuo kikuu ili kuendeleza fikra pepu za hayati Mwalimu Nyerere. Nchi za wenzetu waasisi wa mataifa yao wamewaenzi kwa kuvipa majina ya vyuo vyao mfano mzuri ni *Nelson Mandela University, Kwame Nkrumah University, Kenyatta University, MOI University etc.* naomba chuo hiki kwa umuhimu wake kipandishwe hadhi kuwa chuo kikuu.

Jambo la pili ni shule ya Sekonari Mchinga kupandihswa hadhi na kuwa shule ya kidato cha tano na sita. Wilaya yetu ina shule moja tu ya kidato cha V na VI nayo ni Maliwa Sekondari iliyopo Jimbo la Mtama. Lakini Jimbo la mchinga halina shule ya kidato cha V na VI hata moja. Tafadhalii ninaomba wizara itusaidie kwa kutenga fedha za nyumba za walimu na sisi tutajenga mabweni ili shule hii ipandishwe na kuwa ya kidato cha tano na sita. Ahsante.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyeiti, ninapenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Tunduru Kusini kuna shule za Kata nane na tunategemea kuongeza shule mbili za sekondari ya Misechela na Tuwemacho jumla 10 katika kata 15. Changamoto kubwa ya shule hizo ni za kutwa tunalazimika wanafunzi kuwalaza madarasani kutokana na umbali wa vijiji wanavyotoka watoto hai hivyo madarasa haya mchana na usiku mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tunaomba Serikali kutusaidia kujenga mabweni katika shule hizo ili kupunguza kero za wanafunzi hao kutembea kilomita nyingi kufuata shule na uwezo mdogo wa wazazi kuwapangia watoto wao nyumba za kuishi. Changamoto nyingine ni upungufu wa madarasa kutokana na idadi kubwa ya watoto wanaofaulu kwenda kidato cha kwanza kipindi cha sera ya elimu bila malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni upungufu wa maabara ya sayansi. Tunashukuru Serikali na wananchi kwa kujitolea kujenga maabara ya masomo ya sayansi. Lakini pamoja na jitihada hizo bado majengo hayo hayajakamilika kwa kupewa vifaa vyta maabara. Kwa hiyo tunaomba Serikali kutoa vifaa vyta maabara ili kuzifanya maabara zile zifanye kazi ipasavyo sambamba na upungufu wa maabara kuna upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi kwa masomo ya fizikia, kemia, biolojia na hesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali iendelee na jitihada za kuajiri walimu wa sayansi angalau kila somo apatikane mwalimu mmoja ili kuweza kuwafundisha watoto wetu katika teknolojia mpya ya sayansi na teknolojia. Changamoto nyingine ni kwamba katika shule hizo zote hamna shule yoyote ya *high school* jambo ambalo linalozimisha wanafunzi wengi kukosa kuendelea na masomo ya *high school*. Hivyo ninaomba angalau tupate *high school* mbili kwa kuanzia shule ya sekondari Semeni na shule za

sekondari Mchoteka ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaokwenda *high school*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changanoto nyingine ni kutokuwa na chuo cha ufundu kwa ajili ya kuendeleza vipaji vyta wanafunzi. Hivyo ninaomba fursa itakayopatikana chuo cha ufundu kijengwe katika Jimbo la Tunduru Kusini hususani katika Kata ya Mtina ambako mahitaji makubwa muhimu na ya kutosha yapo, kama vile ardhi, maji safi na barabara inayopatikana wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, VETA ni muhimu sana ili kuendeleza vijana wetu wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne na cha sita ambao wanakosa nafasi za kuendelea mbele kimasomo. Changamoto nyingine ni la nyumba za walimu ambapo walimu wengi wanakaa kwenye nyumba za kupanga vijijiini. Tukumbuke kwamba shule zote hizi zipo vijini ambapo huduma ya nyumba za kupanga si nzuri sana wanazimika kupanga ili waishi. Ni vyema Serikali kuona umuhimu wa kujenga nyumba za walimu ili kupunguza kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni mikopo kwa walimu. Kwa kuwa kipato cha walimu ni kidogo ninaomba Serikali kuona namna ya kuwakopesha usafiri hasa pikipiki ili waweze kujikimu pindi wanapotaka kusafiri kwenda mjini kufuata mahitaji pamoja na mishahara. Walimu wengi wana madai mengi kwenye mabeuli SACCOSjambo ambalo linawafanya waishi katika mazingira magumu sana na kushindwa kufanya kazi vizuri. Hivyo ninaomba mishahara ya walimu iongezwe pamoja na kupewa fursa ya kukopeshwa na Serikali kwa riba nafuu kama zile za vijana akinamama na walemvu ili kuwapunguzia mzigo wa kukopa kwa riba kubwa.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna wakuu wa Idara na wafanyakazi wote kwa kazi nzuri na ngumu mnayofanya. Kwa

niaba ya wananchi wa Urambo pokeeni shukrani za dhati kwa kukubali kuanzisha Chuo cha VETA Urambo asante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ombi tunaomba sana Chuo hicho kiwe na miundombinu hususan Karakana ili wapate ufundi wa aina mbalimbali pamoja na mafunzo yote mafunzo ya udereva (*Driving*) isikosekane kwa kuwa hakuna Urambo inabidi waende Tabora. Hakika ndoto yetu ya kuwa na VETA imetimia. Watoto wa kike watapata mahali pa kukua baada ya kumaliza masomo wakiwa na umri mdogo, Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia mabweni hasa kwa *high schools* za Vyumbu na Urambo. Tutashukuru sana mkituruhusu tuongeze shule mbili za *high school* za Ukondamoyo na Usoji. Tutaleta maombi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii, je, Serikali haioni umuhimu wa kuagiza kwamba shule mpya inapojengwa ianze na vyoo kwa kuwa madarasa yanapojengwa wa fedha huisha na kushindwa kujenga vyoo bora na vya kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri. Pamoja na kwamba mabweni si utatuzi pekee wa suala la mimba shulenii lakini linachangia kwa kiasi kikubwa. Ni vyema kukawa na mkakati wa kujenga mabweni kama ilivyo kuwa maabara na madawati. Nawatakia kila la heri kazini.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha nami kufika mahali hapa na kuchangia Hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya mwaka 2019/2020. Hotuba hii inakwenda kutekeleza llani a Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyoelekeza hususani katika kukuza sekta ya elimu kwa kutoa elimu bure kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la udahili kwa wanafunzi wa elimu ya juu na masuala mazima ya teknolojia. Halikadhalika nitumie nafasi hii kwa mara nyingine tena

kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa hatua kubwa ilizofikia katika sekta ya elimu, uandikishwaji wa wanafunzi wapya katika mfumo rasmi wa elimu nchini unaonesha kuwa hadi Machi, 2019 wanafunzi wa elimu ya awali walioandikishwa ni 1,278.816 sawa na asilimia 92.48 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,382,761.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kati ya hao walioandikishwa wanafunzi 1372 ni wenye mahitaji maalum. Vilevile wanafunzi wapya walioandikishwa kuanza darasa la kwanza ni 1,670,919. Kati ya hao wanafunzi wenye mahitahi maalum walioandiishwa ni 3028, hatua nzuri na ya kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naipongeza Wizara pamoja na ofisi ya Rais- TAMISEMI kwa kuendelea kushirikiana na wananchi na wadau wa maendeleo katika kuboresha miundombinu ya shule za awali na msingi. Takwimu zinaonyesha hadi februari 2019 ujenzi wa vyumba vyaa madarasa 2840 kwa shule za msingi umefanyika na kuongeza idadi ya vyumba vyaa madarasa 2637 viko katika hatua mbalimbali ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti vilevile jumla ya matundu ya vyoo 7067 vyoo vya wanafunzi matundu 6445 na vyoo vya walimu matundu 622 yamejengwa katika shule za msingi na kuongeza matundu ya vyoo kutoka 190,674 yaliyokuwepo Machi, 2018 hadi kufikia matundu ya vyoo 197,741 mwezi Februari 2019 hili ni ongezeko la asilimia 3.5. Aidha, matundu ya vyoo kutoka 3004 yanaendelea kujengwa na yanatarajiwa kukamilika kabla ya Juni, 2019 ni mwanzo mzuri ambao mwelekeo wake ni kuhakikisha changamotoo zilizokuwepo zinakwenda kuisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Serikali imeendelea kufanya kazi nyingine za uboreshaji miundombinu ya elimu zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu 720 na kuongeza idadi ya nyumba hizo kutoka 44320 mwaka 2018 hadi nyumba 45040 Februari, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, jambo lingine la kupongeza ni idadi ya madawati ya wanafunzi watatu watatu kuongeza kutoka madawati 2,858,982 yaliyokuwepo Machi,2018 hadi madawati 2,994,266 Februari 2019 sawa na ongezeko la madawati 135,284. Aidha, kuititia programu ya *Equip-T*, Serikali imetoa jumla ya vyumba vya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yametekelawa katika mikoa tisa yenye halmashauri 63. Yapo mengi sana yaliyofanywa na yanayoendelea kutekelezwa na Serikali yangu siku ya Chama cha Mapinduzi katika sekta hii ya elimu, naishauri Serikali kuendelea kuboresha maeneo mbalimbali kwenye sekta ya elimu, hii ni kutokana na umuhimu wake hasa katika maendeleo endelevu ya kiuchumi na mapinduzi ya nchi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kugusia sasa changamoto zinazohusu sekta ya elimu katika Jimbo la Kibaha Vijijini, ni mdau mkubwa wa sekta hii ya elimu, nimekuwa nikihamasisha wananchi wangu kuhakikisha wanachangia sekta ya elimu, halikadhalika na mwenyewe nikishiriki kama mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejitahidi kufanya mengi sana kwenye sekta hii na mengi hayo ni mazuri yenye tija, lakini bado Kibaha Vijijini tuna changamoto mbalimbali katika sekta ya elimu, tuna changamoto ya upungufu wa nyumba za walimu 342, upungufu wa vyumba vya madarasa 140, matundu ya vyoo 483 nadawati, ofisi za walimu 27 pamoja na samani za ofisi, naiomba Serikali katika bajeti hii kuliangalia hili na kuongeza fedha kwenye bajeti hii hasa katika halmashauri yangu ili kutatua changamoto katika jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, fedha husika zifike kwa wakati ili ziende moja kwa moja katika changamoto husika na kuzitatua. Aidha, tuna changamoto ya mabweni ya shule ya Magindu na bwalo la Shule ya Sekondari ya Soga na kupanda madaraja kwa walimu wetu, pamoja na walimu kupanda madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika bado pia kuna changamoto kubwa jimboni kwangu ya ucheleweshaji wa fedha za uhamisho wa walimu wetu pindi wanapopata uhamisho, hali hiyo imekuwa ikirudisha nyuma hamasa kwa walimu kwani fedha hizo za uhamisho zinapochelewa husababisha walimu kutokufika katika vituo vyao nya kazi kwa wakati, naiomba wizara kuifanyia kazi changamoto hii, na kwenye majumuisho ya majibu wakati wizara itakapotoa majumuisho naomba kupata majibu ya changamoto hii, ni lini walimu wangu wanaodai fedha za uhamisho watapatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kuongelea changamoto zinazowakabili watu wenye mahitaji maalum (viziwi). Kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa wenzetu hasa soko la ajira haliwapi fursa kuweza kupata nafasi za kazi na fursa za kujajiri; ushauri wangu Serikali iangalie mitaala maalum itakayoweza kuwapa wenzetu hawa fursa ya kuingia kwenye soko la ajira ili waweze kuona tija ya elimu wanayopatiwa.

Masomo ya dini (*Bible knowledge na Islamic religion*) kupatiwa thamani kwenye ufaulu wa wanafunzi; Serikali imekuwa ikillipa mishahara kwa walimu wanaosomesha masomo ya dini shulenii na pia Serikali imekuwa ikiingia gharama kuandaa mitihani kwa masomo hayo bila ya kupatiwa thamani kwenye ufaulu. Kwa vile kila mwanafunzi anatarajiwa kuwa muajiriwa mtarajiwa na kwa kila mwajiriwa anahitaji miongozo ya kiroho, Wizara sasa ina haja ya kuona namna ya kuipa thamani masomo haya kwenye ufaulu wa wanafunzi.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niongelee kuhusu mikopo ya vyuo. Vyuo vingi viliahidi utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi hasa udaktari kwa kupata mikopo asilimia 100 lakini wanafunzi wengi hasa wasichana wameacha kozi au kubadilisha kwa ukosefu wa ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, majengo ya shule za zamani. Majengo mengi yamechakaa japo kuna mengine yamefanyiwa ukarabati. Naomba *speediongezeke* ili kuweka mazingira mazuri ya watoto wetu kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, viongozi wa vyuo. Kumekuwa na uteuzi wa maprofesa wengi kumsaidia Rais kazi za siasa na kuacha ombwe kubwa katika sekta ya elimu. Tunaomba kama hakuna haja wangeachwa waendelee na kazi ya kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, siasa vyuoni. Kumekuwa na upendeleo kwa vijana wetu vyuoni kwa kuangalia vyama. Vyuo kama *DUCE* na Mwalimu Nyerere wanatoa kumbi zao kwa vijana wa CCM ili kufanya siasa wazi na kuleta mgawanyiko kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, *pads*. Tunaomba pungozo la bei za taulo za kike na zitolewe kwa wanafunzi husika kwa kutenga fungu na kusaidia tozo ili zifike kwa walengwa.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa ya kuchangia kwa maandishi kama ulivyonipatia hapo awali fursa ya kuchangia moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa usimamizi mzuri wa Serikali. Pia naendelea kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Magu, Kata ya Bujora kuna Shule ya Sekondari ya Lunve. Shule hii imekuwa mkombozi mkubwa kwa wanabujora kwani wanafunzi walikuwa wanatembea umbali mrefu kutafuta elimu toka shule za kata za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa mchango wake katika ujenzi wa shule hiyo japo bado kuna mahitaji makubwa na ni hivi karibuni tumepokea shilingi

milioni 25 kwa ajili ya madarasa mawili (2). Shule ina majengo sita tu yaliyokamilika huku wananchi wakiendelea kujenga madarasa manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule haina madawati ya kutosha na wanafunzi wanakaa chini na matundu ya vyoo ni machache kulingana na mahitaji. Naomba sasa Wizara iweze kuiangalia shule hii kwa jicho la tatu ili ipate uwezesho katika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mwandiko wa kuunganisha herufi. Katika hili, Serikali inabidi iangalie upya mpango huu kwani umekuwa ukileta mkanganyiko kwa wanafunzi wa madarasa ya chini yaani awali mpaka darasa la nne kwa namna ambavyo imekuwa ikiwaletea taabu wanafunzi katika utambuzi wa herufi na namna ya kuanza kuzitambua na hivyo kuwa na mwandiko mbaya. Hivyo basi, Serikali kupitia Wizara hii iangalie namna nzuri ya uumbaji wa herufi toka wanafunzi wakiwa katika hatua za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, maabara za shule za sekondari. Ni vema sasa Serikali ikaelekeza nguvu ili kumalizia maabara za shule zote nchini na kuhakikisha zinanza kufanya kazi kwani tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda. Hivyo, ni vema maabara ziboreshwe na kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, maktaba. Serikali sasa ni lazima itambue umuhimu wa maktaba kwani ndiyo chanzo cha kufanya rejea ya mambo mbalimbali ambayo wanafunzi wanakuwa wanafundishwa darasani kwa muda mfupi. Hivyo basi, Serikali iharakishe ujenzi wa maktaba katika shule zote za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, nilileta ombi la Shule ya Sekondari Mpanda ianzie *Form I – VI* badala ya ilivyo sasa *form four - six*. Je, ombi hilo limefikia wapi na limeshughulikiwa kwa kiasi gani?

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na uzima na kuweza kuchangia katika Wizara hii kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri mama yangu Mheshimiwa Prof. Ndalichako kwa jitihada ambazo amekuwa akizifanya katika kuboresha suala la elimu Tanzania. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara bado kuna changamoto nyingi katika suala la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Asilimia 90 ya wanaaoomba mkopo wazazi wao hawana uwezo lakini pamoja na Serikali kuboresha huduma hii, bado kuna changamoto kwani wapo wanafunzi ambao wana vigezo kabisa vya kupata mkopo lakini hawajapata. Naomba sana Wizara ihakikishe wanafunzi wote wanapata mkopo na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasema inasaidia wanafunzi wasio na uwezo kupata mkopo, sawa tunashukuru sana kwa jambo hili jema linalofanya na Serikali yetu lakini kwa nini Serikali iwasaidie wanafunzi hawa kwa riba? Leo Serikali inampa mwanafunzi mkopo Sh.7,000,000, lakini anakuja kulipa Sh.12,000,000. Sasa huu ni msaada kweli ukizingatia anamaliza chuo anaanza kazi mshahara ni mdogo na hata kupata hiyo kazi ni shida. Kwa nini mwanafunzi asilipe kile ambacho Serikali imempa? Kama digrii amesoma miaka mitatu kwa Sh.8,000,000 basi akianza kulipa alipe hiyo hiyo na siyo Sh.13,000,000 au Sh.14,000,000. Hii sidhani kama ni sawa na kiukweli inaumiza sana. Naomba mtu alipe alichokopeshwa na siyo na riba tena kubwa inakuwa kama umekopa benki, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala upungufu wa walimu hasa masomo ya sayansi. Shule zetu nydingi hazina walimu wa kutosha wa sayansi. Sasa kama kweli tunaenda katika nchi ya viwanda ni lazima tuwekeze katika suala la sayansi katika shule zetu. Niombe sana zijengwe maabara za kutosha ili wanafunzi wetu waweze kufanya mafunzo kwa vitendo, hii itawasaidia sana kwani sayansi ni vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu kwenye shule zetu kiukweli kuna changamoto kubwa kwani maeneo mengi hakuna madarasa ya kutosha. Katika Mkoa wangu wa Kigoma hakuna madarasa ya kutosha kwani kuna shule wanafunzi wanakaa chini. Vilevile shule nydingi hakuna vyoo bora yaani hali ni mbaya sana, watoto wana mazingira magumu sana. Unakuta watoto wanajisaidia hovyo na kupelekea mlipuko wa magonjwa kama kipindupindu. Pia kuna watu wenye ulemavu wanaotambaa chini sasa angalia hali ya choo ilivyo chafu na hakuna maji hawa wanafunzi wanakuwa katika hali gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba bora kwa walimu. Walimu ni muhimu sana, tuwe wakweli wote tumefika hapa kwa msaada wa walimu. Walimu wanafanya kazi kubwa sana lakini wanaishi katika mazingira magumu sana. Wengi hawana nyumba za kuishi na hata zilizopo zina hali mbaya sana kwani hakuna maji wala vyoo bora. Naomba Serikali iwaangalie walimu Tanzania nzima kwa jicho la pili wapatie nyumba bora za kuishi. Hii itasaidia kuongeza *morale* ya utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kupanda madaraja kwa walimu na stahiki zao za likizo na matibabu. Bado kuna changamoto kwani walimu wanapanda madaraja lakini mshahara haupandi, anapanda daraja toka A kwenda B, lakini anaendelea kulipwa mshahara wa daraja A. Hali hii imepelekea mpaka leo kuna wastaafu wamestaafu lakini wamepunjwa mafao yao kwa kufanyiwa kikokotoo kwa mshahara wa daraja A wakati alipanda daraja miaka mingi na amestaafia daraja

jipya. Jambo hili si haki kabisa, huyu mtu ametumikia Serikali kwa moyo wote kwa nini anyimwe haki yake? Ahsante.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya wanafunzi bado ni tatizo, kwanza inachelewa na pili inatolewa bila kufuata taratibu. Mfano, kuna yatima ambao wamejaza vizuri pamoja na yote hayo bado hawapewi mkopo wanapewa ambao wana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha kwa walimu. Hakuna elimu bora bila walimu kupewa motisha. Hata kama mna madarasa mazuri kiasi gani au miundombinu yote iwepo bila kuhakikisha walimu wana ari ya kufundisha ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji mikopo kwa asilimia 15. Tukumbuke kuwa wapo pia walimu ambao wanakatwa mikopo na mshahara yao ni midogo. Ukitata mkopo kwa asilimia hizo unamwacha hana chochote na kushindwa kuwajibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure. Changamoto za elimu bure ni kubwa mno, watoto ni wengi, hakuna madarasa, walimu, vifaa vya kufundishia na maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria za uanzishaji shule. Shule za Serikali zinaanzishwa hata kama hakuna vyoo, madarasa machache ukilinganisha na za binafsi ambazo unakuta hazipati usajili wakati pengine hawana baadhi ya mahitaji madogo tu. Tuangalie na kuwatia moyo wenye shule binafsi kwani wanaisaidia Serikali kielimu hivyo inatakiwa sekta binafsi hii isaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti kushuka. Naomba tuangalie suala hili maana watoto ni wengi madarasani wakati fedha zao hazongezeki, mishahara haiongezwi, hakuna mafunzo ya ziada ya mitaala na sera zinabadilishwa lakini walimu hawapati mafunzo juu ya mabadiliko hayo.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu kuboresha maslahi ya walimu. Suala hili la kuboresha maslahi ya walimu wetu ni muhimu ili kuleta morali kwa walimu na matokeo chanya kwa watoto na hasa kizazi hiki ambacho kinakabiliwa na kuzungukwa na utandawazi ambao unawaathiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mitaala yetu iendane na teknolojia yetu. Kutokana na suala la teknolojia kubadilika kila wakati hivyo mitaala yetu ni vyema kuzingatia mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha za alama kwa wanafunzi wenye ulemavu. Wanafunzi hawa wanahitaji kupata elimu kama wanafunzi wengine ili kuleta usawa na kuondoa malalamiko mionganini mwa wanafunzi ambao wako kwenye jamii zetu zinazotuzunguka. Kwa hiyo, ni muhimu lugha hizi ziwepo katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna upungufu wa walimu wa lugha za alama. Nashauri ili kumaliza tatizo hili Serikali iongeze vyuo maalum kwa ajili ya walimu wa lugha za alama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wa wadau wa elimu wanapotaka kufanya mabadiliko katika masuala ya elimu. Kumekuwa na matokeo hasi kwenye maamuzi mbalimbali yaliyotokea katika masuala ya elimu sababu kubwa ni kutowashirikisha kikamilifu wadau wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo maalum kwa walimu. Kulingana na mabadiliko yanayojitokeza kwenye elimu ni vyema walimu wetu wakawa wanapewa mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya ufundi. Bado kuna upungufu mkubwa wa vyuo vya ufundi nchini kulingana na wahitimu wa ngazi mbalimbali kuwepo mitaani lakini hata vile vichache vilivyopo vina changamoto za walimu kuwa wachache pia hawapelekwi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza pesa kwenye suala la ukaguzi kwa kuwa matokeo chanya ya elimu yatatokana na ukaguzi. Nashauri Serikali ili kuboresha elimu yetu ni vyema kuboresha Kitengo cha Ukaguzi pia Wizara ishughulikie kero zinazotokana na ukaguzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu ina mkanganyiko sana. Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza sera hizi ambazo zimekuwa na mkanganyiko mkubwa?

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa kazi nzuri zinazofanywa na Serikali kuititia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hotuba endapo nitapata jibu sahihi na nitashika shilingi ya mshahara endapo sitapata majibu sahihi ya kujengewa Chuo cha VETA Kwimba ambapo ni ahadi ya Serikali. Waziri na watendaji ni waungwana sana lakini cha kushangaza kwa zaidi ya miaka 15 kumekuwa na ahadi ndani ya Bunge na kwenye vitabu lakini utekelezaji ni zero. Mimi ni Seneta humu Bungeni siyo vizuri sana kukaa naulizia suala hilo hilo kila Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kwimba ilikuwa moja ya wilaya iliyokuwa imepangiwa kujengewa Chuo cha Ufundii miaka 10 iliyopita. Wilaya ya Kwimba kutokana na agizo la Wizara tuliambiwa tutafute eneo ambapo tayari eneo lipo la ekari 60 na lina hati ya umiliki chini ya Halmashauri ya Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kutoka kwa Mkurugenzi wa VETA, ni nani aliyefuta Wilaya ya Kwimba kwenye orodha ya wilaya zilizopitishwa kujengewa chuo cha VETA? Mkurugenzi wa VETA, Dkt. Pancras Bujulu, naomba kuititia Wizara ya Elimu nipate ahadi, dhamira, kukiri, kutimiza ahadi (*commitment*) ya kujengewa Chuo cha VETA ambapo ni ahadi ya Serikali kwa zaidi ya miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri arejee andiko langu hapo juu kuwa sitaunga mkono na

nitashika shilingi endapo sitapata *commitment* ya Serikali. Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako namheshimu sana, naomba ye ye na viongozi wenzake hiki kilio cha VETA kifiki ukingoni.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure (bila malipo). Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la wanafunzi katika kujandikisha kuijunga na shule mbalimbali lakini kuna tatizo kubwa sana la miundombinu kwani miundombinu imezidiwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na elimu msingi, mfano, vyoo, madarasa, ofisi za walimu na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pamoja na idadi ya wanafunzi kuongezeka lakini kuna uhaba mkubwa sana wa walimu kwani uwiano wa wanafunzi na walimu kwenye shule zetu haulingani kabisa. Hivyo basi inapelekea ile dhamira njema ya kukuza na kusaidia kila mwenye uwezo wa kwenda shule aende shule isiwe na tija kwa maana uchache wa walimu unadumaza hiyo nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za miradi na maendeleo. Tumekuwa tukipitisha fedha na bajeti mara kwa mara lakini cha kusikitisha ni kwamba fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo zimekuwa zinatolewa kwa asilimia ndogo sana. Niiombe sana Serikali iwe inatoa fedha zinazopitishwa na Bunge lako Tukufu ili kuweza kufikia yale malengo ambayo Wizara na Serikali kwa ujumla zinakuwa zimejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa walimu. Tumekuwa na upungufu mkubwa sana wa walimu nchini. Mfano kwa wilaya ya Kilosa peke yake, kwenye upande wa shule za msingi, tuna wanafunzi 107,000 lakini tuna walimu 2,393 kwa hiyo tuna upungufu wa walimu 929. Nitumie nafasi hii kuiomba sana Serikali itusaidie kwa kutuongezea walimu

zaidi kwenye shule za msingi Wilayani Kilosa. Pia ituongezee walimu wa sayansi kwenye Wilaya yetu ya Kilosa kwani napo tuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*). Ni vyema sana Serikali ikaona umuhimu wa *COSTECH* ili tuweze kusaidia Taifa letu kwenye masuala ya ubunifu wa mambo mbalimbali kwenye nchi yetu. Tanzania tumebarikiwa sana kuwa na watu mbalimbali wanaovumbua vitu vingi lakini tuna tatizo kwa *COSTECH* kushindwa kuwafikia na kuwasaidia kutokana na ufinyu wa bajeti. Bila bajeti ya kueleweka *COSTECH* haiwezi kuvumbua, kubuni na kusaidia vipaji mblimbali ambavyo kama vingeweza kusimamiwa ipasavyo vingeweza kutuletea maendeleo makubwa sana na kututoa kimasomaso kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu walimu. Zamani unapoingia chuoni unaambiwa ualimu ni wito kama Padre, Askofu au Shekhe. Hii iliwafanya wote wanaochukua mafunzo ya ualimu kuwa na nidhamu katika kazi yao. Sasa hivi tuna walimu ambao wengine hawastahili kuitwa au kuwa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu anatoka shulenii badala ya kurudi kule anakoishi moja kwa moja anakwenda kwenye vilabu vya pombe. Kule analewa kiasi kwamba anakuwa hajitambui hususan walimu wa kiume. Anapita mitaani anayumba watoto ambao wengine ni wanafunzi wake wanamsindikiza kwa kumzomea. Hii inashusha hadhi ya mwalimu na ualimu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee kuhusu walimu kupata mafunzo ya mara kwa mara (*refresher courses*) wakati

wanapokuwa likizo. Hii itawasaidia walimu kwenda na wakati uliopo kwa maana pengine kuna mabadiliko ya mitaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu utoro wa watoto kwa baadhi ya shule. Kuna sababu mbalimbali zinazosababisha utoro kwenye shule zetu. Moja, ni ukosefu wa walimu. Kuna baadhi ya shule hususan shule za vijiji utakuta kuna madarasa saba lakini walimu wanne tu, pale lazima kuwepo na utoro. Pili, watoto kwenda shulen i wakiwa na njaa kwani mtoto mwenye njaa hafundishiki. Tatu, ukosefu wa uzio katika shule kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Nashauri shule ziwe na walimu wa kutosha katika madarasa. Pia shule ziwe na utaratibu wa kuwapikia wanafunzi angalau uji ili waweze kukaa madarasani na kusikiliza mafundisho wanayopewa. Shule nydingi hazina wigo ni rahisi wanafunzi kutoroka na kupotea mitaani kwenda kuungana na wale amba wana tabia mbaya. Kwa hiyo, Serikali ione umuhimu wa kujenga uzio katika shule zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri shule za msingi zifundishe masomo ya ufundi kama useremala, uashi, ushonaji, upakaji nyumba rangi na kadhalika. Serikali ianzishe karakana za kufundishia ufundi huo ili kuwaandaa wanafunzi wale wanaokosa nafasi ya kuijunga na elimu ya sekondari waweze kujajiri au kujilendeze katika vyuo vya VETA na kupata ujuzi mzuri na kujajiri ili kupunguza wimbi la wazururaji.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kuleta mchango wangu kwa maandishi katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza pongezi zangu kwa Waziri na Naibu kwa kazi kubwa mnazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali yetu ya CCM, lazima tujikite katika kuandaa mitaala ambayo itawapa fursa wanafunzi wanaohitimu waweze kuwa na *skills* ambazo zitawafanya waweze kujajiri au kumudu kuendesha maisha yao binafsi katika mazingira ya sasa ya ushindani.

Wanafunzi wengi wanaomaliza vyuo na elimu za kawaida za sekondari, wamekuwa wakitegemea sana kupata ajira rasmi kutoka katika taasisi za Serikali na binafsi. Jambo hili limepelekeea kuwepo kwa wimbi kubwa la nguvu kazi mtaani ambayo haitumiki kwa maana ya kwamba hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufilee wakati muafaka sasa Serikali yetu iandae mitaala ya namna ya kuwapa elimu ya kujitegemea wahitimu wetu ili wapate *technical skill* ambazo zitawasaidia kujajiri au kujitegemea. Hapa tunaweza kupata wahitimu wakaandaliwa katika vikundi mbalimbali tukawapa mikopo ya mitaji hawa ambao tumewaandaa vema ili waweze kuanzisha miradi ya kujajiri na kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulimaliza shule za msingi na kulikuwa na mafunzo ya elimu ya kujitegemea kama vile uselemara, umeme, ufundi wa magari na kadhalika. Naishauri Serikali yangu kuhakikisha watoto wetu wanaohitimu wanapata *skills* ambazo zitawasaidia kujajiri na nchi pia kupata wataalamu ambao tutaweza kuwatumia katika viwanda ambavyo tunavihamasisha vijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naishauri Serikali kupitia mfumo wa kuhakiki vyeti vya wanafunzi wanaoomba mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ambapo kwa sasa utaratibu umetolewa kwa waombaji wanaoomba kupitia *online* kulazimika kuhakiki vyeti jambo ambalo naona ni kuwapotezea muda na gharama watoto wa Kitanzania. Nashauri Serikali irudishe jukumu la kuhakiki vyeti lifanywe na Bodi ya Mikopo yenyewe na liwe *well-coordinated*. Wanafunzi wanapoomba mikopo wanaambatanisha na vyeti vyao vya kuzaliwa moja kwa moja, Bodi ichambue na kupeleka majina na nakala za vyeti viweze kuhakikiwa na hivyo kuwasaidia watoto wetu kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa vyuo vya VETA katika Wilaya ya Ikungi, sisi ni wazalishaji wakubwa sana wa alizeti hivyo uhitaji wa ujenzi wa vyuo vya ufundi hauepukiki ili kupata vijana wenye *technical skills* watakaojiajiri katika usindikaji wa mazao ya kilimo

yanayopatikana katika Wilaya yetu. Naomba sasa ujenzi wa VETA utekelezwe katika Kata ya Minyughe, Wilaya ya Ikungi, mahali ambapo tayari tumeandaa eneo la ujenzi wa chuo hiki ambacho kitakuwa chachu ya maendeleo katika kuwasaidia vijana wa Kitanzania watakaokuwa na uwezo wa kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, natoa rai kwa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuja na mkakati madhubuti wa namna ya kuandaa mkakati wa ujenzi wa nyumba za walimu nchini. Walimu wetu wanateseka sana katika kupata makazi ya kuishi hivyo kuathiri taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Prof. Ndlichako pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Olenasha kwa kazi nzuri wanayoifanya katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zangu, naomba sana Mheshimiwa Waziri aendelee kupigania elimu bora katika nchi hii. Mwaka juzi kuna baadhi ya shule za Serikali na shule binafsi zilipata kashfa ya udanganyifu wa mitihani, hili ni jambo baya wala halikubaliki. Pamoja na adhabu mlizochukua ikiwa ni kufutia mitihani na kuzifungia shule hizo, naomba sana adhabu hizi zisiweze *double standard* kwa kuziadhibu shule binafsi na kuziacha shule za Serikali wakati kosa ni lile lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za binafsi zimenyimwa nafasi ya wanafunzi wao kufanya mitihani katika shule zao, wamebadilishiwa *centre* za mitihani pamoja na kuendelea kuwafundisha wanafunzi katika shule zao na mbaya zaidi hata matokeo yakitoka yanalenga katika shule walizofanya mitihani. Ombi langu adhabu iwe *common* kwa yejote atakayefanya kosa, kubagua ni dhambi. Naomba kuchukua

fursa hii kuwaombea msamaha wenye shule za binafsi kwa muda wote huu watakuwa wamejifunza kosa lao na hawatakuwa tayari kulirudia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri endeleeni kuchapa kazi.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda nichangie Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa uboreshaji wa miundombinu ya elimu katika shule za msingi na sekondari hususani mabweni, madarasa na majengo ya utawala katika Shule ya Msingi Gongali na Sekondari za Endabash, Banjuka, Welwel na Mangola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wanafunzi wa elimu ya juu hawapati mikopo na hivyo kuhangaika sana. Niishauri Serikali kuboresha mifumo ya utoaji mikopo ili kweli wale wanaostahili wapate mikopo hiyo. Wako wanafunzi wameacha masomo baada ya kukosa ada, vipo pia vyuo vikuu vinawakarisha wanafunzi mwaka endapo atashindwa kukamilisha ada, hii si sawa kabisa. Wanafunzi wote wa elimu ya juu wapewe nafasi ya kukopa kisha utaratibu wa kulipa uimarishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi na mafunzo ya VETA hayaepukiki katika Tanzania ya Viwanda tunayojenga. Serikali imesema itajenga Chuo cha Ufundu katika kila Wilaya. Halmashauri ya Wilaya ya Karatu imejenga Chuo cha Ufundu cha kisasa. Tunashukuru Chuo kimesajiliwa lakini bado kinakosa wakufunzi na vifaa. Tunaomba Wizara itusaidie kupata wakufunzi na vifaa vyta ufundishaji katika Chuo cha Ufundu cha *Christimac Tree*, Bashay Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri pia Serikali irudishe mfumo wa zamani wa shule zote za msingi na sekondari kuwa chini ya Wizara ya Elimu badala ya kuwa Tawala za Mikoa

na Serikali za Mitaa. Kwa muundo wa sasa, shule hizi ni kama hazina mwenyewe, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina mambo mengi sana na hivyo kupelekeea eneo hili la elimu kutozingatiwa ipasavyo.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kabisa nimponeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Naibu wake kwa utumishi wao wa unyenyekevu, kujituma na usikivu katika kutekeleza majukumu yao. Nimponeze sana pia Mheshimiwa Rais kwa kutoa kipaumbele cha juu kabisa kwenye suala la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa Mheshimiwa Waziri kunitengeta fedha za kukarabati upya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Malampaka. Naomba sasa ramani za majengo yatakayokarabatiwa zipelekwe kwenye Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Malampaka ili ujenzi na ukarabati uanze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshasubiria kwa muda mrefu sasa ramani hizi hazikamiliki na sababu ya kweli ya kuchelewesha ramani hizi bado haijajulikana. Naomba sana mchakato huu uharakishwe ili ukarabati wa chuo hiki uweze kuanza na hatimaye kuwafaidisha wananchi wa Maswa na Jimbo la Maswa Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu wa jana, napenda kuongeza kwa haya yafuatayo kwa maslahi ya Mkoa wetu wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa tunayo maboma kadhaa na majengo ya nyumba za walimu, madarasa, vyoo na maabara jumla ni 208 lakini kati yake maboma 177 ya maabara bado hayajakamilika na kupelekeea wasiwasi wa kupata mafunzo kamilifu ya sayansi kwa watoto wetu. Tunaomba Mkoa wa Rukwa utizamwe kwa

jicho la pekee hasa mkizingatia tupo pembezoni nasi tulichelewa katika suala zima la elimu, tumekuja kuibukia hivi sasa. Tunaomba fedha ilioandalialiwa kuhusu ukamilishaji wa maboma ya majengo ya elimu, Mkoa wa Rukwa tuwemo katika mgao wa fedha hizo kwa zaidi ya nusu ya maboma hayo ya maabara kwa makusudi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumzia kuhusu matatizo ya kiwango cha pesa zitolewazo kwa ajili ya chakula kwa shule zenyenye wanafunzi wenyenye mahitaji maalum, kwa shule zetu za Mkoa wa Rukwa, tunazo pale Kata za Ndala B, Mwenge A na Malangali kwa mwaka fedha zinazotolewa na Serikali ni kiasi cha shilingi bilioni 22 wakati mahitaji halisi ni shilingi bilioni 72.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachohitaji kuongezea hapa ni usalama wa shule hizi hasa Shule ya Walemvu Malangali. Malangali ni shule ya bweni lakini haina uzio na watoto ambao ni wenyenye ualbino wanakuwa katika wasiwasi wa maisha yao na hata walimu wao wanakuwa na kazi ya ziada ya ulinzi wa watoto hao. Tunaomba Serikali ionye umuhimu wa ujenzi wa uzio wa shule hiyo kwani ni shule inayosaidia na mikoa ya jirani na wakati wa likizo wengi wao hawaendi majumbani kwa kuhofia usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuweka msisitizo kuhusu Chuo cha *FDC* - Chala kwa kuwa majengo hayo yanahitajika kurejea kwenye umiliki wa Askofu wa Kanisa la Katoliki, ingawa miundombinu yake imechakaa kwa kiasi kikubwa sana, wananchi wametoa eneo na majengo kadhaa yameanzishwa kwa nguvu za wananchi.

Kwa kuzingatia na kuheshimu mchango wa wananchi wetu, tunaomba mgao wa fedha hizo za kukarabati Vyuo vya *FDC* kwa Mkoa wa Rukwa zielekezwe kwenye eneo hili tukamilishe Chuo chetu cha *FDC*mbadala wa Chuo cha *FDC* - Chala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali na Wizara kwa jitihada kubwa za kuinua elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kuinua elimu basi ni lazima Serikali iwe na mkakati wa kuongeza idadi ya walimu hasa maeneo ya vijijini, hii inaendana na kuboresha miundombinu ya maeneo ya vijijini. Walimu wengi wanaondoka maeneo ya vijijini kwa sababu tu ya miundombinu mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wengi wanadai haki zao, hili pia ni tatizo. Serikali lazima ijitahidi kuhakikisha stahiki za walimu zinalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, pale Handeni kuna Chuo cha *FDC*. Chuo hiki kina msaada mkubwa sana kwa Mkoa wa Tanga. Naiomba Serikali ikiangalie kwa jicho la karibu kwa kuwa hali yake ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu bila kumsahau Mkurugenzi wa *TEA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya *VETA* ni mkombozi wa vijana wetu hususan wale waliomaliza darasa la saba na kidato cha nne ambao hawakubahatika kuendelea na masomo. Nchi yetu ina Halmashauri 185, ni muhimu Halmashauri zote nchini ziwe na vyuo hivi ili basi vijana wetu wapate elimu itakayowasaidia kujajiri na kupunguza vijana wetu kuijilingiza kwenye vishawishi vya kuingia kwenye wizi na vitendo visivyokuwa na maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, nashauri Wizara iweke mpango mkakati wa kuanzisha vyuo katika Halmashauri zote nchini. Kwa kuanzia naomba Wizara itoe kipaumbele kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, kwani

tunayo misitu mingi inayoweza kuwasaidia vijana kuvuna mbao na kutengeneza samani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri Serikali kuangalia namna ya kusaidia Halmashauri mpya kupata vyombo vyta usafiri. Halmashauri ya Uvinza haina gari na tunazo shule 122 za msingi, 119 zimesajiliwa na shule tatu (3) ziko kwenye hatua za kusajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kutokuwa na gari kunasababisha wakaguzi kushindwa kutimiza majukumu yao ya ukaguzi wa shule na ukaguzi wa ubora wa elimu inayotolewa. Niendelee kumuomba Mheshimiwa Waziri, dada yangu mpPENDWA Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako kutupatia gari angalau tatu; moja ya Ukaguzi na gari mbili, *DEO* Msingi na *DEO* Sekondari. Jiografia ya Jimbo la Uvinza ni ngumu sana tena sana na hivyo kusababisha watumishi wa idara hizi kushindwa kutimiza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya watu wazima, ukurasa wa 15. Naishauri Serikali kuanzisha vituo hivi kwenye kila Kata ikiwezekana huku baadaye kila kijiji ili elimu hii ya watu wazima iwe mkombozi kwa wote wale wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya sekondari, kwanza nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri kwa namna alivyosikia kilio cha wananchi wa kata zangu mbili, Kata za Basanza na Mwakizega. Shule hizi zilizojengwa kwa nguvu ya wananchi na Mfuko wa Jimbo sasa zimesajiliwa, nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, ninazo shule mbili za Kata ya Sigunga, Ukanda wa Ziwa Tanganyika na Shule Kata ya Nguruka. Shule hizi mbili zimeshajengwa madarasa sita, vyoo na darasa moja kama jengo la utawala kwa kuanzia. Namuomba Mheshimiwa Waziri aone namna ya kutusaidia kuzisajili shule hizi kwani hadi leo hii tunao wanafunzi 250 Kata ya Nguruka hawajapata nafasi na wengine 780 wameachwa kwenye shule mbalimbali ndani

ya Halmashauri ya Wilaya yangu ya Uvinza. Ni muombe Mheshimiwa Waziri atusaidie fedha kwa ajili ya kusaidia shule hizi mbili za Nguruka Sekondari na Sekondari ya Sigunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidato cha sita, tunayo Shule ya *Lugufu Boys na Girls*. Shule hizi zilanzishwa kwenye majengo ya wakimbizi. Miundombinu yake ni chakavu sana na ina mazingira ambayo siyo rafiki, hakuna maji wala umeme. Tuiombe Wizara kuona namna ya kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo sambamba na kuwapatia visima ili wapate maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo shule ya walemavu Kata ya Uvinza. Shule hii ni ya msingi, mazingira yake siyo rafiki kabisa, tunaomba msaada kwa ajili ya watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya walimu. Hali ya makazi ya nyumba za walimu ni tete, shule nydingi za msingi, sekondari hakuna nyumba na zile ambazo zina nyumba basi ni chakavu hata vyoo hakuna. Tuiombe Serikali kutuletea fedha za ujenzi wa nyumba za walimu pamoja na matundu ya vyoo kwenye shule za msingi na sekondari kwa wanafunzi na walimu, hali ni tete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwa kuzungumzia maslahi ya walimu wa shule za msingi na sekondari. Walimu wangu wengi wanayo madai mengi wanadai na hawalipwi. Niombe Wizara ya Elimu pamoja na Wizara ya TAMISEMI ione namna ya kuwalipa walimu wanaodai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto ya walimu wapya kucheleweshewa kulipwa posho zao za kujikumu kwa mujibu wa sheria pamoja na kuwekwa hadi miezi sita bila kupata posho wala mishahara. Tutoe rai kwa Serikali kujipanga kwani wanatambua fika ni lini wataawaajiri walimu. Kwa nini pindi wakitoa tangazo la ajira wasipange na fedha zao kwenye Halmashauri zote nchini ili ajira zinapotoka na fedha ziwe tayari kwenye Halmashauri za Wilaya ili kupunguza usumbufu wanaopata walimu wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira za walimu. Hivi karibuni tumeona tangazo la ajira za walimu na tumesikia walioomba ni zaidi ya 80,000. Ombi langu katika hili, Wizara itupe Halmashauri ambazo zina upungufu mkubwa wa walimu kama vile Halmashauri yangu ya Uvinza. Sambamba na hayo, niombe pia Waziri aje kutembelea Jimboni ili apate muda wa kusikiliza matatizo ya walimu wangu wa Jimbo la Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya elimu ya juu. Nimuombe Mheshimiwa Waziri aangalie Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwani wanafunzi wengi wanayo malalamiko makubwa ya kukoswa mikopo hasa watoto wa watu maskini. Nimuombe Waziri atupie macho Bodi hii waache kuwaonea watoto wa maskini hasa wanaotoka vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo, niendelee kumpongeza Waziri na timu yake yote kwa namna wanamsaidia Mheshimiwa Rais kutelekeza llani ya CCM kutoa elimu bure sambamba na kuiendezea elimu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naunga mkono mia kwa mia utendaji wa Waziri na wasaidizi wake wote. Nachoomba kwenye jimbo langu ni kuimarisha chuo kipyaa cha VETA Paramawe kwa vifaa ili kiweze kusaidia vijana wa Nkasi na Mkoa wote wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni muhimu Wizara ione uwezekano wa kuongeza majengo kwa kuwa tuna kiwanja cha ekari zaidi ya hamsini. Pia ikiwezekana chuo kiwezeshwe kutoa kozi zote zinazotolewa na vyuo vingine vya VETA nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kukupongeza Prof. Ndalichako na wasaidizi wake wote, tuko pamoja.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu kwako kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa kutayarisha na kuwasilisha hotuba ya Wizara yao kwa ufasaha zaidi katika Bunge lako hili. Katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara pamoja na Serikali Kuu kwa kuweka Baraza la Mitihani la Tanzania ambalo ni chombo muhimu sana katika Sekta ya Elimu. Hivi karibuni kumekuwa na matokeo ya mara kwa mara ya uvujaji wa mitihani katika daraja tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika suala hili ni kwamba, Wizara iendelee kuwa na makini mkubwa katika kudhibiti jambo hili. Wizara katika kutatua suala hili inabidi ilitafutie Baraza vitendea kazi kama magari ya kuweza kusafirisha mitihani kutoka Makao Makuu au sehemu moja kwenda nyingine. Tukiwa tunasafirisha mitihani hii kwa magari ambayo hayana uhakika, inatoa mianya ya kuvuja mitihani hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naipongeza Wizara hii kwa kubuni na kuendeleza mradi wa ukarabati wa Vyuo vyta Ualimu, mradi amba ni muhimu kwa kuwatengenezea mazingira bora ya walimu. Walimu ni rasimali kubwa katika jamii, ni watu amba wanatakiwa wafanye kazi kwa utulivu ili waweze kufundisha vyema kazi zao. Ushauri wangu ni kwamba, Wizara hii iendelee kuongeza ukarabati huu katika maeneo yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa

siku ya leo kwa kunipa afya njema hata kupata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anafanya na pia wasaidizi wake wote. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na viongozi wote wa Wizara na Taasisi zake zote kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya katika kuboresha Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo machache katika kuboresha sekta hii. Kwanza naomba kuishauri Serikali kurejesha upitiaji wa Sheria ya *Skills Development Levy (SDL)* ya asilimia mbili ya *SDL* iliyopelekwa Bodi ya Mikopo mwaka 2014 kwa dharura. Muda sasa umefika kurejesha hiyo asilimia mbili iende kuboresha taasisi zetu za ufundi. Kwa hali yetu ya uchumi na tunakoelekea, hasa kwa sera yetu ya viwanda na uhitaji wa wataalam katika viwanda (*technicians*) na pia ujuzi katika maeneo mbalimbali ambayo yatatoa fursa kubwa za ajira badala ya Watanzania wengi kwenda katika elimu ya ajira ya utawala na usimamizi tu (*white collar jobs*), tuboreshe shule zetu za ufundi, vyuo vya ufundi na pia kuwa na mfumo kuanzia sekondari ya kufundisha ujuzi mbalimbali ili tuweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, pili, katika sayansi na technolojia, naomba Serikali iweke bajeti ya kutosha; na pendekezo lilikuwa kwa asilimia moja ya bajeti yetu. Nchi haiwezi kwenda bila sayansi na teknolojia. Bajeti inayopelekwa katika utafiti ni ndogo sana. Bajeti yote haikidhi hata haja ya kituo kimoja ya utafiti. *COSTECH* iwezeshe zaidi, kwani ndiyo chanzo kikubwa na pekee nchini kinachoratibu masuala ya utafiti. Fedha zile shilingi tano kwa *unitya TTMS* zirudishwe. *COSTECH* walikosa baada ya Wizara kuwa na muundo tofauti. Ni chanzo cha uhakika cha mapato kwa ajili ya kuboresha utafiti.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri

pamoja na timu yake kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwatumikia Watanzania. Ninaishukuru Serikali yangu Tukufu kwa kupata mgao wa walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto. Kama ujuavyo, Lushoto ni eneo lenye milima na mabonde na miundombinu yake siyo rafiki. Kwa hiyo, zipo changamoto nydingi mno za kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, walimu waliopangisha Wilaya ya Lushoto katika Halmashauri ya Lushoto ni wachache sana kwani hawaendani na shule zilizopo katika Halmashauri ya Lushoto. Uizingatia Lushoto kuna shule nydingi za msingi na sekondari zaidi ya 100 na zaidi. Kwa hiyo, naisihi Serikali yangu sikivu ituongezee walimu ili kuondoa zero katika shule zetu, kwani Lushoto tumekuwa hatufanyi vizuri lakini sababu kubwa ni ukosefu wa walimu. Kwa hiyo, kutotupa walimu wa kutosha ni kufanya watoto wetu waendelee kufeli. Naomba Lushoto iangaliwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Lushoto ni watu wanaojituma sana katika msaragambo, hasa wa kujenga maboma ya shule za msingi pamoja na sekondari. Wananchi wale wanakata tamaa kwani majengo mengi yamejengwa na kufikia usawa wa lenta lakini majengo yale mpaka sasa hivi hayajaezekwa na nguvu za wananchi kuharibika bure. Hii inawakatisha tamaa wananchi wetu. Kwa hiyo, naiomba Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya kumaliza maboma yale yanayotokana na nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna changamoto za mabweni katika sekondari zetu. Lushoto kuna sekondari zaidi ya 20 hazina mabweni na hii pia inachangia sana watoto wetu kufeli, hasa kwa hawa watoto wetu wa kike kupata ujauzito na kushindwa kuendelea na masomo yao. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu itujengee mabweni hasa katika shule za *Gare Secondary, Mgambo Secondary, Malibwi Secondary, Kwemashai Secondary, Balozi Mshangama Secondary, Mdando Secondary, Mkunzi Juu Secondary; Prince Clous Secondary, Lushoto Secondary, Kitala Secondary, Ngwelo Secondary na Mariam Mshangama Secondary*. Shule zote hizi hazina mabweni. Kwa hiyo,

naiomba Serikali yangu ilione hili ili tuweze kuboresha elimu katika Jimbo la Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kupandisha madaraja walimu wetu pamoja na kuwapa motisha, kwani walimu wanafanya kazi kubwa sana. Pia waboreshewe miundombinu ya nyumba zao, hasa ukizingatia Wilaya ya Lushoto shule nydingi zipo vijijiini sana ambako hakuna mazingira rafiki ya kuishi watumishi wetu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Lushoto ni Wilaya kongwe, kwani wilaya hii ni ya tangu Mkoloni, lakini mpaka sasa hakuna Chuo cha *VETA*. Kwa hiyo, hii imechangia kurudisha watoto wetu nyuma, hasa wale wanaomaliza Darasa la Saba pamoja na wale wanaomaliza Kidato cha Nne. Hili limekuwa ni kundi kubwa linaloongezeka siku hadi siku. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu siku itujengee Chuo cha *VETA* katika Jimbo la Lushoto ili watoto wetu waweze kupata stadi za maisha. Sambamba na hilo, nimependekeza Jimbo la Lushoto kijengwe Chuo cha *VETA* kwani ndiyo katikati ya majimbo yote matatu ya Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hizi shule shikizi, naiomba Serikali yangu sikuwe kusajili shule hizi, hata kama ina vyumba vinne. Nayasema hayo kwa kuwa wananchi wakiamua kuanzisha jambo lao huwa halirudi nyuma. Mfano, katika Jimbo la Lushoto nina shule shikizi mbili; *Mgambo Primary School/na Kaghambwe Primary School*. Shule hizi mpaka sasa zina vyumba sita, kwa hiyo, niombe shule hizi zisajiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza mchango wangu kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu wote wanaohudumu kwenye Wizara hii kwa kazi nzuri na kubwa ya kusimamia elimu nchini, hasa Sera hii ya Elimu Bure. Sera

hii imewezesha watoto wengi kupata elimu ambayo ni haki yao ya msingi.

Mheshimwia Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kufanya maamuzi muhimu ya kutekeleza Sera hii ya Elimu Bure ambayo ni hitaji la nchi yetu kwa muda mrefu. Kwa hili Mheshimiwa Rais amethubutu na amefanikiwa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa Taifa letu linaleelekea kwenye uchumi wa viwanda, ipo haja kubwa sana ya kuimarisha vyuo vya ufundi kuanzia vile vya *VETA* hadi vya mafundi mchundo (*FTC*). Katika kuimarisha vyuo hivi ni bora vyuo vya ufundi visichanganywe na kozi nydingine kama vile kozi ya urembo na ulimbwende. Jambo hili limekuwa likivunja hadhi ya vyuo vyetu. Vilevile, Vyuo vya *VETA* visiwe kimbillio la wale waliofeli *Form Four* na Darasa la Saba, ifike wakati hata wale waliofanya vizuri kwenye masomo ya Sayansi wapelekwe *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale ndiyo wilaya iliyo mbali sana na Makao Makuu ya Mkoa wa Lindi ambako kuna Vyuo vya *VETA*, Ualimu na Afya. Hivyo, vijana wengi wanashindwa kumudu kupata elimu ya vyuo hivyo. Hivyo Serikali ione umuhimu wa kutujengea Chuo cha Ufundis, *VETA*. Halmashauri imeshaanza kujenga maboma mawili ya madarasa, hivyo naiomba Serikali kuokoa nguvu za wananchi kwa kuwapatia Chuo cha *VETA*. Vijana wengi wanaoshindwa kuendelea na masomo ya juu kwa kukosa nafasi wangeweza kupata elimu hiyo ya *VETA* kwa karibu badala ya kwenda Lindi ambako ni mbali na gharama ni kubwa. Liwale tuna uhitaji mkubwa wa Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa vyuo vya ufundi ni muhimu sana kuhudhuria mafunzo kwa vitendo, lakini wanafunzi wengi wanashindwa kuhudhuria kikamilifu kutokana na changamoto mbalimbali, kama vile nauzi za kwenda na kurudi makazini na chakula cha mchana wanapofanya kazi viwandani. Naomba Serikali ifikirie

kuwapatia posho za mafunzo viwandani wanafunzi wanaohudhuria mafunzo kwa vitendo. Hakuna maana ya kuwapeleka watoto katika shule/chuo cha ufundi kama elimu hiyo haitaambatana na elimu kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie uhaba wa walimu, hasa walimu wa Sayansi. Hapa napenda nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuanza kuajiri walimu. Nishukuru kwa Halmashauri yangu ya Liwale kuwa mionganini mwa Halmashauri zilizopata mgao wa walimu hao japo limekuwa kama tone la damu baharini, kwani uhaba wa walimu ni mkubwa sana Wilayani Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu nyingi zina walimu watatu tu. Shule zenye walimu wengi ni zile zenye walimu wanenye. Hata pale *RAS* anapotaka kufanya mgawazo wa watumishi mkoani anakosa rasilimali fedha ukizingatia katazo linalomkataza *RAS* kuhamisha mtumishi bila ya kuwa na fedha. Hivyo, naishauri Serikali kutenga fedha mara kwa mara kwa ajili ya kufanya mgawazo kwa walimu hata pale panapokuwa na umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Udhibiti Ubora wa Elimu ni kitengo muhimu sana. Ili kuwe na elimu bora, naishauri Serikali kuongeza uwekezaji katika kitengo hiki kuanzia ikama ya watumishi hadi vitendea kazi ikiwa ni pamoja na magari. Mfano, katika Halmashauri yangu ya Liwale, kitengo hiki hakijawahi kuwa na gari japokuwa mtawanyiko wa kata na shule zetu ni mkubwa sana. Zipo shule hazijawahi kuona Wakaguzi kwa zaidi ya miaka mitano. Ukiuliza watasema hawana usafiri hata wa pikipiki. Hivyo, naiomba sana Serikali kutupatia gari litakalowawezesha wakaguzi na idara ya elimu kwa ujumla. Hadi sasa Idara ya Elimu Msingi na Sekondari wote hawana magari, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ikaitazame Liwale kwenye Idara ya Elimu ili tutoke kwenye kuburuza mkia kwa Mkoa wa Lindi na Taifa kwa ujumla.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa natoa pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri wanayofanya. Pia napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wizara nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napongeza kwa kuongeza fedha za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Ombi langu ni kwa ajili ya angalizo kwa wanafunzi waliotokea kwenye shule za *private*. Kigezo cha kutowapatia mikopo wanafunzi waliopitia shule za *private*, kuwanyima mikopo, nashauri lifanyiwe kazi. Wananchi siku hizi wamepata mwanga na wanapenda watoto wao wasome kwa hali yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wazazi wengine wanasomesha kwenye hali ngumu, hasa wenye mlezi mmoja kama mtoto wa mama ntilie au akina mama wengine wanadunduliza hela ili mtoto wake asome. Mimi ni shahidi Morogoro na mikoa mingine kuna akina mama wanasomesha watoto wao kwa kupitia kulima na kuuza mchicha au kwa kupika maandazi au chapati. Mheshimiwa Waziri, tafadhali sana kigezo cha wanafunzi kusoma *private* kifanyiwe uchunguzi wa ndani, watoto wengine waliopitia mkondo huu wanapaswa kukopeshwa asilimia kubwa kwani hali yao ni duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa kazi nzuri iliyofanyika kwa ukaguzi na kubaini vyuo vikuu venye upungufu kwa ubora wake kama Chuo Kikuu. Namshauri sana Mheshimiwa Waziri kuhusu ufuatiliaji wa mienendo ya vyuo hivi, ni muhimu kuliko kwenda kama zimamoto na kuvifunga vyuo (baadhi) kwa kutokuwa na ubora. Ni bora vyuo vikafuatiliwa na kupewa ushauri. Vyuo hivyo vikijirekebisha kufuatana na upungufu, viendelee na kutoa elimu kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo hivi hasa ni vya binafsi vikiwepo vingi vya dini. Vinapofungwa ghafla wanafunzi wanapata shida kwa kubadilishwa na kupelekwa vyuo

vingine. Walimu waliokuwa wanafundisha vyuo hivyo wanapoteza ajira zao na mpaka sasa hawajui kinachoendelea. Naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kuahirisha, nipate ufanuzi kuhusu hatima ya wanafunzi na walimu waliokuwa kwenye vyuo hivi, hasa walimu na wafanyakazi, hatima yao ya ajira ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kitengo hiki cha ukaguzi kipewe fedha zote zilizotengwa pamoja na miundombinu kama magari. Ili kuboresha elimu yetu, ni muhimu kuboresha kitengo hiki cha ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kuna kanda ambazo hakuna *technical college* hata moja. Vyuo hivi vinasaidia sana wahitimu kujajiri hasa wale waliomaliza *Form IV* na *Form VI*. Mheshimiwa Waziri, Kanda wa Ziwa wanaomba angalau chuo cha ufundi kimoja. Ni mengi mazuri yanayofanywa na Serikali yangu ya Awamu ya Tano, naomba nishauri hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bila utafiti na pia walimu wa sayansi ni tatizo. Nashauri fedha inayotengwa kwenye utafiti na hasa vyuo vikuu zitolewe zote ili utafiti uendelee. Ni muhimu sana kuendelea kupunguza hili tatizo la walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Kila Wilaya Kuwa na Chuo cha *VETA* na hasa wilaya za pembezoni lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Serikali kwa kuendelea kuimarisha elimu nchini. Pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo Msaginya (Katavi) ni muhimu sana kwa kuelimisha vijana

katika sekta mbalimbali kuanzia watoto wenyewe elimu ya msingi. Chuo hiki kimepata ajili ya kuungua moto mara mbili ndani ya mwaka mmoja. Hivyo, tunaomba Serikali kuititia Wizara kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili kwa kuwa watoto wanaishi katika mazingira magumu sana. Hivyo, tunaomba uwezeshaji ufanyike kwa haraka. Uongozi wa chuo umeshaleta barua Wizarani kwa taarifa na utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa kinara katika kutoa elimu isiyo na mfumo rasmi (*non-formal education*). Tunayo *UPE* na Elimu ya Watu Wazima na nyinginezo, napenda kupata maoni ya Serikali, je, mpango upi uliopo wa kuboresha elimu hii? Pia Serikali imetenga kiasi gani kwa ajili ya mfumo huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *Teachers' Professional* imepitishwa lakini bado inahitaji maboresho yafuatayo: Moja, uteuzi wa *regional and district representative*. Katika sheria uteuzi unafanywa na Waziri wa Elimu. Nashauri uteuzi ufanywe na *registrar* kwa kushirikiana na bodi. Pili, *Teachers' Professional*/haina mamlaka ya kuhakiki walimu na taaluma zao, hivyo mitaala iwe inapitiwa na Bodi ya *Teachers' Professional* ili kuhakikisha wahitimu ni watu wenyewe sifa zinazotakiwa, kama *professional bodies* nyingine zinavyofanya, mfano Uhasibu, Sheria (*Law School*) na Manunuzi. Tatu, utunzi wa kanuni uzingatiwe kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba Serikali iendelee kukarabati shule kongwe za msingi katika Halmashauri ya Nsimbo; Songambele, Isinde, Ikolongo, Katambike, Mtapenda, Isanjandugu na Uruwira.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja hii. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na uongozi wote wa Wizara hii kwa kuiongoza vyema Wizara hii na mengi yameonekana kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iongezewe bajeti, hasa katika kuboresha miundombinu katika shule za msingi. Nyumba na madarasa yaliyojengwa kabla ya Taifa kupata uhuru yamechakaa sana na mengi kubomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Wanging'ombe pamoja na Mbunge tumehamashana kujenga maboma ya madarasa na nyumba za walimu. Kwenye llani ya CCM 2015 - 2020 imeelekeza kushirikisha nguvu za wananchi na Serikali itapeleka mchango wake katika bajeti ya TAMISEMI na Wizara. Fedha zimekuwa zinatengwa lakini zimekuwa hazipelekwi kwenye Halmashauri husika. Naomba Wizara iliangalie jambo hili ambalo wananchi wametekeleza wajibu wao. Wilaya ya Wanging'ombe mpaka Oktoba, 2018 inahitaji shilingi bilioni moja kukamilisha maboma katika Sekta ya Elimu Ikiwepo sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wameongelea suala la uhaba wa walimu, ninazo shule zaidi ya 20 zenyne walimu chini ya watatu kwa shule zenyne madarasa hadi darasa la saba. Naomba Serikali iajiri walimu na itoe mgawanyo sawa. Nimeona shule za mijini zina mlundikano wa walimu kwa kisingizio cha kuolewa, kukaa karibu na hospitali na kadhalika. Shule zilizo vijijini zimesahauliwa. Naomba jambo hili lirekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, alipofanya ziara Mkoa wa Njombe, Aprili, 2019, ametoa maelekezo kwamba majengo yaliyopo Kijiji cha Soliwaya, Wanging'ombe ambayo yalitumiwa na wasimamizi wa ukarabati wa barabara ya Nyigo - Makambako - Igawa yaanzishe Chuo cha VETA Wilaya ya Wanging'ombe. Halmashauri ya Wanging'ombe imemwandikia barua Mheshimiwa Waziri juu ya suala hili na nakala iliyopelekwa kwa Katibu Mkuu, ninayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wanging'ombe wanataka kujua, hili agizo la Mheshimiwa Rais litatekelezwa lini? Naomba Mheshimiwa Waziri wakati

unaahirisha bajeti yake aseme kitu, wananchi wa Wanging'ombe wasikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa namwita Mheshimiwa Waziri *Comrade* kwa jinsi alivyo siku kwa hoja za Wabunge na ninayo imani kuwa katika hili atalitengenezea utaratibu; ili litekelezwe wapewe, uwezekano. Tayari Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano wameshaiandikia Halmashauri ya Wanging'ombe utayari wao wa kukabidhi majengo hayo kama tulivyoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wameongelea kuhusu hoja ya kuboresha utaratibu wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Vyuo Vikuu ambao umeleta malalamiko na kiasi fulani kinawabagua wahitaji. Kwa kuwa fedha hizi ni mkopo na utatakiwa kurudishwa, kigezo cha kuangalia aina ya shule walizosoma hakina tija kwa sababu walio wanafunzi wanaopata ufadhilli wengine wazazi wao wamekosa uwezo wa kuapeleka vyuo vikuu. Naomba sana wanafunzi wote wapewe mikopo hata kama viwango vitatofautiana, lakini kuwakatalia kabisa kumesababisha watoto wengi kukosa elimu ya vyuo vikuu.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutupatia fursa ya Elimu Bure. Pamoja na kusaidiwa na Serikali, tuna shule ambazo ni za zamani sana hasa Mbulu *DC* mfano Shule ya Msingi Maskaroda inahitaji ukarabati kwani majengo yake ni ya zamani, tangu 1955 na watoto ni wengi. Tunaomba Wizara ione namna ya kusaidia ujenzi wa madarasa. Pia katika Sekondari wananchi wa Maretadu wamejenga Sekondari ya Kidato cha Tano bwalo na madarasa manne. Tunaomba msaada wa kuongeza bwalo kwani wananchi wameamua kuchangia majengo ili kusaidia kuanzishwa kwa Kidato cha Tano na Sita Mbulu *DC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule maalum zipewe kipaumbele katika bajeti ya Waziri wa Elimu kwani bila kufanya hivyo wanasahaulika sana. Hivyo naomba zipewe kipaumbele. Mfano, Shule ya Viziwi Dongobesh na nyingine

zilizomo katika nchi. Walimu wanahitajika sana katika shule hizi za wale mavu hasa wale wenye ujuzi wa kuunda hao watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo Sekondari Mbulu *DC* zimejengwa na wananchi, zinahitaji msaada wa kujengewa madarasa na nyumba za walimu, mfano Dr. Olsen Sekondari ina wanafunzi wengi na hawana madarasa na bweni; na watoto wa Kidato cha Tano na Sita wanapata taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za Walimu wa Sayansi ni kubwa sana katika Shule nyingi za Sekondari, hivyo kupelekeea ufaulu kuwa chini. Hivyo tunaomba Walimu wa Sayansi waongezwe ili kukidhi haja hiyo.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vyuo vya Ufundji Stadi (*VETA*), ni muhimu kukawa na mtawanyiko mzuri zaidi nchi nzima ili kuwapatia wahitimu husika *Form IV, STD VII*, hata *Form VI/wasiopata fursa nyinginezo "Alternative Route"* kuelekea maendeleo binafsi na Taifa kwa ujumla. Wilaya ya Tunduma iko mpakani, ni ya siku nyingi (1905) na iko mbali na Vyuo vya aina hiyo, (ukiacha chuo kimoja tu binafsi ambacho *accessya* wananchi wengi ni *limited* kutokana na ghamra kuwa juu. Tunaomba Wilaya hii ipewe kupaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za kuwaajiri Walimu waliohitimu katika vyuo na ngazi mbalimbali na wakati kuna uhaba mkubwa wa walimu katika shule zetu, napendekeza Serikali iweke utaratibu wa kuwapa mikataba ya muda mfupi mfupi walimu hao kwa "kujitolea." Ni wazi kutajitokeza mahitaji ya *Resources* kidogo. Hata hivyo, wapo baadhi watajitokeza kufanya hivyo. Wanachohitaji ni kutambuliwa na kuwafanya wawe *active* katika taaluma. Inawezekana pia "motisha" ikawa ni kupata kipaumbele ajira zinapojitokeza.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ina upungufu mkubwa sana wa Walimu na uhaba wa Walimu hasa Walimu

wa Sayansi. Vilevile Walimu wa kike, tunaomba Serikali ituongezee Walimu kwani kutokana na tatizo hili mara nyingi Halmashauri hii inakuwa chini sana katika ufaulu wa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo shule shikizi zifuatazo ambazo zimeanzishwa na kujengwa kwa nguvu za wananchi, lakini Serikali inachelewa kuzifungua na kusababisha watoto wengi kutosoma. Shule hizo ni Kirando na Karanda. Tunaomba shule hizo zifunguliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri Serikali kupandisha madaraja ya walimu ambapo ni kwa muda mrefu hawajapandishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kulipa posho ya mazingira magumu kwa Walimu. Serikali itoe posho kwa Walimu wanaofundisha katika mazingira magumu ya Vijiji kusiko na barabara nzuri, kwani wanatembea umbali mrefu kufuata huduma. Pia wapandishiwe mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya shule za Sekondari za Kata bado hazijapelekewa vifaal licha ya kuwa na majengo ya maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la kukosekana kwa mabweni hasa kwa watoto wa kike ambao wanatembea umbali mrefu unaowasababishia kukumbana na vishawishi vingi na hatimaye kushindwa kuhitimu masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ikiwa ni pamoa na zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana na kwa kumwalika Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph

Magufuli kuja kukifungua Chuo cha VETA cha Namtumbo na hivyo kikipandisha hadhi. Nawaomba mkamilishe nyumba za walimu na mabweni ya wanafunzi ili chuo kianze kutoa mafunzo bila kusahau vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha mlizotoa kuunga mkono ujenzi wa Shule ya Msingi ya Miembeni katika Kijiji cha Likuyu Mandela ni shilingi milioni 180 na shule ya kisasa kabisa imekamiliaka kujengwa na imeanza kutumika. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usimamizi thabiti wa Sera ya kila Kata kuwa na Sekondari moja ya kutwa, sera hii imewezesha Wilaya ya Namtumbo kuwa na Sekondari 23 katika Kata 20. Ni Kata moja tu haina Sekondari kutokana na kuanzishwa hivi karibuni (Kata ya Msisima). Tuombe tu, shule hizi za kutwa zinahudumia Vijiji na Vitongoji vilivyosambaa kwa zaidi ya kilometra 5 - 26 na hivyo kulazimika wanafunzi kupanga ama kuwa na mabweni katika shule hizo kinyume na madhumuni ya kuanzishwa kwa shule hizo za kutwa. Mazingira hayo tuomba yavumiliwe badala ya kupigwa vita na Idara ya udhibiti ubora wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo imeundwa na inafanya kazi vizuri. Hongereni sana, maana Bodi hii imefanikiwa kuwahudumia baadhi ya wanachuo wenyе uhitaji. Katika eneo hili nampongeza sana Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa William Tate Olenasha, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kufuatilia wanachuo wenyе uhitaji mkubwa wa mikopo katika Wilaya ya Namtumbo na nchi nzima kwa ujumla ambao kwa namna moja ama nyingine vigezo vilivyowekwa na Bodi na njia inayotumika, uthibitishaji wa vigezo hivyo vinaifanya Bodi kuwakosa wenyе uhitaji na kuwapa wasio nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri anatusikia Wabunge na ni mwepesi wa kufuatilia taarifa tunazompa na pale inapoabitika kuwa haki haikutendeka, huirejesha haki kwa mhusika. Hakika unaye msaidizi mwenye hekima ya Mfalme Suleiman anayetajwa katika Biblia na anaitendea haki taaluma yake ya Sheria. Hongera sana Profesa Joyce

Lazaro Ndalichako na kupitia kwako tumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukuibua wewe na Naibu wako na kuwakabidhi uongozi wa Wizara hii nyeti ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kipindi hiki muhimu cha mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko sababu nyingi, itoshe kuishia hapa, naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie katika haya yetu wana-Namtumbo:-

(a) Tukamilishiwe ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Namtumbo;

(b) Tuondolewe waraka unaozuia ujenzi wa mabweni katika shule zetu za Sekondari za kutwa;

(c) Turekebishiwe mfumo unaotumika katika kuwapa wahitaji wa mikopo kutoka *HESLB* ili wahitaji halisi wasiachwe solemba na kukatisha ndoto zao za kutaka kuijendeleza kielimu;

(d) Naomba Chuo cha Ualimu kinachomilikiwa na *SONAMCU* kilichoko katika Kijiji cha Nahoro kiwezeshwe kuendelea kutoa huduma; na

(e) Naomba ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Mputa ufanyike kwa wakati uliopangwa ili u-yatima wa chuo kile ufutike miyoni mwa wanafunzi na Walimu wa chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha. Naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri, Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge kwa asilimia mia moja.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi. Tunaishukuru sana Serikali kwa kutuletea zaidi ya shilingi milioni 400 kwa ajii ya kuboresha miundombinu ya shule za msingi. Tumeweza kuboresha shule za msingi kadhaa

ziliwikemo Shule ya Msingi ya Kisesa, Shule ya Msingi ya Mwakipanga, Shule ya Msingi ya Chipukizi Mjini ya Igunga na shule nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru pia kwa Serikali kutuletea zaidi ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Shule za Zekondari Nanga, Bukoko, Igunga na nyingine. Bado changamoto ni nyingi, tumeleta maombi ya kuanzisha shule za *high school* mbili; Shule ya Sekondari ya Bukoko kwa ajili ya wasichana na Shule ya Sekondari ya Igurubi kwa ajili ya walemaru. Je, Wizara imeliingiza ombi letu hili kwenye bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tena kwa fursa hii.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu Mheshimiwa Prof. Ndalichako na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ole Nasha na Makatibu kwa hotuba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Tano ikiwemo ukarabati wa shule kongwe nchini. Ongezeko la mikopo elimu ya juu, ukarabati wa ujenzi wa vyuo nchini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufanuzi kwa mambo yafuatayo: ukarabati wa shule ya Lugalo Sekondari Mkoa wa Iringa. Shule hii inafundisha pia watoto wenyе uhitaji maalum. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha shule hii inapatiwa kipaumbele katika ukarabati wa miundombinu ikiwamo na ujenzi wa uzio kwa sababu wanafunzi wenyе uhitaji maalum wanasoma kwa shida sana? Naipongeza Serikali kwa kupeleka vifaa kwa wanafunzi wenyе uhitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie Sera ya Elimu ya kubadili mitaala mara kwa mara bila kuwapatia mafunzo walimu. Changamoto hii ni kubwa sana. Serikali inaweka mkakati gani wa kuhakikisha kabla ya kubadilisha mitaala waalimu wapatiwe mafunzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wetu wengi wanafanya kazi nzuri katika mazingira magumu. Je, nini mkakati wa Serikali kutoa motisha kwa walimu wa shule zinazofanya vizuri kwenye matokeo ya Kitaifa? Ni vema zingeandalila tuzo maalum ili kuleta hamasa kwa shule na walimu wengi kufanya vizuri. Sambamba na hilo, walimu wamekuwa na changamoto kubwa sana ya upandishwaji wa madaraja kwa walimu walioajiriwa kuanzia mwaka 2012 - 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha inatenga pesa ya kutosha ili tafiti ziweze kufanyika? Kwa sababu maendeleo ya kisayansi na teknolojia ambayo ndiyo msingi wa maendeleo ya kiuchumi katika Taifa lolote lililoendelea tunategemea sana kiwango cha ugunduzi na ubunifu unaotokana na elimu bora inayotolewa. Vijana wetu wamekuwa na ubunifu mbalimbali, sijaelewa Serikali inawasaidiaje wabunifu au wagunduzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mkurugenzi, ameweza kusimamia vizuri sana japo kuwa uangaliwe utaratibu wa kutoa mikopo watoto yatima waliokuwa wanasomeshwa na mfadhili, uwepo utaratibu wa kuwatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuipongeza Wizara kwa wasilisho zuri na jithada zinazofanywa kuboresha elimu. Pamoja na pongezi hizi, nina mchango kidogo kwa baadhi ya maeneo. Elimu yetu ilenge kuibua na kukuza vipaji hasa mashulenii. Kuna watoto tangu shule ya msingi wanaonyesha vipaji vikubwa sana. Laiti watoto hawa wangetiliwa maanani wakaendelezwa kwa namna ya tofauti wangkuja kusaidia sana Taifa letu. Utakuta mtoto ana akili sana ana kipaji fulani lakini wazazi kwa kukosa uwezo mtoto yule anaishia njiani. Hivyo, tunajikuta tunapoteza rasilimali kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni mazingira mazuri ya kusomea. Kuna tatizo ambalo kwa sasa tunaweza tusilione ila baadaye likawa janga la Taifa. Watoto wamekuwa wakibeba mabegi yenyewe mzigo mzito sana kutokana na kutokuwa na ratiba maalum. Serikali ingeangalia uwezekano wa kujenga angalau makabati au kuhakikisha kunakuwa na ratiba maaum na zinafuatiliwa ili kupusha matatizo ya uti wa mgongo yanayoweza kuwapata watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waalimu wawe *motivated* hasa katika mishahara, mathalan wanapofanya kazi kijijini, mshahara uwe juu zaidi ya aliye mjini ili kuondoa tatizo la walimu wengi kukwepa kwenda vijijini. Shule za *boarding* watoto wanahitaji sana uangalizi. Watoto wengi wanaanzisha mahusiano yasiyofaa. Hili lifanyiwe utafiti na awepo mtu wa kuwaangalia watoto hawa hasa kipindi cha usiku. La sivyo, watoto wataendelea kuharibika mashulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la taulo za kike hasa vijijini ni muhimu kwani watoto hawapati nafasi ya kusoma vizuri. Mfano shule unakuta haina vyoo vya kutosha, haina maji kiasi kwamba mtoto katikati ya masomo anaweza kwenda kujisitiri kwa wale wanaotumia njia nyingine zaidi ya *pad*, hivyo kuamua kukaa nyumbani mpaka pale atakapomaliza siku zake. Hivyo, kukosa masomo kwa kipindi chote hicho na wengine wanaenda hadi siku saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi kwa kukosa uwezo wa kifedha kwa wazazi au walezi wao wamejikuta hawana uwezo wa kufika kidato cha nne na kuendelea kwa kujibana na kuhangaika sana. Unakuta wanapata nafasi ya kujifunza ufundi stadi, udereva na ni katika vyuo vyetu vinavyotambulika kama *VETA*, *NIT* lakini linapokuja suala la ajira rasmi wanakosa sifa. Serikali iwaangalie sana hawa vijana na wengi wao wana vipaji vikubwa na ufanisi mkubwa. langaliwe ni jinsi gani wanaweza kuajiriwa au kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure bado ina changamoto nyingi sana. Kuna wazazi, walezi wengine

hawana hata uwezo wa kununua sare za shule, madaftari, vitabu na nauli ili watoto hawa waweze kufikia hiyo elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. LUCIA M. MLLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwako bado na tatizo la utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu hasa watoto wanaotoka katika familia duni ambapo hawana uwezo wa kufuatilia na hawana watu wanaoweza kuwasemea. Nina mfano wa wanafunzi ambao ni wa kike na walifaulu masomo yao ya sayansi na mmoja alikuwa ni mwenye ulemavu, lakini ameomba mkopo mfululizo kwa miaka mitatu hakufanikiwa hadi alipokuja kwangu na kuomba nimsaidie kwa sababu awali shirika langu la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na yatima lilimsaidia toka shule ya msingi hadi sekondari. Baadaye shirika likawaachia ndugu waendelee kumhudumia lakini hatimaye huyu alikatishwa tamaa na kukosa mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifuatailie hasa watoto yatima na wanaoishi maisha hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu kufungia Vyuo vya Dini. Kumekuwa na ufungaji wa Vyuo Vikuu kiholela. Kwa kuwa vyuo hivi vimesajiliwa na Serikali, basi wapate maelekezo na kukaguliwa mara kwa mara; na kunapokuwa na upungufu warekebishwe badala ya kuwafungia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za binafsi zisaidiwe kulipia mitihani. Kwa kuwa elimu bila malipo ni kuwa Watanzania wote, basi naomba watoto wanaosoma kwenye shule binafsi wapewe pia ruzuku kwa ajili ya mitihani na hasa kwa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana wanaotoka katika mazingira hatarishi na yatima ambao wamesaidiwa na mashirika yasiyo ya kiserikali, wamefaulu kwenda VETA za

Serikali, wamefukuzwa. Wanadai mashirika hayo yawalipie wakati mashirika hayo yamekuwa yakijitolea tu. Matokeo yake vijana hawa wanakatishwa tamaa na kuacha vyuo. Nina mfano halisi wa kijana ambaye amefukuzwa kule Chuo cha VETA cha Morogoro, anaitwa John Mwingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mkanganyiko mkubwa sana wa mtaala ya shule za msingi. Kulitoka mtaala wa shule za msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la sita na kwamba watoto wataishia darasa la sita na kujunga na sekondari. Hadi sasa hivi wanafunzi wanaendelea kufundishwa kwa mtaala huo ambapo hata vitabu vyake havipo. Hivyo walimu wanafundisha katika mazingira magumu. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe mwelekeo wa nini kifanyike ili kurekebisha mkanganyiko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni tatizo la uhamisho wa walimu. kuna walimu wanakaa shule za vijijini kwa muda mrefu hadi wanazeeka huko vijijini. Wanaishi katika mazingira magumu bila hata motisha. Naomba wakikaa miaka kadhaa wahamishiwe maeneo ambayo yana unafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kupungua kwa bajeti ya elimu. Bajeti ya Wizara ya elimu pekee imepungua kutoka shilingi triliioni 1.408 kwa mkwa 2018/2019 hadi shilingi triliioni 1.357 kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Upungufu huu ni wa shilingi bilioni 51. Elimu haiwezi kuwa bora kwa mfumo huo. Naomba pesa zinazotakiwa kwenye Wizara hii ya Elimu ziende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Kwa kuwa Jimbo la Isimani lina shule zaidi ya 50 za msingi na 13 za Sekondari na lipo vijijini, vijana wengi wanaomaliza sekondari hawana chuo chochote cha mafunzo ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Isimani ndilo lenye eneo lote la *Ruaha National Park* na wazalishaji wakubwa wa mazao ya kilimo hususan mpunga. Pia wana nia ya ujenzi

wa nyumba bora, hivyo kuwapo kwa Chuo cha Ufundı chini ya VETA itasaidia vijana wa Iringa vijijini hususan Jimbo la Isimani kujifunza masomo ya ufundı mbalimbali na masomo ya utalii na hoteli. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ikubali kujenga Chuo cha Ufundı – VETA Jimboni Isimani wilaya ya Iringa Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza wachangiaji sasa tunaingia upande wa Serikali na tunaanza na Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, katika michango ya Waheshimiwa Wabunge kuna mambo ambayo yamezungumzwa, ambayo yanahusiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kuna hoja zimetolewa na nimejaribu kuititia kitabu cha Kambi Rasmi ya Upinzani, wameandika *data* nyingi humu, lakini nyingi siyo za kweli na nilipojaribu kufuatilia nikagundua kwamba hizi zilikuwa zinaandikiwa pale *African Dream*, wakishirikiana na wenzao. Hizi *data* ni za *African Dream*, kwa hiyo, naomba mnisikilize niwape data za Serikali, ambaye ni *custodian* wa *information* hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walisikiliza vizuri wakati Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Utumishi anazungumza hapa, alitoa tamko la Serikali kwamba madai ya Walimu na madaraja na maslahi mengine yataanza kushughulikiwa kuanzia Mei Mosi, maana yake kesho, lakini pia kuna maelekezo yametolewa kwa vyombo mbalimbali vinavyoshughulika na utumishi wa umma, hiyo kazi itafanyika. Kwa hiyo, kimsingi hili pia halipo kwenye Wizara ya Elimu, lipo utumishi, lakini limeulizwa hapa nikasema nilitolee kauli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hoja imezungumzwa ya elimu msingi bila malipo na kwa bahati mbaya sana nilimsikia Mheshimiwa Yosepher Komba akizungumza, kwa namna ambayo kwa kweli alikuwa

anabeza, lakini kwa kweli ukifuatilia namna ambavyo mpango huu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Awamu ya Tano umewasaidia Watanzania walio wengi, *enrollment* imeongezeka, watoto wa shule ya msingi na madarasa ya awali wameongezeka sana. Kila mwezi Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, anapeleka shilingi billioni 23 kwa ajili ya elimu msingi bila malipo. Kwa hiyo, siyo jambo la kubeza kwa kweli ni jambo la kupongeza na Watanzania wengi walio maskini, watoto wao wanaingia shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wamezungumza kwamba watu wanafelifeli, siyo kweli, tunao watoto ambao wamefaulu vizuri sana kutoka shule za kata na wameenda mpaka shule za vipaji na tutawapa taarifa ya majina yao kwa ajili ya kumbukumbu kwa ajili ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwaka 2016/2017, Serikali iliajiri Walimu wa sayansi 3,081, mwaka 2017/2018, walimu 2,767 wa sekondari na msingi, lakini hapa tunapozungumza, tumesambaza Walimu 4,500, mionganii mwao Walimu 3,088 wote ni Walimu wa sayansi, *no*, ni Walimu wa shule ya msingi, lakini 1,400 ni Walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge alizungumza, maeneo yale ambayo yalikuwa na upungufu mkubwa sana kwa upande wa masomo ya sayansi tumepeleka. Ni kweli kwamba hawatoshi lakini wameenda. Kumbukumbu ya kitabu chao hili cha *African Dream*, kinaonesha kwamba ni upungufu karibu Walimu 91,000, siyo kweli. Tuna upungufu wa Walimu ni kweli tunakubali, 66,485 kwa shule za msingi na Walimu 14,080 kwa shule za sekondari. Mpango uliopo, kila mwaka tutakuwa tunaajiri Walimu kupunguza *gape* hili na hawawezi kuchukua miaka 10 kama walivyosema, siyo kweli, itachukua muda mfupi kwa mpango ambao Mheshimiwa Rais amesharidhia, tunaziba ma-*gape* ya watu waliofariki dunia, watu waliosimamishwa kazi kwa makosa ya kiutumishi na mambo kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile madarasa yamejengwa, kwa mfano, mpaka kufikia Februari, 2019 shule za msingi yamekamilishwa madarasa 2,840, tunaendelea kujenga madarasa 2,638, hapo yanaendelea kujengwa. Matundu ya vyoo 76,700 na yanaendelea kujengwa 3,004, nyumba za Walimu 720 na tunatengeneza madawati 135,000. Hii kazi kubwa inafanyika chini ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mpango wa shule shikizi, tumejenga shule shikizi kupunguza umbali kati ya shule na shule 255,000 kwa kutumia bilioni 18.5 zimefanya kazi kwenye mikoa tisa na halmashauri 63, madarasa 502, Ofisi 251, matundu ya vyoo 1,255, maktaba 34 na maboma 223.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametoa hoja hapa ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwamba aliahidi kutoa fedha za mabona shilingi bilioni 29, naomba nitoe taarifa kwamba juzi tulitoa fedha shilingi bilioni 29.9 kwa kuhusiana na Wizara ya Elimu na tumepeleka kujenga maboma mbalimbali zaidi ya 2,300 yanaendelea kujengwa. Hapa tulipo tunapeleka mpango mwingine wa kukamilisha maboma ya shule za msingi nchi nzima kwenye halmashauri zote na majimbo yote ikiwezekana. Hii ni kazi nzuri ambayo inafanyika ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi, chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye mpango wa 2019/2020 tutajenga nyumba za Walimu 364 kwa kutumia shilingi bilioni tisa, lakini sekondari maalum 26 kila mkoa kwa ajili ya watoto wa kike, kuititia mradi wa *SEP*, lakini *EP4R* tunanunua magari 26 kuratibu elimu kwa ngazi ya mkoa, kila mkoa watapata gari jipya, tunajenga majengo ya utawala 50, nyumba za Walimu 800, mabweni 300, matundu ya vyoo 1000, kumbi za kufundishia kwa maana ya kumbi za wanafunzi zile mbalimbali 2,000 zinajengwa, lakini shule kongwe zinakarabatiwa 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni mambo makubwa ambayo yanafanyika katika nchi hii na ni muhimu sana tukaitia moyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja la mwisho, kuna hoja inapotoshwa kwamba Serikali imesema elimu bure, kwa hiyo, michango hairuhusiwi. Umetolewa Waraka wa Wizara ya Elimu ambaao umeanza kufanya kazi Januari, 2019, mwongozo umetolewa. Tukubaliane nchi hii kwa ukubwa wa taifa hili na upungufu wa fedha uliopo, haiwezekani tukaishi kama ndege bila kuchangia chochote. Serikali ilitoa fedha, bure, tumeondoa ada na shule za sekondari zingine tumepeleka fedha na mabweni yanajengwa miundombinu inaimarishwa na Walimu wanalipwa na watumishi wengine wa Serikali, lakini wananchi wenye uwezo watachangia kadri ambavyo uwezo wao utaruhusu na Serikali imetoa huo mwongozo, kuanzia ngazi ya kijiji, ngazi ya kitongoji, ngazi ya kata, Waheshimiwa Wabunge, kwenye mikoa. Kilichozuiliwa ni kwamba, asitolewe mtoto darasani eti kwa sababu ya mchangano mzazi wake au mlezi hajachanga, hapana. Kama mtoto anadaiwa, mzazi na Walimu wasimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tukasema Walimu wasisimamie michango, kwa sababu ilionekana kwamba Mwalimu anapokwenda kudai michango kwa wazazi anajenga chuki na usimamizi unakuwa mgumu. Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi watasimamia zoezi la michango, wenye uwezo wananchi wa kawaida, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wengine wachangie kile ambacho wanaweza. Ukichimba kisima cha maji sawa, ukijenga darasa sawa, tundu la choo sawa, darasa sawa, nyumba ya mwalimu sawa, hii kazi ni ya Watanzania wote, tushikamane, tuunge mkono kazi nzuri ya Serikali ili mambo yaweweze kuboreshwa na Watanzania wote na watoto wetu waweze kusoma vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Jiandae Naibu wa Wizara ya Elimu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naomba niazé kwa pongozi mahususi kwa Mwalimu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na timu yake mahiri ya Walimu waliobobe aambao amewapa kazi ya kusimamia sekta hii ya elimu hususan dada yangu Profesa Ndalichako. Shemeji yangu Dkt. Ole-Nasha na timu nzima ya Maprofesa aambao wamekaa kule nyuma ya kioo kwa kazi nzuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kabisa kwa kusema naunga mkono hoja. Kulikuwa na hoja kwamba fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka huu wa fedha, zitolewe zote kabla ya tarehe 30 Juni, 2019. Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Fungu hili lilitengewa shillingi triliioni 1.4 na mpaka kufikia tarehe 29 Aprili, Fungu hili likuwa limepewa shillingi bilioni 890.58, ambayo ni asilimia 63 ya bajeti kwa Fungu hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kutambua umuhimu wa kipekee wa elimu kwa maendeleo ya nchi yetu, Serikali inapenda kuwahakikisha Watanzania kwamba katika kipindi kilichobaki, Serikali itatoa fedha kwa *Vote 46* kama Sheria ya Bajeti na hususan kifungu cha 45 (b) kinavyoelekeza. Naomba nikisome ili tuelewane vizuri: *Funds disbursements to Vote shall be based on performance approved budgets and funds availability.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya bajeti ya elimu inashuka na kuwa bajeti ya maendeleo imetuwa na mserereko wa kupungua, ni kweli, ukiangalia takwimu zinaonesha bajeti ya elimu inapungua katika asilimia kutoka asilimia 17 ya bajeti yote 2015/2016, asilimia 16 mwaka 2016/2017, asilimia 15 mwaka 2017/2018, asilimia 14 mwaka huu na asilimia 14 mwaka ujao wa fedha. Hata hivyo, si kweli kuwa bajeti ya maendeleo imetuwa na mserereko wa kupungua, uki-decompose hizi namba, unaona kwamba kilichopungua

ni bajeti ya matumizi ya kawaida na imepungua kwa miaka miwili iliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2015/2016, bajeti ilikuwa bilioni 3.2 na hii ni *recurrent*, ikaongezeka kwenda bilioni 3.7 mwaka 2016/2017, mwaka 2017/2018, ndiyo ikashuka kidogo kuwa bilioni 3.5 na bilioni 3.4 mwaka huu wa fedha na kwa mwaka kesho inashuka kidogo kuwa bilioni 3.1. Kwa hiyo, hiyo ni *recurrent* na hii inatokana na hatua ambazo Serikali ilichukua ikiwemo kuwaondoa watumishi hewa kutoka katika sekta ya elimu, lakini *restructuring* ambayo imefanyika katika taasisi mbalimbali ambayo imeondoa baadhi ya watumishi kutoka kwenye taasisi mbalimbali katika Fungu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia upande wa fedha za bajeti ya maendeleo, hizi zimeongezeka kutoka bilioni 0.6 mwaka 2015/2016 kwenda bilioni moja mwaka 2016/2017, bilioni 1.1 mwaka 2017/2018, bilioni 1.2 mwaka 2018/2019 na bilioni 1.3 kwa mwaka ujao wa fedha. Kwa hiyo, ni vizuri kufanya *decomposition* ili uweze kusema kweli bajeti inateremka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu vilevile, Waheshimiwa Wabunge wakatambua mchango mkubwa wa wadau wengine katika elimu nchini na hususan wamiliki wa shule binafsi lakini pia taasisi za kidini, lakini pia ni muhimu kuzingatia kwamba sekta nyingine nazo ni muhimu kwa maendeleo ya elimu yenye. Kwa hiyo, ni lazima nazo zipewe fedha, kwa mfano, bajeti ya ulinzi na usalama, vyuo, vijana wetu walioko vyuoni, walioko shule za msingi na sekondari, wanaweza wakasoma pale tu ambapo tunawahakikisha ulinzi na usalama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, afya, maji, kilimo, miundombinu ya umeme na *ICT* nayo ni muhimu ili kuweza kuboresha elimu. Kwa hiyo, ni muhimu tuangalie mambo yote hayo ili tuweze kuona mwenendo mzuri unaofaa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi, ni ukubwa wa keki yetu, kwa hiyo, kazi yetu ambayo tunatakiwa tufanye, kwa kweli tujielekeze tupate mapato zaidi, lakini tuweke vipaumbele vizuri vya kisekta na vya kitaifa ambavyo tukivitekeleza vizuri tutakwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba fedha za udhibiti wa ubora wa shule zitolewe zote kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika. Serikali haina pingamizi kabisa na ushauri huu na kama nilivyoeleza awali, fedha zitatolewa kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, kazi zilizokwishafanyika hadi sasa na mpangokazi kwa kipindi cha miezi miwili iliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bodi ya Mikopo kwamba ipewe Fungu lake linalojitegemea, tunawashauri Bodi ya Mikopo kuandaa andiko la maombi ya kuwa na Fungu lake linalojitegemea baada ya kushauriana na Wizara mama. Utaratibu wa kuanzisha Fungu unazingatia majukumu na muundo ambao umepitishwa na Ofisi ya Rais (Utumishi) ili kuweza kubainisha ule mnyororo wa mamlaka za utendaji, ili tujiridhishe kwamba fedha ya umma itasimamiwa vizuri na kwa mwongozo zaidi wanaweza wakaonana na Ofisi ya Rais (TAMISEMI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya *COSTECH*; umuhimu wa *COSTECH*, kwa kweli unafahamika na ndiyo maana inatengewa bilioni 9.18 kwa mwaka ujao wa fedha na hili tumezingatia tu wigo wa mapato na mahitaji mengine ambayo ni lazima yagharimiwe na Serikali. Hata hivyo, ni vizuri pia kutilia maanani kwamba utafiti ni suala mtambuka na linatekelezwa kwenye taasisi nyingine, ikiwa ni pamoja na vyuo vikuu, lakini pia taasisi kama *TILDO*, *NYUMBU*, *TAWIR*, *TAFOR*, *CARMATEC*, *SIDO*, *VETA*, ambazo nazo kwa kiasi cha kikubwa zinategemea fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuliambiwa Serikali iheshimu makubaliano ya kimataifa, ikiwemo lile Azimio lile la *SADC*, kwamba Serikali itenye asilimia 20 ya bajeti yote kwa

ajili ya elimu. Ni kweli, lakini yapo maazimio mengine ambayo Tanzania iliyakubali, ikiwemo Azimio la Maputo ambalo linatutaka tutenge asilimia 10 ya bajeti yote kwa ajili ya kilimo, afya asilimia 15 ya bajeti yote, utafiti asilimia moja ya pato la Taifa, asilimia 0.05 ya bajeti kwa ajili ya takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuliambiwa Serikali iheshimu makubaliano ya kimataifa, ikiwemo lile Azimio la SADC kwamba Serikali itenye asilimia 20 ya bajeti yote kwa ajili ya elimu. Ni kweli, lakini yapo Maazimio mengine ambayo Tanzania iliyakubali ikiwemo Azimio la Maputo ambalo linatutaka tutenge asilimia 10 ya bajeti yote kwa ajili ya kilimo; afya asilimia 15 ya bajeti yote; utafiti asilimia 1 ya pato la Taifa; na asilimia 0.05 ya bajeti kwa ajili ya takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Maazimio yote haya yatakelezwala sekta tatu tu peke yake zitachukua asilimia 45 ya bajeti yote. Sijui kipi hicho kitasalia kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu yetu, ulinzi na usalama, maji, ikiwemo na bajeti ya Mhimili wa Bunge, tutafanyaje? Kwa hiyo, ni muhimu sana huko mbele pengine tukifika lazima tuweze kuyapanga vizuri badala ya kwenda tu kusema tutatekeleza Maazimio haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme moja la mwisho, niliulizwa hapa kwamba upo Waraka wa Serikali unaonesha kwamba Waziri wa Fedha alifuta baadhi ya kodi kwa wamiliki wa shule binafsi na kwamba huo Waraka uko wapi. Serikali haijawahi kutoa Waraka unaofuta kodi kwa wamiliki wa shule binafsi. Mabadiliko mbalimbali ya kodi huwa tunayafanya kuititia Sheria ya Fedha au Gazeti la Serikali kwa mwaka husika na hilo halijawahi kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia namshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kunituea katika nafasi hii. Nampongeza kwa kazi kubwa anayofanya katika kuwaletea Watanzania maendeleo. Vilevile sina budi kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa ushauri na maelekezo yao muhimu katika utendaji kazi wangu wa kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeverti wa Bunge ukiwemo wewe mwenyewe kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima, busara na weledi mkubwa. Naishukuru pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia. Hii ni moja kati ya Kamati bora sana ambayo Wajumbe wake wanauelewa mpana wa sekta ya elimu na hivyo kuendelea kutoa ushauri muhimu katika kuboresha elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa uongozi wake thabiti ndani ya Wizara. Pia nawashukuru Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara kila mmoja kwa nafasi yake kwa ushirikiano wanaonipatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru familia yangu kwa upendo na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Ngorongoro kwa imani yao yangu kwangu na ushirikiano ambao wanani pa ambao umetusaidia Jimbo letu kupiga hatua kubwa sana ya maendeleo katika kipindi kifupi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, sasa naomba kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa sababu ya

muda hatutaweza kujibu kila hoja zingine tutazileta kwa maandishi, lakini naomba nijielekeze katika hoja chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamependekeza Serikali kuweka utaratibu wa ada elekezi katika shule binafsi. Ni muhimu ikafahamika kuwa shule za binafsi zinatoa huduma lakini pia zinafanya biashara. Hivyo, ni vigumu kwa Serikali kutoa ada elekezi na badala yake itaendelea kuacha nguvu ya soko iamue kama ilivyo katika sekta nyingine ikiwemo afya. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia utoaji wa elimu katika sekta ya umma na binafsi ili kuimarisha utoaji wa elimu na elimu iwe bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia juu ya umuhimu wa kuimarisha Idara ya Udhibiti Ubora wa Shule. Wizara yangu inatambua umuhimu wa Idara ya Udhibiti Ubora wa Shule katika kuboresha utoaji elimu bora nchini. Katika kuimarisha Idara hiyo, Wizara kwa mwaka 2018/2019, ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya ukaguzi wa shule na hadi kufikia Machi 2019, Idara ishaporea kiasi cha shilingi bilioni 1.8 sawa na asilimia 51.30. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imetenga kiasi cha shilingi bilioni 4.1 kwa ajili ya ukaguzi wa shule na pia Wizara inajenga ofisi 100 za Udhibiti Ubora wa Shule katika Wilaya 100 na inakarabati ofisi 40 za Udhibiti Ubora wa Shule katika Wilaya 40. Vilevile Wizara imenunua *computer* 353 na *printer* 153 kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Ofisi za Wilaya za Kanda ambazo hazikuwa na vitendea kazi. Aidha, Wizara ishapeleka magari 45 katika Wilaya 45 ili kuhakikisha kwamba shule nyingi zinafikiwa na kufanyiwa tathimini kwa lengo la kuboresha utoaji wa elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maslahi ya Wadhibiti Ubora wa Shule na kuboresha mishahara yao, Wizara imepokea michango ya Waheshimiwa Wabunge tena kwa uzito mkubwa na itafanya kazi ili kuwapa motisha ya kazi Wadhibiti Ubora wa Shule. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia sana kuhusiana na masuala ya Bodi

ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Badhi ya Waheshimiwa Wabunge wamechangia juu ya umuhimu wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kushirikiana na *NIDA* kubaini wanafunzi wanaostahili kupewa mikopo lakini pia kurejesha baada ya kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imeanza kufanyiwa kazi, ambapo Bodi ya Mikopo imekutana na *NIDA* Februari, 2019 kwa lengo la kuweka utaratibu wa kubadilishana taarifa za kimfumo na kuwa na mifumo ya taasisi bora zaidi ya kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuanganisha na mifumo ya taasisi zingine zinazotoa huduma kwa wananchi. Aidha, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imeendelea kufanya mazungumzo kama hayo na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*) na Mamlaka ya Uhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) kwa lengo la kuwa na mifumo inayoendana kubadilishana taarifa ili kuongeza ufanisi katika upangaji na urejeshaji wa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wabunge pia wameshauri Bodi ya Mikopo ifanye malipo ya fedha za mikopo kupitia akaunti za benki za wanafunzi moja kwa moja ili kuondokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza. Ushauri huu ulishaanza kutekelezwa kwa majoribio ambapo katika awamu ya kwanza mwaka 2017/2018 jumla ya wanafunzi 37,184 kati ya wanafunzi 123,285 sawa na asilimia 30 wanaopata mikopo waliunganishwa katika mfumo wa kielekitroniki wa malipo unaofahamika kama *Digital Disbursement Solution*. Wanafunzi wengine waliobaki wataunganishwa katika awamu inayofuata, katika mwaka unaokuja wa fedha. Utaratibu huu tunaamini utaongeza ufanisi na kuondoa kero kwa wanafunzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge pia ambao wamechangia hotuba yetu wamechangia kuhusu baadhi ya wanafunzi wasio na uwezo kukosa mikopo ya elimu ya juu. Napenda ifahamike kwamba mikopo hutolewa kwa wanafunzi wote wenye uhitaji na huongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura 178 inayotaja vigezo vikuu ambavyo ni

pamoja na kuwa Mtanzania kwa maana mwombaji lazima awe raia, lazima awe amepata udahili, asiwe na chanzo kingine cha kugharimia masomo yake, pia awe ameomba mikopo kwa usahihi. Aidha, kipaumbele cha mikopo kuzingatia makundi maalumu yaani yatima, wenyewe ulemavu au wenyewe wazazi wenyewe ulemavu walifadhiliwa katika masomo yao ya sekondari au stashahada ambao katika maombi yao wamethibitisha taarifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kumekuwa na changamoto katika uwasilishwaji wa taarifa kwa waombaji. Kwa mfano, katika mwaka 2018/2019 wanafunzi wa mwaka wa kwanza wapatao 16,797 kati ya wanafunzi 81,425 waliwasilisha maombi yenyewe dosari mbalimbali. Wito wetu kwa wanafunzi na kila mmoja wetu ni kuhakikisha kwamba wakati wa kuomba mikopo kila mmoja achukue muda wake vizuri ajaze zile fomu vizuri kwa sababu ukikosea kuomba inakuwa ni vigumu wewe kupata ule mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa athari za changamoto hii, katika mwaka 2018/2019 Bodi ya Mikopo imeendelea kutekeleza programu za elimu ya uombaji mikopo kwa wanafunzi wa sekondari Tanzania Bara na Zanzibar. Kati ya mwezi Februari na Aprili, 2019, Bodi imeendesha programu hizi katika shule mbalimbali za sekondari 49 na kuelimisha wanafunzi wapatao 25,000 kati ya wanafunzi 81,300 wanaotarajiwa kufanya mtihani ya kidato cha sita mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Bodi iliwafuata wanafunzi 25,000 wanaotegemea kumaliza kidato cha sita katika shule wanazosoma kutoa elimu ya namna ya kujaza fomu. Tunategemea mwaka huu hatutakuwa na changamoto kubwa ya waombaji wengi kukosea kujaza fomu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia juu ya umuhimu wa kutoa mikopo kwa asilimia 100 kwa wanafunzi wa sayansi hasa wale wanaomba kusomea udaktari na ualimu. Mikopo ya elimu

ya juu hutolewa kwa kuzingatia sheria ambayo imepishwa na Bunge hili. Masomo ya sayansi, udaktari na ualimu ni sehemu tu ya vigezo vingi vya utoaji mikopo. Vigezo hivyo ni pamoja na uhitaji wa waombaji wanaotoka katika makundi yale ambayo tunesema yatima, wenyewe ulemavu au wenyewe wazazi wenyewe ulemavu waliofadhiiliwa katika masomo ya sekondari na wanaotoka katika kaya zenyewe vipato duni. Hivyo, waombaji wote ambaao ni wahitaji na ambaao wamepata udahili katika programu za kipaumbele ikiwemo masomo ya sayansi hasa udaktari kupewa kipaumbele katika kupangiwa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, upangaji wa mikopo hutegemea idadi ya wanafunzi wanaopata udahili na uhitaji. Kwa kuzingatia hilo, katika mwaka wa fedha 2018/2019, wanafunzi 2,118 wanaosomea programu ya sayansi ya afya walipangiwa mikopo ambayo ni asilimia 5 ya wanafunzi wote walipangiwa mikopo. Kati yao, wasichana walikuwa 636 sawa na asilimia 30 na hao walipangiwa mikopo katika programu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamependekeza kwamba tutoe kipaumbele cha Kipekee kwa wanafunzi wanaopata madaraja ya kwanza na ya pili wakati wa kutoa mikopo. Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wenyewe uhitaji kwa kuzingatia vigezo vya upatikanaji wa fedha. Kulingana na vigezo vilivyowekwa, siyo wanafunzi wote wanaopata udahili wanakuwa na sifa za kupata mikopo ya elimu ya juu. Mikopo inayotolewa na Serikali huongozwa na Sheria na Sera ya Uchangiaji wa Huduma za Kijamii ikiwepo elimu. Aidha, utoaji wa elimu hiyo huongozwa na Sheria ya Mikopo, Sura ya 178 inayolenga Watanzania wahitaji na wenyewe udahili lakini wasio na uwezo wa kumudu gharama au sehemu ya gharama za mafunzo ya elimu juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge vilevile wamezungumzia kuhusu umuhimu wa kutoa elimu. Kama nilivyosema, tayari elimu hiyo ya namna ya

kujaza fomu zile imeshatolewa mwaka huu kwa wanafunzi 25,000 ambao tunategemea wataomba mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imechangia kwa hisia kubwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ni suala la wanafunzi kutoruhusiwa kufanya siasa vyuoni. Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 345 ya mwaka 2005 (Toleo la 2002 la Sheria za Tanzania) pamoja na Kanuni za Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2013, kifungu cha 51(1)(2) inakataza wanafunzi kujingiza katika siasa za vyama wawapo vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuzuia wanafunzi kujingiza katika vyama vyaa siasa ni kujenga mazingira tulivu kwa wanafunzi kujisomea na kumaliza masomo yao ndani ya muda uliopangwa. Lazima tuseme, lengo ni zuri tunataka wanafunzi wetu waweze kufanya kile ambacho walikifuata vyuoni na ni kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, haimaanishi kwamba hawaruhusiwi kufanya siasa ya aina yoyote, siasa inayokatazwa ni siasa ya vyama vyaa siasa ndani ya vyuo, wanaweza wakaendelea kuwa ni wanachama wa vyama vyaa siasa, wakaenda kufanya siasa hiyo nje lakini ndani ya vyuo wanaruhusiwa kufanya siasa za wanafunzi (*student politics*) na ndiyo maana wana Serikali zao, wanafanya chaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile uongozi wa vyuo ni lazima wajabike kuhakikisha kuwa chaguzi za wanafunzi zinafanyika kwa kufuata demokrasia lakini siyo kwenda kukwaza au kuingilia chaguzi zile. Kwa hiyo, tunachosema kimsingi ni kwamba siasa wanaweza wakafanya kama *students politics* lakini siyo siasa za vyama ndani ya vyuo kwa sababu inaingilia masomo na inavuruga utulivu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imezungumziwa kwa hisia kubwa sana ni suala la ni namna gani nchi yetu imejitayarisha kuelekea katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (*The Fourth Industrial Revolution*). Serikali inatambua uhusiano kati ya Mapinduzi ya Nne ya Viwanda na Tanzania ya Viwanda ambayo tunajaribu kujenga huku tukitaka kuelekea kwenye uchumi wa kati. Mapinduzi ya Viwanda ya Awamu ya Nne ni mageuzi makubwa ya nne toka mapinduzi yale maarufu kama Mapinduzi ya Kwanza ya Viwanda yaliyotokea karne ya 18 (*Industrial Revolution*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapinduzi hayo yanajumuisha muunganiko wa teknolojia mbalimbali ambapo mifumo yote inaunganishwa *ki-digital* ikihusisha sayansi na teknolojia ya hali ya juu ambayo ni ukusanyaji, utunzaji na uchakataji wa takwimu na uimarisaji wa mifumo ya mawasiliano. Mipango ambayo tayari imeshaanza ndani ya nchi yetu kwa kweli ni mingi katika kujaribu kuelekea katika *The Fourth Industrial Revolution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mipango hiyo ni upatikanaji wa *computerkubwa* zenyet uwezo wa kuchakata kwa kasi taarifa za maendeleo ya jamii (*supercomputing*) katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salam vilevile Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. Pia upatikanaji wa mitaala ya kufundishia masuala ya *TEHAMA*, *big data* katika Vyuo vya *DIT* na Nelson Mandela. Upatikanaji wa maabara za mashine za kisasa za viwandani yaani *mechatronics labs* kwa ajili ya kuendeleza wataalam wa viwandani na kuboresha mafunzo ya ufundu kwa wanafunzi katika Taasisi za *DIT* na *MUST*. Pia taasisi mbalimbali za sayansi na teknolojia kupitia utaratibu wa *COSTECH* zimeanza kujikita katika kufanya tafiti zinazojibu mahitaji ya Mapinduzi ya Viwanda Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vyetu vingi vimeshaandaa mitaala mbalimbali inayojibu mahitaji ya sayansi na teknolojia. Mfano, Chuo Kikuu cha Nelson Mandela tayari wamerekebisha mitaala ili waanzishe Digrif

ya Umahiri katika Mifumo Bebwa na Jongevu (*Master of Science in Embedded and Mobile Systems*). Pia wanaanza kufundisha Digrii ya Umahiri katika Mifumo ya Habari na Usalama Mtandaoni (*Masters in Information System and Network Security*). Vilevile Digrii ya Umahiri katika Mawasiliano ya Pasiwaya na Jongevu (*Masters in Wireless and Mobile Communication*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DIT* wao wanajitayarisha kufundisha Digrii ya Umahiri ya Uhandisi wa Sayansi ya Komputa (*Masters of Computer Science Engineering*). Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wao wamejitayarisha kufundisha *Masters of Science in Health Molecular Biology* yaani Digrii ya Umahiri ya Sayansi katika Biolojia ya Molekiuli ya Afya Jumuishi. Pia Digrii ya Umahiri ya Sayansi katika Uzazi wa Wanyama na Bioteknolojia. Vilevile Digrii ya Awali ya Bioteknolojia ya Sayansi ya Maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Teknojia Mbeya wao wamejiimarisha na wataanza kutoa Digrii ya Awali ya Sayansi katika Uhandisi wa Akili Bandia. Pia Digrii ya Awali ya Sayansi katika Sayansi Data lakini vilevile Digrii ya Awali ya Uhandisi Baitiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Cha *UDOM* wao wamejitayarisha kufundisha Digrii ya Awali ya Sayansi katika Uhandisi wa Akili Bandia. Pia Digrii ya Awali ya Sayansi katika Uhandisi wa Sayansi Data. Vilevile Digrii ya Awali ya Sayansi katika Uhandisi wa *Internet* Vifaa na Digrii ya Awali ya Sayansi katika Uhandisi na Usalama Mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana haifahamiki sana huko nje kwa sababu haizunguzwi lakini nchi yetu na vyuo vyetu vimejikitika katika kuanza kuingia katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda ili iweze na sisi kutusukuma na tuweze kuingia katika ushindani katika dunia ambayo tunaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vikuu pia hufanya utafiti katika maeneo mbalimbali ambayo ni muhimu kwa ajili ya Mapinduzi ya Nne ya Viwanda. Kwa mfano, Taasisi ya

Teknolojia ya Dar es Salaam imeingia mkataba na kushirikiana na kampuni ya Belfrics ya nchi Malaysia ili kuwajengea uwezo wataalam wa Kitanzania katika eneo la *blockchain technology* ambayo ni teknolijia ya uhifadhi wa taarifa na takwimu za *ki-digital* kwenye sayansi ya *computer* ambayo huongeza ufanisi katika *TEHAMA*. Kwa ujumla vyuo vitaendelea kubuni mitaala mipya na kupitia iliyopo ili kukudhi mahitaji ya sasa ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kupitia Mradi wa Kukuza Ujuzi, Tume ya Vyuo Vikuu imeshatoa mafunzo kwa Makamu Wakuu wa Vyuo 40 kuhusu jinsi ya kusimamia mafunzo na uanzishaji mitaala inayoendana na mahitaji ya kuanzisha mashirikiano kwenye masuala ya viwanda. Kupitia mradi huu, *TCU*imeshafanya mafunzo ya jinsi ya kutengeneza mitaala inayoendana na soko na tunategemea wanataluma angalau 132 wataendelea kunufalka na mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mtoha hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuhitimisha hoja ambayo niliwasilisha mbele ya Bunge lako mnamo tarehe 29 Aprili, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba nikushukuru wewe kwa kuuongoza vyema mjadala wa hoja yangu, lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa michango mizuri katika bajeti ambayo nimewasilisha leo kuhusu Fungu Namba 46 pamoja na Fungu Namba 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukurani za kipekee kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na

Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kutoa katika Wizara yangu na kwa kweli kwa mara nyingine nishukuru sana Uongozi wa Bunge kwa kuisuka vyema Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambayo hakika imesheheni Wajumbe ambao wanaifahamu vyema sekta ya elimu. Kwa hiyo wamekuwa na michango mizuri ambayo hakika inachangia sana katika kuboresha elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nishukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii. Tumepokea michango mingi sana na michango mizuri ambayo yote ilikuwa na lengo moja na kuhakikisha tunaimarisha na kuboresha elimu katika nchi yetu na kuweka mazingira rafiki kwa vijana wa Kitanzania ili waweze kujifunza vizuri. Kwa hiyo, nianze kusema tu kwamba kwa moyo mkunjufu, Wizara imepokea michango yote ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 114 walichangia hoja yangu na kati yao, Waheshimiwa Wabunge 63 wamechangia kwa maandishi na Wabunge 51 wamechangia kwa kuongea. Naomba kwa sababu ya muda siwezi kuwataja lakini naomba orodha yao iingie kwenye *Hansard* waweze kutambulika.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Omari M. Kigua, Mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mheshimiwa Husna S. K. Mwilima, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Rhoda E. Kunchela, Mheshimiwa Joseph L. Haule, Mheshimiwa Joseph M. Mkundi, Mheshimiwa Aida Joseph Kheneni, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Mbaraka Kitwana, Mheshimiwa Shaabani O. Shekilindi, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Zuberi M. Kuchauka, Mheshimiwa *Engineer* Gerson H. Lwenge, Mheshimiwa Hamidu H. Bobali, Mheshimiwa Ally M. Kessy, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Ruth H. Mollel, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Dkt Chrestine G. Ishengoma,

Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mheshimiwa Suzana C. Mgonukulima, Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mheshimiwa Flatei G. Massay, Mheshimiwa *Engineer* Edwin A. Ngonyani, Mheshimiwa Lucia U. M. Mlowe, Mheshimiwa Zainabu M. Amiri, Mheshimiwa Lucy S. Magereli, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika, Mheshimiwa Abdallah D. Chikota, Mheshimiwa Kiza H. Mayeye, Mheshimiwa Mary D. Muro, Mheshimiwa Anatropia L. Theonest, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Sonia J. Magogo, Mheshimiwa Zainab M. Bakar, Mheshimiwa Silafu J. Maufi, Mheshimiwa Mussa B. Mbarouk, Mheshimiwa Cosato D. Chumi, Mheshimiwa Timotheo P. Mnzava, Mheshimiwa Joyce B. Sokombi, Mheshimiwa Lolesia J. Bukwimba, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Marwa R. Chacha, Mheshimiwa Juma O. Hija, Mheshimiwa Omari A. Kigoda, Mheshimiwa Mashimba M. Ndaki, Mheshimiwa Qambalo W. Qulwi, Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, Mheshimiwa Elibariki I. Kingu, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Devotha M. Minja, Mheshimiwa Rev. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Maria N. Kangoye, Mheshimiwa Salma R. Kikwete, Mheshimiwa Catherine N. Ruge, Mheshimiwa Zainabu N. Mwamwindi, Mheshimiwa Khadija N. Ali, Mheshimiwa Dkt. Dalaly P. Kafumu na Mheshimiwa Richard P. Mbogo.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge waliochangangia hotuba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa kuzungumza ni pamoja na Mheshimiwa Yosepher F. Komba, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa Joram I. Hongoli, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mheshimiwa Pascal Y. Haonga, Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Phillipo A. Mulugo, Mheshimiwa Joseph M. Mkundi, Mheshimiwa Sikudhani Y. Chikambo, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mheshimiwa Abdallah D. Chikota, Mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mheshimiwa Edward F. Mwalongo, Mheshimiwa Shaaban O. Shekilindi, Mheshimiwa Daimu I. Mpakate,

Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Engineer Edwin A. Ngonyani, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa Angelina A. Malembeka, Mheshimiwa Vedasto E. Ngombale, Mheshimiwa Salma R. Kikwete, Mheshimiwa Jumanne K. Kishimba, Mheshimiwa Sixtus R Mapunda, Mheshimiwa Zainab M. Bakar, Mheshimiwa Dkt. Immaculate S. Semesi, Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Dkt. Jasmine T. Bunga, Mheshimiwa Rashid M. Chuachua, Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus B. Kamala, Mheshimiwa Joseph K. Mhagama, Mheshimiwa Tauhida C. G. Nyimbo, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Hamidu H. Bobali, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Marwa R. Chacha, Mheshimiwa Maria N. Kangoye, Mheshimiwa Fatma H. Toufiq, Mheshimiwa Kemilembe J. Lwota, Mheshimiwa Dkt. Charles J. Tizeba, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Khadija N. Ali, Mheshimiwa Sebastian S. Kapufi, Mheshimiwa Goodluck A. Mlinga na Mheshimiwa Mwita M. Waitara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao wamechangia hoja yangu. Kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Kaka yangu Waziri wa Fedha amejibu vizuri na kitaalam hoja zinazohusu masuala ya fedha lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI na yeye kwa ufanuzi wa hoja ambao ameutoa. Kwa ujumla kwa kweli Wabunge wote kwa umoja wenu michango yenu imekuwa ni mizuri na kipekee kabisa nimshukuru Waziri Kivuli Mheshimiwa Susana Lyimo hakika safari hii umekuja kivingine na hotuba yako imesheheni ushauri. Kwa hiyo tunashukuru sana na kwa mara ya kwanza, Mheshimiwa Susan Lyimo ameipongeza Taasisi ya Elimu Tanzania, nashukuru sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba sitaweza kwa muda niliopewa kujibu hoja zao zote lakini hoja zote zitajibowi kwa maandishi na tutahakikisha kwamba kabla ya kumaliza Bunge hili basi tutaweza kukabidhi majibu yetu kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa hiyo, naomba sasa nizungumzie tu hoja ambazo nitaweza kuzzungumza

kutokana na muda nilionao na nitaanza na masuala ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza na suala la uchapaji wa vitabu; suala la uchapaji wa vitabu limejitokeza na hii ninaamini ni kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wanatambua kwamba vitabu na Taasisi ya Elimu ndiyo moyo wa sekta ya elimu. Kwa hiyo Taasisi ya Elimu ispoanya vizuri ni dhahiri kwamba elimu yetu itakuwa haiko vizuri. Baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia ni kutokuwepo kwa vitabu vyaa baadhi ya masomo na kutokuwepo kwa vitabu vyaa elimu ya msingi, vyaa darasa la Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kabisa nianze kuwashukuru Wabunge wote waliochangia kuhusiana na suala la vitabu kwa sababu suala la ufundishaji na ujifunzaji haliwezi kwenda vizuri kama hatuna vitabu ambavyo ni vizuri kwa hiyo maoni yao na msisitizo ambaao wanauweka unaendana pia na namna ambavyo Serikali imekuwa ikiisimamia Taasisi hii ya Elimu na ndiyo maana hata katika Bunge hili nadhani ni kwa mara ya kwanza ambapo tunazungumzia Bajeti ya Wizara ya Elimu na hakuna vitabu vibovu ambavyo vimeletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka ilikuwa mwaka 2013 Mheshimiwa Mbatia aliingia na sanduku la vitabu ambavyo vimejaa makosa na ndiyo maana Serikali ikaamua, wakati huo hivyo vitabu vilikuwa vinachapwa na Kampuni binafsi Serikali ikaamua sasa hilo jukumu kurudisha Taasisi ya Elimu Tanzania. Lakini bahati mbaya Taasisi ya Elimu Tanzania na yenye ilipoanza wanassema Waswahili "mwanzo ni mgumu" haikufanya vizuri katika baadhi ya maeneo lakini, Serikali tulikuwa wakali kweli kweli na vile vitabu vyote vyenye makosa tuliviondoa shulenii na sasa hivi Taasisi ya Elimu imesimama vizuri na kazi yao imetukuka kwa hiyo tunakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyoo napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu vitabu vyaa darasa la Tano vilishasambazwa

shuleni nakala milioni 2,867,400 waliochelewa kupata walipata Mwezi Februari, na kwa sababu kuna tabia ya baadhi ya watu kufungia vitabu, tunapeleka shuleni lakin havifiki kwa walengwa, kwa hiyo, nilivyosikia tu Waheshimiwa Wabunge wanachangia nilifuatilia hata kwenye hizo halmashauri kuuliza kulikoni wakati tunajua vitabu vimepelekwa inakuaje Waheshimiwa Wabunge wanakuja kuuliza huku Bungeni? Kwa hiyo, nimejiridhisha na hata sehemu ambazo waliuliza maswali vitabu vilivyochelewa kufika vilikuwa ni Mwezi wa Pili kwa hiyo vitabu viko shuleni na wanafunzi wanavisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyininge ilihu su kutokuwepo kwa mtaala na mihtasari kwa shule zinazotumia lugha ya Kingereza; naomba niliarifu Bunge lako Tukufu, mitaala kwa lugha ya Kingereza ilishaandaliwa tangu Mwaka 2016 na inapatikana katika duka la vitabu la Taasisi ya Elimu Tanzania na Maduka ya Mawakala wa Taasisi ya Elimu Tanzania ambayo yanapatikana katika Mikoa yote nchi nzima.

Mheshimiwa Mwewyekiti, aidha, Wizara kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imekamilisha kazi ya kuandaa vitabu vya kiada kwa shule zinazotumia lugha ya Kingereza kama lugha ya kufundishia kwa Darasa la Kwanza, la Pili na la Tatu na vitabu hivyo nilisema katika hotuba yangu, kwamba tumeanzisha Maktaba ya Mtandao. Kwa hiyo, vitabu hivi ambavyo nimekuja na sampuli kuwaonyesha Waheshimiwa Wabunge vinapatikana katika Maktaba mtandao kwa hiyo vitabu vya lugha ya Kingereza viro hivi hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge watembelee tovuti yetu kama inavyoonekana pale ambayo ni www.tie.go.tzili waweze kujipatia kwa urahisi vitabu ambavyo tayari Serikali imekwisha viandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyininge ambayo ilizungumzwa na Mheshimiwa Ndugu yangu na rafiki yangu kabisa Mheshimiwa Phillipo Mulugo kuhusiana na suala la vitabu ambavyo vilikuwa na dosari. Baada ya marekebisho

ambayo Serikali imefanya, amesema kwamba kuna baadhi ya wadau wetu ambao walikuwa wamevinunua na hivyo wamepata hasara kubwa sana kwa sababu vitabu vilivyokuwa Serikalini vimeondolewa lakini wale wadau wengine ambao walikuwa wamenunua nje ya mfumo wa Serikali wao wamepata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ambazo tunazo, Serikali haikuwa imeuza kitabu chochote kwa mtu yoyote kwa sababu makosa yalibainika mara tu baada ya kusambaza hivyo vitabu. Kwa hiyo, naomba niseme mbele ya Bunge lako tukufu, kama kuna mtu wa yoyote ambaye alikuwa amenunua vitabu ambavyo vina makosa ninaomba awasilishe vilelezo (*receipt*) yake na vitabu ambavyo vina makosa na Serikali itambadilishia kwa sababu tayari Serikali imetoa tamko la kuviiondoa vitabu hivyo shulen na havitakiwi kutumika mahali popote na havitakiwi kuwa kwenye *circulation* kwa sababu watoto wadogo wanaweza wakakutana nacho wakakitumia. Kwa hiyo, ni msimamo wa Serikali vile vitabu ni marufuku kutumika mahali popote. Kwa hiyo, kama kuna mtu ana kitabu na alikuwa amekinunua akirudishe na atapewa kitabu kingine ambacho ni kizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine limezungumzwa na Ndugu yangu Mheshimiwa Esther Mahawe ambaye ni Rais wa *TAPIE* (Wamiliki wa Shule Binafsi) na alikuwa anazungumzia suala la gharama za mafunzo kwa ajili ya walimu wa shule binafsi. Nimesikia hapa lugha zinazungumzwa kwamba utoaji wa elimu bure kwamba kunakuwa na ubaguzi kwenye shule za Serikali wanafanya mitihani bure au wanakuwa wanafanya mafunzo bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hakuna kitu cha bure, shule za Serikali zinalipiwa na Serikali ndiyo maana Waziri wa Fedha kila mwezi anatoa bilioni 23.8 kwa hiyo hakuna cha bure, inategemea tu kwamba gharama inalipwa na nani. Kwa hiyo, Serikali inalipia Walimu wanapokuwa wanakwenda mafunzo kazini, Serikali inawalipia wanafunzi

wanapokuwa wanafanya mitihani. Na shule binafsi tungeziomba zichangie katika grarama za mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la gharama ya mafunzo ambayo iliwekwa, kwa taarifa nilizonazo ni kwamba walikaa kikao wakawa wameshauriana Wamiliki wa Shule Binafsi na Taasisi ya Elimu Tanzania na niwaombe kwa sababu kwa kweli tunafanyakazi vizuri na shule binafsi, kama hizo fedha ambazo mlikuwa mmekubaliana baadaye mmeziona kwamba ni kubwa, rudini tu mkakae kwenye mazungumzo. Nia yetu ni moja kuhakikisha kwamba tunaendeleza elimu yetu, sidhani kama tunaweza tukashindwa kuelewana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi ni malalamiko kuhusiana na kubadilika kwa mtaala mara kwa mara. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba tangu tumepata uhuru mwaka 1961 mtaala umebadilika mara nne tu. Tangu tumepata uhuru mwaka 1961 mtaala ya elimu imebadilika mara nne tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza ni mara baada ya kupata uhuru, mara ya pili ni baada ya Azimio la Arusha mwaka 1967, mara ya tatu ulibadilika mwaka 1979 kuingiza masomo ya michepuo na mara ya nne ulibadilika mwaka 1997 baada ya mfumo wa vyama vingi vya siasa kwa hiyo kulikuwa na *context* ambazo zilibadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tunakuwa tunafanya maboresho ya mtaala. Nitatoa mfano, kwa mfano, mwaka 2005 kumezaliwa Nchi ya Sudan Kusini ni lazima tufanye maboresho haya siyo mabadiliko. Ni maboresho katika mtaala kuonyesha kwamba nchi za Afrika idadi imeongezeka kwa sababu kuna nchi mpya imezaliwa, haya hauwezi ukasema ni mabadiliko. Kwa hiyo, kumekuwa na maboresho ambayo yanafanyika madogo madogo ya kawaida, maboresho yanayozingatia mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia, lakini mabadiliko makubwa yamefanyika mara nne tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na suala hilo, watu wamezungumzia sana mfumo wa elimu yetu na vilevile wamzungumzia sana hata suala la kwamba sasa hivi elimu yetu inakuwa inakwenda ndivyo sivyo na nilikuwa natafuta hapa *quotation* ya Mheshimiwa Susan Lyimo alioanzanayo. Katika kitabu chake alianza na *quotation* ya kuonyesha kwamba "ukitaka kuangamiza nchi yetu basi uchezee mfumo wa elimu na kwamba ukiwa na watu wenyе vyeti feki, ukiwa na watu ambao wamekaa wanafanya kazi mahali ambapo sipo basi itakuwa ni silaha kubwa ya kuangamiza nchi yetu".

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie kwamba Serikali ya Awamu ya Tano iko makini sana na inatambua kwamba bila mfumo imara wa elimu basi mambo hayawesi kwenda vizuri na ndiyo maana Serikali ilifanya uhakiki wa watu wenyе vyeti feki. Jumla ya watumishi 15336 wameondolewa kwenye Utumishi lakini pia Serikali kwa kutambua kwamba ukimuweka mtu mahali ambapo hana sifa nazo hawezи kufanya vizuri. Zaidi ya watumishi 5300 ambao walikuwa wameajiriwa katika fani ambazo hawana ujuzi nazo wameondolewa. Wanataka Serikali ifanye nini zaidi ya hapo kuonyesha kwamba inatambua na kujali umuhimu wa elimu katika nchi yetu ya Tanzania? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumziwa, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango amejibu vizuri na kitaalam masuala ambayo yanahusiana na masuala ya fedha. Lakini naomba tu nifafanue moja. Kuna suala moja ambalo kwa kweli niseme hapa na Ndugu zetu Washirika wa maendeleo wako pamoja na mimi walikuja hapa jana na Kiti kiliwatambulisha na hata sasa wanafuatilia mjadala wetu. Haipendezi hata kidogo kwa mtu ambaye ni mstaarabu, mtu ambae ni muungwana, mtu ambae anashirikiana na wewe katika maendeleo tunatumia maneno ya ajabu ajabu kuwasema Washirika wetu wa maendeleo, siyo jambo jema hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwanza hii dhana ya kusema kwamba Serikali imekuwa tegemezi sana siyo sawa. Ukiangalia bajeti ya Wizara kwa miaka mitatu iliyopita;

Mwaka 2017/2018, mchango wa Serikali ulikuwa ni asilimia 66.2 na mchango wa Wafadhili ulikuwa ni asilimia 33.8 lakini katika Mwaka huu wa fedha wa Bajeti hii ambayo Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba kwa unyenyekevu kabisa muidhinishe mchango wa Serikali ni asilimia 67.6 na mchango wa Wafadhili ni asilimia 32.4, kwa hiyo, Serikali imeendelea kuwa inapunguza utegemezi. Lakini Waheshimiwa Wabunge naomba niwaulize swalii; hivi kama Serikali ina mahusiano mazuri na wafadhili, ina marafiki kutokana na Utawala Bora, wako tayari kuja kutoa misaada katika nchi yetu, kuna kosa gani Ndugu zangu? Kwa sababu inakuwa kama vile ni dhambi. Kwa nini inakuwa kama vile ni dhambi Serikali ikipata misaada kutoka nje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri mngeipongeza Serikali, haiwezekani mtu aje akuletee fedha zake kama wewe huna usimamizi mzuri, kama wewe huna Utawala Bora, kama wewe husimamii vizuri zile fedha ambazo zinaletwa. Kwa hiyo, Ndugu zangu sioni kama kuna sababu yoyote ya kuhangaika na nitoe tu taarifa kwamba hata sasa hivi tunapoongea Serikali ya Uswisi imetoa msaada wa jumla ya shilingi bilioni 14,900,000,000 kwa ajili ya kuendeleza ujuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hizi hata kwenye kitabu chako hazionekani kwa sababu ni makubaliano ambayo tumeingia hivi karibuni na tarehe 31 Mei tutazindua rasmi huu mpango. Lakini nitoe taarifa zaidi kwamba kupitia *Global Partnership in Education*, mfuko huu umetoa Dola milioni 90 kwa Tanzania mwanzoni mwa Mwezi huu wa Nne ambao ni sawa na bilioni 200 za Kitanzania na huo ni msaada kutokana na Utawala Bora katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kuhusiana na fedha maana mengi Mheshimiwa Waziri ameyajibu; kumekuwa pia na dhana kwamba bajeti ya Wizara imepungua, mwaka uliopita ilikuwa triliioni 1,407,000,000,000 na Mwaka huu ni triliioni 1,388,000,000,000. Waheshimiwa Wabunge naomba niwahakikishie Serikali hii ya Awamu ya Tano iko makini sana na Bajeti ya Wizara ya Elimu ndiyo

maana mmeona kuna mambo mengi mazuri yamefanyika. Naomba niwaambie kwamba fedha za elimu hazijapungua isipokuwa tumekuwa na mabadiliko kidogo katika *program* yetu ya lipa kulingana na matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha shilingi bilioni 90,088,000,340 za Lipa Kulingana na Matokeo tumezipeleka katika Fungu Namba 56-Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo, kama zingebaki katika Fungu Namba 46 kama ambavyo ilikuwa katika bajeti ya 2018/2019, bajeti yetu ingesomeka triliioni 1,478,000,000,000. Kwa hiyo, endeleeni kumuamini Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli yuko makini sana katika maeneo ambayo ni muhimu katika Taifa hili, na kamwe hawezi kuchezea mfumo wa elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala ambalo limekuwa likijitokeza ambalo Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu wamekuwa wakitushauri kama Serikali. Kwa kweli kama nilivyosema tunaheshimu sana na kuthamini michango ambayo inatolewa na Kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii lakini nikiri tu kwamba wakati mwagine siyo kila ushauri unaweza ukafanyika au ukatekelezeka kwa mara moja na haina maana kwamba usipotekeleza umepuza. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tunaposema Serikali imepokea ushauri mtuelewe hivyo kwamba kuna mambo mengine ambayo tunapaswa kama Serikali kuyazingatia na kujiridhisha kabla ya kutekeleza moja kwa moja ushauri ambao umetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ushauri ambao umetolewa kwamba tuvipange Vyuo vyetu Vikuu katika madaraja mbalimbali. Mifano imetolewa kwamba tuangalie nchi kama Marekani; ukiangalia Nchi ya Marekani, ukiangalia Nchi za Ulaya zenyewe zimeendelea sana katika mifumo yao ya elimu. Sisi katika Elimu ya Juu vyuo vyetu vingi bado ni vichanga na kwa maana hiyo Serikali ina wajibu wa kuvilea na kuhakikisha kwamba vinakuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tukianza kuweka madaraja ukasema kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Daraja la Kwanza, ukasema labda kwa mfano, Chuo Kikuu cha Mzumbe sijui Daraja la Tatu, tayari utakuwa unawapa picha Watanzania kwamba hapa siyo mahali pazuri pakwenda; na ukianza kuangalia kwamba Serikali ina vyuo, sasa Serikali yenyewe ikianza kupanga vyuo na ni ukweli usiofichika kwamba tukipanga vyuo vya Seriakli ndiyo vitakuwa katika madaraja mazuri. Sasa kesho mtarudi hapa na kusema kwamba Serikali inanyanyapaa vyuo binafsi. Tuache Watanzania wenyewe wataamua kwamba waende wapi na ndiyo maana Serikali imetoa uhuru, hatuwapangii wanafunzi mahali pakwenda kusoma. Kila mwanafunzi yuko huru kuchangua Chuo anachotaka kwenda kusoma mwenyewe. Lakini tumeshuhudia viro vyuo ambavyo vinapata tabu sana kupata Wanafunzi.

Kwa hiyo tayari madaraja yamejipanga miongoni mwa Watanzania wanafahamu wapi wakienda watapata elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumejaribu kuangalia uzoefu katika Nchi za wenzetu ambao wanapanga hayo madaraja. Kunakuwa na changamoto kwa sababu unapoweka madaraja kunakuwa na changamoto kama vile kuwepo kwa malengo na vigezo tofauti na vinavyotumika katika ushindani au kunakuwa na vyuo vinajikita zaidi katika yale maeneo ambayo yanajua kwamba ndiyo haya yanayotumika katika kuwapanga katika madaraja. Lakini pia katika Nchi za wenzetu, jukumu la kuvipanga vyuo katika ubora halifanywi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika nchi za wenzetu jukumu la kuvipanga vyuo katika ubora halifanywi na Serikali. Kwa hiyo, pia nishauri kwamba Kamati ya Makamu Wakuu wa Vyuo na Wakuu wa Vyuo Vishiriki hapa nchini wanaweza wakalichukua hilo jambo wakaliangalia lisiwe jambo la Serikali. Kama wataona inafaa, sisi Serikali hatuna tatizo lolote, lakini upande wa Serikali tukianza kupanga Vyuo vya Serikali viro daraja la juu, vyuo vingine vinaweza vikafa ikaonekana kama vile kuna namna ambayo Serikali inasema kwamba huku hakufai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Serikali, tutaendelea kuhakikisha kwamba tunakagua na kujiridhisha kwamba vyuo vyote nchini vinazo sifa stahiki ambazo zinaruhusiwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambacho Mheshimiwa Amina Makilagi alizungumzia, lakini na ndugu yangu Mheshimiwa Getere akampa taarifa ambayo alikuwa anachomekea, kweli ali shindilia, kwa hiyo, nimepokea maoni yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na mwaka huu tunatimiza miaka 20 tangu ameondoka duniani, Serikali inamthamini sana na Serikali ina dhamira ya kumuenzi kwa kuanzisha Chuo cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo kama ambavyo hata imeonesha katika llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu sasa kwa sababu limeulizwa hapa Bungeni, ni bahati mbaya kwamba hiki chuo pamoja na kwamba kuna majengo ambayo yalitolewa, lakini yalitolewa kwa maneno, kama Serikali hatujapata hati za kukabidhi na Serikali imekuwa ikifanya kazi kubwa sana kufuatailia, lakini mpaka leo ninavyozungumza, hati miliki hazijapatikana. Kwa hiyo, nisingependa kulizungumza sana, lakini naomba wanaohusika nitoe wito wakamilishe taratibu haraka kwa sababu dhamira ya Serikali ya kuanzisha chuo hiki iko pale pale kama ambavyo imeainishwa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa noamba nizungumzie uimarishaji wa mazingira ya wanafunzi wenyе mahitaji maalum. Suala la wanafunzi wenyе mahitaji maalum Serikali inalichukulia kwa uzito mkubwa sana. Kwa kutambua matatizo makubwa ambayo yapo katika shule hizi na Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamelizungumzia, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 11.2 katika bajeti hii

kwa ajili ya kununua vifaa visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenyе mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kutambua changamoto za ufundishaji, Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019 imeanzisha kozi ya stashahada katika Chuo cha Ualimu Patandi kwa ajili ya walimu wanafunzi wenyе mahitaji maalum. Pia Serikali imejenga Shule Maalum ya Sekondari katika Chuo cha Walimu Patandi ambayo inaweza kuchukua wanafunzi 640.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la kuhusiana na Wanafunzi Wenyе Mahitaji Maalum ni kuhusu muda wa kufanya mtihani, kwamba ule muda wanaopewa hautoshelezi. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Baraza la Mitihani la Tanzania huwa linatoa muda wa nyongeza kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalum na huwa linatoa dakika 10 za ziada kwa mitihani ya sanaa za jamii na dakika 20 za ziada kwa kila saa kwa somo la hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ina maana kama ni mtihani wa masaa matatu, mwanafunzi mwenye mahitaji maalum atapewa masaa manne ya kuyafanya kwa sababu anaongezewa dakika 20 kwa kila saa ya mtihani na kwa masomo ya *Arts* anaongezewa dakika 10 kwa kila saa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Serikali inawathamini sana watoto wenyе mahitaji maalum. Kama muda huu ambao tunaongeza dakika 20 kwa kila saa, utaonekana hautoshi, sisi tuko tayari kufanya *review*, lakini kwa sasa naomba tutambue kwamba Serikali inaongeza muda kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalum, lakini hata mwaka 2017 Baraza la Mitihani lilitifanya mapitio ya muundo wa mitihani kwa ajili ya wanafunzi wenyе mahitaji maalum ili kuzingatia namna ya maswali ambayo yanaweza yakaulizwa kulingana na mahitaji maalum waliiyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Sera ya Elimu na Mafunzo ambalo pia limezungumzwa na

Waheshimiwa Wabunge wengi; na hususan ni suala la muda wa elimu kwamba je, elimu yetu ni miaka sita au saba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba nilishawahi kujibu katika Bunge lako Tukufu, naomba nirudie kusema tena. Muda wa Elimu ya Msingi ni miaka saba, haujabadilika. Kwa sasa hivi Serikali haina mpango wowote wa kubadilisha muda huo kwa sababu Serikali imejikita zaidi katika kutatua changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge mmezizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba mitaala yetu inaishia Darasa la Sita, siyo kweli. Mtaala wa Elimu ya Msingi ambao taasisi ya elimu imeutoa uko mpaka Darasa la Saba. Kwa hiyo, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba watoto mwaka ule wa saba wataenda kucheza. Hakuna muda wa mchezo, hii ni Serikali ya kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu; na kazi ya mwanafunzi ni kusoma. Kwa hiyo, hata wanafunzi nao watasoma darasa la saba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la Vyuo vya Ufundu Stadi (*VETA*). Nikiri kwamba katika vyuo hivi kumekuwa na ahadi za muda mrefu na hata imekuwa kero kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kila siku wanakuja kuuliza maswali Bungeni kuhusiana na vyuo vyao. Wanahoji kwamba sasa je, Serikali ina dhamira kweli ya kujenga Vyuo vya Ufundu Stadi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba dhamira ya Serikali iko pale pale na sasa hivi dhamira iko kubwa zaidi kwa sababu tunajenga uchumi wa viwanda. Tunapojenga uchumi wa viwanda tunahitaji mafundi stadi na mafundi mchundo wengi zaidi. Kwa hiyo, dhamira ya Serikali ya kutekeleza sera ya kujenga *VETA* katika mikoa na Wilaya iko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema, kupitia fedha ambazo nasikitika sana kwamba wengine wanatumia maneno mabaya ya kuzungumzia kwa Washirika wetu wa Maendeleo, Serikali imeamua na inakwenda

kufanya. Kwanza sasa hivi tunaendelea na ujenzi wa *VETA* Mkoa wa Rukwa na Geita, tunakamilisha maandalizi ya ujenzi wa *VETA* kwa Mikoa ya Njombe, Simiyu na Kagera. Pia Serikali imekamilisha *VETA* ya Wilaya ya Namtumbo; na sasa hivi tuko katika hatua za ukamilishaji na usimikaji wa vifaa katika Wilaya ya Ilala, Nkasi, Urambo, Newala, Muleba na Simanjiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inaendelea kukamilisha matayarisho ya *VETA* Wilaya ya Itilima, Kasulu Halmashauri ya Wilaya, Babati na Ngorongoro. Pia Serikali inakamilisha kupata wataalam elekezi kwa ajili ya kujenga *VETA* katika Wilaya ya Ruwangwa, Kongwa, Halmashauri ya Mji wa Kasulu na Nyasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumaeamua katika bajeti yetu ya mwaka 2019/2020 Serikali imetenga jumla ya shilingi billioni 40 na tunakwenda kujenga *VETA* katika Wilaya zifuatazo: Chunya, Kilindi, Korogwe, Ukerewe, Chemba, Igunga, Pangani, Kishapu, Rufiji, Uyui, Kwimba, Bahi, Mafia, Longido, Mkinga, Uvinza, Ikungi, Iringa Vijijini, Lushoto, Mbarali, Monduli, Buhigwe, Ulanga, Masasi na Butiama.

Waheshimiwa Wabunge, mnataka nini tena ndugu zangu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwa kweli kwa sababu ya muda kama nilivyosema, nisingependa unifukuze kwa kengele, lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba sisi tumepokea maoni yenu lakini labda sambamba na hili la Vyuo vya Mafunzo ya Ufundu Stadi kumekuwa na maombi ya Waheshimiwa Wabunge kubadilisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kuzifanya ziwe *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vimeanzishwa kwa malengo mahususi, kwa hiyo, Serikali isingependa kuvibadilisha. Tutashirikiana na Wajumbe katika maeneo husika, kama kutakuwa na fedha, kwa sababu hata hizi Wilaya ni kwa kuanzia, lakini zoezi la kuendelea kujenga

VETA katika Wilaya litakuwa endelevu. Kwa hiyo, tutaweza kuwasiliana na katika maeneo ambayo tutakuwa tumeyafanya tathimini kwa kuangalia taratibu ambazo tunazitumia, basi hakuna dhambi yoyote ukiwa na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi na ukawa pia na vhuo cha VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutakarabati Vyuo vyote vya Maendeleo ya Wananchi na pia tutaboresha mafunzo yake lakini suala la *VETA* na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ningemba sana Waheshimiwa Wabunge tuache kama vitu viwili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie tena kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kweli kwa michango mizuri ambayo wameitoa. Niwahakikishie kwamba Serikali hii katika mambo ya elimu, kama kuna vitu ambavyo Mheshimiwa Rais ameviweka katika kipaumbele, ni elimu. Mumsikilize, mahali popote anapoongea, hawez akamaliza kuzungumza bila kuzungumzia masuala ya elimu. Hazungumzi maneno tu, lakini hata fedha tunapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika mwaka kwa fedha ulioisha 2017/2018, mpaka kufika Juni, 2018 tulipata bajeti ya maendeleo kwa asilimia 86 na tulipata bajeti ya matumizi mengineyo kwa asilimia 107, yaani tulipata zaidi ya kile kiasi ambacho kimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ninayo imani kubwa sana na Serikali kwamba katika kipindi hiki cha miezi miwili iliyobaki, Wizara ya Fedha itaendelea kutoa fedha kwa miradi ambayo ilitengewa fedha lakini mpaka sasa haijapata ili kuhakikisha kwamba tunaweza kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie pia kwa kuishukuru familia yangu kwa kuendelea kuniunga mkono; nimshukuru mwanangu Dajosi ambaye yuko hapa pamoja na mdogo wangu Benjamini Ndalichako. Nawashukuru sana Washirika wetu wa Maendeleo ambao wamekuwa nasi katika Bunge hili tangu jana tulipowasilisha hoja hii. Naomba

tu waelewe kwamba kuna lugha za Kibunge. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote wanathamini michango yao na ninaomba waendelee kushirikiana na Serikali kuiunga mkono nchi yetu katika sekta ya elimu ili iweze kusonga mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukurani za dhati sana kwa Watanzania wote wenye mapenzi na mema na Sekta ya Elimu ambao wamekuwa wakinipa maoni na ushauri mbalimbali ambayo yamekuwa chachu ya kuboresha elimu yetu. Niwahakikishie kwamba nitaendelea kuwa napokea maoni yenu na mnivumile wakati mwingine unakuta una *message* zaidi ya 350, siyo rahisi kuyapokea kwa wakati mmoja, lakini huwa najitahidi kusoma na kufanyia kazi kile ambacho mnanishauri kwa maslahi ya nchi yetu. Kwa hiyo, naomba msichoke kutoa ushauri na Wizara yangu itaendelea kulipokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia sana suala la mfumo wa elimu na kuwa na mjadala. Kama ambavyo wenzetu wa madini wamefanya kwa kukutana na wadau wao, naomba nimwagize Katibu Mkuu wangu aangalie uwezekano wa kuwa na mkutano mkubwa wa wadau wa Sekta ya Elimu ili tuweze kupata mawazo yao. Hakuna tatizo lolote. Serikali ipo tayari kusikiliza na iko tayari kufanyia kazi mawazo ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawashukuru sana ndugu zangu wa Mkoa wa Kigoma, ndugu zangu wa Wilaya ya Kasulu ambao wamekuwa wakinitia moyo katika jukumu langu la Kitaifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote waunge mkono bajeti hii ili tuweze kwenda mbele, tuweze kuchapa kazi, tuweze kuendeleza elimu katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naamini kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wataunga

mkono bajeti hii kwa sababu elimu haina itikadi, watoto wote wa Kitanzania wanastahili kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Kif. 1001- *Admin. and Human Resource Management*.....Sh. 7,524,038,930/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa tulishapata majina ya wachangiaji wa mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Naanza na Mheshimiwa Mwita Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuanza kuchangia. Baada ya kusikiliza maelezo mengi sana ya Mheshimiwa Waziri na kumwona jinsi anavyojibu, nilitaka kupata ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza mambo mengi sana hapa; nataka kupata ufanuzi wa majengo au maboma ya maabara katika maeneo mbalimbali ya nchi hii na vifaa vyatayansi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri akizungumza hapa mambo ya viwanda; na tunapozungumza mambo ya viwanda, tumezungumza mambo ya VETA. Nchi yetu leo inaenda katika sayansi na

teknolojia, kama hatuna wanafunzi wanaosoma katika masomo ya sayansi kwenye maeneo haya, hivi Vyuo Vikuu viliviyotajwa karibu 40 ambavyo vinatakiwa kuanzisha mitaalaa mipyaa ya kupokea wanafunzi wa sayansi watatoka wapi kama kwenye shule za sekondari hakuna mahali ambapo wanasomea? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika eneo langu la Bunda katika Jimbo zima kuna zaidi ya sekondari tisa za maboma, yako maboma 18 yamejengwa 2015 mpaka leo hayajaisha, yameezekwa tu; vifaa vingine vyaa sayansi vinakaa nje. Kwa hiyo, nilitaka kujua ni lini sasa Serikali; najua watashirikiana na TAMISEMI, yako mambo ambayo tunataka kufahamu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ndiyo inapokea fedha za wahisani. Wahisani wanatambua Wizara ya Elimu, siyo TAMISEMI. Kwa hiyo, unapoleta Wizara ya Elimu inakuwa na fedha za kusaidia huko kwenye maeneo ya sekondari. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi, anawezaje kumaliza tatizo hili la maboma ya sayansi katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu na hasa katika Jimbo langu la Bunda?

Mheshiwi Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, yakinitosheleza, nitakaa kimya mama uendelee na shughuli zako, lakini kama yasiponitosheleza nitashika shilingi. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namwomba sana
Mheshimiwa Getere asinishikie shilingi, ninalea wajukuu
wanahitaji sana hiyo shilingi tafadhalii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba *commitment* ya Serikali katika kuimarisha miundombinu ni kubwa sana na ukiangalia katika bajeti ya 2019/2020 kiasi cha fedha ambacho kimetengwa kwenye miundombinu ya elimu ya sekondari, Ofisi ya Rais TAMISEMI wana shilingi bilioni

172,321 na kwenye Fungu Na. 46 tuna shilingi bilioni 146. Kwa hiyo, jumla ya fedha za miundombinu ziko shilingi bilioni 238,993.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani hiyo inaonesha ni *commitment* kubwa ya Serikali na fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vyta kufundishia ikiwa ni pamoja na vifaa vyta maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mtu anapokuwa anazungumza mambo haya, nimemuona Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hoja hizi na ametuambia ana watoto wake wako humu ndani alikuwa anafanya *commitment* kutoka moyoni, nashukuru kwa haya aliyoatoa ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi pia nilikuwa nashauri na ninaamini Mheshimiwa Waziri wa Fedha kidogo amejaribu kuigusia. Suala la fedha za mikopo ya wanafunzi ambayo kwa mwaka huu ni shilingi bilioni 450, ukiangalia fedha nzima ile ya Wizara ya Elimu ambayo iko kwa upande wa maendeleo (*development*) sehemu kubwa ni fedha za mkopo wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza, kama alivyoelekeza Waziri wa Fedha kwamba wataifanyia kazi, ingerudishwa iende kwenye matumizi ya kawaida (*recurrent*). Ukipata kule, huku kwenye *development* itabaki ile halisi, lakini tukishapata ile ya kwenye *recurrent* ukichukua *40 percent* yake itabidi tuongeze tena pesa nyingine za *development*. Ina maana tutapata pesa zaidi kwa upande wa *development* na fedha nyingi hizo tungezielekeza kwenye vyuo hivi vyta ufundi (*skills*

development) na ujuzi ili Watanzania wengi watakapokwenda kwenye sekta hiyo watakuwa na ajira za kutosha na huko tunakoelekea kwenye uchumi wa viwanda hao ndio tunatakiwa tuwe nao wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo langu ni kwamba hata ikiwezekana kwa sasa hivi kwenye bajeti hii, tuweze kuipeleka kwenye *recurrent*. Hakuna kinachobadilika ila asilimia zile za fedha ambazo zinatakiwa kuja kwenye *development* zitaongezeka ili ziweze kwenda kwenye masuala ya ufundi. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wenzangu waniunge mkono hoja ili tuweze kuijadili kwa upana.

MWENYEKITI: Ahsante.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikia hoja ya Mheshimiwa Jitu Soni. Kwa *convention* ilivyo, mikopo hii kwa wanafunzi ni sehemu ya *development*, huwezi ukai-*classify internationally* kama *recurrent*.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia hoja ya Mheshimiwa Jitu Soni, kwa *convention* ilivyo mikopo hii kwa wanafunzi ni sehemu ya *development*, huwezi ukai-*classify internationally* kama *recurrent*. Kwa hiyo, njia sahihi ni hii ya Bodi ya Mikopo kama nilivyosema iombe *a separate Vote* ili kuweza kuitofautisha, lakini sio kui-*classify* kama *reccurent*. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, nafikiri umeridhika Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi, isipokuwa naomba basi ifanyiwe kazi mapema. Nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hamidu Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nisiporidhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri

nakusudia kutoa shilingi. Hoja yangu ni ile ambayo nilianza kuizungumza wakati nachangia muda wa mchana, kwamba, matokeo ya ufaulu ya darasa la saba, ya sekondari, yaani namaanisha *O-Level* na *A-Level* yatenganishwe kati ya *private schools* na *government schools*. Lengo ni sisi kupata kufahamu hii *input* ya Serikali inayofanyika inaleta *output* ya namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo panapotolewa matokeo ya kidato cha nne, *let say*, yanatolewa maelezo kwamba, matokeo yameongezeka, ufaulu umeongezeka kumbe inawezekana kilichoongezeka ni idadi ya shule za *private* nydingi, ambako kunapatikana A nydingi, B nydingi, inakuja ina-subsidise na matokeo yale ya F na D nydingi katika shule za Serikali. Sasa, ili tuweze kujua *performance* halisi ya ya shule za Serikali, kwa nini Serikali haifikirii au kwa nini Wizara hii isitoe matokeo ya *private* kwake na Serikali kwake. Hili lina *advantage, advantage* yake ni kwamba, mikoa yenye shule za *private* chache kama ulivyo Mkao wa Lindi una shule tatu za *private*, mara zote unawekwa kwenye *list* ya mwisho kwa sababu, ni watoto wale katika shule za Serikali tu ndio wanaokwenda kupambana na shule zile za *private* ambao wanafanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka Serikali itueleze ipo tayari kutoa matokeo *separate, private* kwao na Serikali kwao, ili tuweze kupima *performance* ya shule za Serikali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Bobali aturudishie tu shilingi asije akaishika kwa sababu, hoja ambayo ameiletu kwa kweli ni hoja ambayo ni nzuri na kwa vyovypate vile tuko tayari kwenda kuifanyia kazi. Hata hivyo, nataka tusaidiane vilevile kufahamu kwamba, hata tukiondoa shule za *private* tukitenganisha na shule za umma, haimaanishi kwamba, tutakuwa tumeongeza ufaulu wa mwanafunzi mmoja mmoja, kwa hiyo, sisi katika Wizara ya

Elimu lengo letu na ndio kazi kubwa tunaifanya, ni kuhakikisha kwamba, mwanafunzi mmoja mmoja anafaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani, tunaweza tukaondoa tukapeleka huko shule za *private zikawa* zenyewe na za umma zikawa zenyewe, lakini baadaye bado kutakuwa na *division 0*, bado ufaulu hautakuwa mkubwa. Kwa hiyo, hata kama tutabeba hii hoja, lakini ifahamike kwamba, sisi tutaendelea kuboresha elimu ...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri umeeleweka.

Mheshimiwa Bobali hoja yako wameipokea na wanaifanya kazi.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yake kidogo yamejikanganya kwa hiyo, naomba nitoe hoja...

MWENYEKITI: Aah, Mheshimiwa Bobali...

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Ndio.

MWENYEKITI: Ngoja nikwambie Mheshimiwa Bobali, Serikali imeshaji-*commit*, meshasema wanapokea hoja, wanaifanya kazi, wakaeleza zaidi kuwa hakutakuwa na mabadiliko mbele. Sasa wewe unataka nini?

Mheshimiwa Susan Lyimo. (*Makofij*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba, katika hoja zote ambazo Mheshimiwa Waziri amezijibu kwa takribani *one hour* hajagusia suala la Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu ndio kila kitu katika elimu na Wabunge karibu wote walioongea wameongelea matatizo makubwa ya Walimu na natambua kwamba, pamoa na kwamba, Walimu wapo kwenye maeneo mengi,

Iakini Wizara hii ndio Wizara mama ya kuhakikisha kwamba, maslahi ya Walimu, ndio mlezi au ndio mama. Sasa kama Walimu Mheshimiwa Waziri hajawatambua, anategemea elimu yetu itakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kujuu kwanza upungufu huo mkubwa wa Walimu uliopo ni kwa sababu gani? Pia ni lini sasa watahakikisha kwamba, maslahi ya Walimu wetu, *including* nyongeza za mishahara, kupandishwa madaraja na nilileta barua hapa ya kuonesha jinsi gani ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan, hoja yako ni moja tu.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Walimu. Nataka kujuu Wizara inasema nini kuhusiana na masuala ya Walimu? Kwa maana hiyo, kama sitapewa majibu ya kuridhisha nitaomba niungwe mkono, ili tujadili jambo hili kwa sababu, Walimu ndio wametufikisha sisi hapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hiyo hoja imezungumzwa mara kadhaa na wakati wa majumuisho juzi suala la madaraja Mheshimiwa Waziri wa Utumishi wa Umma ameshatoa Kauli ya Serikali kwamba, kuanzia Mei Mosi yatafanyiwa kazi na suala la nyongeza ya mishahara limeshazungumzwa na Mheshimiwa Rais na tunajipanga, uwezo ukipatikana wataongezwa mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu, tunatambua kwamba, tuna Walimu wa shule za msingi zaidi ya elfu 86 wanadai zaidi ya shilingi bilioni 43 na sekondari shilingi bilioni 18. Madai ya Walimu kwa ujumla wake kwenye ngazi zote shilingi bilioni 61 na zaidi na Serikali imeshafanya

mchakato huo, madeni yametambuliwa, tunajipanga tukipata uwezo wa kutosheleza wataanza kulipwa madeni yao kwa hiyo, maslahi yao yanazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana sasa baada ya kuangalia ili tusiwe na madeni makubwa, tumetangaza ajira baada ya kujiridhisha. Wale Walimu ambao wengine wamestaafu na wengine wameacha kazi kwa sababu mbalimbali ili akiajiriwa aweze kulipwa maslahi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa yote, kuna maelekezo kwamba, kama Mwalimu anataka kuhamishwa kutoka eneo moja kwenda lingine asihamishwe kabla ya kulipwa haki yake ili kutoendelea kuongeza madeni na kuongeza mzigo ndani ya Serikali. Nashukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Susan *commitment* hiyo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waitara kwa sababu, toka akiwa Waziri wa Utumishi Mheshimiwa Celina Kombani masuala ya Walimu mishahara yao kwa muda mrefu imekuwa hailipwi, leo tunaambiwa bado Walimu wana deni la zaidi ya shilingi bilioni 61 baada ya uhakiki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan, Serikali imejibu ...

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kwa sababu, Walimu wana matatizo makubwa.

MWENYEKITI: Ngoja basi, ngoja mimi, ngoja Mheshimiwa Susan. Kuridhika kutokuridhika bado hakukupi nafasi ya, kaa kwanza, kaa chini kwanza, kaa kwanza; Waziri wa Utumishi amejibu vizuri juzi, Kauli ya Serikali imetolewa Bungeni imeeleza mkakati wa Serikali na *Road Map* ya madaraja haya na maslahi ya watumishi wote wa Serikali. Mheshimiwa Waitara ame-reteret hayohayo ya Serikali, sasa msitake ku-*politicise* hivi vitu. (*Makof*)

Sasa Mheshimiwa Susan, ngoja sijamaliza na wala lisikutese. Haya, funga hoja yako. (*Kicheko*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waitara au na majibu ya Serikali kwa sababu, suala la kupandisha madaraja ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Komu, Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Mpango, Mheshimiwa Simbachawene umesimama au? Mheshimiwa Mollel, Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Kunti na Mheshimiwa Waitara.

Tunaanza na Mheshimiwa Kunti.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na niombe kumuunga mkono Mheshimiwa Susan Lyimo kwenye hoja yake. Tunazungumzia maslahi ya Walimu na sote humu ndani bila Walimu hakuna ambaye angekanya humu ndani au nafasi tulizonazo siamini kama watu tungkuwa nazo kama Walimu hawa kipindi hicho wasingeweza kujaliwa maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waitara amesema Walimu wanadai bilioni 61. Jiulize swali, kama Walimu hawa leo wanadai bilioni 61 ni Mbunge gani ndani ya Bunge hili anayeidai Serikali bilioni 61? Kwa nini Walimu wadao bilioni 61, Wabunge sisi tunapomaliza muda wetu tunapewa cha kwetu tunaondoka halafu watu hawa waendelee kudai bilioni 61? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu hiki hakikubaliki. Hatuwezi kuendelea kuwanyanyasa Walimu hawa kwa madeni yao ambayo ni stahiki zao, hawaombi msaada hawa

watu. Wamefanya kazi, wanatakiwa wapande madaraja, walipwe hela zao, wahamishwe kwa wakati na stahiki zao wapewe kwa hiyo, suala la kusema kwamba, wnafanya mchakato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili wamefanya makusudi, wameamua Wizara ilete...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha; angalia shingo hiyo, kaa chini, muda wako umekwisha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo. Nilipochangia leo asubuhi hapa nilieleza umuhimu wa Walimu wakiwa walezi wa Taifa letu. Bahati nzuri tena ameingia Mwalimu mwingine huku, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu na ye ye ni Mwalimu pia, Mwalimu Waitara, Mwalimu Dotto na ye ye yuko pale na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa walezi wa Taifa letu nimetoa mchango hapa ndio maana naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo. Tunapitisha bajeti, Serikali inasemaje, je, maslahi yao yote na madai yao yote yako kwenye bajeti hii? Kwa sababu wanaposema kwamba, watasubiri wakishahakiki ndio waweze kupata maslahi yao, aidha, huo uhakiki unachukua miaka mingapi? Au watuhakikishie kwamba, kauli ya kesho ya Mbeya ya *May Day*, marupurupu yao yatapanda na mishahara yao itapanda?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mbatia. Mheshimiwa Komu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo kwa sababu, juzijuzi hapa nilikuwa nasoma taarifa fulani

ya Haki Elimu nikakuta wamesema morali ya Walimu imepungua kwa asilimia 40. Hapa Mheshimiwa Mbatia ambaye ni mbobezi sana kwenye mambo haya ya elimu ananiambia ni asilimia 60 sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni hatari, lakini tunavyopewa kauli hapa za kisiasa kwamba, matatizo yao yanashughulikiwa, kwa kweli, tunaliangamiza hili Taifa. Kwa sababu, tunaambiwa hapa wanadai bilioni 61, nijambo gani muhimu zaidi kwenye hii nchi ambalo ni zaidi ya kuwalipa Walimu haki zao? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyoongea hapa sasa hivi wako Walimu walioajiriwa toka mwaka 2014 hawajapandishwa madaraja. Leo nimeambiwa kuna zuio la Waziri Mkuu la kuhamisha Walimu kwa sababu yoyote ile. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mollel.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwombe mama yangu mpendwa ambaye amefanya *presentation* ya elimu nzuri sana kwamba, amuachie Waziri shilingi yake kwa sababu, kwanza utaona *trend*. Mambo yaliyokuwa kero huko nyuma na ambayo hayafikiki kwa sasa kwa mfano kwenye bajeti ya maendeleo Mheshimiwa Waziri huyu amefika zaidi ya asilimia 86, lakini utaona kwenye mambo mengine yale zaidi ya asilimia 107, lakini utaona Serikali kwenye ile miundombinu ya msingi kama *Stiegler's* na zingine kuna pesa kubwa zimeenda upande ule na hizo zitaongeza pato la Taifa badaye na kuongeza viwanda. Maana yake kuna matumaini kwamba, matamko ya Serikali na maelekezo kwamba inatekelezeka na tumeona kwa vitendo kwa hiyo, hata hili hatuna sababu ya kutokuiamini Serikali kama imewezezana haya ambayo yalikuwa ni sugu kwa muda mrefu hata hili linawezekana. Kwa hiyo, namuomba mama yangu afanye hivyo. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwigulu.

MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge watambue jitihada ambazo Serikali imefanya kutoka kwenye madeni ya zaidi ya bilioni 260 zilizokuwepo zamani wakati Walimu wanadai mpaka kwenye bilioni 61 ambazo takwimu zimetolewa. Maana yake hiyo peke yake inaonesha kwamba, Serikali inaweza kulimaliza jambo hili. Hizi zilizopo ni kwa sababu tu aina ya madeni haya ni madeni ambayo ni endelevu kwa maana ya hivyo vitu vinatokea kila wakati. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maslahi yao pamoja na maslahi ya watumishi wa umma kwa ujumla, turejee pia, takwimu kwamba, tulishafika kwenye space ambayo illikuwa haiwezi kuwezesha Serikali kuongeza maslahi yao, lakini Serikali au Rais anachofanya ni kuongeza wigo wa kuweza kupata mapato ambayo yataweza kuwezesha kuwalipa Walimu kwa kiwango kikubwa zaidi. Sasa kwa kuwa, Waziri ameshatoa tamko jinsi ambavyo watakwendwa kulishughulikia hili, Waziri wa Elimu pamoja na Utumishi, tutoe fursa wala hamna anayebisha kuhusu umuhimu wa Walimu, wala hamna anayebisha umuhimu wa watumishi wa umma, lakini ni kwamba, Serikali inafanya kazi mambo haya kwa ujumla wake na itakuja na majibu ambayo yatawaridhisha Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, turidhie kwamba, kwa kazi ambayo Serikali inafanya hata Walimu wenyewe wanajivunia kazi kubwa ambayo Serikali inafanya. Kila mtu ambaye yuko hapa nchini anachangia katika shughuli ambazo zinafanywa na Serikali, hata Walimu watajisikia kwamba na wenyewe wamechangia kwamba, kuna wakati walifunga mkanda, sio kufungwa mkanda, walifunga mikanda ili Serikali iweze kutengeneza fedha nyingi na badaye Watanzania wote waweze kulipwa vizuri zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sasa hapo ndipo ninapofikiri kwamba, wakati wote adui ni adui tu. Mimi sikutegemea kama Mheshimiwa Susan angeanza kuwa na ubishi juu ya Waziri kwa sababu, amemjibu kila kinachofanyika. Maombi yake yote amejibu, lakini bado yupo tu anamuatafuata nyuma, sasa sijui kwamba, kinachotokea ni kitu gani kwa sababu jana na juzi, mimi ni shahidi mke wangu alikuwa Dodoma...

MHE. JOHN W. HECHE: Kuhusu Utaratibu. Kuhusu Utaratibu, Kuhusu Utaratibu.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: ...amekimbia Bunda kwenda ku...

MWENYEKITI: Mheshimiwa neno lile ni *metaphor* tu, wala haina *consequence*.

MHE. JOHN W. HECHE: Kauli ile atoe. Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Hapana, kaeni, kaeni.

MHE. JOHN W. HECHE: *We are not enemies here.*

MWENYEKITI: Basi kaeni, ni *metaphor* tu, kaeni.

MHE. JOHN W. HECHE: *We are not enemies here.*

MWENYEKITI: Sawa, kaeni.

MHE. JOHN W. HECHE: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Sawa, kaa.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema Walimu sasa hivi wote wamepewa, ni gazeti limeandika, wamepewa siku tano kurekebishiwa maeneo yao yote ya mapunjo.

MHE. MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, na sasa hivi wako kwenye kazi hizo wanafanya hizo kazi.

MWENYEKITI: Mimi ndio na-*control*, nimeshasema kaeni chini.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: ... watu wanawashughulikia.

MBUNGE FULANI: (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: Nitakupa baadaye, kaa chini.

MBUNGE FULANI: (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: Unabishana na mimi?

MBUNGE FULANI: Afute basi ile nanihii.

MWENYEKITI: Unabishana na mimi sasa? Kaa chini, *Chief Whip* kaa chini. (*Kicheko*)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha, kaa chini na wewe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Labda kwanza niseme naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa kwamba, shule za msingi Walimu wanadai bilioni 43 na shule za sekondari bilioni 18. Sasa niombe tu kwamba, walimu wapewe fedha zao, kwa sababu, zamani watu walikuwa mtu anaposoma anajifananisha na Mwalimu na kila mtu anataka kuwa mwalimu, lakini siku hizi walimu maisha yao yamekuwa magumu. Siku hizi imefika mahali mwalimu anakwenda shule kama mjasiriamali, anabeba deli la *ice cream*, anabeba karanga, anabeba kashata, anabeba ubuyu, anabeba na vitu vingine kwa sababu, anataka kuongeza kipato. Mwalimu na yeye ni mzazi anasomesha watoto. Sasa Serikali ituambie lini inawaongezea mshahara wao? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata pale wanapopandishwa madaraja mwalimu anapandishwa daraja mwaka huu, lakini bado anamaliza miaka mitatu mshahara anaolipwa ni uleule wa daraja alilokuwa nalo zamani. Kwa hiyo, naiomba Serikali na kuitaka ituambie lini italimaliza hili tatizo? Iribidi iongeze fedha Walimu walipwe fedha zao. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sijui hapa tunabishana nini kwa sababu, kwanza suala la maslahi ya watumishi wa umma Wizara ya Utumishi imeshapitisha bajeti yake hapa na mwenye Wizara ametoa kauli Bungeni kwamba, kuanzia Mei Mosi madaraja yatapandishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kunti anapozungumza watumishi, Walimu katika nchi hii ni zaidi ya asilimia 62 ya watumishi wote wa umma. Kwa hiyo, tunapozungumza *figure* ya shilingi bilioni 61 usifikiri kama ni mtu mmoja-mmoja, haya madai yalikuwa fedha zaidi ya hizi. Baada ya uhakiki tukapata bilioni 61, yaani madai kwa ujumla wake, haya madeni tunayozungumza, uhamisho na kila kitu yote bilioni 61. Serikali imehakiki imeondoa madeni hewa, sasa tunasema mpango uliopo ni kulipa fedha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, hapa hata kama tunafanya siasa ya kesho tuzungumze, Rais hawezi kushinikizwa. Rais ndio amealkwa kesho Watumishi wa Serikali, wafanyakazi kesho, kama ana kauli yake hawezi kulazimishwa humu. Amewasikiliza huyu Rais wa nchi hii, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni Mwalimu. Kwa hiyo, hakuna mtu mwenye uchungu zaidi yao, tусidanganyane hapa. Kama tunafanya siasa maslahi ya Walimu, hakuna mtu anapenda watumishi hawa Walimu kama Serikali yenewe ya Chama cha Mapinduzi. Ndio imewaaajiri, inajenga nyumba, inalipa maslahi, inawahamisha na tunaajiri kulingana na uwezo wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshajipanga, tumejua deni la walimu na Rais ameelekeza mwalimu asihamishwe bila kulipwa. Hivi sasa tuna shilingi bilioni karibu 16 imapelekwa mikoani, mwalimu akitoka kituo A alipwe kwanza ili tusiwe na madeni mengine mapya, tumalize madeni. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mwalimu arudishe shilingi Profesa afanye kazi yake njema ili shughuli iweze kusonga mbele. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kumwomba sana dada yangu Mheshimiwa Susan Lyimo, unajua wale wajukuu wa dada yangu ukimuondolea hiyo shilingi maana yake awahamishie kwangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la msingi zaidi ni kwamba Serikali hii ina-*commitment* kubwa ya kulipa maslahi ya walimu. Kila mwezi sisi pale Hazina tunalipa shilingi bilioni

5.06 kwa ajili ya posho ya Walimu Wakuu pamoja na Waratibu wa Elimu Kata na hii ni sehemu ya maslahi ya walimu. Siyo hivyo tu mpaka kufikia 29 Aprili, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imekwishalipa shilingi billioni 27.89 kwa ajili ya madai mbalimbali ya walimu 28,115. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan Lyimo, nimalizie tu kukuhakikisha kwamba kwenye mkakati wa Serikali wa kulipa madai mbalimbali ya watumishi wa umma, wakiwemo walimu, tumefanya maamuzi kwamba *tuta-fast track* madai ya walimu na watumishi wengine wa umma. Kwa maelezo hayo, nakuomba sana Mheshimiwa Susan Lyimo muachie dada yangu hiyo shilingi tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, malizia.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimwombe sana Mheshimiwa Susan Lyimo, Waziri Kivuli wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa kweli asiondoke na shilingi kwa sababu ufanuzi mzuri wa Serikali tayari umetolewa na dhamira na *commitment* ya Serikali kwa watumishi wa umma inafahamika. Kwa hiyo, Serikali imekwishalipokea na suala hilo kama ambavyo wenzangu wamesema linafanyiwa kazi, kwa hiyo, *commitment* ya Serikali ipo. Naomba Mheshimiwa Susan Lyimo, tafadhali shilingi yangu usiondoke nayo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan (Seneta), Serikali imeshaji-*commit*.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuji-*commit* na majibu mazuri sana na kwamba hii Serikali ya Awamu ya Tano inafanya kazi kwa wanavyosema lakini huu siyo mwaka wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Tano, huu ni mwaka wa nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hivi, suala kwamba *Stiegler's Gorge* inajengwa, kwa hiyo, walimu shilingi

bilioni 61 zao hazipo, watuambie *framework*, hii shilingi 61 bilioni inakamilika lini ili sasa niweze kusema kwamba nitarudisha hiyo shilingi. Tuambiwe tu *framework, commitment* ya Serikali *to make sure* kwamba hawa walimu wanalipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kada nyingine yoyote hapa nchini inayodai zaidi ya walimu na walimu hawa ndio wanatengeneza taifa hili. Kwa hiyo, nataka *commitment* kuna *framework* yoyote ambayo inasema kwamba hili deni litaisha mwezi fulani, mwaka fulani, hiyo tu. Wakiniambia hivyo mimi nitarudisha shilingi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan, Waziri wa Fedha amesimama ametoa *commitment*, yeye ndiyo *custodian* wa fedha. Sasa Mheshimiwa Susan ukianza kusikiliza watu wallionuna huku hii kitu halendi. Ngoja ngoja Mheshimiwa Susan, sasa mimi nafanya *ruling*, hoja hii naipeleka kwenye Kamati ya Bajeti. (*Makofi/Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Kalanga.

MHE. JULIUS L. KALANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama sitapata maelezo mazuri ya Waziri, nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mimba za utotonii kwa wanafunzi wetu limeendelea kuwa kubwa pamoja na kwamba Serikali imetunga sheria nyingi za kumlinda mtoto. Ukiangalia mazingira halisi ya shule zetu ambapo hakuna mabweni hasa watoto wa wafugaji, wavuvi na wale watu wa pembezoni, tatizo hili ni kubwa na sioni *commitment* kubwa ya Serikali kuhakikisha kwamba inawalinda wototo hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali ni namna gani na mikakati gani mahsusii Serikali imeweka kwa ajili ya kuwalinda watoto hawa wanaopata mimba wakiwa shulenii na hata wakipata mimba, mazingira gani Serikali imeandaa kwa ajili ya kuwapatia elimu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana mdogo wangu Mheshimiwa Kalanga asije akashika shilingi kwa sababu hili suala tayari linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejikita kuhakikisha kwamba mimba za wanafunzi hazitokei ikiwa ni pamoja na kutunga sheria, tulifanya marekebisho ya Sheria ya Elimu ili kufanya ni moja katika makosa makubwa kwa mtu ambaye ametembea/amempa mwanafunzi mimba, kifungo chake ni miaka thelathini. Kwa hiyo, tumechukua hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumejitahidi kujenga miundombinu na hasa mabweni kwenye maeneo ambayo ni hatarishi zaidi, ambayo wanafunzi wanatembea umbali mrefu. Lengo likiwa ni kuwanusuru watoto hawa wa kike wasije wakapata mimba wakiwa wanafunzi kwa sababu ya umbali mrefu wa kwenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeweka utaratibu mzuri sana kwamba hata wale wachache ambao kwa bahati mbaya wakapata mimba bado watakuwa na fursa zingine za kupata elimu kwenye mfumo wetu wa kawaida wa Elimu ya Watu Wazima. Vilevile ndiyo maana tunajenga *VETA* nchi nzima, tunakarabati *FDCs* zote 55 zilizopo nchini, yote ni kwa ajili ya kutengeneza mazingira wasije wakakosa fursa za elimu. Kwa hiyo, namwomba mdogo wangu asije akashika shilingi.

MHE. JULIUS L. KALANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa *commitment* ya Serikali lakini waone tu kwamba suala la utekelezaji na utungaji wa sheria ni vitu viwili tofauti. Tunalo tatizo kubwa la usimamizi wa sheria tulizotunga kwa ajili ya kumlinda mtoto wa kike. Kwa sababu amesema watalisimamia basi tuone linafanyiwa kazi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kiteto.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Suala la kutoa elimu kwa Watanzania ni la kisera na linasimamiwa na Wizara ya Elimu hapa Tanzania. Wapo wananchi ambao hawapati elimu katika mfumo ulio rasmi bali kupitia mfumo ambao sio rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wapo watoto ambao wanazidi miaka tisa (9) ambao hawawezi kujunga na darasa la kwanza kwa sababu wamezidi ule umri ambao mwanafunzi anatakiwa kujunga darasa la kwanza lakini wapo watoto wa kike ambao wanapata mimba shulenii na sasa hivi wamezuiliwa hawawezi kurudi shulenii na wao pia wanatakiwa kupata elimu kwa mfumo ambao siyo rasmi. Pia wapo watu wazima ambao wao wanatakiwa kupata elimu ya watu wazima ambao hawajui kusoma, kuandika wala kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata jibu la kuridhisha nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha mfumo huu wa elimu usio rasmi ili kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata haki ya elimu ili kufuta ujingga hapa nchini Tanzania? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ningemwomba dada yangu asiondoe shilingi kwa sababu katika mipango yetu, tumeeleza dhahiri dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaendeleza elimu ya watu wazima. Nafikiri hata katika kuchangia kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja aksauliza yaani leo hii ndiyo mnaweka mkakati lakini kila jambo lazima ikifika mahali unajipanga na unaangalia namna ya kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Kiteto Koshuma kwamba Serikali tayari inayo mipango ya elimu nje ya mfumo rasmi. Kwa mfano, kwa wanafunzi ambao hawajaweza kwenda shule kwa wakati, tunao mpango wa

elimu kwa watoto waliyoikosa ambao una kundi rika mbili; kundi rika la kwanza ni kwa wale wanaoingia darasa la kwanza mpaka la nne na kundi rika la pili ni kwa wale wanaoingia darasa la tano mpaka la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua wanaosoma katika mfumo huo wanafanya Mtihani wa Taifa na wale wanaofaulu kama umri wao haujazidi miaka 19 wanachaguliwa na wanajiunga katika shule za Serikali. Tunao mpango kama huo kwa shule za sekondari pia na wanaofanya mitihani nje ya mfumo rasmi wakifaulu mtihani wao wanachaguliwa na kwenda kidato cha tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu chetu cha bajeti tumeonyesha kwamba Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ambayo ndiyo imepewa dhamana ya kuhakikisha inaendeleza elimu kwa watu wazima nchini, imetengeneza mkakati kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaimarisha mfumo huu. Nikiri kwamba kidogo tulikuwa tumelegalega kwenye elimu ya watu wazima lakini *commitment* tayari ipo kwenye kitabu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiteto.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo ni kubwa sana, nitaomba tulijadili suala hili kwa mapana na mrefu ili kuangalia ni namna gani mambo hayo aliyojasema Mheshimiwa Waziri yatatekelezwa na hasa ukiangalia kwamba katika Kitabu cha Maendeleo, ukurasa wa 38 na 39 hamna hata shilingi moja iliyotengwa, tutayatekeleza vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja Wabunge waweze kuniunga mkono ili tujadili suala hili kwa kuwa tatizo ni kubwa sana. Ahsante.

MWENYEKITI: Hawajatimia, kwa hiyo, hoja yako imekufa. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusudii sana kushika shilingi lakini kama maelezo yatakuwa haya jitoshalezi nitafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu Septemba, 2018 lilitunga na kupitisha Sheria ya *The Tanzania Teachers Professional Board* ambayo. Napenda kujua kwa upande wa Serikali ni mkakati upi uliopo katika uanzishaji wa hii bodi hasa tukizingatia maudhui mahsus ya kuanzisha bodi hii ni tuwe na walimu ambaao ni *professional*/kama zilivyo bodi zingine, kwa mfano, Bodii za Uhaisibu, Wanasheria, watu wa Manunuzi na *ma-Engineer*. Katika ile sheria ilikuwa hajjanyumbulisha namna bora ya ile mitihani itakavyokuwa inapitiwa katika chuo na shule mbalimbali ambazo walimu wanasoma ili wakihitimu tayari wanakuwa ni *professional*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo mazuri ya Serikali katika sheria hii pamoja na kanuni zake nini kimekwishafanyika na bodi inaanza lini. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwombe kaka yangu Mheshimiwa Mbogo asishike shilingi kwa sababu Serikali imelifanyia kazi suala hilo na kwa sasa hivi tumekwishakamilisha rasimu ya kanuni kwa ajili ya Bodii ya Kitaalam ya Walimu. Pia tumetengeneza muundo ambaao upo katika hatua za kuidhinishwa ili baada ya hapo sasa watumishi waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba hili suala la kanuni tutafuatilia kwa sababu Serikali yote ipo hapa Dodoma ili kuhakikisha kwamba kabla ya Bunge hili kuisha, kanuni hizo zinakuwa zimekamilika. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbogo, *commitment* hiyo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *commitment* hiyo, niombe tu Mheshimiwa Waziri

tusisubiri mpaka kauli ya Mheshimiwa Rais ndiyo jambo liende kwa wakati. Kwa hiyo, niombe tuende kwa wakati ili azma ya sheria ile iweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namrejeshea shilingi yake.
(Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ka kunipa nafasi. Mimi langu ni moja tu, mwaka jana wakati tunajadili bajeti moja ya jambo ambalo Mheshimiwa Waziri aliahidi kulitekeleza ni kuhakikisha marekebisho ya sheria na sera ya Wizara yanasmamiwa vizuri. Mojawapo ikiwa ni kuendelea kurekebisha nyaraka na miongozo mbalimbali ambayo ilikuwa imetoka na mpaka sasa inaonekana ni miongozo miwill tu katil ya miongozo yote ndiyo imeshughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilitaka kupata kauli ya Mheshimiwa Waziri na siyo kusudio langu kushika shilingi lakini nini kauli ya Serikali juu ya jambo hili ambalo kwa kweli ndiyo linaleta changamoto zote hizi kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kidogo imekuwa na uzito katika kufanya mabadiliko kwa sababu ni Wizara ambayo tumekuwa tunatuhumiwa kwamba tunafanya kazi kwa matamko na kadhalika.

Kwa hiyo, Wizara inajiridhisha na kuhakikisha kwamba mabadiliko yoyote kabla ya kufanyika yanashirikisha wadau kikamilifu. Naamini hata wadau watakulaliana name, hata wamiliki wa shule binafsi wapo, hizi nyaraka mbili ambazo anazzungumzia zimeshirikisha wadau kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeendelea kushirikisha wadau hata katika maeneo mengine na tunategemea kuja na mabadiliko ya sheria na taratibu mbalimbali katika maeneo takribani saba ambapo sasa hivi tupo katika hatua ya mwisho. Kikubwa jambo lolote kabla ya kufanya mabadiliko ni lazima tujiridhishe kwamba kuna haja na wadau wetu watuelewe ili tusilete mkanganyiko katika sekta ya elimu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mipango ni mizuri lakini inawezekana mingi tunafeli kwa sababu hatuna *time frame*. Mheshimiwa Waziri atuthibitishie muda wa kukamilisha haya, maana kati ya nyaraka 128 ni mbili tu zimekamilika kwa mwaka mzima. Sasa atuambie watamaliza kwa muda gani ili angalau tuwe tunafahamu kuliko kuja hapa kuwa tunabishania jambo ambalo linatuongoza wote kwa pamoja.

MWENYEKITI: Ahsante, amekuelewa na kwa vile hukutoa shilingi, hoja yako Serikali inaibeba watalifanyia kazi.

Tunaendelea na Dkt. Sware.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nitakayoyasema kama sitakuwa nimeridhika basi nina lengo la kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri...

MWENYEKITI: Hata wewe? (*Kicheko*)

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Ili tuweze kufikisha suala hili pale inapotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye suala la mtaala. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwa umuhimu wake mara ya mwisho kufanya mabadiliko

makubwa ni mwaka 1997, miaka 22 baadae. Hata hivyo, tunajua kwamba mtaala ndiyo dira ya tunafundisha na tunajifunza nini ili kujenga maarifa au taratibu fulani fulani ili kufikia malengo fulani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunasimama na kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu lakini hatuwezi tu kufanya kazi tu kama hakuna maarifa ile kazi inakuwa ni bure. Kwa mantiki hiyo hiyo tunasema sasa hivi nchi yetu tunajikita katika kukuza uchumi wa viwanda ili tufikie uchumi wa kat. Sasa hatuwezi kufikia malengo hayo kama huku kwenye *foundation* ya elimu na mtaala uliopo sasa hivi ni wa tangia 1997 na malengo ya 1997 siyo ya sasa hivi ya 2019. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate ufanuzi kutoka ka Wizara husika inayolea elimu nchini ambayo pia imebeba hiyo sera ya mtaala, wana mkakati gani au lengo gani tuone ipo *reflected* kwa hii bajeti tunayoipitisha kwamba tunajitathmini vipi katika mtaala wetu ili tuweze kufikia huo uchumi wa kat. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Dkt. Sware asije akashika shilingi kwa sababu jambo ambalo amelileta mbele yetu ni la msingi sana na tayari linafanyiwa kazi na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema kwamba mitaala na mfumo wetu wa elimu uko *centered* kwa mwalimu kuliko kwa mwanafunzi. Wizara imeona kuna hitaji la kuhakikisha kwamba elimu yetu inamjenga mwanafunzi zaidi kuwa mbunifu vilevile mtu ambaye anajiamini ili katika safari yake ya masomo awe ni mtu ambaye anaweza kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa muda sasa imekuwa ikijaribu kubadilisha mitaala ikiwa ni pamoja na mitaala ya vyuo vyaya ualimu kwa sababu kimsingi ni suala la

ufundishaji, ni namna unavyomfundisha mwanafunzi kuliko hata kubadilisha *content*. Kwa hiyo, siyo tu kwamba tunafanya mitaala yetu marekebisho lakini ukiangalia hata kwenye vyuo vyetu tayari tunaelekea kwenye hiyo *approach* ambayo ni *competency based* zaidi kuliko *knowledge based*. Kwa hiyo, namhakikishia kwamba katika kipindi kifupi tutaona mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata kwenye vyuo vyetu vya ufundi tumebadilisha namna tunavyofundisha. Ndiyo maana hata kwenye *FDCs* zetu tayari tumeshakuja na mitaala ya Kiswahili. Cha msingi tunakuja na utaratibu wa kufundisha ambao unamjengea mwanafunzi uwezo zaidi wa kujamini lakini kuwa mbunifu ili aweze kupambana na maisha kwa sababu hasa ndiyo lengo la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba asishike shilingi kwa sababu suala hili tayari linafanyiwa kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Sware.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kushika shilingi ili wajumbe wenzangu wachangie kwenye suala hili kwa sababu ni jambo nyeti sana. Tunachokitaka hapa siyo yale marekebisho ya mitaala mbalimbali bali mabadiliko makubwa kama hayo manne ambayo yalishatokea kwa sababu nyakati za sasa hivi zimebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Mmetimia kumi kweli? (*Kicheko*)

Haya Mheshimiwa Susan, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Mch. Msigwa, Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Tendega, Mheshimiwa Ally Saleh (Alberto), Mheshimiwa Anatropia, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Waitara na

Mheshimiwa Dkt. Mollel. Haya tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Mollel.

Mheshimiwa Suzan, Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Henche, Mheshimiwa Tendega, Mheshimiwa Albert, Mheshimiwa Anatropia, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Godwin Mollel. Mheshimiwa Mollel.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumuomba dada yangu amuachie Mheshimiwa Profesa shilingi yake kwa sababu suala analolizingumzia, tatizo tulilonalo kwenye nchi hii kwenye *creativeness* na *innovation* sio tu linatokana na mtaala lakini vilevile linatokana na kulea mtoto toka akiwa tumboni kwa maana ya *development* ya *brain*, na utaona ni namna gani Serikali imewekeza hela nyngi kwenye *nutrition* na kutoa elimu ya akina mama na watoto na jinsi ya kulea watoto, pesa nyngi sana zimeelekezwa kwenye eneo hilo. Kwa hiyo ni hatua za kwanza za kuanza kujenga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu unaweza ukatengeneza mtaala lakini mwisho wa siku, ukifika darasani usiwe na hiyo *brain* ambayo inaweza ikachukua kile kitu unachokitengeneza. Kwa hiyo, kwa juhudhi hizo ambazo Serikali inafanya ninakuomba dada yangu umuachie Mheshimiwa Profesa kwa sababu ni wa kuongezewa shilingi sio wa kunyang'anya shilingi, ukiangalia jinsi hii Wizara sasa hivi imetulia kama meli ambayo hakuna mawimbi tena kwenye bahari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna changamoto mbalimbali ambazo ziko mbele lakini haziwezi kutatuliwa kwa miaka mitatu. Nakuomba dada yangu hebu sikiliza muachie shilingi, mtie moyo aende mbele. (*Makofii*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. hoja aliyo*-raise* Mheshimiwa Dkt. Sware ni ya msingi sana. Hatuwezi kuwa na elimu bora kama hatuna mitaala bora, na nadhani wengi hatuelewi mitaala maana yake ni nini; ni ule mpangilio wa mambo ambayo mwanafunzi

anapaswa kujifunza, anayosaidiwa kujifunza na vilevile falsafa. Falsafa ya nchi yetu ni ya ujamaa na kujitegemea, lakini mambo yanayoendelea sasa hivi yanakwenda kwenye soko huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hoja ya msingi ni kwamba tunataka mitaala hii tunataka ibadilike, sio maboresho. Tunataka tuifumue kabisa, kwa sababu gani; kwa sababu lazima iendane na mazingra ya sasa hivi. Haiwezekani mtu wa kule Lushoto afundishwe mambo ya kule Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninadhani kuna kila sababu ya kuubadili kabisa huu mtaala ili uendane na hali halisi ya sasa hivi, ili uendane na mazingira, lakini vilevile itamsaidia mwanafunzi kutokukariri, itamsaidia mwanafunzi kuwa *more creative*. Ahsante

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi kwa misingi ya kwamba, kwa unyenyekevu kabisa wakati wa Mwalimu Nyerere tulikuwa na itikadi ya ujamaa, falsafa ikiwa ni kujitegemea, na mitaala yote tangu uhuru mpaka ule wa 1997 tulikuwa na falsafa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Sera ya mwaka 1995 inaonekaa tu kwamba ilifanyiwa maboresho kwenye mitaala ya 1997, je Sera ya 2014 imezaa nini wakati nchi yetu leo tunasema elimu msingi, ile ya mpaka Darasa la Sita na ile ya sekondari. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo linatugusa sote, ili tuweze kuliokoa Taifa hili Serikali ikubali na *iji-commit* kufanya *total overhaul/tuweze* kuwa na mitaala tunayoiangalia karne yetu kwa miaka 30 ijayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mambo ya maboresho tu wakati tunakwenda kwenye sera, tunakwenda kwenye mitaala na Mheshimiwa Mwalimu Kassim Majaliwa aliwahi kusema kwenye Bunge hili akijibu hapa kwamba sera,

mitaala miuhtasari, vitabu, sasa Mheshimiwa Mwalimu Kassim Majaliwa labda angetusaidia kujibu hapa kwamba Serikali inajili-*commit* namna gani kama alivyosema hapa ili aweze kulisaidia Taifa hili kuwa na mitaala ambayo tunaangalia taifa kwa miaka 20 ijayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono sana Mheshimiwa Mwalimu Dkt. Sware Semesi.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hali ambayo tuko sasa tunashindania kazi humu ndani kwa sababu zinakuja teknolojia mpya, lakini pia tunashindana na majirani zetu ambao huwa tunawaogopa. Sasa hivi tunawaogopa sana Wakenya kwa sababu tunaona kwamba wao wako mbele zaidi, lakini pia tunashindana katika *level/ya* kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kuna haja ya *ku-overhaul*, miaka 20 kwa sera kukaa hajabadihwa au mtaala kukaa miaka 20 hajabadihwa lazima tutaachwa na matukio ya kidunia na tukikubali kuachwa na matukio ya kidunia hapo tutakapobadilisha tutakuwa hatuvezi kuwapata tena wenzetu na ndiyo maana hivi leo pengine nchi jirani zetu nyngine zinasonga mbele zaidi kwa sababu zimekubali kubadilika, zimekubali kuweka sera mpya, zimekubali kuweka mtaala mpya, wanakwenda mbele, tunabaki kusema Rwanda wanafanya vizuri, uchumi huu unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiri kuna haja ya kujipanga vizuri na Serikali isikilize katika hilli. Tunalisema kwa kutaka *commitment* tu hapa kwamba sasa hivi umefika wakati baada ya *20 years* angalau kufanya mabadiliko ili twende na wakati tusije tukaachwa halafu maendeleo yote tunayoyafanya bado tutakuwa na vibarua katika wananchi wetu, watakuja watu wengine watachukua kazi tutabaki kuzuia kwa nguvu lakini watu wetu hawakutayarishwa kukamata kazi ambazo Sera ya Viwanda ambayo tunataka tuitekeleze hatujaijengea msingi mzuri. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwigulu.

MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaombe wenzangu waridhie kwamba jambo hili ambalo limewekwa Mezani si jambo la kuamuliwa Bungeni, ni jambo la kufanyiwa kazi na Serikali, na Profesa ni mbobez i kwenye sekta hii tunayoiiongelea, na kwa kuwa tayari ameshaanza kufanya kazi mambo haya, tumuache achambue, yale ambayo yana umuhimu kuendelea kuwa nayo tuendelee nayo na yale ambayo wataona yanatakiwa yafanyiwiwe marekebisho yaweze kufanyiwa marekebisho. Lakini tukisema tu twende na hii *total overhaul* tutakwenda kuacha na vitu ambayyo wenzetu tunaosema tunawagopa wanavililia wavione kutoka Tanzania. Kuna vitu vingi ambavyo Kenya inajifunza kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata hii mnayosema tunawaogopa sijajua tunawaogopa kwenye lipi. Kwa sababu kwenye *performance* hata vyuo vyetu bado viko juu, hata kwenye akili tumesoma nao tulikuwa tunawashinda, hata kwenye miradi kuna miradi tunawashinda, hata kwa uendeshaji wa uchumi kuna mambo mengi tunawashinda. Kwa hiyo, nadhani tumuachie Mheshimiwa Profesa aendelee kuchambua yale ambayo yanastahili kwa nchi yetu yabaki, na yale ambayo ni mwafaka kwa karne tunayokwenda nayo na kwa majira tunayokuja nayo mbele aweze kuyaweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa jambo ambalo linahusu labda kuongeza au kupunguza fedha ingekuwa sawa wenzetu kutushawishi hapa tuweze kuona namna gani tunaweza kumuongezea fedha, lakini haya ya kiuchambuzi tumuachie Mheshimiwa Profesa aendelee kuyafanya kazi na timu yake na wataitendea haki nchi hii kama ambavyo tumeona hatua kubwa ambayo ameshaifanya Mheshimiwa Profesa katika Sekta hii ya Elimu.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nimuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Sware kwa hoja hii aliyotoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia mtaala tuangalie kwamba kuna mambo gani ambayo tunataka yafikiwe katika nchi yetu. Tunahangaika, tulikuwa na falsafa ya ujamaa na kujitegemea, tuko kwenye soko huria, kwa hiyo tunahangaika kuweka viraka katika mtaala tulionao. Sasa hivi viraka vinavyozidi vikizidi utakuta unakosa hata sehemu ya kushona kama ni nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nasema ni bora tuwe na *total overhaul* ya *curriculum* ili tuweze kuweka misingi ya elimu katika nchi yetu na tuone jinsi ambavyo tunaweza tukatimiza nia yetu katika elimu. Kwa mfano unavyotaka mafunzo yaweje, unavyotaka vitabu viweje, tunakuwa kwenye mtazamo wa soko huria kama ni falsafa au viwanda kama tunasema ni viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, masuala ya kusema kwamba tunarekebisha leo tumepata viwanda tuweke kidogo, keshokutwa tutapata kitu kingine tutaweka kidogo, siku nyingine tunapata kingine, mwisho wake tunakuwa tumeweka viraka vingi ambavyo hata walimu hawajapata mafunzo na matokeo yake tunazidi kuwapa dozi kubwa wale wanafunzi ambao wanafundishwa kule na mwisho wake ndio tunasema wamefeli kumbe ni sisi ambao tunaandaa ndio tunakuwa tumeshindwa kuweka msimamo mzuri katika elimu. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Unapozungumza kubadilisha mtaala kwa kweli tunahitaji utafiti wa kutosha sana, kwa hiyo hili ni jambo ambalo kwa kweli likiamuliwa kwa kura ntawashangaa sana Waheshimiwa Wajumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri hakuna mtu ambaye ana wasiwasi na Mheshimiwa Profesa Ndalichako, huyu alikuwa mtendaji wa *NECTA* mnakumbuka, huyu ndio amekuja hapa watu wanalamika yale maswali ya kuchagua ya hesabu, angalau wanafunzi wafanye mahesabu kwa kazi ili aweze kupata jibu sahihi. Mheshimiwa

huyu ameondoa vyeti feki amehakikisha imefanyika hiyo, ku-*verify* ili watoto wawe na uwezo huo mkubwa. Huyu Mheshimiwa Profesa ndio ameondoa mambo ya *GPA* turudi kwenye mfumo wa zamani, mambo kama haya muhimu makubwa ndijo watu wanajenga maabara ili watoto wawewe kufanya vitu kwa vitendo waende kwenye soko la ushindani, tumeyaboresha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesema tumechukua jambo hili linafanyiwa kazi. Hili jambo ni mchakato, ni lazima twende hatua kwa hatua, ni utafiti gani umefanyika hapa kuonesha tunabadilisha kitu gani hapa, nini tunataka kubadilisha? Kwa sababu Serikali imeshachukua hatua, tumekubaliana kwamba sasa hivi tunakwenda kwenye mambo ya TEHAMA, hata vyuo vya ualimu, tumejenga VETA, ili anayekwenda kwenye mfumo rasmi aweze kushindana akiajiriwa na Serikali, au aweze kujajiri. Kwa hiyo, kuna mambo makubwa, mengi, mazuri ambayo yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupewe nafasi Serikali mkakati ambao Wizara imepanga. Na Mheshimiwa Profesa bahati nzuri Wizara hii angalia juu yupo Mheshimiwa Profesa Ndalichako, hakuna mtu anayehozi uwezo wake; Katibu Mkuu, Dkt. Akwilapo hakuna anayehozi, Manaibu Katibu Wakuu, Dkt. Samakafu, Profesa Mdoe, yaani hapa, mwanasheria Mheshimiwa Olenasaha, wote hawa, hii Wizara kwa kweli imesheheni. Na katika kipindi muhimu sana cha kuwapa watu nafasi wafanye kazi yao tuwapime kwa matokeo ni kipindi hiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Sware rudisha shilingi Mheshimiwa Profesa akajipange na watu wake, kama una maoni uyapeleke, wewe ni mtafiti, utafiti ukafanyike, eneo gani libadilishwe tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasilishe.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Inawezekana kuna watu wanachangia humu

hata mitaala hawajui; mitaala labda kwa lugha rahisi ni jumla ya mambo yote yale ambayo tunataka tuwafundishe wanafunzi wetu; mipango, falsafa. Sasa unapoinuka hapa unazungumza mitaala ambayo iko *outdated*, sasa hivi tuko kwenye dunia ya teknolojia, ninyi wenyewe uchumi mnaozungumza wa viwanda, mitaala yenu ina-reflect hicho tunachokizungumza? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo mambo tunayoyasema hapa kwa ajili ya nchi. Sasa mtu anasimama hapa porojo haelewi hata anachosema, sasa kuna vitu hapa havihitaji siasa, vinahitaji tu kuelewa na kukiweka kwenye *perspective* tusaidie nchi. Mheshimiwa Profesa sifa hizi unazosifiwa ziwe *reflected* kwenye mambo tunayoyaamua hapa kwa sababu anachosema Mheshimiwa Dkt. Sware, tukubaliane mitaala tuliyonayo imeshapitwa na wakati sasa tunataka kwenda huko mbele, tunakuja na mitaala ya aina gani. Utupe *commitment* hapa kwamba mimi kuanzia hapa mpaka hapa ntafanya utafiti baada ya hapa tutaleta mitaala mipya, ndicho tunachozungumza hapa...

MWENYEKITI: Si Waziri ameshasema Mheshimiwa Heche? Waziri amechasema mchakato unaendelea na wao *they are working on it*. Tatizo huwa saa nyingine hamsikilizi. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuombe sana dada yangu, Mheshimiwa Dkt. Sware, anirudishie shilingi kwa sababu kwanza suala la kubadilisha mtaala ni suala la mchakato, huwezi tu ukakaa hapa unasema unabadiilisha kwa sababu kuna uchumi wa viwanda, lazima twende ndani tuangalie ni kitu gani ambacho kinatakiwa kubadilika katika somo lipi. Yaani hatuwezi tukakaa tu hapa tumekaa tunasema kwamba kuanzia sasa tumebadilisha mtaala, ni suala la kitaalam ambalo linatakiwa kufanyiwa uchambuzi wa kina. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na suala la kusema kwamba tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda tunazingatia. Kwa

sababu katika kufundisha masomo, masomo ya sayansi, kwanza kuna mambo mengine hata miaka nenda miaka rudi yako vilevile; *Newton laws of motion*, bado iko vilevile hata ukibadilisha mtaala. Kwa hiyo tuiseme tu kubadilisha mitaalaa kwa sababu ya muda, kwamba umekaa, lazima tuangalie kwanza jambo la msingi la kubadilisha ni nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema kwamba wachangiaji wanazungumzia kwamba nchi yetu tulikuwa tunaamini katika suala la ujamaa na kujitegemea; bado nchi yetu inaamini katika Azimio la Arusha, hatujafuta, kwa hiyo, bado tunaamini katika misingi ya kujitegemea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujitegemea kunapaswa kuanzia nyumbani, watoto wetu tunavyowalea leo hii hata kufagia nyumba mtoto mdogo kila kitu anafanyiwa na *house girl*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, hebu kaa kwanza. Waheshimiwa muda wetu umekwisha; Katibu.

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

| | |
|---|----------------------|
| Kif. 1001 – <i>Administration and HR Management</i> | Sh. 7,524,038,930/= |
| Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> | Sh. 619,946,744/= |
| Kif. 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> | Sh. 2,146,781,006/= |
| Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> | Sh. 1,150,846,692/= |
| Kif. 1005 – <i>Procurement Management Unit</i> | Sh. 609,268,592/= |
| Kif. 1006 – <i>Government Communication Unit</i> | Sh. 363,904,890/= |
| Kif. 1007 – <i>Legal Unit</i> | Sh. 196,579,860/= |
| Kif. 1008 – <i>ICT and E – Learning</i> | Sh. 493,375,703/= |
| Kif. 2001 – <i>Basic Education Development Office</i> | Sh. 70,769,737,893/= |
| Kif. 2002 – <i>School Quality Assurance</i> | Sh. 30,168,484,198/= |

| | |
|--|-----------------------|
| Kif. 2003 – <i>Regional and Inter Education Affairs Coordination Unit</i> | Sh. 0 |
| Kif. 2004 – <i>Education Sector Performance Coordination Unit</i> | Sh. 0 |
| Kif. 3001 – <i>Basic Education</i> | Sh. 0 |
| Kif. 3002 – <i>Adult Education and Non Formal Education</i> | Sh. 0 |
| Kif. 4001 – <i>Secondary Education</i> | Sh. 0 |
| Kif. 5001 – <i>Teacher Education</i> | Sh. 26,020,225,604/= |
| Kif. 7001 – <i>Higher Education</i> | Sh. 291,483,115,591/= |
| Kif. 7002 – <i>Technical and Vocational Training Division</i> | Sh. 53,884,219,082/= |
| Kif. 8001 – <i>Science, Technology and Innovation</i> | Sh. 38,358,398,227/= |
| <i>(Vifungu viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)</i> | |

Fungu 18 – Tume ya Taifa ya UNESCO

| | |
|--|---------------------|
| Kif. 1001 – <i>Administration and HR Management</i> | Sh. 2,156,017,000/= |
| <i>(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)</i> | |

MATUMIZI YA MAENDELEO

Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

| | |
|---|-----------------------|
| Kif. 1001 – <i>Administration and HR Management</i> | Sh. 250,000,000/= |
| Kif. 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> | Sh. 177,170,496,000/= |
| Kif. 2001 – <i>Basic Education Development Office</i> | Sh. 71,227,862,624/= |
| Kif. 2002 – <i>School Quality Assurance</i> | Sh. 17,000,000,000/= |
| Kif. 4001 – <i>Secondary Education</i> | Sh. 0 |
| Kif. 5001 – <i>Teacher Education</i> | Sh. 29,595,917,591/= |
| Kif. 7001 – <i>Higher Education</i> | Sh. 539,925,136,493/= |

Kif. 7002 – *Technical and Vocational Training Division*..... Sh. 5,000,000,000/=
Kif. 8001 – *Science, Technology and Innovation*..... Sh. 22,550,387,552/=

(Virfungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Tukae! Mtoa Hoja.

TAARIFA

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako, likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofii)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja liamuliwa na kuafikiwa)*

(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2019/2020 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Hongera sana Mheshimiwa Waziri, Wabunge wote, kwa pande zote mbili, mmefanya kazi nzuri. Hivi ndivyo Bunge linavyofanya kazi, kikanuni, ikifika muda tunasimamisha mzungumzo yote, hakuna mtu kununa, Kanuni ya 104, habari ndiyo hiyo!

Naahirisha Shughuli za Bunge...

MBUNGE FULANI: Mwongozo.

MWENYEKITI: ...mpaka Alhamisi saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 2 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*